# *Neno Lililonenwa Ndilo Mbegu Ya Asili* [1]

Asante, Ndugu Neville. Mtakuwa na ibada ya ubatizo katikati ya wakati? [Ndugu Neville anasema, "Mara baada ya wewe kumaliza."—Mh.] Nikiisha kumaliza. Kweli? Uh-huh.

2 Habari za asubuhi, marafiki. Nina furaha sana kuwa hapa! Na asubuhi ya leo tunaanza mapema kidogo. Na sikuzote nasikitika kuona hakuna nafasi ya kutosha kuwaketisha watu. Nami najua ni vigumu kwenu kusimama. Basi nimetangaza, asubuhi ya leo, kwamba huu ungekuwa ndio wakati ambapo nilitaka kuwa na muda mwingi. Nami nafikiri ingekuwa vizuri sana, inapoendelea, wakati ibada ikiendelea, kwamba kama wengine wangeketi chini, wengine wasimame, na kwa namna fulani wapumzishane. Na kama unataka kutoka nje na kutembea huku na huku kwa muda kidogo tu, kumbuka, kwa kuwa ni ibada ndefu, i—itakuwa sawa kabisa. Halafu tunaweza kubadilishana. Na sasa wao ni . . .

3 Tunajua wako kwenye mradi wa ujenzi, hapa maskanini, kwa ajili ya kanisa pana zaidi na kubwa zaidi linaloweza kuwa na nafasi ya kutosha ya kuketi. Nami nafikiri kanisa hapa litaketi tu karibu watu mia mbili hamsini, mia tatu. Na labda kuna mia zaidi ya hao hapa ndani sasa. Kwa hiyo itaninii . . . Nami niliingia, nikawaona watu wakiendesha magari huku na huko, wasingeweza kupata mahali pa kuegeshea, kote. Na—na, bila shaka, wanapokuja hapo mlangoni na kuona kumbi zimejaa, kuta zimesongamana, na kadhalika, na watu, basi, kote jukwaani na kadhalika, basi wa—wanaondoka. Nasi tunataka kila mtu ausikie Ujumbe wa Bwana, tunapojaribu kuuleta.

4 Ninataka kutangaza kwamba, mara moja, nitajaribu kuzungumza hadi saa sita. Halafu baada ya . . . Nami nitawaachilia saa sita, na hilo litampa kila mtu wakati wa kwenda kutafuta chakula. Katika wakati huu, mhudumu, mchungaji, Ndugu Neville hapa, atakuwa na ibada ya ubatizo wakati huu. Na—na ninyi watu mwondoke polepole mwende mkale, kisha tutarudi. Nami nitajaribu kuwa mimbarani saa nane kamili, kisha niendelee alasiri ya leo.

5 Basi nimekuwa katika maombi sana juma hili. Na hata ni—nisingemaliza kama sikuwa nimekatilia mbali labda robo yake, ama labda theluthi moja, juu ya yale ninayotaka kuwaambia watu. Sasa, kwa hiyo, tunawashukuru kwa ushirikiano wenu mzuri wa kuja mikutanoni, na—na yale mmetufanyia, na kutusaidia na kutuombea.

6 Nami nilikuwa na majaliwa, dakika chache zilizopita, ya kuzungumza na m—mzee na mwanamke mkongwe, ambao ni . . . Tunawajua kama Ndugu na Dada Kidd, ambao wamekuwa waaminifu sana miaka yote. Nao walisimama dakika chache zilizopita. Nikawaambia wapitie hapa, nilitaka kuwaona kwa dakika moja. Basi ilikuwa ni majaliwa jinsi gani kuzungumza na wazee, waliokuwa wakihubiri Injili nilipokuwa ningali katika m—mtoto mchanga. Nayo hii Injili tukufu ya kale inakuwa bora zaidi wakati wote, tunapokaribia mwisho wa safari.

7 Na sasa kuna vitambaa vya maombi vilivyowekwa hapa, nami ninataka kuviombea, baada ya kitambo kidogo. Na sasa hebu na tuinamishe tu vichwa vyetu kwa muda kidogo wa maombi.

8 Baba yetu wa Mbinguni, Wewe ulisema katika Neno Lako, "Nikiinuliwa juu ya nchi, nitawavuta watu wote Kwangu." Na hilo ndilo kusudi letu maishani, ni kuinua, mbele ya kizazi cha watu kinachokufa, kwamba Yesu Kristo angali ni Mwana wa Mungu, Mwokozi wa ulimwengu. Nami nina furaha sana kujua kwamba ninaishi ambapo kuna watu wanaoamini hilo, na pamoja na maelfu ambao wamemkubali kama Mwokozi wao.

9 Na tukijua, ya kwamba, baada ya maisha haya kumalizika, kutakuwako na maisha kwenye ng'ambo ya pili, ambayo yatakuwa na utukufu sana, ambapo hizi taabu na saa chache tunazopitia, utusitusi huu na vivuli vya maisha hapa katika uwanja wa majaribio, kwamba tunaingia tu kwenye mzingo sasa, tukingojea kule kuhesabu kinyumenyume. Kwa kuwa, hivi karibuni utakuja wakati ambapo wakati wa Mungu umetimia, ule mkono mkuu ambao umeuzuia wakati kwa muda mrefu, hatimaye utaachilia na Kanisa Lake litaondoka duniani, angani, huko nje kwenye Nchi ambako hakutakuwa na magonjwa, huzuni, uzee, mauti. Hiyo ndiyo sababu tumekusanyika leo, Bwana, ni kuonyesha hisia zetu kuhusu mambo haya.

10 Tuna furaha sana kujua ya kwamba huku si kuwaleta watu pamoja kwa ajili ya kitu bure; kwamba imethibitishwa ndio ukweli mkuu sana ulimwengu umewahi kujua, ya kwamba Mwana wa Mungu hajafa, Yeye aliyefanya zile ahadi, bali yu hai miongoni mwetu hata milele. Nasi tuna furaha sana asubuhi ya leo, Bwana, zaidi ya mambo yote, ingawa tunamiliki ulimwengu na tunaweza kuwa vijana kwa mamia ya miaka, kuufurahia, bali ingekuwa tu ni msimu mmoja ukilinganishwa na wakati uliowekwa kwa ajili ya wale wampendao. Kwa hiyo, tunajaribu kuwaelekeza ndugu yetu na dada kwenye saa hii kuu inayotukaribia. Nasi tunapouona wakati huo ukija, Bwana, mioyo yetu inawaka moto. Tunataka kujiweka tayari.

11 Na mmoja mmoja tunashuka kwenye uchochoro. Ndiyo kwanza tumalize kumzika mmoja kutoka miongoni mwetu. Dada yetu Bell, akienda upesi, kulingana na ombi lake; upesi

sana, tusingeweza kumfikia, kuomba pamoja naye. Lakini ilikuwa ni ombi lake kwenda, kuona jinsi Wewe ulivyo mwema kutupatia mambo yote tunayotamani mioyoni mwetu. Humwachi hata mmoja wao. Uliahidi hilo.

12 Sasa, tunaomba ya kwamba utaileta mioyo kukuelewa Wewe leo, wale wasiokuelewa. Walete wenye dhambi kwenye toba, walete wagonjwa kwenye maarifa ya uponyaji wa Mungu. Ee Mungu, wabariki watakatifu Wako na uifunge mioyo yao pamoja. Na wakati kanda hizi zikienda kwenye mi—miji na makanisa, kote kote katika mataifa kote ulimwenguni, jalia ndugu wahudumu, ambao labda wakati mmoja wamekosa kuelewa, waelewe sasa, Kanisa Lako lipate kuwa tayari.

13 Na sasa, Ee Bwana, uliyenitenga na mama yangu, uliyenilisha siku zote za maisha yangu, umenifikisha kwenye saa hii; kwa neema Yako, nikihisi ilikuwa ni mapenzi Yako kwamba ninapaswa kuwaelezea watu, kwa nini nimetenda na kufanya jinsi nimetenda, jalia iwe ni kwa njia ambayo watu watakuwa na ufahamu bora zaidi, Bwana, wa upekee wa watumishi Wako. Tujalie mambo haya, Baba. Na Maandiko haya, na somo na maneno ambayo tumeandika hapa kote katika juma hili, tukiomba na kujifunza, jalia yaanguke kwenye udongo mzuri kila mahali yanaposikiwa, udongo unaoweza kuyashikilia na kuyalisha. Na ndipo sifa zote zitatolewa Kwako, kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

14 Kwa watu huko nje kwenye magari, ambao hawawezi kuingia, ninaambatanisha chombo kidogo hapa sasa. Basi fungulia redio yako kwenye elfu moja mia moja na hamsini, elfu moja mia moja na hamsini, nawe utaupata huu Ujumbe moja kwa moja kwenye redio kwenye gari lako. Sasa, huu ndio mwunganisho? Imefunguliwa, sivyo, kwa ajili ya ka—kanda?

15 Sasa, kwa marafiki zangu wote, hapa na popote kanda hizi zinakoweza kwenda, ninajisikia kwamba ninawiwa na watu, maelezo ya mambo mengi ambayo nimesema na kufanya. Mara nyingi sana, watu wamenijia, na kusema, "Mchungaji wetu anasema. . .Kwa nini ufanye *hivyo*, Ndugu Branham? Kwa nini ulisema *hivi*? Na ni kitu gani kinachokufanya ufanye *hivi*?" Sasa, kwa moyo wangu wote, kila kitu ambacho nimefanya, nimekifanya kwa nia nzuri sana nijuayo. Na kila kitu ambacho nimesema, nimekisema kutoka moyoni mwangu. Nami nimefanya hivyo kwa kusudi fulani. Nami nitajaribu, asubuhi ya leo, kwa msaada wa Mungu, kueleza kutoka kwenye Biblia kusudi, na ni kwa nini nimefanya hivyo.

16 Na sasa hapo, labda, katika kundi la watu la ukubwa huu, labda kuna wahudumu wengi wanaoketi hapa. Na kutakuwa na wengi watakaosikia hili. Na laiti tungalikuwa na wakati wa kutosha ambao mimi. . .kuweka yote niliyokuwa nimewazia, na kuyaweka kimaandiko, nikayaleta Maandiko, hasa, kwa—

kwa watu. Lakini, kwa ndugu zangu, ijapokuwa huenda hamkukubaliana nami; sasa ninazungumzia hapa na kwa ajili ya kanda pia. Huenda hamkukubaliana nami, sana, kwa sababu ya . . . msimamo wangu kwa yale ninayofikiria kwamba ni sahihi. Nanyi mna haki ya kutokubaliana nami, kwa kuwa mnaweza kuliona vinginevyo. Lakini natumaini kwamba mimi, kwa msaada wa Mungu asubuhi ya leo, nitaweza kuwaonyesha sababu ya mimi kuchukua msimamo huu. Na—mami kamwe . . .

17 Kumekuwa na mara nyingi ambapo nimeyakemea makanisa, madhehebu, mavazi ya wanawake, matendo ya wanaume. Nafikiri nimeunga mkono hilo kikamilifu kwa Maandiko. Na hakuna wakati mmoja, Mungu akiujua moyo wangu, ambapo nimewahi kuwa na hisia mbaya kwa mtu yeyote. Haidhuru kama walitofautiana nami, kadiri Mashariki ilivyo mbali na Magharibi, ningali niliwapenda. Na maadamu nina Roho wa Mungu ndani yangu, daima nitalipenda Kanisa Lake, watu Wake. Haidhuru wanafanya nini, ama jinsi wanavyonitendea, hilo halitakuwa na uhusiano wowote nalo. Ningali ninawapenda.

18 Ninakumbuka, wakati mmoja mtu mmoja jina lake Musa. Watu hao sikuzote, tungesema katika usemi wetu wa kusini, walimkera, daima walimweka chonjo, kila kitu kilikuwa ni manung'uniko ama kulalamika, na kadhalika. Lakini, Musa, ilipofikia kwenye shindano la kuamua, wakati Mungu aliposema, "Jitenge nao, maana nitakuchukua na kuanzisha taifa," Musa alijibwaga mwenyewe katika njia ya ghadhabu ya Mungu. Kasema, "Nichukue mimi, wala si hao watu," ambao alikuwa amewaita waasi, uasi dhidi ya Mungu na dhidi yake. Hata hivyo, aliwapenda sana hata akasema, "Nichukue, ukawaokoe." Huyo alikuwa ni Kristo ndani ya Musa.

19 Na kama mtu, haidhuru ni kiasi gani mwingine asingekubaliana naye, kama hajisikii hivyo, basi amepungukiwa na Kristo, naamini, ikiwa kutoka moyoni mwake (si midomo yake, bali moyoni mwake) kama hajisikii hivyo kwa wanadamu.

20 Nilishangaa sana wakati mmoja, si kwa ajili ya ucheshi tu wakati huu. Lakini kulikuwako na m—mkutano wa Chicago, basi mtu mweusi alikuwa ameketi pale, naye akaendelea kusema, "Ninataka kumwona Dk. Branham." Alikuwa amevaa kofia kubwa mno, misalaba mikubwa mno, urefu na upana wa inchi nane ama kumi, kifuani mwake, na majoho, na amevalia kiajabu sana, pamoja na pete na shanga za ajabuajabu, na kadhalika. Nikamwambia Ndugu Baxter, ambaye alikuwa mwenzangu, "Mwambie. Mleteni mle chumbani. Ni—ninataka . . . nitamwona."

Ndipo akaketi chini mbele yangu, na kusema, "Je, nikutambue kama 'baba,' au kama 'kasisi,' au kama 'mzee'? Au ungetaka nikutambue jinsi gani?"

Nikasema, “Kama unanipenda, niite ‘ndugu.’” Naye, kwa heshima, akafanya hivyo.

21 Naye akanipa sifa zake, ambazo, loo, ningechukua mistari michache kuandika kwenye karatasi, vyeo vya jina la kanisa, na cheo chake kanisani. Lakini alisema jambo moja ambalo daima limedumu nami. Alisema, “Ninavutiwa na hii, Ndugu Branham. Mimi . . . ” Akaniambia yale yaliyomvutia, kanisani mwake na mambo haya. Akasema, “Ninavutiwa na jamii moja,” akasema, “hiyo ni jamii ya binadamu.”

Nikasema, “Hapo tutapeana mikono.”

22 Jamii ya binadamu, kwa kila mtu, kwa kila kanuni ya imani, kwa kila rangi, na kwa kila mtu ambaye Kristo alimfia, hiyo ndiyo shauku yangu asubuhi ya leo. Nami nimejaribu daima kuifanya shauku—shauku yangu.

23 Sasa nataka kusoma. Na—na halafu nininii tu . . . Sina lengo la kuhubiri, kwa sababu labda ingekuwa angalau, yale niliyo nayo hapa ya kusema, labda yatanichukua saa nne au tano. Kwa hiyo baada ya yapata saa mbili sasa, basi tutafumukana twende kula chakula cha jioni, kisha turudi kama saa nane. Tuwe hapa kabla ya saa nane, maana ninataka kuanzia saa nane kamili. Iweni hapa yapata saa saba na nusu, mkiweza. Ndipo tutaondoka kwa wakati unaofaa kwa ajili ya usiku wa leo.

24 Inanibidi kuondoka alasiri ya leo, bado, kwenda Tifton, Georgia, ambako nitafanya ibada kesho usiku, na ukumbi wa shule ya upili kule, ibada tu ya mahubiri. Halafu basi kutoka hapo, sijui, popote tu aongozapo kutoka huko. Mahali pengi, Ndugu Arganbright na hao wengine wamepiga simu kutoka ng’ambo, nianze mara moja kuelekea kule; kote Magharibi, huko nje Canada, kote ulimwenguni. Lakini nitaninii . . . mtajua . . . amini . . .

25 Ninaamini mtajua vizuri zaidi baada ya mimi kumaliza. Kama Mungu atanisaidia kuwapa jinsi nilivyopewa, basi, baada ya ibada, mtaelewa, natumaini. Halafu basi kukiweko na maswali yoyote, msiyoyaelewa, nitawaomba mlete vitabu vyenu. Na—na halafu ninyi mlio na vinasasauti, mnaweza kuchukua hizo kanda na kuziweka nyumbani mwenu, na kuketi chini kwa moyo mkunjufu, moyo wazi tu. Liweke tu, useme, “Bwana, nimepumzika tu sasa. Nitasikiliza.” Ndipo unaposhika kitu fulani, zima kinasa sauti na uende uchukue Maandiko.

26 Nayo Biblia ilisema, Yesu alisema, “Hayo Ndiyo yanayonishuhudia Mimi.” Mnaona? Na hebu tuyaangalie Maandiko yote tuone kama ni sawa. Sasa nataka kufungua . . .

27 [Mtu fulani anazungumza na Ndugu Branham—Mh.] Samahani? Papa *hapa* ndani. Alikuwa akinionyesha maikrofoni mbalimbali za kutumia. Kuna lundo kubwa sana la hizo hapa asubuhi ya leo, sijui nianzie na ipi.

28 Sasa hebu na tugeukie ya Kimaandiko. Nitaanzia katika Mwanzo, kisha nimalizie usiku wa leo katika Ufunuo. Ninaamini Neno. Mwanzo, kuanzia mlango wa kwanza, ningependa kusoma sehemu ya Neno. Na sasa kama mtu fulani angetaka, mtu fulani kuchukua ninii . . . mna penseli zenu na karatasi, na kadhalika, maana nina Maandiko mengi. Ninataka kuendelea kusoma wakati wote juu ya Maandiko haya.

> *Hapo mwanzo Mungu aliumba* mbingu *na . . . nchi.*
>
> *Nayo nchi ilikuwa ukiwa, tena utupu; na giza lilikuwa juu ya uso wa kilindi. Na Roho ya Mungu ikatulia juu ya uso wa maji.*
>
> *Mungu akasema, Iwe nuru: ikawa nuru.*
>
> *Mungu akaiona nuru, ya kuwa ni njema: Mungu akatenga . . . nuru na giza.*
>
> *Mungu akaiita nuru Mchana, na giza akaliita Usiku. Ikawa jioni ikawa asubuhi, siku ya kwanza.*
>
> *Mungu akasema, Na liwe . . . anga katikati ya maji, likayatenge maji na—na maji.*
>
> *Mungu akalifanya anga, akayatenga maji yaliyo chini ya anga na yale maji yaliyokuwa juu ya anga: ikawa hivyo.*
>
> *Mungu akaliita lile* anga *Mbinguni. Ikawa jioni ikawa asubuhi, siku ya pili.*
>
> *. . . Mungu akasema, Maji yaliyo chini ya* mbingu *na yakusanyike mahali pamoja, ili nchi kavu ionekane: ikawa hivyo.*
>
> *Mungu akapaita pale pakavu Nchi; na makusanyiko ya maji* akayaita . . . *akayaita* Bahari: *Mungu akaona ya kuwa ni vyema.*
>
> *Mungu akasema, Nchi na itoe majani,* na mboga . . . na *mbegu, na* miti *ya matunda izaayo matunda kwa jinsi yake, ambayo mbegu zake zimo ndani yake, juu ya nchi: ikawa hivyo.*
>
> *Nchi ikatoa majani na* mboga, ikatoa *mbegu kwa jinsi yake, na* miti ikazaa *matunda, ambayo mbegu zake zimo ndani yake, kwa jinsi yake: Mungu akaona ya kuwa ni vyema.*
>
> *Ikawa jioni ikawa asubuhi, siku ya tatu.*

29 Sasa nataka kuanza asubuhi ya leo, na somo langu, kutumia hili: *Neno Lililonenwa Ndilo Mbegu Ya Asili*. Sasa hilo ndilo ninalotaka kuweka somo juu yake. *Neno Lililonenwa Ndilo Mbegu Ya Asili*. Sasa kama mtaangalia, Mungu alisema, “Na izae, kwa jinsi yake.” Chochote kile, hakina budi kuzaa kwa jinsi yake.

30 Sasa, Neno hili la Mungu ni la Milele. Mungu, akiwa hana kikomo, hawezi kunena jambo moja na halafu, baadaye, kulibadilisha kuwa jambo lingine, kwa uamuzi bora zaidi. Kwa sababu, kila uamuzi wa Mungu ni mkamilifu. Hawezi. Neno Lake likiisha kunenwa, haliwezi kufa kamwe. Linaendelea kuishi, na kuendelea, na kuendelea, wala haliwezi kufa kamwe, kwa sababu ni Mungu. Neno Lake haliwezi kufa si zaidi ya vile anavyoweza kufa. Hiyo ndiyo sababu tunasoma katika Yohana wa Kwanza, ama, Yohana Mtakatifu, mlango wa kwanza, kwamba, "Hapo mwanzo alikuwako Neno, naye Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili." Neno lile lile lililonenwa hapo mwanzo, pamoja na kusudi Lake la Milele, lilikuja likafanyika mwili na kukaa miongoni mwetu. Neno la Mungu!

31 Miaka kadhaa iliyopita, nilisikia ya kwamba mwanamke fulani. . . Sasa, huenda hili lisiwe sahihi. Ambaye aliramba radiamu kwa ulimi wake, wakati akiichanganya, apate kuiweka kwenye nyuso za saa za mezani na za mkono; ikamwua huyo mwanamke. Ndipo miaka kadhaa baadaye, wakiliweka fuvu lake kwa uchunguzi wa maiti, kitu kama hicho, walisema ungeweza kuchukua vyombo, chochote wanachotumia, na kuweka kwenye mfupa huo wa fuvu, na, kwa m—mngurumo, ungali ungeweza kusikia radiamu hiyo ikiendelea, katika fuvu la kichwa chake, akiisha kufa, kwa miaka mingi. Radiamu sikuzote inaendelea.

Neno la Mungu linaendelea daima.

32 Ninaambiwa, ya kwamba kama tungeweza kuchukua chombo ambacho kingeweza kuinasa, kwamba sauti ya mwanadamu, sauti yangu ninayonena leo, miaka elfu kumi tangu sasa ingali ingeweza kunanaswa hewani. Kama vile kuangusha petali katikati ya kidimbwi. Na hayo mawimbi madogo sana, baada ya kukoma kuonekana kwa jicho, yanaendelea mpaka yanafikia ukingoni. Nalo wimbi la hewa la sauti zetu huendelea kusafiri kote na kuuzunguka ulimwengu. Kwa hiyo, basi, sauti yetu, kile tunachosema, kitakuwa hukumu yetu. Ushuhuda wetu utainuka moja kwa moja dhidi yetu. Sauti zetu wenyewe zitatoa mwangwi masikioni mwetu wenyewe, kwenye Hukumu ya Mungu, wakati chombo Chake kikuu kinaponasa kila sauti ambayo imetamkwa, kila neno lililotamkwa.

33 Na sasa kuna njia moja tu ya kukomesha sauti hiyo ambayo ni mbaya, hiyo ni, kutubu. Mungu pekee ndiye anayeweza kuikomesha. Isipokomeshwa, itaendelea na kukutana nawe katika Umilele. Kwa hiyo, Mungu, akiwa mkamilifu, na Sauti Yake ni ya Milele, Sauti Yake Mwenyewe itabidi iifikie. Kwa hiyo, Yeye hana budi kuwa mkamilifu katika kila uamuzi, kwa kuwa, akiisha kusema jambo fulani, halina budi kuendelea hata mwisho kisha lirudi Hukumuni.

34 Sasa kama mtakuwa na ufahamu halisi, ama kujaribu kuwa nao, mtaona ni kwa nini daima nimechukua huo msimamo kwa ajili ya Neno la Mungu, nililo nalo; kwa sababu mambo mengine yote hayana budi kuangamia. Mungu ni wa Milele, nalo Neno Lake ni la Milele. Sasa, mnaposoma. . . Nami nitajaribu kuzungumza kirefu niwezavyo, ili kwamba mtayapata hayo maneno, nami ninafanya hivyo kwa ajili ya kanda pia. Kwamba, lazima mjue ya kwamba Biblia hii ni Neno la Mungu.

35 Sasa, tunajua ya kwamba tunaelekea Hukumuni, kwamba Sauti ya Mungu itatufikia, mahali fulani, kwa sababu kila mwanadamu alipewa kuisikia. Wahudumu wanawajibika kuichukua. Na kama Sauti hii ya Mungu haina budi kumfikia kila mtu, basi tuna. . . huna budi kuisikia, ama hapa au kwenye Kiti cha Hukumu.

36 Kwa hiyo, kama kanisa linayo Sauti ya Mungu, basi huna budi kuisikia sauti ya kanisa, kama vile watu wetu wa Katoliki ya Kirumi wanavyotwambia. Na wakati wao, wenyewe, wamechanganyikiwa sana na wanatofautiana katika mafundisho yao, ya Kirumi, ya Kiyunani, na aina mbalimbali, basi hapawezi kuwa na mahali popote pa kuaminia. Kwa sababu, Kanisa ni lipi? Je, kanisa la Kirumi ni la kweli, ama kanisa la Kiyunani ni la kweli, ama baadhi ya makanisa mengine ni ya kweli? Je, Walutheri ni wa kweli, Wabaptisti ni wa kweli, Wamethodisti ni wa kweli, Wapresbiteri ni wa kweli? Ama, wa kweli ni akina nani, wakati kuna tofauti nyingi sana ndani yao? Mmoja yuko mbali kama Mashariki ilivyo mbali na Magharibi, mmoja na mwingine.

37 Lakini, nionavyo mimi, Sauti ya Mungu ndiyo Hakimu. Kwa hiyo, Sauti ya Mungu, na kama ni kamilifu hivyo, haina budi kutoka kwenye chanzo fulani kikamilifu.

38 Na kama watu wakilileta kwa njia moja na nyingine, pamoja na tofauti zao za madhehebu, basi kwa kweli ha—hakuna njia ya kuamini yale wanayosema. Natumaini hilo ni dhahiri. Mnaona? Kwa sababu, na kama mmoja akisema iko *hivi*, mmoja anasema, "Huna budi kujiunga na kanisa *hili*. Kanisa *hili*, pekee, lina wokovu." Hiyo ndiyo tafsiri ya Katoliki. Walutheri wanakuja na kusema wao ndio njia. Hii hapa Methodisti inakuja na kitu kingine, Baptisti na kitu kingine, Pentekoste na kitu kingine. Na inaonekana kuna lundo kubwa sana la machafuko.

39 Ndipo, unapowapelekea ndugu zetu Neno hili lililoandikwa, wengi wao husema, "Vema, siku hizo sio sasa." Mwingine anasema, "Ni historia tu." Huyo mwingine anasema, "Ni kitabu cha mashairi." Huyo mwingine anasema, "Kanisa lina haki ya kulibadilisha." Basi tunasimama wapi? Pako wapi mahali pa kupumzikia kwa imani?

40 Wakati, Mungu, akiwa wa Milele. . . Ninaamini, kama tutahukumiwa, na daima tumehukumiwa, kwamba kama

tunapaswa kuhukumiwa kwa chochote, itakuwa ni kwa Neno la Mungu ambalo limetoa agizo.

41 Halafu, kama tutahukumiwa kwa Neno hilo, basi Mungu angekuwa ni Mungu asiye haki, kuleta mchafuko kama huo duniani, na maskini akili ya mwanadamu imechanganyikiwa sana, haijui la kufanya. Na mmoja atajiunga na *hili*, kisha ajiunge na *lile*. Maskini jamaa ayenajaribu kuwazia, anajaribu kupata mahali panapofaa, atalisikiliza dhehebu *hili*, kisha atasikiliza dhehebu lingine. Nalo *hili* linaonekana kuwa bora kuliko *lile*; ataenda. Na, jambo la kwanza, amerudi kwenye la kwanza tena. Kamwe hajui la kufanya.

42 Lakini kama Mungu atauhukumu ulimwengu kwa kitu fulani, itakuwa ni kwa Neno Lake. Ninaamini hilo.

43 Na, sasa, ndugu zangu. Sasa, ninaposema hivyo, nimaanisha sio tu kundi hili dogo hapa asubuhi ya leo, lakini ninamaanisha mahali ambapo kanda hizi zitatumwa kote ulimwenguni. La—laiti mngenivumilia kwa muda kidogo, na kuwazia jambo hilo, ya kwamba hapana budi kuwe na mahali fulani panapokuja kwa ajili ya Hukumu.

Ndipo baadhi yao husema, "Toleo la King James, ama toleo lingine. Na sasa wanatengeneza to—toleo la Standard, ama kitu fulani."

44 Ninaamini, kama Mungu ni Mungu mwenyezi, kama vile alivyo, Yule wa Milele, hana budi kulishughulikia. Ni juu Yake. Kama ninataka kwenda Mbinguni, Kwake, ni juu Yake kunipa mahali ambapo nitajua la kufanya, mahali fulani ambapo unaweza kuweka mkono wako na kusema, "*Hapa* Ndipo." Mnakubaliana na hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Inabidi . . . Ni juu Yake.

45 Angekuwa asiye haki . . . Kama ningesema, "Bwana, nilikuwa Mlutheri," na huyo mwingine aseme, "Vema, ni—nilikuwa Mkatoliki." Vema, hao hapo wawili wako, wakipingana. Sasa, mtu maskini atafanya nini? Vema, vipi kama kanisa Katoliki ni la kweli? Basi Walutheri wote wamepotea. Mbona, kama Walutheri ni wa kweli, Wakatoliki wote wamepotea.

46 Mnaona, huna budi kuwa na mahali fulani ambapo imani inaweza kuchukua mahali pake pa kutulia. Na kwangu mimi . . . Sijui jinsi mnavyojisikia kulihusu. Lakini, kwangu mimi, Biblia ni Neno la Mungu lisilokosea. Nami ninaamini ya kwamba Mungu amelilinda Neno Lake, hata hakuna hata kituo kimoja kisicho mahali pake.

47 Binti yangu huko nyuma, Rebekah, alikuwa akisema, "Baba, shuleni tulithibitisha ya kwamba ninii . . . kwamba ulimwengu huu una umri wa mamilioni na mamilioni ya miaka. Basi hilo si linahitilafiana na Biblia?"

"La, bwana," nikasema. "Sivyo."

48 "Vema," kasema, "ikiwa u—uchunguzi mbalimbali wa miamba na miundo, na stalaktiti na stalagmiti na kadhalika, unathibitisha kule kudondoka kwa mamilioni ya miaka, huku Mungu akisema aliumba mbingu na nchi katika moja ya saa ishirini na nne, hilo si linakosoa, linakanusha Biblia?"

Nikasema, "La."

49 Kama utaangalia, Mungu akimwambia Musa kuhusu Biblia, Yeye alisema, "Hapo mwanzo Mungu aliumba mbingu na nchi." Nukta! Kwamba ilichukua muda gani, hiyo si kazi yetu. Ndipo anaendelea na kuanza kuleta wakati Wake wa kuweka mbegu duniani. Lakini, "Hapo mwanzo," huenda ilikuwa ni mamia ya mabilioni ya matrilioni ya miaka, kipindi cha wakati usiopimika, lakini, "Mungu aliumba mbingu na nchi." Nukta! Hilo latosha. Hiyo ndiyo hatua ya kwanza. Unaona? Yeye hafanyi makosa.

50 Paulo, yule mhubiri mashuhuri, alisema, alimwambia Timotheo, "Soma, ujithibitishe, ukiligawanya Neno la Mungu kwa halali." Lisome, kwa moyo mkunjufu. Na hivyo ndivyo ninavyojaribu kufanya.

51 Sasa, huku imani yangu ikiwa katika Neno namna hiyo, basi siwezi kuchukua tafsiri ya kibinafsi, kwa maana Biblia inasema ya kwamba Biblia si ya kufasiriwa apendavyo mtu. Sasa Roho amelifunua hili hivi punde tu. Niliyajua hayo Maandiko, lakini sasa hivi sijui ni wapi hasa katika Maandiko. Lakini, ninyi mnaoyaandika, mtayapata. Nafikiri ni katika Petro, ambapo, "Biblia si ya kufasiriwa kama apendavyo mtu yeyote." Kwa hiyo, kama mwandishi aliyevuviwa alisema, na kama Hiyo si kweli, basi ni kiasi gani cha sehemu zingine Zake zisizo kweli? Ama zote ni kweli au zote si kweli. Huwezi kulifanya vinginevyo.

52 Kwa hiyo, wewe, "Vema, kuhusu kanisa," unasema, "vema, basi, kanisa!" La. Kama ukienda kanisani, basi ni kanisa gani lililo sahihi? Ni kanisa gani lililo sahihi? Unaona?

53 Huna budi kurudi tena kwenye kitu ambacho imani haina budi kutulia. Na, kwangu mimi, ni juu ya Neno la Mungu, nikiamini ya kwamba Biblia hii ndiyo mpango wa Mungu kwa ajili ya watu. Daima imekuwa hivyo!

54 Yesu alisema, "Maandiko hayana budi kutimizwa," yaani, kwamba, "yote yaliyoandikwa katika Maandiko." Sasa kumbukeni hili, maana mnapata kanda sasa. Mwishoni mwa kanda hizi, mtaona ninarejea kwenye hilo tena, kwamba yote yaliyo katika Maandiko hayana budi kutimizwa. Sasa hebu niache hilo lizame kwa dakika moja tu, enyi darasa. Mnaona? Yote yaliyo katika Maandiko hayana budi kutimizwa. Basi, kama Mungu alisema jambo lolote, haya basi, halina budi kutimizwa.

55 Ama, kama halitimii, hilo si Neno la Mungu. Basi, kama ndilo, hilo si Neno la Mungu, basi tuko wapi? Hebu na tupate kitu kinachoonekana kama Mungu, ama chochote tunachotaka kufanya; kama Biblia ilivyosema, "Hebu tule, tunywe na kushangilia, kwa maana kesho tutakufa." Mnaona? Sasa, kama hilo si Neno la Mungu, basi sote tumepotea.

56 Na kama ni Neno la Mungu, Mungu anawajibika kabisa kwa heshima. Mungu, ambaye ni chemchemi ya heshima yote, aliye mwanzo wa heshima yote, aliye chimbuko la heshima yote, aliye chimbuko la Kweli yote, hana budi kusimama na yale aliyosema.

57 Na kama Hili si Neno la Mungu, basi Mungu ni nani, Mungu yuko wapi, au je, kuna Mungu?

58 "Loo," unasema, "Ndugu Branham, ninamhisi." Loo, ka—kafiri anaweza kukwambia jambo lile lile, juu ya sanamu yake. Kusafiri kunakufanyia jambo fulani, unapojionea mwenyewe. "Kwa hiyo ni—ninaamini ningeweza kuangalia na kuona jambo *hili*." Naam. "Ninaamini kama. . .Ni—ninaamini kwa sababu ni—nilibadilishwa namna *hii*. Kwa sababu. . . " Mimi hufanya hivyo, pia. Lakini, kumbukeni, makafiri hufanya jambo lile lile.

59 Mbona, maadili ya Afrika yangeninii. . .Baadhi ya hayo makabila yangewafanya Wamarekani hapa, wajiitao Wakristo, wajionee aibu, uadilifu na usafi miongoni mwa watu wanaoabudu sanamu za kipagani. Kwa hiyo, "Labda huyo ni Mungu"? Mnaona ninalomaanisha?

60 Mna—mnaona, unapoangalia kitu hicho usoni, kuna duara kubwa hapa unayopaswa kufunika, kwa hiyo huna budi kuwa na mahali fulani pa kurejea na kuweka mikono yako.

61 Sasa hebu na tuchukue madai ya Kilutheri; yanashindwa. Hebu tuchukue madai ya Katoliki; yanashindwa. Hebu tuchukue madai ya Kibaptisti, Wapentekoste; yanashindwa. Kwa hiyo huwezi kuweka imani yoyote kwao.

62 Lakini hakuna jambo moja lililoandikwa katika Biblia hii pasipo Mungu kulithibitisha, kwa mtu fulani, kwamba ni Kweli. Mnaona? Ni Kweli. Mara nyingi nimesema, labda imani yangu haitapanda mahali Henoko alipopanda, lakini bila shaka nisingemzuia mtu yeyote ambaye angeweza kupanda pale, imani kuu.

63 Sasa, tukipata msingi huu, ya kwamba, sababu za mimi kuiamini Biblia. Na hapo ndipo ninapochukua somo langu.

64 Sasa, jambo lingine ninalotaka kusema, ya kwamba, siamini Biblia inajipinga Yenyewe. Nimetoa changamoto, kote ulimwenguni, kwa watu wowote, wanaodai hivyo, waje wanithibitishie. Mnaona? Njoo, uthibitishe. Biblia haijipingi Yenyewe. Wewe ndiwe unayepinga Biblia. Mungu hawezi kujipinga Mwenyewe. Kama akifanya hivyo, basi Yeye si Mungu. Na kama Neno hili ni Mungu, basi, na linajipinga, basi

unamfanya Mungu kujipinga Mwenyewe. Basi Mungu wako yuko wapi basi? Kwa namna fulani linakuwa gumu, sivyo, linakuwa na utata? Kama Mungu akijipinga Mwenyewe, Yeye si zaidi ya nilivyo mimi, ama si zaidi ya ulivyo wewe, kwa kuwa anaweza kujipinga Mwenyewe. Neno lipo hapo, bali limefichwa kutoka kwa macho ya wenye hekima na akili.

65 Hiyo ndiyo sababu mtu anasema, ya kwamba, "Mathayo 28:19, ambapo, 'Enendeni mkawafundishe mataifa yote, mkiwabatiza katika Jina la Baba, Mwana, Roho Mtakatifu.' Matendo 2:38 ilisema, 'Tubuni mkabatizwe, kwa Jina la Yesu.' Inahitilafiana."

66 Haihitilafiani. Kila mtu aliyewahi kubatizwa, hana budi kubatizwa katika Jina la Baba, Mwana, Roho Mtakatifu. Na kama hujabatizwa, kwa kutumia Jina la "Yesu Kristo," hujabatizwa katika Jina la Baba, Mwana, Roho Mtakatifu. Umebatizwa katika baadhi ya vyeo vinavyohusu Jina. Kama huo ndio . . . sio ufunuo sahihi, basi Biblia ingekuwa imekosea wakati ilipoendelea na kila mtu akabatizwa kwa Jina la "Yesu Kristo." Lakini kama Biblia, ilibatiza, kila mmoja wa mitume, kote katika wakati, alibatiza katika Jina la "Yesu Kristo," baada ya Yesu kuwaagiza kuwabatiza katika jina la "Baba, Mwana, Roho Mtakatifu," basi Biblia inajipinga Yenyewe kabisa. Lakini ukiliangalia, sivyo. Walifanya tu yale Yeye aliyosema. Si vyeo; bali Jina! Kwa hiyo, hakuna ukinzani.

67 Ni mangapi zaidi ningeweza kutoa humu, ambayo hata nimeyaandika, ambayo watu wanasema yanajipinga Yenyewe. Nimeomba, kwa miaka ishirini na mitano, karibu thelathini sasa, mtu fulani anionyeshe. Hakuna. La, bwana.

68 Iko, ile Kweli, Kweli yote, Kweli tupu. Nayo imani yetu inatulia papo hapo, papo hapo juu ya yale Mungu aliyosema. Usi—usijaribu kulifasiri. Liseme tu jinsi inavyolisema. Usiweke tafsiri yoyote ya kibinafsi. Nami ninaamini ya kwamba hakuna kitu kingine chochote.

69 Sasa, natumaini, ya kwamba kama hili likiudhi, ya kwamba si—si katili. Ninajaribu kusema ni kwa nini ninaamini yale ninayoamini, na jinsi nimetenda jinsi nilivyotenda, juu ya mambo niliyofanya. Ninajaribu kujionyesha mwenyewe kwa ulimwengu, kwamba nimefanya hivi kwa sababu hii ndiyo imani yangu.

70 Ninaamini ya kwamba neno lolote lililoongezwa kwenye Biblia hii, na yeyote aliye na hatia ya kufanya hivyo, ataondolewa sehemu yake kwenye Kitabu cha Uzima. Ufunuo 21. "Kila atakayeongeza kwenye Hili, ama kuondoa katika Hili." Siamini ya kwamba kanuni yoyote ya imani, fundisho lolote la sharti, chochote kile, ila tu Neno halisi la Mungu, ni mpango wa Mungu. Kitu kingine chochote ni dhambi, na kitashughulikiwa, na kitapotea Milele; mtu yeyote, kanuni yoyote ya imani,

dhehebu lolote, ama chochote kitakachoongeza ama kupunguza kwenye kiakifishi kimoja cha Neno hili.

71 Mungu, ambaye si mungu wa jana, ambaye aliandika kitabu na kukikabidhi kwa lundo la mikono ya mwanadamu, na—na kuacha kichafuliwe na chochote kile, kisha auhukumu ulimwengu kwa kitabu hicho.

72 Lakini Mungu aliyekiandika, yu hai, anaishi ndani Yake, na hulithibitisha Neno Lake. Sasa, katika kuzichunguza kanda, ninawatakeni mzichunguze hizo kwa makini sana papo hapo, tamshi hilo. Unaona?

Sasa, ninaanzia kwenye Mwanzo.

73 Niko kwenye Ufunuo sasa, nikileta hili pamoja, ya kwamba hili ni Neno la Mungu. Ufunuo unasema, ya kwamba, "Kila atakayeondoa Kwake ama kuongeza Kwake, huyo ataondolewa, sehemu yake, kutoka kwenye Kitabu cha Uzima." Nitalifikia hilo Andiko, nilinukuu, baada ya kitambo kidogo. Ufunuo, mlango wa mwisho.

Huo ni mlango wa kwanza, unaonyesha sasa. Ati nini?

74 Neno ni nini? Sasa, ni la Milele. Halipaswi kuchezewa, kuongezewa, wala kuondolewa. Mnaona? Halipaswi kuchezewa. Mungu hushughulikia hilo. Halipaswi kuongezewa, chochote Kwake. Hakuna kitu kinachoweza kuondolewa Kwake, kwa sababu ni la Milele. Mnaona?

75 Sasa, sasa kuwekea msingi, kuwaonyesha ya kwamba yale ninayojaribu kusema ni kati ya hivi, Mwanzo hadi Ufunuo, Halitachanganyikana na kitu kingine chochote. Sasa, hapa ndipo tutakapotofautiana, kutoka hapa hadi saa kumi na moja alasiri ya leo. Mnaona? Hapa ndipo tutakapotofautiana. Ni wangapi watakaokubali ya kwamba *Hiki* ndicho Kitabu cha Hukumu cha Mungu, kwamba tutahukumiwa kulingana na Neno la Mungu? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] "Hakitaongezewa, wala kuondolewa." Basi kwa nini hili limefanywa? Sasa tunalifikia. Kwa nini hili limefanywa kwa njia fidhuli hivyo? Sasa tutalipata, kati ya Mwanzo na Ufunuo, moja kwa moja kufikia wakati wetu, huko chini kwenye nyakati zingine.

76 Sasa, hebu nifanye hilo dhahiri sana, kwa ajili ya kanda. Sasa, baada ya kuwaambia ni kwa nini ninaamini Neno, na yale Mungu aliyosema kulihusu, na jinsi ambavyo halipaswi kuondolewa ama kuongezewa, kuondolewa, ninataka kuingia kwenye kilindi chake, kwenye muktadha wa kifungu hiki kirefu ambacho nimetoa, na kuwaelezea, na kuwaonyesha yaliyotukia. Ndipo mnaweza kuona sababu ya mimi kuamini yale ninayoamini. Mnaona? Sasa, haliwezi kuchanganywa, wala halitachanganyishwa na chochote kile. Halitachanganyana.

77 Leo ni siku kuu ya kuchanganya mbegu za wanyama, mahindi, ngano, kutengeneza bidhaa iliyo bora zaidi, bali haifai kitu. Imeoza. Hamna uhai ndani yake. Inakufa; haiwezi kujizaa yenyewe. Imekufa.

Kwa sababu, kila kitu tulicho nacho duniani siku hizi, katika hali yake ya asili, ni Neno la Mungu lililonenwa.

78 Hiyo ndiyo sababu kwamba nyumbu, mnyama haramu ambaye ni chotara, hawezi kujizaa tena. Mungu aliumba farasi, na akamwumba nyumbu. . . ama akamwumba punda. Ukiwazalisha hao wawili pamoja, una nyumbu. Ni chotara, kwa hiyo hawezi kujizaa tena.

Tutaufikia uzao wa nyoka, baada ya kitambo kidogo, sasa. Hawezi kujizaa tena.

Sasa somo langu ni lipi? *Neno Lililonenwa Ndilo Mbegu Ya Asili.* Sasa nataka kuthibitisha hilo.

79 Hebu tufungue sasa Mathayo 24:35, kwa muda kidogo tu. Na—na tunapoyachunguza Maandiko haya, kwa kitambo kidogo, nami nitaona muda tulio nao. Nami ninataka kusoma hapa Neno ambalo Yesu alisema. Mathayo 24, na kifungu cha 35. Mlango wa 24, kifungu cha 35, inaonyesha jinsi Neno hili lilivyo la Milele, yale tumekuwa tukizungumzia. "Amin. . . " 34.

> *Amin, nawaambia, Kizazi hiki hakitapita, hata hayo yote yatakapotimia.*
>
> Mbingu *na nchi zitapita, lakini maneno yangu hayatapita kamwe.*

80 Sasa, waweza kuchanganya chochote na hayo basi? Sasa, katika Kitabu cha Ufunuo, mlango wa 22 na kifungu cha 19, ningetaka kusoma hili. Ufunuo, mlango wa 22 na kifungu cha 19, tuone hili linasema nini. Hebu tuanzie kwenye kifungu cha 18. "Kwa maana namshuhudia kila mtu. . . " Sasa kumbukeni, kutoka Mwanzo, ambapo Yeye alinena Neno. Mnaona?

> *Kwa maana ninamshuhudia kila mtu* (yaani kasisi, papa, askofu, mzee wa jimbo, ama yeyote yule) *yeye ayasikiaye maneno ya unabii wa kitabu hiki, Mtu ye yote akiyaongeza, Mungu atamwongezea hayo mapigo yaliyoandikwa katika kitabu hiki:*

81 Vipi kuhusu mafundisho yenu ya sharti? Vipi kuhusu kanuni zenu za imani zisizo za kimaandiko mnazosikiliza? Kati ya madhehebu yote, hakuna hata moja lililoachiliwa.

> . . .*mtu akiondoa katika maneno* (akisema si yale yale, mwajua, mnaona) . . .ondoa, *katika maneno ya unabii wa kitabu hiki, Mungu atamwondolea sehemu yake katika kitabu cha uzima, na kutoka katika mji ule mtakatifu, na katika mambo yaliyoandikwa katika kitabu hiki.*

82 Ingawa yeye ni mhubiri, mnaona, ingawa yeye ni mfuasi wa kanisa, maishani mwake mwote, ingawa yeye ni askofu, ama papa; yeyote atakayeondoa Neno moja la *Hiki*, Neno moja tu!

83 Mnatambua ilikuwa ni Neno moja ambalo Hawa alitilia shaka, ambalo lilisababisha matatizo yote? Neno moja la Mungu lililonenwa, Hawa alitilia shaka kuwa ni Kweli, nalo likasababisha kila maradhi, kila ugonjwa, kila mtoto anayeteseka. Likasababisha kila hospitali kujengwa, kila upasuaji uliowahi kufanywa, kila kifo kilichowahi kufiwa, kwa mtu mmoja kuamini moja...kutokuamini Neno moja. Haya basi. Hawa alijaribu kufanya nini? Kulichanganyisha, kulichanganya na kitu fulani.

84 Huna budi kulichukua jinsi Mungu alivyolinena. Halitachanganyikana na chochote. La, bwana. Yesu wakati mmoja alisema, "Ukiwa na imani kama mbegu ya haradali." Ninaambiwa ya kwamba mbegu ya haradali haitachanganyana na nyingine. Huwezi kuichanganya na chochote. Unaweza kuchanganya punje zingine, bali huwezi kuchanganya mbegu ya haradali, unaona, maana haitachanganyana. Laiti ungalikuwa na imani ya namna hiyo!

85 Hilo ni moja, kuchukua Neno moja la Mungu, hapo ndipo wainjilisti wengi sana wanapopata kichaa. Tutalifikia baadaye. Jinsi wanavyosema, "Loo, tunaamini *hili*." Nao watachukua hilo, nao wanaamini Neno hilo moja, na wanaweza kulifanya hilo litende kazi. Lakini vipi kuhusu hilo lingine lililo karibu nalo?

86 "Heri yeye afanyaye maagizo Yake yote, amri." Mnaona? "Yeye atakuwa na haki ya kuingia katika Mti wa Uzima. Kwa maana huko nje wako wachawi, mbwa, na wazinzi, na kadhalika."

87 Sasa, nina darasa la mchanganyiko, lakini nina muktadha mwingi hapa wazi wazi kwelikweli. Kwa hiyo ninawatakeni ninyi akina dada mfahamu, mnaona, hakikisheni mnaelewa.

88 Sasa, hiyo ndiyo sababu tunaliamini. Nalo ni Neno la Mungu. Kwa hiyo, Neno la Mungu lililonenwa ni la asili. Na kila kitu ambacho Mungu aliumba, alichonena kikawepo, ni cha asili.

Nawe unaweza kuchanganya baadhi ya viumbe Vyake, tena.

89 Hiyo ndiyo sababu Hawa angeweza kufanya yale aliyofanya, kwa uzao wake mwenyewe, kwa sababu hakuwa katika uumbaji asili. Yeye ni zaotuka la mwanamume, hakuwa katika uumbaji wa Mungu. Mungu aliumba kitu hicho chote, kisha akachukua sehemu ya uumbaji Wake na kufanya msaidizi.

Hiyo ndiyo sababu unaweza kuchanganya punda na farasi, lakini hatadumu. Ni mauti.

Lakini ya asili ina uhai. Inarudi tena. Natumaini mnaweza kuliona sasa. Ya asili ina uhai.

90 Kwa hiyo hiyo ndiyo sababu nafikiri ya kwamba madhehebu, na mashirika, hufa. Historia inathibitisha hayo, kila moja, limekufa. Kamwe hayakuinuka tena; kamwe hayatainuka. Hayawezi kujizaa tena; hayana kitu cha kujizalishia. Ni tasa. Hiyo ndiyo sababu watoto wa Hawa hufa.

91 Ninachukua muda wangu, ili kwamba, kanda, niwape watu wakati wa kutafakari. Sitaki kuwa na haraka yoyote. Ninataka tu kuchukua muda wangu. Sijui kitakachotukia tangu hapa na kuendelea, lakini na—nataka hili liwaendee watu. Kwamba, ingawa siku moja Mungu ataniondoa ulimwenguni, kama sitaishi kuona Kuja Kwake, Ujumbe ungali utaendelea kuishi. Kweli. Dumuni na Neno.

92 Sasa, kumbukeni, kila Neno la Mungu lililonenwa ndilo Mbegu ya asili. Mungu alipanda kila kitu duniani, kwa Neno Lake. Na mradi tu unadumu na ile mbegu ya asili, itajizaa moja kwa moja na—na kujizaa tena. Ukiichotarisha, inakufa.

93 Naye Hawa, yule mwanamke, alikuwa ndiye kitu chotara cha kwanza kilichopata kuwako. Sasa, natumaini hamtazima kanda mpaka tutakaposhuka na kuthibitisha hilo baada ya kitambo kidogo, mnaona, kuwaonyesha ni kwa nini hasa. Alikuwa mchanganya mbegu, bibi-arusi. Angalieni, kupitia hapo yakaja mauti, kwa kujaribu kulichukua Neno la Mungu na kuchanganya hekima fulani Nalo. Mnaona? Hupaswi kufanya hivyo.

94 Na kama unaamini ni . . . una hekima ya kulielezea. Sema tu, "Mungu alisema jambo hilo, na hilo latosha. Pia Mungu alisema hivyo, na ni hayo tu." Kama huwezi kulielezea, achana nalo. Lakini sema tu, "Ndivyo lilivyo, maana Mungu alisema hivyo." Unaona? Jambo ndilo hilo. Mungu alilisema.

95 Sasa angalieni. Sasa, halitachanganyikana. Halipaswi kuchezewa. Mungu atamwadhibu yule anayefanya jambo hilo. Wala halitachanganywa na kitu kingine chochote. Ni Neno la Mungu, pekee. Mungu hahitaji neno lako pamoja na Lake. Hatupaswi kunena neno letu wenyewe. Tunapaswa kulihubiri Neno Lake, Neno la Mungu.

96 Sasa, basi, uhai wa kweli unaweza tu kuja ama kujizaa wenyewe kwa kuzaa kwake kwa asili. Mnaona, uhai! Sasa ke- . . . Sasa ichunguzeni hiyo, sasa, mnapozichunguza kanda. Na ichunguzeni sasa. Uhai, u-h-a-i, unaweza tu kuzalishwa upya kwa kuzaa kwake kwa asili, jinsi ulivyoanza hapo mwanzo, kisha unajizaa wenyewe. Mnaona? Haujizai, ni chotara, unafifia. Baadhi yake ulififia, kizazi cha kwanza. Mnaona? Umekwisha papo hapo. Hivi karibuni utajikuta umerudi. Hauwezi kuleta uhai sahihi, kwa sababu ni chotara.

97 Mwanzo 1:11, Biblia ilisema. Yes- . . . Mungu alisema, "Kila mbegu na izae kwa jinsi yake." Sasa, Mungu aliposema jambo hilo, hilo latosha. Daima imetatuliwa. "Kila mbegu na izae kwa

jinsi yake." Kuichanganya, huleta mazao bora sana. Ni zao bora la nini?

Sikilizeni sasa. Hebu tulifuatilie. Kulichanganya... Ninajaribu kushikilia. Hayo masomo kama hayo, ningeweza kuhubiri juu yake. Lakini nitajaribu kujizuia kufanya hivyo.

98 Kulichanganya, kutaleta zao bora sana, kama ilivyothibitika. Lakini ni zao la aina gani? Zao la uongo, mauti. Zalisha mahindi yako kwa kuchanganya mbegu, yatazaa mazao makubwa, mazao bora zaidi, yanayoonekana mazuri zaidi, bali yamekufa. Yapande tena; hayawezi kujizaa tena. yamekwisha. Yamekwisha.

99 Kama vile Hawa, mnaona, yeye alizaa zao chotara. Tuangalie siku hizi, nawe unaweza kuangalia kote na kuona hiyo ni kweli. Uh-huh. Unaona? Hakika alifanya hivyo. Halikuwa ni kusudi la Mungu. La, bwana. Inanibidi tu kujizuia, kwa ajili ya jambo ninalowazia sasa hivi. Unaona?

100 Kulichanganya, huzaa zao chotara. Nalo zao chotara ni zao lililokufa, tukinena kuhusu kuzalisha tena. Halitajizaa tena. Haliwezi, maana Mungu alisema hivyo. Haina budi kuzaa kwa jinsi yake, nawe umeichanganya. Sasa mnaweza kuona kanisa papo hapo, ambapo tuta—tutaishia. Lilifia pale, kwa maana haliwezi kuzaa kwa jinsi yake. Kwa nini? Limechanganyikana. Huwezi kufanya lolote nalo. Limekufa. Limekwisha. Vema.

101 Hiyo ndiyo sababu kila kizazi kina uamsho wake chenyewe, kupewa nafasi kwenye Neno, kusudi Mungu mwenyezi kwenye ile Hukumu...Kundi la John Wesley litainuka, na hawa Wamethodisti waliooshwa kwa wanga wa siku hizi watawajibika. Luther atainuka. Wakatoliki watainuka (kutoka huko nyuma ya Ireneo, Martin, Polycarp, na hao) na itawabidi kusimama kwenye ile Hukumu, kwa kulichanganya Neno la Mungu na mafundisho ya sharti. Kundi hili la Walutheri lililoufuata uamsho wa Luther litawajibika kwa jambo lile lile. Kundi la Baptisti lililofukuzwa lililofuata uamsho wa John Smith litafanya vile vile. Alexander Campbell atafanya vile vile.

102 Nao Wapentekoste watafanya vile vile. Uamsho ule wa asili, wakati Roho Mtakatifu aliposhuka, akawaita watu fulani watoke, naye Mungu akijaribu kuwaletea Neno Lake. Nao wakaliundia madhehebu, wakaketi hapa, na kujiundia madhehebu, na wakafa papo hapo.

103 Mnasema, "Lakini angalia kile wanachofanya." Tutafikia jambo hilo, baadaye kidogo, leo. Mnaona? Tunashuka moja kwa moja kwenye ninii yote...Ninaweka tu Mbegu ndani sasa. Ndipo tutawaonyesha, baada ya kitambo kidogo, kilichotukia. Uh-huh.

104 Sasa, hiyo ndiyo sababu kila uamsho una kuamsha kwake...Kila kizazi kina uamsho wake. Mungu hujiinulia mtu, akamweka pamoja na Neno Lake, na kumtuma na ujumbe wa

wakati huo. Na mara mtu huyo anapoondolewa jukwaani, mtu mwingine anaushika na kuuchotarisha. Yote inarudi kwenye ukamilifu, kila kitu, huenda . . .

Ningeweza kusimama hapa kwa dakika moja. Hatuna haraka. Mnaona?

105 Turudi nyuma. Hivyo ndivyo ilivyoanza hasa, huko nyuma kabisa, katika Mwanzo. Mungu aliweka zao Lake la jamii ya binadamu, naye Hawa akalichotarisha. Mnaona kilichotukia? Kwa hiyo kuna hukumu kwa Hawa.

106 Luther akaondoka. Wengine wote! Kristo akaondoka. Mitume wakaondoka. Manabii wakaondoka. Hivi Yesu hakusema, "Ni nani kati yenu, ambaye baba zenu hawajawatesa manabii waliotumwa na Mungu?" Hivi Yeye hakufundisha ya kwamba mfalme mmoja wakati mmoja alimtuma mtumishi wake, kisha akamtuma mtumishi mwingine, na kumtuma mtumishi mwingine, na kadhalika, ndipo hatimaye akamtuma mwanawe? Mnaona?

107 Kila kizazi kikipokea, maana ni marudio ya moja kwa moja kwenye Ha-. . . Ha-. . . Adamu na Hawa, tena, lile zao la kwanza, bustani ya Edeni. Nusu yao walipotea; mwanamwali mwenye busara, mwanamwali aliyelala. Nusu yao, mmoja alilitimiza Neno, huyo mwingine akalichotarisha; moja kwa moja huku na huko, upesi tu iwezavyo kwenda, moja kwa moja namna hiyo. Imekuwa moja kwa moja kote katika nyakati. Tutalithibitisha kwa Neno la Mungu na kwa historia hapa. Hiyo ni kweli. Kuchanganya mbegu!

108 Kuchanganya mbegu kwanza kulianza huko Edeni, kulianza katika Mwanzo. Ni mwanzo, hapo ndipo. Na kunaishia hapa katika Ufunuo, kwenye kule Kuja kwa pili kwa Kristo.

109 Sasa kumbukeni, kwa usahihi. Hiyo ndiyo sababu kila kizazi kina uamsho wake chenyewe, kinapata nafasi kwenye Neno. Kisha wanalichanganya. Badala ya kuendelea, wanaenda mahali pengine.

110 Kazi yangu, ambayo ninaamini ya kwamba Mungu ameniitia . . . Si—sina budi kusema mambo ya kibinafsi leo, kwa sababu hivyo ndivyo nilivyowaambia nitafanya, mnaona, na kuuambia ulimwengu. Kazi yangu, ninaamini, duniani, ni (gani?) ni kulitangulia Neno lijalo, mnaona, Neno lijalo ambalo ni Kristo. Naye Kristo, ndani Yake, ana ule Utawala wa Miaka Elfu, na ana kila kitu papo hapo, kwa sababu Yeye ni Neno. Mnaona? Vema.

111 Yesu alisema, katika Yohana 3:5. Sasa, mkitaka kuandika hilo, Yohana 3:5. Sote tunajua jambo hilo, ama labda nitafungua. Labda mtu fulani kwenye kanda huenda asingeweza kufungua kwenye wakati huo. Nami nitasoma hapa katika Yohana Mtakatifu, mlango wa 3 na kifungu cha 5. Nasi tutaona yale Yesu aliyosema. Huenda tukaanza kidogo tu kabla ya hapo, cha 3.

*Yesu akajibu, akamwambia, Amin, amin, nakuambia, Mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi kuuona ufalme wa Mungu.*

*Nikodemo akamwambia, Awezaje mtu kuzaliwa, akiwa mzee? aweza kuingia tumboni mwa mamaye mara ya pili na kuzaliwa?*

*Yesu akajibu, Amin, . . . nakwambia . . . nakwambia, Mtu asipozaliwa kwa maji na kwa . . . Roho, hawezi kuingia katika ufalme wa Mungu.*

112 Hiyo ni Mbegu? Kila Neno la Mungu lililonenwa ni Mbegu. Hiyo ni kweli. Nitathibitisha hilo katika dakika moja tu, ambapo Yesu alisema hivyo. Kila Neno la Mungu lililonenwa ni Mbegu.

113 Halafu, "Mtu asipozaliwa mara ya pili." Kwa nini ni lazima azaliwe mara ya pili? Amekufa, kwa mwili aliomo. Yeye ni chotara. Hana budi kuzaliwa mara ya pili. Kwa nini? Yeye alizaliwa katika dhambi, kutoka katika dhambi ya Hawa, akaumbika katika uovu; akaja ulimwenguni, akisema uongo. Yeye ni mwongo, kwanza kabisa. Haidhuru jinsi alivyo mwerevu, mwenye elimu, chochote zaidi alicho, yeye ni mwongo. Biblia inasema ndivyo alivyo. Jinsi wazazi wake walivyokuwa watakatifu, ama chochote kulihusu; yeye ni mwongo, kwanza kabisa. Na njia pekee anayoweza kusema Kweli, ni kusema yaliyo Kweli, kwa midomo yake mwenyewe. Hivyo tu ndivyo Kweli inavyoweza kuja. Chochote kinyume na Neno hilo, yeye ni mwongo, bado. Hilo ni wazi wazi sana, bali hivyo ndivyo Mungu alivyosema. Uh-huh. "Neno la kila mtu na liwe uongo, na Langu liwe kweli." Mnaona? Chochote kinachotoka kinywani mwake, kinyume, kulikana Neno hili, ama kuliweka katika jamii nyingine ama kizazi kingine, ama chochote kile, yeye ni mwongo. Hiyo ni kweli kabisa. Hana budi kuzaliwa mara ya pili, ndipo anaona kila Neno. Njia pekee anayoweza kuzaliwa mara ya pili, ni ule Uzima wa Mungu ndani yake, kuuzaa tena huo Uhai.

114 Mbegu haina budi kupata maji, ipate kukua. Sasa, hebu uitie mbegu ardhini. Kama hakuna unyevu ardhini, ni mavumbi, basi haitakulia mavumbini. Haiwezi. Haina budi kuwa na asilimia fulani ya unyevu, la sivyo haitakua. Hiyo ni kweli? "Andiko huua. Roho huleta Uzima." Mnaona? Sasa, lazima liwe na unyevu, lipate kukua.

115 Neno Lake ni Mbegu. Sasa kuthibitisha hilo, hebu na tufungue Luka mlango wa 8, kifungu cha 11, tuone kama hili ni kweli ama si kweli, kama—kama Biblia inasema Neno Lake ni Mbegu. Luka, mlango wa 11 ama . . . Mlango wa 8, hasa, na kifungu cha 11, nasi tutaona yale Mungu aliyosema juu yake; Mlango wa 8, kifungu cha 11. Sasa Yeye anaendelea na kuanza kuwaambia. Kuna mambo mengi ya kusema juu yake. Hebu tuanzie kwenye cha 4, tusome tu.

*Hata mkutano mkubwa ulipokutanika, na wale waliotoka kila mji wakamjia, alisema kwa*. . .mifano:

*Mpanzi alitoka kwenda kupanda mbegu zake*. . . *kupanda mbegu za—zake: naye alipokuwa akipanda, nyingine zikaanguka kando ya njia*; *zikakanyagwa, ndege wa angani wakazila.*

*Nyingine zikaanguka penye*. . .*mwamba; na*. . . *zilipoanza kumea, zikakauka, kwa kukosa unyevu.*

116 "Unyevu." Wabaptisti, Wapresbiteri, Walutheri, bila ya Maji. Na wakati anapoongoka kwa mara ya kwanza, anamtazama Kristo moja kwa moja; anaamini. Na muda si muda mwajua, dhehebu hilo linamfungia mahali fulani, ndipo unyevu wa Roho umemtoka. Anakuwa wa kimadhehebu, naye amekufa. Si Baptisti tu, bali Pentekoste. Hamwamini hilo, najua wengi wenu hamwamini. Lakini ngojeni tu kidogo, tutaona mahali Biblia inapolisema sasa, ama la. Vema. "Kwa kukosa unyevu," neno la mwisho katika kifungu cha 6 cha mlango wa 8. "Ukosefu wa unyevu."

*Nyingine zikaanguka kati ya miiba; na*. . .*ikamea pamoja nazo, ikazisonga.*

117 Mnaona? Hiyo ilikuwa ni nini? Yeye anaendelea na kusema ya kwamba nyingine, mara zilipofikia kuwa. . . Sitacheza hata kidogo leo, juu ya chochote. Mnaona? Jinsi tu ninavyowazia hawa Wafanyabiashara Wakristo, na hao wengine, wa madhehebu haya ya Kipentekoste, na watu hawa wanaojenga vitu hivi vikubwa vyote vya mamilioni ya dola, utajiri wa ulimwengu umesonga utukufu na Roho wa Mungu. Yanakufa, kwa sababu yamesongwa. Ulimwengu, mahangaiko ya ulimwengu yamewasonga yakawamaliza.

118 Wanawake wanataka kuwa wachangamfu, na kukata nywele zao na kukata nywele kichwa-maji, kuvaa kaptura, na kuonekana kama walimwengu wengine. Mhubiri anasimama mimbarani, pamoja na. . .wanafanyia mazoezi "amina" zao, na kuogopa Neno la Mungu, kwa ajili ya riziki. Kama hawawezi kuendesha Kadilaki, basi hata hawahesabiwi kuwa ni wa kiroho tena. Hiyo ni kweli. Kama hawawezi kuvaa nguo zilizo bora sana, na kufanya mengine yote, wana—wanahesabiwa, "Wamerudi nyuma. Wao si *akina nanii.*"

119 Mzee mmoja kule nyuma, mzee Ndugu Kidd, aliniambia asubuhi ya leo, hawamtaki tena, kwa sababu yeye ni mzee na anadumu moja kwa moja na Neno. Kuna shida gani? Wamekosa unyevu. Vema. "Zikaanguka juu ya. . ."

Nyingine *zikaanguka penye udongo mzuri, zikamea, zikazaa tunda*. . .

. . .*alipokwisha kusema mambo haya, alipaza sauti, Aliye* na sikio, *na asikie.*

120 Loo, ni mfano wa jinsi gani! Jinsi ningependa kuhubiri somo juu ya hilo sasa, mahubiri. "Alipokwisha kusema mambo haya," mlango wa 8, ama kifungu cha 8 na mlango wa 8.

> . . .nyingine *zikaanguka penye udongo mzuri, zikamea, zikazaa moja mia. Basi alipokwisha kusema mambo haya, akapaza sauti,* . . .

Akapiga mayowe, labda kitu kama hiki, wakati Yeye aliposema, "Itazaa moja mia":

> . . .*Aliye* na sikio . . .*na asikie.*

Uh-huh. Kwa maneno mengine, "Ikiwa sikio lako lina uwiano na Mungu, na asikie." Mnaona?

> . . .*wanafunzi wake wakamwuliza, Maana yake nini mfano huu?*
>
> *Akasema, Ninyi mmepewa kuzijua siri za ufalme* . . .

"Zile siri." Mnaona kile anachozungumzia hapa? Sasa angalieni. Siri za Ufalme ni nini? Angalieni kwa dakika moja tu.

> . . .*siri za ufalme wa Mungu: bali wengine kwa mifano; ili wakitazama* waone . . .*wasione, na wakisikia wasielewe.*

Mnaona? Lakini Neno la Mungu linashuka moja kwa moja kwenye Hukumu, kuwahukumu, maana kweli waliliona. Lilikuwepo.

> *Basi huo mfano maana yake ni hii: Mbegu ni neno la Mungu.*

121 Mbegu ya Uzima ni nini? Neno la Mungu. Kwa hiyo, ili kupata Uzima, huwezi kupitia kanuni ya imani. Huwezi kupitia madhehebu. Huna budi kurudi kwenye Neno, sasa, Mbegu ya Uzima. Vema.

122 Neno Lake ni Mbegu Yake, na Roho Yake ni Maji. Sasa turudi moja kwa moja kwenye Yohana 3:14, hapo mnalipata tena, mnaona. Mnaona? Roho huinua . . .ndiyo Maji. Sasa, angalieni, Yohana 3:14. Tunafahamu maana yake. Mkitaka kulisoma.

> . . .*kama Musa alivyomwinua yule nyoka wa shaba nyikani,* . . .*vivyo hivyo Mwana wa Adamu hana budi kuinuliwa:*

123 Mnaona? Sasa, kama Musa alimwinua yule nyoka wa shaba, kwa sababu ile ile aliyoinuliwa Kristo. Sasa ni kitu gani? Musa alimwinua yule nyoka wa shaba ili kwamba watu waliokuwa wakiangamia wapate maji kwa ajili ya uhai. Tazama, Yesu . . . Ee Mungu! Yesu ni Neno la Mungu.

Sasa tutalishindilia hilo, alasiri ya leo, mnaona, kulithibitisha.

124 Yesu ni Neno la Mungu. Naye alipasuliwa, Uzima huo. Uhai umo ndani ya Mbegu. Ambapo, Uhai huu, ambao ni Roho, Maji yanayotiririka; Roho juu ya Mbegu ya Mungu, atazaa Uhai wa Mbegu. Na kama akizaa kitu kingine, kuna aina nyingine ya mbegu hapo basi. Amina. Mnaelewa? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Kama Roho wa Mungu akija kuitia hiyo Mbegu maji, kama hiyo inayotiwa maji ni Mbegu, itazaa Uhai wa hiyo Mbegu. Hiyo ni dhahiri? ["Amina."] Itatoa Uhai wa hiyo Mbegu, kwa kuwa ilitolewa kwa kusudi hilo.

125 Ninaamini Biblia ni—ni Neno, Kweli yote. Naye Yesu ni Neno lililodhihirishwa. Yeye na Neno Lake ni Mmoja na ni kitu kimoja. Yeye alikuwa nini? Sasa angalieni. Yeye alikuwa yule Mzao.

126 Sina budi kushikilia kitu fulani, kusudi, nikiingize hapa jioni ya leo, mnaona. Ni vigumu.

127 Yeye alikuwa yule Mzao ambaye Hawa alipaswa kumzaa. Mnalipata? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Yeye alikuwa ndiye yule Mzao ambaye Hawa alininii. . .kuzaa. Lakini aliuchanganya, kwa kutokuliamini Neno la Mungu.

128 Kwa hiyo, Yeye alikuwa ndiye huyo Mzao. Na njia pekee ambayo Uhai ungeweza kutokea, katika kule kuzaliwa tena kwa Uhai, ilibidi Uhai uje kupitia Mbegu hiyo. Nayo Mbegu hiyo ilibidi ife, kusudi ipate kuueneza huo Uhai. Loo! Hivi hamwezi kuliona? Hiyo ndiyo sababu Maji yalitolewa, kuinywesha hiyo Mbegu. Roho Mtakatifu, aliyekuwa katika bustani ya Edeni, alikuwa aitie maji hiyo Mbegu.

129 Mwanadamu hakuumbwa apate kufa; aliumbwa apate kuishi. Lakini kuchanganya mbegu kulileta uhai, ama, mauti pale, hasa. Alilichanganya Hilo. Sasa ati mnakana uzao wa nyoka? Basi nitawaulizeni ni kwa nini ninyi. . .Ibada hizi za mazishi zinahusu nini? Yeye alikuwa chotara. Kila mmoja wetu ni chotara kutoka kwa asili. Hiyo ndiyo sababu daima mnakufa.

130 Lakini, Ee Mungu, kuna Seli zazi ya Uhai inayotokana na ile Mbegu halisi ambayo Mungu alithibitisha ilikuwa ni Mbegu Yake; Alimfufua tena. Mnaona? Kwamba, kupitia Uhai huo unaopitia juu ya Mzao wa asili, kama uliopewa Hawa, juu ya Kanisa Lake halisi, analeta Uzima tena, kwa Kuzaliwa, kupitia tumbo la uzazi la Bibi-arusi Wake. Mnaona? Loo, limekolea na ni tukufu! Ninalipa wakati kidogo kutafakari, ili liweze kuzama ndani. Yeye ndiye Uzao huo. Yeye ndiye Mzao yule aliyezaliwa na Neno la Mungu. "Na iwe kwangu kulingana na Neno Lako." Huyo hapo yule Mzao, mnaona, akilichukua Neno. Mnaona?

131 Sasa, Yesu ni Neno lililodhihirishwa. Yeye na Neno ni Mmoja na yeye yule, na hiyo ndiyo sababu lilidhihirishwa sana ndani Yake kikamilifu sana. Hiyo ndiyo sababu Mungu alijidhihirisha Mwenyewe kikamilifu sana katika Yesu, kwa sababu Yeye alikuwa ni Neno-Mbegu, Neno-Seli Zazi, Lenyewe. Ile Seli Zazi iliyo ndani ya Mbegu, hiyo ndiyo Uhai uliomo ndani ya Mbegu.

Mnalipata? Mnaona? Ilikuwa ni. . . Yeye alikuwa ndiye Neno-Seli Zazi la Mungu. Hyo Seli Zazi ni Roho; Seli Zazi ni Maji.

132 Na ilibidi Yesu apasuliwe pale, kusudi Mbegu hiyo iutoe Uhai Wake, ipate kumwagilia maji mbegu zingine zilizokuwa zikija. Loo! Mnaona? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Hata Yeye alisema, "Kondoo wengine mimi. . . ambao hata si wa zizi hili, ninao. Wataona jambo Hilo. Watalipata hilo Neno na kudumu moja kwa moja Nalo. Nami ninamtuma Roho kulitia maji, nalo litazaa sawasawa kabisa." Litafanya miujiza. Litazaa Nguvu za Mungu. Litazaa. Wala halitakana chochote, kwa sababu ni uzao wa ukoo mmoja na yule Mzao.

133 Haliwezi kusema, "Bw. Gugu, njoo ukaishi pamoja nami." La. La, bwana. La, la. Haitafanya hivyo. La, hasha. Kamwe halitachanganyikana. Huwezi kuchanganya mauti na Uzima. Huwezi kuwa umekufa na ukawa hai wakati uo huo. Uh-huh. Unaona?

134 Kwa hiyo mnaona ninalomaanisha? Ni ile Seli Zazi hai inayotokana na yule Mzao. Ndivyo alivyo. Yeye ni Neno la Mungu lililodhihirishwa kikamilifu. Hiyo ndiyo sababu ndani Yake mlikuwa. . . Nini? Hicho kilikuwa ndicho kitu ambacho. . . Yeye kwa usahihi ndiye yule Mwana kutoka kwa Adamu wa kwanza, alikuwa ndiye Mwana aliyeahidiwa kupitia kwa Adamu, apate kuiendeleza jamii ya binadamu. Naye Hawa akaichanganya, kwa yule nyoka, na kuzaa kizazi cha watoto haramu, waliozaliwa wapate kufa, bila Uzima. Ndipo Yesu akaja, naye alikuwa ndiye huyo Mzao. Alithibitisha jambo hilo. Kila kitu ambacho Adamu alipoteza, Yesu alikuwa hicho. Mnaliona? Yeye ndiye wa kweli. Hawa hatimaye angemzaa Mtoto huyo. Lakini aliichanganya, akamwingiza yule nyoka, akisikiliza apate hekima, ufahamu, maarifa.

135 Sasa ngojeni mpaka tutakapoingilia Bibi-arusi pamoja na hilo. Mnaona? Hilo ndilo. . . Hiyo ndiyo sababu ninaamini yale ninayoamini. Halina budi kurudi kwenye Neno hili.

136 Hiyo ndiyo sababu ninasema, kama mtu fulani anataka ku—kujadiliana nami, kuzungumza nami kuhusu Neno hili, njoo. Hiyo ni kweli. Nimetoa hiyo, wakati wowote. Kama unafikiri ya kwamba Jina la "Yesu Kristo" si njia sahihi ya kubatizia, njoo uzungumze nami kulihusu. Uh-huh. Kama huamini kuna kitu kama uzao wa nyoka, njoo unione, hebu na tulichukue tu Neno. Kama huamini ya kwamba wanawake wanapaswa kuwa na nywele ndefu, na hizo ndizo kifuniko chake, njoo uzungumze nami juu yake, kwa Neno. Kama huamini ya kwamba mwisho wa wakati umekaribia, na mambo haya ninayozungumzia ndivyo yalivyo, njoo uzungumze nami kuyahusu. Unaona? Njoo pamoja nami. Ndugu, Mzao, njoo tu. Vema.

137 Huwezi kuwa Mzao na usikubaliane na Neno, kwa sababu Neno ndilo Mbegu. Na kama wewe ni Neno, unawezaje

kukosa kukubaliana Nalo? Ungekuwa ukipingana na nafsi yako. Ungekuwa ukiangamiza kusudi lako mwenyewe.

138 Kama vile mtu fulani alivyosema, "Ni nini ambacho ungeninii . . . Kwa nini unatembea na watu kama hao?" Vema, kama sikufanya hivyo, ningekuwa nikiangamiza kusudi lenyewe nililotumiwa hapa. Hapana budi kuwe na Nuru.

139 Sasa tunapozidi kushuka chini, tutaviingiza vitu hivyo na kuonyesha jinsi tu wanavyojiweka katika utaratibu, sawasawa kabisa na Neno. Sasa . . . Naam, bwana. Yeye ni . . .

140 Hiyo ndiyo sababu Mungu angeweza kufanya kazi kupitia Kwake. Naye alisema nini alipokuwa hapa duniani? "Sifanyi lolote mpaka Baba anionyeshe." Kikamilifu.

141 Na lolote alilofanya, daima lilithibitishwa na Maandiko. Yeye alisema, "Yachunguzeni Maandiko, kwa kuwa Hayo Ndiyo yanayonishuhudia Mimi. Na kama sifanyi mambo ambayo Hayo yalisema waliyafanya, basi mimi si yule Mzao wa asili. Lakini kama nikifanya jambo hilo, basi kwa nini msiniamini Mimi?" Hiyo ni kweli. "Kama hata hamwezi kuniamini Mimi, jinsi ninavyosimama, basi aminini Neno nisemalo, aminini kazi nizifanyazo, maana Uzao Wangu unaweza tu kuzaa kile nilicho Mimi."

142 Gugu linaweza tu kuwa ni gugu. Ungeweza kulizalisha na chochote kile, bali lingali ni gugu. Hiyo ni kweli. Litalidhihirisha. Hiyo ndiyo sababu kwamba, wa namna mbili, ni mnafiki. Hiyo ni chotara. Mtu anayedai kuwa ni mtu wa Mungu, na kulikana Neno, yeye ni mnafiki. Nyumbu anayedai kuwa farasi, yeye si farasi. Alisema, "Mimi ni punda," wala si hata mmoja wao. Wewe ni mnafiki, mzao-haramu, hasa. Hiyo ni wazi wazi, lakini hivyo ndivyo ilivyo. Yeye hakukusudia kufanya hivyo. Mwanadamu alifanya hivyo kwa hekima yake. Hapo ndipo anapofikia. Hapo ndipo hekima yote ya mwanadamu inapoishia, kuzaliwa kiharamu. Vema.

143 Sasa, hiyo ndiyo sababu Yesu alidhihirishwa kikamilifu sana, Mungu alidhihirishwa kikamilifu sana katika Yesu, kwa sababu Yeye alikuwa ni Neno la Mungu. Alikuwa ni Neno la Mungu. Hiyo ndiyo sababu lisingeweza kuzaa chochote ila Mungu hasa. Na ikiwa Mungu yuko ndani yako, unaweza kuwa nini zaidi?

144 Hivi Yesu hakusema, juu ya manabii ambao Neno la Mungu liliwajilia . . . Neno la Mungu liliwajia akina nani? [Kusanyiko linasema, "Manabii."—Mh.] Manabii. Hivi Yesu hakuwaita "miungu"? ["Amina."] Kwa nini? Mungu alidhihirishwa ndani yao. Ilikuwa ni kitu gani? Neno lililonenwa likidhihirishwa. Mnaona? Jambo ndilo hilo. Kasema, "Unawezaje kukana, useme . . . Kama ungekuwa na hekima yoyote, ungeelewa." Yeye alisema, "Mimi . . . Mnawezaje kusema nyinyi . . . Tunawaita . . . Mungu Mwenyewe aliwaita 'miungu.'" Kisha kasema,

"Mnawezaje basi kusema mnawaamini, na kunikana Mimi, ninaposema Mimi ni Mwana wa Mungu?" Kwa nini hawakuona jambo hili wakati huo? Jambo lile lile leo. "Mimi ndimi ule Uzao uliokuwa uje, Uzao wa mwanamke."

145 "Nitakupa Uzao." Kwa nyoka, nyoka alikuwa tayari amemtia unajisi. Akasema, "Lakini Uzao wako, nitakaokupa, atakiponda kichwa chake." Atakirudisha kitu hicho tena. Amina. Laiti... Laiti kila mtu angeweza kuona jambo hilo. Mnaona? "Nimekuja kushinda, na kusahihisha kile Hawa alichofanya. Na njia pekee niwezayo kufanya hivyo ni kupitia kwa mwanamke aliyemwamini yule Mzao; ambapo, mwanamke hakuamini yule Mzao." Mwanamke mmoja aliliamini Neno; ambapo, mmoja hakuliamini.

146 "Mimi ndiye yule Mshindi. Mimi Ndimi niliyekuja kutoa Uzima, ili kupitia kifo Changu, kulipia adhabu ya yale aliyofanya. Kupitia Uzima Wangu, mtapewa, upate kutiririka juu yenu. Nanyi mtakuwa wana wa Mungu, na binti za Mungu, mnaona, maadamu huo Uzao uko mle ndani."

147 Mkiuchotarisha, basi hamna kitu ila mtoto haramu, wa kimadhehebu. Hivyo tu. Kitu chochote kinachokana Neno. Samahani, akina dada. Na—nawatakeni...Sina budi kusema tu jinsi linavyolisema *Hapa*. Mnaona? Na hivyo—hivyo ndivyo ilivyo.

148 Wana wote wa Mungu hawana budi kuwa sawa. Naam, bwana. Kuzaliwa kwa Neno na Roho, kunaturudisha kwenye Neno lililonenwa tena, kama katika Yohana 3. Mnaona? Kuzaliwa kwa Maji na kwa Roho, kunafanya nini? Basi kunakurudisha moja kwa moja tena mahali ambapo ulipaswa kuwa hapo mwanzoni. Mnaona? Hiyo ndiyo sababu ya kifo cha Kristo, kinaturudisha moja kwa moja tena kwa (wapi?) wana wa Mungu.

149 Kama Hawa angalimzaa Mtoto huyo...Hatimaye angefanya hivyo. Hivi Mungu hakumwambia, "Mkaongezeke mkaijaze dunia"?

150 Lakini ilimbidi atembee hapa, aigize sehemu ya kahaba. Vema, mnasema tu, "Hilo ni wazi wazi, Ndugu Branham." Lakini ngoja kidogo tu, tutaliingilia hilo baadaye kidogo. Mnaona? Mnaona? Mnasema, "Haiwezekani." Vema, tutaona tu mahali Neno linasema ndivyo ilivyo, au la. Mnaona? Basi, ni kweli. Wao si...Halijafichika. Kama limefichika, limefichika kwa wale waliopotea. Mnaona? Vema. Mnaona?

151 Sasa, sasa, hili linawarudisha moja kwa moja kwenye Neno lililonenwa, ndipo sisi ni Neno la Mungu lililodhihirishwa. Mnaona? Yesu alisema jambo lile lile. "Yeye aniaminiye Mimi, mambo...na kwamba mimi ni Nani, kile kilichonileta, na kusudi ninalofanya, kumrudisha mtu apate kuliamini Neno

la Mungu na asichukue chochote kingine pamoja Nalo, kazi nizifanyazo, yeye naye atazifanya." Haya basi.

Kwa nini hayafanywi leo? Ni machotara, watoto haramu, waliochanganyikana. Haninii. . . Ni nyumbu. Hajui anachoamini.

Nyumbu hajui baba yake ni nani, mama yake ni nani. Hajui. Yeye si ukoo safi. Hakuna chochote kwake. Yeye ni kiumbe haramu.

152 Hivyo ndivyo mtu yeyote, anayedai kumwamini Mungu wala haliamini Neno Lake, atakavyochukua kanuni za imani za kimadhehebu na kuzichanganya kwa Neno. Unaona, wewe si wa Mungu. Umekufa. Huwezi kuwa umekufa na hai, wakati ule ule. Kwa hiyo hata Neno la Mungu hata halikui, unatimiza tu sehemu ya mnafiki. Acha hilo liende kwa askofu, kasisi, kadinali, yeyote yule. Hiyo ni kweli. Halina budi kuwa ni Neno, la sivyo umekufa, mwana haramu tu, Neno la Mungu (sehemu ya Mungu) halitakua. Huenda ukakulia kwenye shamba lile lile, kama tunavyoliendea moja kwa moja, bali ha—hakika hu—huko zizini. Halitakua. Vema. Vema.

153 Tunaona basi, Mnaona. Neno lililonenwa, basi sisi ni Neno la Mungu lililodhihirishwa. Hivyo ndivyo Mungu anavyolitaka Kanisa Lake, ni kujidhihirisha Mwenyewe. Anawezaje kujidhihirisha Mwenyewe isipokuwa Mbegu Yake Mwenyewe iwe ndani ya mtu huyo?

154 Unawezaje kutumia mawazo yako mwenyewe, na Mungu ajidhihirishe Mwenyewe kupitia kwako? Unawezaje kuchukua imani yako mwenyewe, na kusema, "Vema, mchungaji wangu anafundisha, kanuni ya—ya—yangu ya imani inasema, ya kwamba siku hizi za miu-. . . " Utafanyaje jambo hilo, na halafu uwe mwana wa Mungu aliyedhihirishwa? Utafanyaje jambo hilo? Kifo cha Yesu hakikuwa kitu kwako. "Loo, ninamkubali kama Mwokozi wangu." Humkubali! Unasema unamkubali, bali humkubali. Matendo yako yanathibitisha kile ulicho.

Yesu alisema jambo lile lile. "Kama mnafikiri nimezaliwa kiharamu. . . "

Walisema, "Sisi ni wana wa Ibrahimu, wala hatuhitaji mtu wa kutufundisha."

155 Kasema, "Kama mngalikuwa watoto wa Ibrahimu, mngalinijua Mimi." Kasema, "Ni nani kati yenu anayenihukumu kwamba nina dhambi, kutokuamini? Nionyesheni jambo moja ambalo Mungu aliahidi juu Yangu, ambalo halijatimizwa." Huh! "Nionyeshe jambo moja ambalo Baba aliahidi, ambalo sijatimiza. Dhambi ni kutokuamini. Hebu tuwaone mkizifanya basi." Hiyo, hiyo iliwang'oa pembe. Mnaona? Bila shaka. Kasema, "Ni nani anayenishtaki Mimi? Ni nani awezaye—ni nani anayeweza kunihukumu kwamba nina dhambi, kutokuamini? Mnaona? Kama siamini, basi kwa nini Baba anafanya kupitia

Kwangu kama anavyofanya, kila Neno aliloahidi? Sasa hebu nione mahali mlizo nazo kwenu."

156 Ni nani aliyezaliwa haramu basi? Walikuwa, watoto haramu wanaokiri kwamba ni Mungu. Yesu alisema, "Ninyi ni wa baba yenu ibilisi, na kazi zake mnazifanya." Ibilisi alifanya kazi za aina gani? Kujaribu kulichanganya Neno la Mungu, kupitia kwa Hawa.

157 Hilo ndilo jambo lile lile hasa ambalo madhehebu haya makubwa hufanya siku hizi. Kazi za ibilisi, baba yao, wanazifanya. Wanajaribu kuchukua kanuni ya imani na kuichanganya na Neno la Mungu. Hivyo ndivyo Shetani alivyofanya hapo mwanzo, baba, ibilisi. Mungu awabariki, ndugu. Ondokeni kwake! Yesu alisema hivyo. Ukiwa na mkwaruzo mmoja mdogo wa Mungu ndani yako, unapaswa kuangalia na kuona Hiyo. Chotara! Loo, jamani!

158 Kazi ambazo Yesu alifanya! Kama mtu ana Mbegu ya Mungu ndani yake, huku Roho wa Mungu akiitia hiyo Mbegu maji, kazi zile zile ambazo Yesu. . .zilizodhihirishwa katika Yesu, Yeye akiwa ndiye Mzao asili wa Mungu, kifo Chake kinakurudisha kwenye Uzao asili wa Mungu. Na ikiwa Roho yule yule aliyekuwa ndani Yake, yuko ndani yako, basi kazi zile zile zitadhihirishwa.

159 Huamini hilo? Vema. Hebu tufungue Yohana Mtakatifu 14:12. Unasema, "Mimi ni mwaminio, Ndugu Branham. Hakika mimi ni mwaminio." Vema. Nitaona kama Yesu angekuita hivyo, nione kama Neno la Mungu linakuita hivyo.

> *Amin, amin,* (kabisa, kabisa), *nawaambia, Yeye aniaminiye mimi, kazi nizifanyazo mimi, yeye naye atazifanya; na kubwa kuliko hizi atafanya; kwa sababu ninaenda* kwa *Baba.* (Ni kitu gani? Uzao ule ule.)

160 Huwezi kuweka. . .Unawezaje kupanda ngano *hapa*, na ngano *hapa*, na kusema, "Nitapata matango *hapa,* na ngano *hapa*"? Huwezi kufanya hivyo. Njia pekee utakayopata matango, ni kupanda matango. Ukizichotarisha mbegu, basi haitakuwa ni tango. Itakuwa ni mnafiki. Hiyo ni kweli? Itakuwa ni mnafiki, enyi marafiki. Si—sina budi kulisema. Si mmojawapo. Si tango ama kile ulichotarishia nacho. Ni chotara, na ni zao baya. Nalo limekufa, lenyewe, wala haliwezi kujizaa tena. Limekufa, papo hapo. Kurudi, halitaendelea mbali zaidi. Hilo linalimaliza. Hivyo tu. Lakini kama ukitaka tango, anza na tango.

161 Ukitaka Kanisa, anza na Neno la Mungu. Ukitaka Uzima wa Mungu, anza na Neno la Mungu. Likubali Neno la Mungu katika utimilifu Wake, kila kipimo Chake. Halafu basi. . .Na kama huo ni utimilifu wa Mungu ndani yako, basi mvua inayonyesha itazaa kile hasa kilicho katika bustani yako.

162 Halafu, sasa, Mvua yako ya Vuli inakujia wapi? Mnaona mahali hiyo inapoelekea baada ya kitambo kidogo, sivyo?

Kupitia juu ya hayo matango-mwitu aliyopata Eliya, naye akafikiri yalikuwa matango, ama ambayo hiyo shule ya manabii kule juu, dhehebu hilo waliyokuwa nayo. Wakakusanya matango mwitu, nao wakafikiri yalikuwa—yalikuwa ni choroko. Loo, vema.

163 Ndipo, zile kazi zitakazodhihirishwa ndani yake, ni zile zile, kwa kuwa ni Neno-Mbegu la Mungu. Mwana wa Mungu alikuwa ndiye Mzao Wake kielelezo, na jinsi Maisha Yake yalivyokuwa wakati Roho alipomwagwa juu Yake baada ya ubatizo Wake. Ndipo Roho Mtakatifu akaja juu Yake. Maisha yale yale aliyoishi, vema, Roho yuyo huyo wa kumwagilia maji wa Roho Mtakatifu ataleta Maisha ya namna ile ile, akifanya jambo lile lile alilofanya, iwapo ni Mzao ule ule. Uzao wa Mwana wa Mungu utazaa Mbegu ya mwana wa Mungu.

164 Sasa, jioneeni aibu ninyi wanawake mliokata nywele. Jioneeni aibu ninyi wahubiri mnaoikana Kweli hiyo, mnasema, "Hilo ni sawa. Nywele hazina uhusiano wowote Nalo." Lakini Mungu alisema zinao. Mnaona mahali lilipo? Mnaona?

165 Hiyo ndiyo sababu ninaamini Neno. Ni Mbegu. Na kama Mvua ikiinyeshea hiyo Mbegu, itazaa kwa jinsi Yake.

Sasa kuna shida gani na miamsho hii? Tunafanya nini? "Kupata milioni moja zaidi katika mwaka wa '44," Wabaptisti, Wapresbiteri, na wowote wale, Wapentekoste.

166 Lakini liko wapi hilo dhihirisho la kazi za Yesu Kristo, "Sitendi neno mpaka kwanza Baba anionyeshe"? Uzao wa namna hiyo unatoka wapi? Roho Mtakatifu atatia maji na kuchipusha Mbegu hiyo. Ndiye Maji ya hiyo Mbegu. Kama Mbegu imepandwa, hiyo ndiyo sababu hasa ya Maji.

167 Kama Maji yakikushukia, unasema, "Mungu abarikiwe, hebu nikwambie jambo fulani, mhubiri! Mimi ni *Nanii*, wala siamini katika Kitu hicho." Wewe ni wa kimadhehebu. Wewe ni maskini mnafiki tu, kwanza kabisa. Hiyo ndiyo aina ya mbegu iliyopandwa.

168 Usi—usi—usi—usinielewe vibaya. Nakupenda, kipenzi. Ninajaribu kuwaelezea Hili. Mnaona? Nita—nita—nitaachia hapo, nitakapomaliza leo. Nitaliachilia. Lakini ninawatakeni mjue, wakati mmoja, yaliyo kweli, na sababu ya mimi kuamini ninayoamini. Ninaamini ibilisi amewadanganya. Kusema kweli, ninajua amewadanganya. Kulingana na Neno la Mungu, haliwezi kushindwa. Amewadanganya. Naam, bwana. Hiyo ndiyo sababu ninahubiri mambo hayo jinsi ninavyohubiri, kwa sababu Neno la Mungu lilisema hivyo.

"Loo," wasema, "vema, Ndugu Branham, hii ni siku tofauti." Ni Neno lile lile, hata hivyo.

169 Walipata ngano kutoka ghalani huko nyuma, iliyokuwako katika wakati wa Yusufu, na kuiweka na kuipanda hapa, miaka

michache iliyopita. Mliona hilo kwenye gazeti? Nayo ikazaa zao la ngano. Bado ilikuwa ni ngano, hiyo ndiyo sababu. Kitu pekee ilichohitaji, maji kidogo tu.

Neno la Mungu ni kama tu lilivyokuwa wakati Yeye alipolinena huko nyuma, maelfu ya miaka iliyopita. Kitu pekee inachohitaji ni Maji.

170 Kwa nini tusipate mazao? Kwa sababu tulipanda aina mbaya ya mbegu. "Ni wangapi, ninyi nyote mngetaka, kubadilisha barua zenu?" Mara mbili mtoto wa kuzimu kuliko ulivyokuwa wakati ulipoanza. "Ni wangapi wenu Wamethodisti wangetaka kuwa Wabatisti? Ninyi Wabaptisti mngetaka kuwa Pentekoste? Leteni tu uanachama wenu hapa." Loo, masalaale! Upuuzi mtupu! Takataka! Takataka za ibilisi. Hamna Uhai ndani yake, hata kidogo. Ni chotara, ya kinafiki, imekufa, imekufa maradufu, imeng'olewa toka mizizini. Hivi Yesu hakusema, "Kila pando asilolipanda Baba Yangu wa Mbinguni litang'olewa"? Dhehebu, hata liwe lipi, litang'olewa.

Neno la Mungu, pekee, litasimama. Kweli! Hivyo ndivyo alivyosema. "Kila neno la mwanadamu ni uongo, bali Langu ni Kweli."

171 Basi tutaenda wapi? Afadhali mrudie fahamu zenu. Lakini huwezi kulisikia isipokuwa umechaguliwa tangu zamani kulisikia. Tunaingia katika jambo hilo. Si ajabu linaanguka kama maji kwenye mgongo wa bata, ameumbwa kuyamwaga maji, si kuyafyonza.

172 Ile safina ilitengenezwa kwa mti wa mvinje na mti wa mshita. Ndio ninii zaidi. . . Si kitu ila utupu tu. Hakuna kitu ndani yake ila utupu. Kila kitu kimeondolewa kwake; unakua hivyo, mti mwepesi kuliko yote iliyopo, mwepesi kuliko balsamu. Kwa nini wakafanya hivyo? Ili aweze kuulowesha kwa lami. "Kama ungalikuwa mwaloni," unasema, "mwaloni si ungefaa vivyo hivyo?" La, bwana. Hautanyonya chochote. Unakiondosha. Hu—huondosha; na huu ni mfyonzaji.

173 Nayo Mbegu halisi ya Mungu ni kifyonzaji cha Roho. Umadhehebu wote umeondolewa. Kutokuamini kwote kumeondolewa. Ndipo Roho Mtakatifu anapoingia kwenye Seli zazi hiyo ya Uhai inayokaa pale, inazaa Mbegu nyingine, sawa kabisa. Mwana mwingine wa Mungu anazaliwa. Amina. Mungu mwingine mdogo, mwana wa Mungu!

174 Mimi ni Branham kwa sababu nilizaliwa na Charlie na Ella Branham. Hiyo inanifanya Branham, kwa sababu mimi ni mzao wao. Makubaliano yao mawili, pamoja na mbegu yao pamoja, ilifanya uzao, na hiyo ikanifanya mimi.

175 Wakati Mungu na Neno Lake wanapokuwa Mmoja (Haleluya!), hiyo. . . Wakati Roho wa Mungu anapoimwagilia maji Mbegu ya Mungu, Neno la Mungu, humzaa Mungu. Wala si mtu binafsi. Ni Mungu, kwa kuwa (kitu gani?) umekufa. Wewe

si nafsi yako tena. Unajihesabu kuwa umekufa, umefanywa tupu, ukingojea Mbegu-Seli zazi. Basi ni kitu gani? Si wewe tena; si mtu huyo. Ni Mungu ndani ya mtu huyo. Ni Mbegu-Seli zazi, kama hapo mwanzo, Neno lililonenwa. Ni Neno la Mungu lililodhihirishwa katika mwanadamu. Basi, si huyo mtu; ni mtu aliyekufa. Hawezi kuwa chotara na mwana, wakati uo huo. Yeye ama ni mwana wa mauti au mwana wa Uzima. Kwa hiyo kama yeye ni mwana wa mauti, mkabidhi ibilisi apate kumwua. . .Mkabidhi Mungu, nilimaanisha, na kumwacha amwue ibilisi aliye ndani yako, amfukuze, akufanye tupu. Ndipo, umwache Mungu apande Uhai Wake Mwenyewe ndani yako, ndipo si wewe tena. Ni Uzima wa Mungu, kwa sababu ni Neno la Mungu lililotiwa maji na Roho Mtakatifu, litazaa kitu kile kile. Mnaliona?

Ninapenda tu kuhubiri juu ya hilo kwa dakika chache; lakini nikiwa na kurasa thelathini ama arobaini za Maandiko hapa, nami nina tatu tu kufikia sasa. Jamani! Vema.

176 Zikidhihirishwa, kazi zikidhihirishwa vivyo hivyo na—vile vile nasi, kwa kuwa ni Neno lile lile. Sasa, ukitaka kufanya kazi za Kristo, fanya jambo lile lile alilofanya. "Yeye aniaminiye Mimi atakuwa na kazi Zangu." Ni kitu gani hicho? Aaminiye (nini?) ya kwamba Yeye ndiye Mbegu-Seli zazi asili iliyokuja. Ule Uzao uko wapi?

Hapa, hebu nichukue leso hizi. Huyu *hapa* mtu aliyepaswa kuwa. Papa *hapa*, huyu ndiye mtu aliyepaswa kuwa.

Nini kilitukia? Hawa alilichotarisha, akalizalisha, ndicho kilichotukia. Basi ilifanya nini? Ikageuka ikawa mauti; kuendelea tu kufa, kufa. Sasa huyu akaja, ambaye kutoka . . .

177 Sasa *hapa* linadumu Neno, vivyo hivyo tu. Hili *hapa* Neno limewekwa hapa, vivyo hivyo tu. Sasa ni jambo gani lililotukia? Hili *hapa* Neno. Sasa, Neno ambalo Mungu alinena, "Kuongezeka na kuijaza nchi," halingepata mahali pa kutua.

178 Hatimaye, Neno *hili*, lilishika katika tumbo la uzazi la bikira. Tutazungumza juu ya hayo matumbo mawili ya uzazi, alasiri ya leo, zaidi. Basi ilikuwaje? Kutoka Kwake ikatokea Seli zazi ya Uzima, kitu kinachotoa, Maji yanayokipa ki—ki—kiini nafasi yake ya kujizaa tena. Roho ilitoka Kwake ikapanda juu.

179 Sisi *hapa*. Tunakuja. Inakuwaje? Tunaliamini. Tunaliamini. Sasa, Yesu alisema nini? "Yeye aniaminiye Mimi." Mnaona? "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi, dhihirisho ambalo. . .Roho Mtakatifu alikuja katika mfano wa hua, akaja juu Yangu na kufanya hivi, si kwa kuchanganya mbegu, bali kwa kuzaliwa na bikira." Si mwe—mwe—mwenendo wa—wa maisha, kama kuzaa mtoto, mume kwa mke; la, si hilo. Si kuchanganya mbegu, bali kuzaliwa na bikira. "Sasa, kupitia jambo hili, ninatoa Uzima huu, kwamba kama wewe, kwa imani, utakubali kile Baba, manabii wote, Neno lote la Mungu, nitamwaga Uzima

huu juu yenu, nanyi mtaninii. . .huwezi kufanya jambo lingine ila kuzaa kitu kile kile nilicho mimi! Haya basi. Kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya." Yeye alifanya nini? Kama tu vile Baba alivyomwongoza, yale aliyoona. Yohana Mtakatifu 5:19, ninii tu. . . "Sitendi neno mpaka Baba anionyeshe."

180 Yeye alikuwa nini? Alijifanya Mwenyewe Mwanadamu. "Mungu alifanyika mwili, akakaa miongoni mwetu. Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu." Neno la Mungu lililonenwa, kupitia kwa bikira, lilileta m—mwili. Na katika mwili huo yakaja Ma—Maji, Roho. "Na kuoshwa kwa Maji ya Neno." Ndipo akaingia ndani Yake, akakaa ndani Yake, na hapo ukaja Uzima wa Mungu akijidhihirisha Mwenyewe kupitia Kristo. Mungu alikuwa ndani ya Kristo, Yule aliyetiwa mafuta. *Kristo* maana yake ni "Yule aliyetiwa mafuta," Mtu aliyetiwa mafuta. "Na Mungu akiishi ndani Yake." Ilikuwa ni kitu gani? Ile Seli zazi iliyo na mwili, Yule aliyetiwa mafuta, mwili ukitiwa mafuta na Roho wa Mungu, ulileta Neno la Mungu lililodhihirishwa. "Nasi tukamwona, Mwana pekee atokaye kwa Baba, amejaa neema." Mnaona?

181 Sisi hao hapo, mnaona. Yeye alikuwa ni Neno la Mungu lililodhihirishwa. Na, sasa, Yeye alikufa kusudi alipe deni ya uchotara wetu. Jamani! Jamani! Hilo hapo. Ni kitu gani? Kwamba ungeweza kufa kwa nafsi yako, mpaka iwe si wewe mwenyewe tena, na ujazwe na Neno Lake, ukiamini Neno Lake. Ndipo Roho Mtakatifu, aliyekuwa ndani Yake, anashuka kulitia Neno hilo maji, kulifanya likue. Unaona? Na basi ni kitu gani? Mungu akidhihirisha, akiendeleza kazi ya Mwanawe wa kwanza, Mwanawe wa pekee, mnaona, aliyekufa kwa ajili ya maisha yetu ya kuchanganya mbegu; ili apate kutupatanisha tena, tupate kuwa wana na binti za Mungu, kusudi kupitia Kanisa uweze kutiririka Uhai ule ule, kwa Neno, kuiendeleza kazi inayodhihirishwa kama ilivyokuwa katika Kristo. Kristo alikuwa ni Neno la Mungu lililodhihirishwa. Naye alikufa, akautoa Uhai Wake, apate kumtuma Roho; akaupandisha mwili Wake juu, na kumtuma Roho tena, kutia maji, kulipa gharama ya ukombozi, kama tutaamini. Hilo hapo papo hapo: kama unaliamini. "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi. . . " Ndipo akaja Roho Mtakatifu juu ya Neno lile lile la Mungu.

"Sasa," unasema, "una—unaitupa wapi juu ya Biblia basi?"

182 Biblia haina budi kuwa ndani yako. Neno ni Mbegu. Maadamu limekaa *hapa*, halitafaa kitu. Lakini linapoingia *hapa* ndani, linapoingia moyoni, ndipo linaanza kudhihirisha, kwa Roho Mtakatifu, kazi za Mungu. Ndipo maono yanakuja, nguvu zinakuja, unyenyekevu unakuja. Ujuaji wako wote umekwisha. Unakuwa si kitu. Kristo anakuwa hai. Unakufa; Yeye anaishi. Hilo hapo. Maana, Yeye alikufa, ninaishi. Ninapokufa, Yeye—Yeye anaishi tena. Na ninakapokufa, Yeye aliniahidi Uzima. Nami nilikufa kwa nafsi yangu, kusudi nipate Uzima Wake.

Nami ninafanyaje hilo? Kwa kuchukua Neno Lake, Mbegu Yake. Weka Mbegu Yake *hapa* ndani, kwa imani, na uuamini, ndipo unaleta yale hasa Biblia iliyosema.

Sasa, ndugu zangu, tafuteni kote nchini. Tunapata uigaji mwingi sana.

183 Hebu tuendelee kwa muda kidogo tu zaidi. Mnaona? Vema. Matendo, yale yale yaliyodhihirishwa katika Kanisa Lake, kwamba yangekuwa, yaliyodhihirishwa katika Kristo. Yeye alisema hivyo, Yohana Mtakatifu 14:12. "Mbingu na nchi zitapita, bali Neno Langu halitapita." Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Vema.

184 Tumechaguliwa tangu zamani, kama Yeye alivyochaguliwa, kunalifanya mwili Neno-Mbegu. Afadhali nikomee hapo sasa. Labda msingeninii, lakini mtu fulani huko nje kwenye nchi ya kanda huenda akaele-. . .huenda akaelewa. Kuchaguliwa tangu zamani! Wana wote na binti za Mungu wamechaguliwa tangu zamani. Tutayafikia Maandiko, baada ya kitambo kidogo. Ninawanukulia tu. Waefeso, mlango wa kwanza, kifungu cha 5. Vema. Tumechaguliwa tangu zamani. Kwa nini? Kristo ndiye Mbegu ya asili. Na Mbegu hii ya asili ilichaguliwa tangu zamani kwa kujua tangu zamani kwa Mungu, akijua ya kwamba kule kuanguka kungekuja, ndipo akamchagua tangu zamani kupachukua mahali petu. Mnalipata? Wana wote na binti za Mungu wamechaguliwa tangu zamani.

"Lakini," unasema, "basi atawahukumu wengine?" La, bwana.

185 Uko hapa kwa uhuru wa kujichagulia. Lakini sababu ya Yeye kujua. . .Yeye, akiwa ni Mungu, Yule asiye na kikomo, kama nilivyowaambia habari zake, Yeye alitangulia kujua kila kitu kitakachokuwako. Alijua walikuwa ni akina nani.

Sasa, Yeye hakumfanya Hawa kufanya hivyo. Hakumfanya afanye hivyo, bali alijua angefanya hivyo.

186 Sasa, si ajabu, ninaamini, katika mlango wa 12 wa Luka Mtakatifu, ninaamini ndio, Yeye alisema. Mimi. . .Msiandike hilo. Nitalipata. Nimeliandika, baadaye kidogo, hilo. Alisema, "Wana macho, bali hawaoni. Wana masikio, bali hawasikii. Isaya alinena vema juu yenu. Isaya alitangulia kuwaona." Nao hao hapo, wameketi pale, wakiwa na macho, masikio, na chochote kile, bali hata hivyo hawawezi kuona. Kwa nini? Wao ni wakinzani kwa Neno la Mungu. Ndipo Yesu akasema, "Loo, enyi wanafiki. Ninyi ni—ninyi ni watoto wa ibilisi, na kazi zake mnazifanya; kisha mnanihukumu Mimi," Yeye alisema, "kuikataa huduma Yangu." Wakati, nionyeshe mahali ambapo huduma yenu inatoa Neno lote la Mungu, kama Yake ilivyokuwa. Mnaona? Mnaona?

187 Sasa, kuchaguliwa tangu zamani, kama Yeye alivyokuwa. Sasa mnasema, "Huko kuchaguliwa tangu zamani huja kwa njia

gani?" Mungu, kwa kawaida. . . Sasa, kama kila mtu haelewi hili, ninakutaka uinue mkono wako sasa nitakapomalizia. Unaona? Mungu, hapo mwanzo, aliwaagiza Adamu na Hawa wazae wakaijaze nchi. Hivyo ndivyo kujuana kimwili kulivyotolewa, hiyo ndiyo sababu kulitolewa. Lakini ni kitu gani kilichosababisha kuchanganya mbegu? Kuleta mauti. Sasa tutapata jambo hilo alasiri ya leo, katika matumbo mawili ya uzazi. Mnaona?

188 Sasa angalieni. Sasa, katika jambo hili, Mungu alitangulia kuona na kuchagua tangu zamani ulimwengu wa wana na binti. Aliwachagua tangu zamani wawepo. Na kwa sababu ya kuchanganya mbegu. . . Kutokuamini Neno la Mungu kulisababisha kuchotarisha mbegu. Mungu amekurudisha moja kwa moja, tena, kwamba si lazima uwe chotara tena. Unaweza kurudi moja kwa moja kwenye Neno la asili na uwe mwana wa Mungu kama tu vile ulivyopaswa kuwa hapo mwanzo. Unaona?

189 Kristo asingeweza kujizuia kuwa kile alichokuwa; alikuwa ni Mwana wa Mungu. Jambo ndilo hilo. Mnaona ninalomaanisha sasa? Unaona, kama ulikusudiwa, unaliona Neno la Mungu, unaliamini. Kwa sababu gani? (Kuna jambo jipya.) Unaona? Kwa nini?

190 Umewahi kusikia kuhusu nasaba, katika familia? Mmoja, mwa—mwa—mwana, kwa namna fulani atamwiga baba yake ama—ama mama, ama babu, nyanya. Nasaba hiyo, katika familia. Mmesikia habari zake. Sivyo?

191 Vema, hilo ni jambo lile lile kutokana na kuchaguliwa tangu zamani. Ulipaswa kuwa hapa kwa njia sahihi, hapo mwanzo. Lakini, kwa kuwa ulikuja jinsi ulivyokuja, uko katika hali ya kuanguka. Lakini, kwa kuwa umechaguliwa tangu zamani, unalisikia Neno. Linakurudisha moja kwa moja mahali ulipochaguliwa tangu zamani. Amina. (Sijawahi kuona hilo hapo awali.) Linakuleta moja kwa. . . Ni—ni kitu gani kinachokufanya uliamini Neno la Mungu, na kuyakataa mambo haya mengine? Ni kwa sababu ulikuwa. . . Kuna Kitu fulani ndani yako. Huko nyuma kabisa, unapa-. . . Ati nini? Umeumbwa upate kuishi hapa milele.

"Ninataka Maandiko kwa ajili ya jambo hilo, mhubiri."

192 Hili hapa linakuja. "Wote aliotangulia kuwajua, amewaita; wote aliowaita, amewahesabia haki; na wote aliowahesabia haki, tayari amewatukuza."

"Kuna haja gani kuhubiri, Ndugu Branham?"

193 Kuna ninii—kuna mazao huko nje. Jambo pekee ninalofanya ni kuvua kwa juya. Ninalitupa tu huko nje, nione mahali litakapoenda. Kama wao ni wafukuzaji, grisi ya kinyaa cha ulimwengu na madhehebu yakitupilie mbali, siwezi kulizuia. Lakini kama kuna mmoja huko nje anayeweza kulifyonza,

atageuka kuwa mwana na binti ya Mungu, kweli kabisa, amina, maana umechaguliwa tangu zamani.

194 Hiyo ndiyo sababu Mungu angeweza kufanya kazi Zake kupitia Yesu, Yeye alikuwa Mwana aliyechaguliwa tangu zamani. “Yeye alikuwa Mwana-Kondoo aliyechinjwa kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu.” Kabla ya miaka bilioni trilioni milioni laki moja iliyopita, ambayo tulisema Mwanzo 1:1 ilinena habari zake, muda mfupi uliopita, Yeye papo hapo alichaguliwa tangu zamani kupachukua mahali Pake. Amina. Hiyo ndiyo sababu ma—mapenzi ya Baba aliyafanya. Yeye alikuwa ni Neno lililodhihirishwa.

195 Na kila mmoja wa hao wana wengine atakuwa na dhihirisho lile lile, na hao ndio waliochaguliwa tangu zamani. Kundi hilo dogo, katika kila kizazi, litafufuka katika ufufuo, kote kote tangu mwanzo wa ulimwengu. Na sababu yake, wanalishikilia. Hata Paulo alinena habari zake katika Ufunuo, ama katika—katika Waebrania mlango wa 11, kasema, “Wanazunguka-zunguka wamevaa ngozi za kondoo na za mbuzi, nao walikuwa wahitaji, wakiteseka, na wakitendewa mabaya; ambao ulimwengu huu haukuwastahili.” Amina. Hawakuwa na chakula, na kukimbia huku na huko, na kuchimba, na kuteswa, na kukatwa kwa misumeno, kama vile Isaya alivyokatwa, na wengi wa hao wengine. Paulo akinena habari za hao watu. Yeye alikuwa ni nani, kasema, aliyesemekana “alikatwa kwa msumeno”? Isaya, nabii, aliyechaguliwa tangu zamani hata kabla ya ulimwengu kuanza. Alipaswa kupitia kwenye tumbo la uzazi la Hawa. Lakini basi akaja kupitia tumbo—tumbo la uzazi la mwanamke fulani; ilibidi roho yake ije hapa ipate kuwa shahidi.

196 Kwa hiyo Yesu alikuja, pia, alikuja kwa ajili ya kushuhudia mauti, kuzikwa, na kufufuka; kwamba mwanadamu atakufa, bali ataishi tena kupitia Kwake, kwa kuwa Yeye ndiye Mbegu ambayo haina budi kuchipuka. Amina. Natumaini mnaliona. Vema.

197 Kwa kuwa ulichaguliwa tangu zamani kama alivyokuwa, hulifanya Neno-Mbegu kufanyika mwili ndani yako, Kanisa Lake, Neno la Mungu.

198 Unasema, “Hakika, Ndugu Branham. Kila Neno, ninaliamini.” Basi msirudi nyuma mnapopata mapokeo yenu. Unaona?

199 Dumu moja kwa moja na Neno hilo. Na udumu na Hilo, uone litakalotukia. Sema, “Ee Bwana, ninaliamini. Mtume Roho Mtakatifu.” Kisha uangalie. Ndipo kama akianza kushuhudia, basi unajua umempokea. Si kwa mhemko fulani; pepo hufanya hivyo. Si kwa mwujiza fulani; pepo hufanya hivyo. Lakini kwa imani yako ya sikuzote katika Neno la Mungu, na maisha

unayoishi, bila kukana chochote. Vema. Hilo hulifanya Neno kufanyika mwili, unaona, mwili na Roho-Maji yule yule.

Sasa, ngojeni kidogo. Siwezi kupita hili. Mnaona?

200 Yesu alikuwa Mzao wa Ibrahimu, tukinena kimwili. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Uzao wa Ibrahimu uliochaguliwa tangu zamani. Na wakati Roho aliposhuka juu Yake, Yeye alileta Maisha ya namna gani? Alileta Maisha ya imani. Ati Maisha ya namna gani?

"Unataka kusema Yeye atakuwa mgeni kama Ibrahimu?"

201 Hapo ndipo watu wanapochanganyikiwa sana siku hizi. Wanajaribu kuwazia ya kwamba mtu wa Mungu hana budi kufanya *hivi*, na kufuata *hili*, na kufanya *lile*. Loo, rehema, la. Nini ilikuwa . . .

202 Kristo alikuwaje Uzao wa Ibrahimu? Si katika ninii Yake . . . sana katika mwili Wake. Maana, Isaka, huo uzao wa Isaka hatimaye ulianguka ukafa, ulirudi nyuma na ukawa chotara, pia. Tutalifikia, moja kwa moja. Mnaona? Lakini yule Uzao wa imani wa Ibrahimu, ambapo aliamini Neno la Mungu haidhuru hali ya mambo ilikuwaje! Haya basi. Whiu! Mwajua, ninajisikia kupaza sauti. Angalieni. Mnaona? Angalieni. Uzao wa imani ya Ibrahimu, ilikuwa ni nini? Si mwili wa Ibrahimu, bali imani ya Ibrahimu. Imani ya Ibrahimu katika (kitu gani?) Neno la Mungu. Haidhuru ni kitu gani kilichokuja, aliita chochote kinyume Chake kana kwamba hata hakikuwepo. Loo, jamani, hilo si lingeyararua madhehebu haya vipande-vipande? Hum, hum, hum, hum! Hakika lingeyararua.

203 Kama Ukweli wa hata *Ndoa Na Talaka* ungelidhihirishwa tu katika nuru yake iliyo humu ndani, katika Biblia, ungevunja kila kanisa katika mji huu, mji mwingine wowote, kujaribu kurudi kwake. Wao, pande zote mbili, zimekosea. Ninaweza kulithibitisha kwa Neno. Zote mbili zimekosea. Vema. Kama mtu anapaswa kufanya *hivi* ama kufanya *vile*, ama mwanamke *hivi* ama *vile*. Sitasema jambo hilo, kwa sababu nina mchafuko wa kutosha sasa miongoni mwao. Mnaona? Uh-huh. Yesu alisema, "Waacheni. Kipofu anamwongoza kipofu mwenzake." Mbona, vema, wanazozana tu juu yake. Wasingeamini jambo hilo. Kama wamezaliwa wapate Uzima wa Milele, wataliamini Neno. Mnaona? Sawa. Wasipoamini, Mungu atajidhihirisha Mwenyewe kwao. Kama hawaliamini, mbona, hawataliamini. Hivyo tu.

204 Hebu na tuliendee jambo hili, kwanza. Huenda tukafikia hilo, baadaye wakati fulani. Lakini hebu tulishughulikie hili, kwanza, mnaona, ili tuone ni kwa nini hatuna budi kuamini mambo haya, jinsi tunavyopaswa kuyaamini. Huna budi kuyaamini. Usipoyaamini, umepotea. Umepotea.

"Kuamini nini, Ndugu Branham? Wewe?" La, bwana, si mimi. Mkiniamini mimi, na . . .

205 Ninasema Neno. Siweki chochote hapa. Ninawaambia tu yale Biblia isemayo kuhusu kuamini Neno hili. Na hivyo ndivyo nimefanya, ni kujaribu kuamini Neno hilo jinsi tu lilivyoandikwa; siongezei chochote, kuondoa chochote. Ninalisoma tu jinsi lilivyo, na kuliamini tu namna hiyo. Na kwa neema na msaada wa Mwenyezi Mungu, Yeye amelithibitisha.

206 Nami naomba mtu yeyote alikanushe. Sasa, ninyi mlio kwenye kanda, njoni mfanye hivyo. Niambieni wakati mmoja nilipowahi kuwaambia jambo lolote baya, halikutimia. Niambieni chochote, wakati wowote, ambapo Mungu kamwe hakuthibitisha na kulifanyia kazi sawasawa kabisa na vile lilivyosemwa. Vema.

207 Akiwa amechaguliwa tangu zamani, kama Yeye alivyokuwa, hulifanya Neno-Mbegu Maji yale yale juu ya (kitu gani?) Kanisa hili leo. Je, Bibi-arusi amechaguliwa tangu zamani? Je, Mungu alisema angekuwa na Bibi-arusi asiye na waa wala kunyanzi? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Basi limechaguliwa tangu zamani. Sivyo? ["Amina."] Mnaona? Vema, Kristo alichaguliwa tangu zamani. Yeye alikuwa ni Uzao wa Kifalme wa Ibrahimu, nao ulifanya nini? Wakati Roho alipokuja juu ya Kristo, Yeye alishuhudia Neno la Mungu. Na wakati ninii—wakati Roho-Maji anaposhuka juu ya Neno-Mbegu, ule Uzao wa Kifalme wa imani ya Ibrahimu katika Neno la Mungu utazaa mazao ya aina ile ile.

Wasema, "Siamini hilo."

208 Vema, hebu tuone. Hebu twende sasa tuone. Je, sisi ni Uzao wa Ibrahimu? Mwanzo 17. Turudi katika Mwanzo na tufungue mlango wa 17. Ninaacha mengi ya haya hapa, lakini si—sina budi kugusia baadhi yake hapa ndani. Maana, mkosoaji fulani huenda akaja na kusema, "Siamini hilo." Kwa hiyo, tutaweka tu kidogo humo ndani, kusudi Yeye aweze kumzuia asiseme jambo hilo. Mnaona? Vema, 17:7, hebu tuanzie kwenye kifungu cha 6.

> *Nami nitakufanya uwe na uzao* mwingi *sana* (Uzao wa Ibrahimu), *nami nitakufanya kuwa mataifa* mengi, (Mataifa na kadhalika) . . . *na wafalme watatoka kwako.*
>
> *Na agano langu nitalifanya imara* (sasa angalia) *kati ya mimi na wewe, na uzao wako baada yako, katika vizazi vyao kuwa agano la milele, kuwa—kuwa Mungu kwako na kwa uzao wako baada yako.*

209 Uzao wa Ibrahimu ni nini sasa? Sio mwili wake. Paulo alisema, "Myahudi, aliye Myahudi kwa nje, si Myahudi. Yule Myahudi kwa ndani." Mnaona? Uzao wa Ibrahimu ni nini? Wale wanaoamini Neno lote la Mungu, haidhuru kile dhehebu, ama baba, ama mama, mtu mwingine yeyote asemacho. Wanaamini Neno lote la Mungu. Mungu alisema, "Nitalifanya imara agano langu sasa hivi, nitalikusudia tangu zamani agano hili pamoja nawe na pamoja na yule Uzao, katika kila kizazi baada yako, kitakachoamini." Haya basi, Uzao wa Ibrahimu. Sasa

unasema . . . Sasa angalia. Mungu alisema, "Nitalithibitisha kwa Mzao."

"Vema," unasema, "Ndugu Branham, hilo linampa kila mt- . . ."

210 Ngojeni sasa kwa dakika moja tu. Hebu na twende katika Waefeso sasa, kwenye Kitabu cha Waefeso, na tutaanzia mlango wa kwanza wa Waefeso. Na ndipo tutasoma kidogo hapa na kuona tu kile Mungu anachosema kuhusu so—somo hili. Sasa sikilizeni. Paulo, sasa angalia jinsi anavyolizungumzia hili sasa.

211 Kila mtu asimame kwa—kwa miguu yake sasa, hatuna budi, ama, mwe waangalifu. Tuna dakika chache tu sasa, kisha tutaninii . . . Yapata dakika arobaini na tano, kitu fulani, ndipo tutafumukana kwa ajili ya chakula cha mchana. Sasa angalieni.

> *Paulo, mtume . . .*

212 *Mtume* ni nini? "Mtu aliyetumwa." "Paulo, mtu aliyetumwa na Yesu Kristo." Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] "Kwa mapenzi ya Baraza la Wazee "? Nilisoma hayo vibaya, sivyo? "Kwa mapenzi ya—ya Luther, ama ninii . . . "? Vema, hata hivyo:

> *Paulo*, mtu aliyetumwa *wa Yesu Kristo kwa mapenzi ya Mungu, kwa watakatifu . . .*

Ni kwa nani, kila mtu? La, bwana. Kila mtu hawezi kulichukua. Uh-huh. Hiyo ni kweli.

> *. . . kwa watakatifu walioko Efeso, na wanaomwamini Kristo Yesu:*

213 Wale ambao tayari wako humo ndani. Hao ndio ninaotumaini ninawazungumzia, katika kusanyiko hili asubuhi ya leo, wale ambao tayari wako "ndani ya Kristo Yesu." Sasa, hapo ndipo haya yameandi- . . .

214 Unaona, huwezi kuwaambia akina nanii . . . hao—hao watoto wachanga huko nje juu Yake. Hawawezi kula nyama. Inawabidi kunywa maziwa. Wamedumaa. Mnaona? Kwa hiyo, kumbukeni, hawawezi kula nyama ngumu.

> . . . sasa *wanaomwamini Kristo Yesu:*

> *Neema na iwe kwenu, na amani, zitokazo kwa Mungu Baba yetu, na kwa Bwana Yesu Kristo.* (Vema.)

> *Atukuzwe Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, aliyetubariki . . .*

215 Sasa, anazungumza na Kanisa, sasa. Hili si huko nje. Hili ni Kanisa.

> *. . . kwa baraka zote za ro—rohoni katika ulimwengu wa roho . . .*

Kama vile asubuhi ya leo, wale ambao wanalipenda wanalila tu. Mnaona?

> . . .*ulimwengu wa roho katika Kristo:*
>
> *Kama vile alivyotuchagua* . . .

Je, tulimchagua Yeye? Huh?

"Loo, Ndugu Branham, sa—samahani. Nilimchagua."

La. Wewe, kulingana na Neno, hukumchagua.

216 Yesu alisema, "Kamwe hamkunichagua Mimi. Niliwachagua ninyi." Loo, naam. Yeye alilichagua lini? Wakati Yesu alisema alilichagua Kanisa Lake lini? "Kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu."

217 "Kama vile alivyotuchagua katika Yeye," kwenye uamsho wa mwisho ambao Dk. *Nanii* alikuwa nao? La, la. Huenda ukasoma hilo katika kanuni za imani, kitabu cha kiada, bali si katika *Hiki*. Unaona?

> *Kama vile alivyotuchagua katika yeye kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu,* . . .

218 Tulichaguliwa lini, kwenye ule uamsho wa mwisho, usiku tuliookoka? Mbona, wakati—wakati hakukuwako na ulimwengu, hakukuwako na nyota, hakukuwako na atomi, hakuna molekuli, hapo ndipo tulipochaguliwa. Amina. Loo, usiniache nianze kuhubiri juu ya jambo hilo. Ninajaribu tu kuelezea jambo fulani hapa. Vema.

> . . .*kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, ili tuwe* . . .

Ati nini? "Washiriki"? La. "Inatupasa, loo, baada ya kuokoka, tunafanya tu utakavyo"? Hapana.

> . . .*tuwe watakatifu, watu wasio na hatia mbele zake katika* . . .

219 "Uanachama"? La, la. Ni "pendo." Sivyo? Hiyo ni kweli. Vema. "Katika upendo." Samahani. Ninakata tu, nadhani, sasa. Sipaswi kufanya hivyo. Vema.

> . . .*katika pendo:*
>
> *Kwa kuwa* (Nini? A-l-i-t-a-n-g-u-l-i-a k-u-t-u-c-h-a-g-u-a. Loo!) *alitangulia kutuchagua ili tufanywe wanawe* (ule Uzao tangu mwanzo, mnaona). . .*ili tufanywe wanawe kwa njia ya Yesu Kristo sawasawa na uradhi wa mapenzi yake,*

220 Ni nani aliyefanya jambo hilo? Mungu. Alilifanya lini? Kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Ndipo kama tukija kwa kuzaliwa kiharamu kwa upotovu wa Hawa, akitufanya sisi sote watoto wake na walio katika hali ya kufa, basi Mungu mwenyezi hana budi kufanya njia ya kuwakomboa watoto Wake. "Na wote alionipa Baba watakuja Kwangu. Wala hakuna mtu awezaye kuja asipovutwa na Baba Yangu." Loo, jamani! Sasa liko wapi jambo lako kuu ulilofanya? Hukufanya lolote.

Unapaswa kuona aibu. Mungu Ndiye aliyefanya mambo yote! Gurudumu linafanya kazi vizuri tu.

221 Mtu fulani alikuja, hivi majuzi, akasema mtu fulani alisema jambo baya kunihusu, na—na kunishtakia kitu kibaya. Nami nikasema, "Loo, sahau hilo."

Kasema, "Unawezaje kulichukulia namna hiyo? Hilo linahusu familia yako, hilo."

222 Nikasema, "Loo, jamani!" Nikasema, "Huyo alichaguliwa tangu zamani kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, apate kunijaribu." Nikasema, "Loo, jamani, jamani, jamani! Hakika. Kwa hiyo hilo ni sawa."

Kasema, "Unafanyaje jambo hilo?"

Nikasema, "Kama niliangalia moja kwa moja chini *huku*, ningekuwa nikianguka wakati wote."

223 Hivyo ndivyo ilivyo na watu siku hizi. "Kama nikikubali Kweli ya Neno la Mungu, Ndugu Branham, wangenifukuza." Vema, kwa nini unaangalia *hapa*? Angalia huku nje kwenye mwisho wa safari. Mnaona, mtu anayeonekana *hivi*, hajui anakoelekea, yeye anaangalia *huku*. Lakini ukiangalia huko nje, hujali kinachoendelea sasa, unajua unakoelekea. Unaona? Jambo ndilo hilo. Angalia unakoenda. Dumu umelainika sawasawa na Neno. Vema.

224 "Alituchagua tangu zamani sasa tupate kufanywa wana wenye mamlaka." Sasa mnaamini tulichaguliwa tangu zamani? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Sasa, je, Yesu alichaguliwa tangu zamani? ["Amina."] Alikuwa ni Mwana-Kondoo wa Mungu, tayari amechinjwa kabla hakujakuwako na nuru, kabla hapajakuwapo na kimondo, kabla hakujakuwako na molekuli, atomi, chochote kile. Alikuwa ni Mwana wa Mungu, aliyechinjwa. Loo, ukuu wa Mungu!

225 Halafu maskini bongo hizi duni kabisa kutoka kwenye maskini kiangulio fulani cha kujitengenezea huku, zinajaribu kulijadili Hilo na kusema si sahihi. Hiyo ni aibu. Kwani u nani wewe?

226 Hata baadhi yao wakisema ati, "Hakuna kuzimu." Nawe umeketi juu ya chungu chake kila siku, unene wa maili elfu nane, chini yako tu, volkeno; kisha unaangalia juu na kumwasi Mungu na Neno Lake. Unapoliasi Neno, unamwasi Mungu. Sawa.

Loo, jamani, jinsi Wewe ulivyo mkuu, Bwana! Jinsi tunavyopaswa kuwa na shukrani! Vema.

227 Kwa hiyo, waaminio, wa Neno na Roho, hawana budi kuwa mmoja. Mnalipata? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Waaminio, Neno na Roho, ni kitu kimoja kabisa. Hufanyi mawazo yako mwenyewe. Hutumii akili yako mwenyewe. Hilo si ni zuri sana? Nia iliyokuwa ndani ya Kristo iko ndani yenu. Mnaona? Nia iko ndani ya Kristo, nawe utalichukua Neno

kama tu Yeye alivyofanya, maana Yeye alikuwa ni Neno. Na nia ya Kristo ndani yako, wewe ni Neno. Ninyi ni Neno la Mungu lililo hai, wawakilishi Wake, hapa duniani, hiyo ni kweli, mkiiendeleza ile kazi. Kanisa linapaswa kuwa hivyo. Na linapokuwa hivyo, Biblia inadhihirishwa tena kama katika siku za mwanzoni za wale wanafunzi. Ni kama tu yule mwanafunzi, Biblia inaishi tena, ndani yako.

228 Sasa hebu tuone. Sina budi kujaribu kupata angalau, yapata kurasa kumi na tano hapa, upesi sana. Ninachukia tu kufanya hivyo. Lakini itanibidi tu kulipitia upesi. Maana, sininii, basi nitakuwa alasiri ya leo . . . Nina mkutano kesho, na—na sina budi kuharakisha sasa. Vema. Sasa tutajaribu kulifanya upesi zaidi kidogo tu, tukiweza, kuliingilia kwa haraka. Je, mnaamini? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Vema.

229 Na inapokuwa hivyo, Biblia inadhihirishwa tena kama katika siku za mwanzoni za Kristo. Mnaona? Maana, wewe ni Uzao uliochaguliwa tangu zamani kama tu Kristo alivyokuwa. Na wakati Mvua inapoinyeshea hiyo Mbegu, huo Uhai hujizaa Wenyewe, wakati Roho Mtakatifu anaposhuka.

230 Wakati alipowashukia hao Mbegu ambao Yesu alisema aliwachagua (lini?) kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, basi walikuwa ni Mbegu iliyochaguliwa tangu zamani. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Basi, hapa wanajinyanyua juu, katika chumba cha juu, hizi Mbegu, Neno. Nalo Neno lilikuwa limewekwa pale, bila Uzima ndani Yake. “Mara ghafla kukaja sauti kutoka Mbinguni wakati Maji yalipoanza kububujika, na kweli ikaijaza nyumba yote walimokuwa wameketi.” Ndipo hizo Mbegu zikaanza kukua. Likaanza kujidhihirisha Lenyewe, Neno la Mungu likidhihirishwa. Vema.

Kwa nini basi mioto ya uamsho imepungua?

231 Sasa, nina kama Maandiko kumi hapa, kama mngeweza tu kuyaona hapa, ambayo yanipasa kuyasema. Lakini sina budi kuruka mengi yake, ili kwamba tu mpate muhtasari wake. Vema.

232 Kwa nini basi mioto ya uamsho imepungua? Sasa sina budi kutaja majina. Sitafanya hivyo baada ya hili isipokuwa Mungu aniambie nifanye hivyo. Lakini sina budi kutaja majina. Sina budi kusema mambo ambayo sitaki kusema, lakini, ili kufanya jambo hili dhahiri.

233 Mnaweza kuona sasa mahali ninapofikia, sababu ya mimi kufanya yale niliyofanya. Ninaamini *Hili* ndilo Neno. Nami ninaamini ya kwamba Kristo analo Kanisa, nalo Kanisa ndilo shamba. Tutalifikia, baada ya kitambo kidogo. Nawe huna budi kuliweka Neno shambani kabla Roho hajaweza kufanya lolote. Unaona?

234 Kwa nini basi mioto ya uamsho imepungua? Hatusikii mengi zaidi juu ya Billy Graham, kama wainjilisti mashuhuri.

Oral Roberts, hawashi moto nchi kama alivyokuwa akifanya. Mikutano yangu hata haisikiki. Kuna watatu tu. Kuna shida gani?

235 Sasa tutapata mafundisho yenye kilindi sana. Mnaona? Itanibidi tu kuitumia sasa. Na kama kanda hii itaangukia mikononi mwa Billy Graham, Oral Roberts, ninawatakeni mjue, ndugu zangu, ya kwamba siwadharau. Ninajiingiza mwenyewe, kama mkiangalia, mle ndani, kama ndugu mwenzenu katika Injili. Nami nafikiri, baada ya jambo hili, mtakuwa na ufahamu bora zaidi, ndugu, kwa nini nimefanya yale niliyofanya. Nami natumaini ya kwamba nimepata neema machoni pa Mungu, na mbele zenu, katika kuwa mwaminifu na mkweli kuwaambia sababu yake.

236 Sasa, Billy Graham, ulimwengu ulikuwa unawaka moto hapa si muda mrefu uliopita kwa Billy Graham. Ni kwa nadra sana mnasikia habari zake sasa. Angali anaendelea, lakini kuna nini? Oral Roberts, mbona, akiiwasha tu dunia; anafifia. Tommy Osborn. Wote ni watu wema, watauwa. Nini kimetukia? Nikiamini ya kwamba Mungu aliniita kwa ajili ya huduma fulani, yangu imepatwa na nini? Sasa hapa tutajibu maswali fulani. Mnaona? Imekuwaje?

Mnasema, "Ndugu Branham, yako imekufa sana kuliko zote." Hiyo, hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli.

237 Billy Graham anasikika zaidi kuliko ninavyosikika, pia Billy anasikika zaidi kuliko Oral. Oral anasikika zaidi, katika siku moja, kuliko ninavyosikika katika miezi sita. Tommy Osborn, Tommy Hicks, yeyote wa hao watu watauwa, wanasikika zaidi. Kwa hiyo, kuhusu mabadiliko hayo, yangu iko mbali sana kuliko zote. Imekuwaje?

238 "Ndugu Branham, wewe unasema hivyo, kwamba unatuambia hapa sasa kwamba kweli unaamini Neno na kila kitu, vema, umepatwa na nini basi? Ni kitu gani kilichotukia?" Hilo ndilo tunalotaka kujua. Hilo ndilo tunalotaka kujua.

Sasa, mweke moyoni mwako sasa. Vuta mwavuli chini na utikise mvua imwagike, na ufungue moyo wako kwa dakika moja tu ukasikilize.

239 Kumbukeni, Biblia ilisema katika Mwanzo, mlango wa kwanza tuliyosoma, kuwekea msingi wazo letu kwa ajili ya siku hii, ni, "Kila mbegu kwa jinsi yake." Itabidi izae kwa jinsi yake. Hiyo ni kweli. Kila mbegu itabidi izae. Kumbukeni, dunia imejaa mbegu, nayo mvua huifanya izae kwa jinsi yake.

240 Ninaamini wakati wa mavuno umekaribia. Hivi hamwamini hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Nyote mnakubaliana na hilo. ["Amina."] Tumekaribia wakati wa mavuno. Sasa, mbegu zimepandwa. Hiyo ndiyo shida yake. Mbegu zimepandwa. Loo!

Ee Mungu! Laiti mngaliweza kuona yaliyopita mbele yangu wakati huo.

Mbegu zimepandwa. Kumbukeni, kuna wakati wa kupanda, halafu wakati wa mavuno. Wanajua walisema hivyo. Vema.

241 Sasa, kumekuwa na aina tatu mbalimbali za mbegu zilizopandwa. Ya kimadhehebu, Billy Graham, alikuwa ndiye mpanzi mkuu. Oral Roberts, kwa ajili ya Wapentekoste. Mbegu ya Kipentekoste imepandwa; ninazungumza juu ya madhehebu sasa. Na, kisha, Neno limepandwa. Sasa itawabidi kuelewa, jamani. Sisemi jambo hili tena isipokuwa Mungu aniambie. Ninawatakeni mlipate hili vizuri na dhahiri. Mbegu tatu zimepandwa.

242 Hiyo ndiyo sababu, kule kupanda, karibu kumekwisha. Mnaona? Yote yamekwisha. Mbegu hazina budi kupandwa kabla ya Mvua kunyesha. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Ama, vinginevyo, Roho. Sasa mtakosa kukubaliana hapo, lakini ngojeni tu kwa dakika moja. Mnaona? Mbegu lazima zipandwe; halafu basi Mvua inanyesha, kuipa Mbegu maji. Hiyo ni kweli? ["Amina."] Sasa nataka . . .

Kuna mtu yeyote humu ndani anayeelewa Kiebrania, anayejua maneno ya Kiebrania? Vema. Lichunguzeni mkitaka.

243 Sasa, tunasikia mengi sana, na madhehebu mengi sana na kadhalika yakizungumza juu ya, "Tuko katika mvua ya vuli." Upuuzi. Hakuna kitu kama hicho sasa.

244 Loo, jambo fulani linatukia. Ninaweza tu kuliona likipita mbele yangu. Tayari limeshika Roho. Mnaona? Amina. Ninajua hii ni Kweli. Ni BWANA ASEMA HIVI. Kwa ono, mnaona, kusonga tu, kuja. Ni vigumu kuangalia hapa chini. Mnaona? Kila ninapoangalia, ninaiona ikisogea tu mbele yangu, namna *hiyo*, na kutokea; na kusogea *huku*, na kuangalia *huku*. Nimekuwa nikijaribu kuwaangalia jamaa fulani wameketi hapa chini. Naangalia kwingine, na kila mahali ninapoangalia, inaonekana kana kwamba ni hiyo hapo. Mnaona? Vema.

Hebu turudi nyuma na kuijaribu tena sasa, tuhakikishe kwamba nimeipata mle ndani. Sijui ni kitu gani hasa kilichotukia kwenye mstari huo. Angalieni.

245 Ninaamini ya kwamba wakati wa mavuno umekaribia. Mbegu zimepandwa, mbegu ya kimadhehebu ya makanisa, kama vile Wainjilisti, kama vile Baptisti, na Presbiteri, na Lutheri. Nazo mbegu za Kipentekoste zimepandwa katika madhehebu ya Kipentekoste, na watu mashuhuri kama Oral Roberts, Tommy Hicks, na Tommy Osborn, watu mashuhuri wa Mungu. Mnaona? Nami ninaamini ya kwamba Neno la Mungu limepandwa, lisilોghoshiwa, mbali na lolote la madhehebu hayo. Jambo ndilo hilo. Mnaona? Mbegu haina budi kuwa . . .

Mmea wa Mbegu hauna budi kuwa na Maji ya Mbegu kabla ya kuweza kukua. Haina budi kuwa na Maji, kuanguka, kabla Mbegu iliyopandwa haijaweza kukua.

246 Sasa, "Vema," unasema, "Ndugu Branham, kumekuwa na ninii yetu . . . " Ninajua. Hiyo ni kweli. Ninashika wazo lako sasa, unaona. Kamwe huwezi kulificha sasa. Uh-huh. Vema. Kwa hiyo, iweni waangalifu kwa yale mnayowazia.

Sasa, Mbegu haina budi kupandwa. Halafu haina budi kuwa na Maji, ipate kukua.

247 Sasa, unasema, "Vema, Ndugu Branham . . . " Nitaelezea wazo lako, wazo hapo. "Tumekuwa na Maji." Na iwe hivyo. Hiyo ni kweli. Mmekuwa na Maji.

248 Umewahi kupanda kabichi ama chochote kile, ama mbegu, ama kitu kama hicho? Kwa kawaida, wanapata maji pale, wanayamwagilia tu kidogo. Unaona? Vema.

Lakini, sasa, ngoja. Tulikuwa na nini katika wakati huo wa kupanda? Mvua ya masika.

"Loo," unasema, "Ndugu Branham, upuuzi!"

249 Sasa ngoja kidogo tu. Hebu chukua neno *masika* katika Yoeli 2, na uliangalie, uone kama neno la Kiebrania, nenda kwenye Kiebrania, uone kama sivyo, ukitaka kuliandika, m-o-u-r-e-h, *moureh*, kisha uchukue hilo neno la Kiebrania, ulifasiri, uone *moureh* inachomaanisha, "kufundisha." Mvua ya mafundisho imenyesha.

250 Mvua ya mafundisho ya kimadhehebu imenyesha, "Milioni moja zaidi katika mwaka wa '44," Wabaptisti. *Fulani-wa-fulani*, *fulani-wa-fulani*, washiriki kanisani. Oral Roberts na hao ndugu walio na mwenendo wa Kipentekoste, ninii wa kiuchumi . . . ule mwenendo mkuu wa Kipentekoste, waliongezeka wakafikia mamilioni. Mnaona? Hiyo ni kweli. Nayo Mbegu imetoka, Neno, kwa ajili ya walio wachache, lile kundi.

251 Sasa angalieni, sasa kumbukeni, neno m-o-u-r-e-h, *moureh* linamaanisha "mafundisho." Mvua ya masika, Inasema, "Mvua ya moureh," mvua ya mafundisho. Mvua ya mafundisho ilinyesha. Billy Graham ameupiga ulimwengu; Wapentekoste waliupiga ulimwengu; nalo Neno limeupiga ulimwengu.

252 Sasa, kuna nini sasa? Sasa linangojea "mvua ya vuli." Hapo ndipo linapozaa matunda yake. Loo! Hum! Natumaini mnalipata. Ndipo aina ya mbegu uliyopanda shambani mwako itakuwa ndiyo aina ya mazao utakayovuna. Kama madhehebu yanataka wafuasi wengi zaidi, hao ndio watakaopata; hilo ndilo walilopata. Wapentekoste wanataka Wapentekoste zaidi; hao ndio watakaopata. Sawa. Lakini Neno litazaa wana na binti za Mungu. Uh-huh. Uh-huh. Sawa. Hilo linakuja, pia. Angalieni. Angalieni ile mvua kuu ya vuli inayopaswa kutokea, jinsi ambavyo wangekimbia juu ya ukuta, waruke juu, na jinsi

wangekuwa ni jeshi linalokuja. Ngojeni tu kidogo. Uh-huh. Aina ya mazao utakayopata, ni aina ya mbegu unayopanda shambani mwako. Vema.

Aina hizo mbili za kimadhehebu, mnaelewa, hizo aina mbili za kimadhehebu zitaungana pamoja, ili ziende Sodoma.

253 Lakini Neno litadumu pamoja na Wateule, Uzao wa Kifalme. Amina. Mnaona? Yesu alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika Kuja kwake Mwana wa Adamu."

254 Malaika wawili walishuka, wahudumu wawili waliotiwa mafuta walishuka kwenda Sodoma, kujaribu kumtoa mtu aliyekuwa amerudi nyuma, aliyekuwa na chembe ndogo ya Mungu ndani yake. Naye mke wake, bibi-arusi wake, mnajua kilichompata; aliaibika. Kisha waangalie binti zake; uone kilichotokea kuwa baada ya yeye kutoka nje. Daima mambo yalikuwa mabaya. Mnajua hiyo ni kweli. Samahani kwa usemi huo; lakini, mwajua, ni kero. Kwa hiyo hiyo ni . . . Ilikuwa hivyo daima. Tunajua hilo. Sasa, huwezi kukana Neno la Mungu.

255 Lakini kulikuwa na Mmoja aliyekaa na Ibrahimu, aliyetoa ishara. Naam. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Vema. Vema. Mmoja alibaki nyuma.

256 Ibrahimu na kundi lake waliitwa nani? Mbegu teule ambayo haikushuka kwenda kamwe. Walikuwa ni wasafiri. Walisafiri *hapa*, wakasafiri *kule*; walisafiri *hapa*, wakasafiri *kule*; wasio wa kimadhehebu.

257 Lakini yule wa dhehebu alishuka na kujifanyia mji. Naye Lutu akawa kuhani, ama askofu, ama ninii . . . mwajua, chochote kile pale, bosi, aliketi—aliketi mjini na kutoa hukumu, anayesema (askofu, mzee wa jimbo), "La, hatutakuwa na jamaa huyo miongoni mwetu. La, bwana. Yeye hakubaliani na theolojia yetu. Hatuwezi kumpokea." Huyo hapo mzee Lutu. Huyo hapo ameketi. "Kama hatabeba hati za utambulisho kutoka kwenye kundi letu, hatutamkaribisha, hata kidogo." Ni nani aliyekufanya hakimu juu ya Nyumba ya Mungu, ewe chotara? Uh-huh. Huh! Neno la Mungu litahubiriwa, kwa vyovyote vile.

258 Mtakatifu Martin alienda kwenye kundi kama hilo, na jamaa huyo hata asingesimama, kumpa heshima, baada ya kuyavunja malango. Mungu hata aliteketeza vazi lake kutoka kwake, mgongoni mwake, akamfanya aamke na kumsalimu nabii huyo wa Mungu aliyeingia mjini. Uh-huh. Hiyo ni kweli. Kiti chake kilishika moto, mahali alipokuwa ameketi, kiti cha enzi alichokalia. Hiyo ni kweli. Mmesoma hiyo historia ya kanisa. Naam, bwana. Akashuka akaenda kule akiwa na Neno la kweli, akafanya miujiza na ishara; na kuthibitisha, juu ya Neno, kwamba ndivyo alivyokuwa. Walikuwa na uaskofu wao wenyewe, nao wakapata walichotaka, na hicho ndicho tu walichotaka. Lakini Mungu atahakikisha kwamba . . . Huenda

kulikuwako na watoto walioteuliwa mle ndani, naye ilimbidi kwenda kuwachukua. Hiyo ni kweli.

259 Kwa hiyo, kumbukeni, ilikuwa ni nini? Sasa hebu na tusimame hapa kwa dakika moja. Lutu wakati mmoja alikuwa na chaguo la kuwa asiye wa kimadhehebu, yeye mwenyewe. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Wakati mmoja alikuwa na chaguo la kusafiri pamoja na Ibrahimu, lakini kuupenda ulimwengu kukamkaba roho. Hivyo ndivyo ilivyo siku hizi.

260 Pia, kumbukeni, wale huko chini Sodoma kamwe hawakuona mmoja wa hiyo miujiza ya kimbinguni. Walishikwa na upofu. Nako kuhubiri Neno huyapofusha macho ya asiyeamini. Hivyo ndivyo Billy Graham na hao wengine wamefanya, kuyapofusha macho ya hao wasioamini huko nje. Hiyo ni kweli.

261 Sasa huwezi kukana ya kwamba Yesu alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kule Kuja." Hili hapa, katika Biblia. Mnaona? Litakuwa ni jambo lile lile katika Kuja kwake Mwana wa Adamu.

262 Sasa angalieni. Lakini kulikuwa na Mmoja ambaye alikuwa ni Neno. Yeye alikuwa ni Neno, Naye alikaa wapi? Pamoja na aliyeahidiwa, yule mteule. Neno lilibaki na mteule. Nalo Neno la Mungu, leo, litadumu pamoja na Mteule, Uzao wa Kifalme wa Ibrahimu, kwa ahadi.

263 Lilifanya kazi za aina gani? Wakati lilipodhihirishwa yapata miaka mia nane baadaye, katika mfano wa Yesu Kristo, lilifanya kazi zile zile ambazo Huyo alizifanya pale, Neno lilifanya, kwenye lango la hema ya Ibrahimu. Aliketi huku ameelekeza mgongo Wake kwenye hema, akamwambia Ibrahimu jina lake lilikuwa ni Ibrahimu; si Abramu, jinsi lilivyokuwa sikuzote, jina lake. Lakini jina lake lilikuwa Ibrahimu, maana Mungu alikutana naye siku chache kabla ya hapo, akamwambia jina lake lilikuwa Ibrahimu. Kasema, "Yuko wapi mkeo," si S-a-r-a-i. S-a-r-a, "Yu wapi mkeo, Sara?" Kana kwamba Yeye hakujua.

Kasema, "Yuko hemani, nyuma Yako."

264 Akasema, "Nitakurudia." "Mimi," kiwakilishi nafsi, "Nitakurudia, kwa muhula wake," loo, "nawe utampata mtoto huyo mchanga ambaye umemngojea."

265 Mvua ya vuli inakaribia kunyesha. Umeishikilia hiyo Mbegu mle ndani muda mrefu vya kutosha sasa, kwa kuamini. Nawe unamtazamia Mwana ajaye, Naye yuaja. Amina. Hilo ndilo Kanisa halisi leo, mnaona, ile Mbegu teule. "Mmekuwa mkimtazamia, nami nitamtuma kwenu." Amina. Ni kitu gani kilichosema hivyo? Neno.

"Loo," unasema, "ati hilo lilikuwa ni Neno?" Samahani.

266 Ibrahimu alimwita, "Elohimu," Huyo ni Mwenyezi, Yeye anayeishi peke yake. Yeye alikuwa ni Neno, Elohimu.

267 Alikuja wapi? Uzao wa Ibrahimu. Sasa, kumbukeni, Yeye hakuwa na uhusiano wowote na hayo madhehebu. Alikaa moja kwa moja pamoja na Wateule, na kuhubiri, hiyo ni kweli, na kuonyesha ishara. Naye Yesu alisema . . . Sasa ngojeni kidogo tu.

268 Halafu, Sara, nafsini mwake! Angalieni upotovu huo, mnaona. Sasa, kwa kweli, kutokuamini Hilo, Mungu angalimwua papo hapo. Mlijua hilo? Naye akatoka na kukana. Ibrahimu . . . Alicheka kifichifichi, kwa maneno mengine, moyoni mwake. Sasa, kamwe, labda, hata hakutoa tabasamu. Lakini, chini moyoni mwake, ye—ye—yeye kwa namna fulani alicheka kidogo. "Mimi, mwanamke mkongwe, mwenye umri wa miaka mia moja; miaka hamsini tangu kukoma hedhi, wakati wa uhai. Niliishi naye miaka hiyo yote! Vema, hatujaishi kama mume na mke, kwa miaka ishirini na mitano, labda thelathini. Mnaona? Halafu unataka kusema nitapata raha na bwana wangu, Ibrahimu?" Mumewe!

269 Hao ndio aina ya wake nyote mnapaswa kuwa, inawapasa kuwa. Paulo alisema jambo lile lile. Mpende mumeo kiasi hicho. Si kitu fulani chotara hapa nje. Mnaona? Kumbukeni, mawazo yenu . . . Tutalifikia hilo, alasiri ya leo, "tumbo la uzazi, wazo." Kwa hiyo sasa . . . Lakini, katika jambo hilo, alimpenda Ibrahimu sana alimwita bwana wake.

270 "Bwana wangu akiwa mzee, pia, na mimi ni mkongwe, nami nipate raha naye tena?" Naye . . . [Ndugu Branham anaiga kicheko cha kimya cha Sara—Mh.]

Naye Malaika akamwonyesha Ibrahimu kwamba Yeye alikuwa ni Nani, ya kwamba Yeye alikuwa ni Neno. Akasema, "Kwa nini Sara akacheka?"

Kwa hiyo akamwita, naye akasema, "Sikucheka kamwe."

Akasema, "Lakini ulicheka."

271 Ati nini? Hiyo ni neema. Mnaona? Papo hapo, Mungu angalimwua papo hapo, bali asingeweza. Loo! Mnaona ujinga wetu? Angemwua kila mmoja wetu, bali hawezi. Kumwua Sara, ilimbidi kumchukua Ibrahimu, maana Sara alikuwa ni sehemu ya Ibrahimu. Walikuwa mmoja, katika muungano. Na kulichukua Kanisa na kuliangamiza, Yeye hawezi kufanya hivyo, kwa sababu ni sehemu Yake Mwenyewe, Kristo; sehemu Yake, Neno likifanyika mwili. Loo! Neema ya ajabu, jinsi inavyosikika tamu! Asingeweza kufanya hivyo. Mnalipata? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Asingeweza kumwua. Asingeweza kuutoa uhai wake, kwa sababu alikuwa sehemu ya Ibrahimu. Mnaona? Alikuwa nyama ya nyama yake, na mfupa wa mfupa wake.

272 Katika makosa yetu, usiseme, "Vema, ni—nilifanya kosa." La, hilo haliwafanyi . . . Ibrahimu alifanya makosa, pia. Mnaona?

273 Lakini Yeye asingeweza kulichukua Kanisa. Hawezi kumwua Mteule, hawezi kuuchukua uhai wako, kwa sababu wewe ni sehemu Yake. Wewe ni Neno. Neno liko ndani yako. Linajidhihirisha Lenyewe, likijithibitisha Lenyewe; upendo, furaha, amani, uvumilivu. Maneno yote ya Mungu, amini kila moja ya Hayo hufanya kazi, na Mungu akitenda kazi kupitia kwako. Unaona? Wewe ni sehemu ya Neno, ambalo ni Kristo. Nasi tunafundishwa ya kwamba Yeye ni Neno. "Nasi tu nyama ya nyama Yake, na mfupa wa mfupa Wake." Haya basi.

Sasa tunafikia jambo fulani.

274 *Moureh*, *moureh*, mvua, mvua ya masika, mvua ya kupanda imenyesha. Sasa ni jambo gani lililotukia? Ile mvua ya masika ilikuwa ikipandwa; mvua ya vuli ikanyesha. Ilikuwaje? Sodoma na Wasodoma wake ukateketezwa; Ibrahimu akampokea mwana aliyeahidiwa. Yesu alisema, "Acheni vikue pamoja. Magugu yatafungwa, yatafungwa matita, na kuchomwa moto. Gha- . . . Ngano itawekwa ghalani." Mnaona? Mvua ya vuli imekaribia sana. Tutapata . . .

Sitaki kungojea muda mrefu sana juu ya hilo, maana nina kitu kizuri sana hapa nyuma juu ya hilo, najua. Mnaona?

275 Hayo madhehebu mawili yataungana, ya Kipentekoste na haya mengine, nayo yataungana. Lakini Ne—Neno litadumu na Uzao wa Ibrahimu ulioahidiwa, kama lilivyofanya wakati huo. Yesu alisema, "Kama ilivyokuwa wakati huo . . . " Mna masikio ya kusikia, macho ya kuona, ufahamu wa kuelewa? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Yesu alisema, "Kama ilivyokuwa, si imeandikwa . . . " Je, angesema, kama angalikuwa amesimama hapa asubuhi ya leo, hivi si—si angesema hivi, "Si imeandikwa, ya kwamba, kama zile siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu"? Hivi hamwoni yale mavuno mawili yakija hapa, yakipokea mvua yao ya mwisho? Yamekuja kufikia kwenye mvua hiyo ya mwisho. Mnaona? Ndipo ikawaje? Hao malaika na Bwana wakatoweka. Ndipo mvua ikanyesha. Vema.

276 Sasa angalieni kwa makini sana sasa. Sasa, ninaamini nilikuwa kwenye somo hili hapa, naam, juu ya mvua, na vu- . . . kwa ajili ya mvua ya vuli. Ishara zote zinaelekeza kwenye mwisho sasa. Kila mtu, anayeamini Neno la Mungu, anajua hilo. Hata . . .

277 Hebu nisimame kwenye lingine papa hapa. Itanibidi kutaja jina. Simaanishi kuwa fidhuli, lakini sina budi . . . Mimi . . . Nilimwambia Mungu si—si—sitawachezea, Ningekuja papa hapa na kueleza yale hasa niliyojua maishani mwangu mwote, halafu kuna mambo fulani hapa mwishoni nitakayolazimika

kuyazuilia, najua, bali ni—nita—nitawaelezea, kadiri Yeye atakavyoniruhusu kufanya hivyo. Kwanza, mimi . . .

278 Bibi Wood anajua ya kwamba baada ya mimi kupata hili, na kurasa nyingi zaidi kando ya huu, Roho Mtakatifu alisema, "Usifanye hivyo." Je, nilikuita, Bibi Wood, na kusema, "Yeye aliniambia nisifanye hivyo"? Kwa hiyo nikarudi na kuomba. Ndipo usiku huo Yeye alinijia katika ono, kasema, "Nenda ukafanye *hivi*. Chukua Hili na uliweke pale, maana hawataelewa *Hili*. Wakati wa *Hili* bado haujawadia. Weka *Hili* hapa." Nami nikafanya hivyo. Hiyo ni kweli. Mnaona? "Kutii ni bora kuliko dhabihu." Mnaona? Vema. Kutii!

279 Sasa, sasa angalieni. Sisi ni . . . Kuwaonyesha tuko katika wakati wa mwisho, hata wasi- . . . Ule mfano wa mwanamwali mwenye busara na mwanamwali—mwanamwali mpumbavu uko pamoja nasi. Sasa, angalieni. Yule mwanamwali—mwanamwali mpumbavu . . . Samahani. Mwanamwali mpumbavu atakuwa chotara. Mnaona? Alikuwa na Mbegu, bila ya Mafuta, ule unyevu wa kuifanya ikue. Sasa, naye anafanya nini? Hayo—hayo makundi mawili, kundi la Kipentekoste na madhehebu ya ulimwengu (makundi ya kiinjilisti), yanajitokeza pamoja. Mnaona? Kwa sababu gani? Wakielekea Sodoma, mnaona, mnaona, sasa angalieni, kuvuna mavuno haya. Angalieni yule mwanamwali—mwanamwali mpumbavu.

280 Mmeona ya kwamba, hata mmoja wa marafiki zangu wakuu, msomi halisi, mtu ambaye ni mwerevu, mwenye akili, mwerevu sana, Mpentekoste? Nami naona ndugu zangu katika Wafanyabiashara Wakristo wanaimba sifa za Mungu, kwa sababu, mle ndani, wana wahubiri wa Kiepiskopolia, makasisi wa Kikatoliki. Sijui kama watu hao wamelala fofofo. Mnatambua? Wanasema, "Loo, ndilo jambo kuu kuliko yote ulilopata kusikia, Ndugu Branham. Mbona, hawa Waepiskopolia wanakuja huku na kusema wana Roho Mtakatifu. Walinena kwa lugha. Walifanya mambo haya. Utukufu kwa Mungu! Ninawaambia, wana—wana—wananinii tu . . . Mbona, kanisa lao limefanyiwa mapinduzi." Loo, jamani!

281 Enyi ndugu, hivi hamjui hiyo ni nini? Ndiyo ile ishara. Wakati mwanamwali mwenye busara anapotaka Mafuta . . . Ama, yule mwanamwali mpumbavu, hasa, anapotaka Mafuta, na, wakati akiyanunua, huo ndio wakati Bwana-arusi anapokuja. Loo, enyi Wapentekoste, kuna shida gani? Vema, hamwezi kuliona isipokuwa Mungu awaonyeshe, hilo ni jambo moja hakika. Kama—kama hukuzaliwa huko nyuma, ukachaguliwa kwake tangu zamani, utalikosa. "Heri masikio yanayoweza kusikia." Heri mioyo inayoweza kuelewa, kwa maana wakati umekaribia. Kila ishara inaelekeza kwake. Mnaona?

Angalia ni miamsho ya namna gani waliyo nayo. Miamsho mikubwa, wamekuwa nayo. Inaonekana ni mizuri, sivyo?

Mnasema, "Vema, Ndugu Branham, sasa umetusukumia kwenye tawi." Hapo ndipo nilipowataka.

"Mtajuaje mema na mabaya?"

282 Lipe jaribio la Neno. Hiyo ndiyo njia ya kujua kama ni kweli ama si kweli. Hiyo ni, li—lipe tu jaribio la Neno, uone linachosema kuhusu Neno. Roho yoyote, angalia inalosema kuhusu Neno. Kama ikilikana Neno, si ya Mungu. Unaona? Haidhuru ni nini, kama ikilikana Neno, si ya Mungu. Angalieni, ifanyie jaribio la Neno, uone kitakachotukia.

283 Yesu alituonya juu ya mambo haya. Mathayo mlango wa 24 na kifungu cha 35, ninataka tu kurejea kwenye hilo, maana, kwa ajili ya kanda. Hebu kidogo sasa. Hatuna ila yapata dakika ishirini zaidi kabla ya kuondoka, na—nami nina hakika hata hatutafikia theluthi moja ya kumalizia, lakini sina budi kusoma hili kwa vyovyote vile. Mnaona? Mathayo 24:35. Sasa sikilizeni kwa makini sana yale Yesu aliyosema. Sasa, jinsi hii. . .Jinsi alivyotwambia, ya kwamba, "Roho hizo mbili zingefanana sana, zingewapoteza walio Wateule. . . " Mnajua hilo. Sivyo? Sasa, je, itakuwa kweli? Naam, bwana. Mathayo 24:35 inasema:

> Mbingu *na nchi zitapita, lakini maneno yangu hayatapita kamwe.*

284 Mnaona? Sasa yeye. . .Kwamba roho hizo mbili zinafanana sana, sasa haina budi kuwa hivyo. Haina budi kuwa hivyo. Dhe—dhehebu la Kipentekoste halina budi kutenda halisi sana, kama la halisi, mpaka Yesu akasema ya kwamba ni Wateule tu ambao hawatadanganywa. Hilo nusura liniue. Lakini, ndugu zangu wa kimadhehebu, hivi hamwezi kuona ni kwa nini—ni kwa nini nimefanya yale niliyofanya? Mnaona? "Karibu sana, hata ingewadanganya walio Wateule, kama yamkini."

285 Lakini, kwa Wateule, walioteuliwa kwa ajili ya Uzima wa Milele. Sasa, nena kuhusu kulifikia hili, tutalifikia baada ya kitambo kidogo, tuligonge kweli kweli. Mnaona? Ninii. . . Kumbukeni, ni, Wateule ndio pekee watakaolishika.

"Vema," mnasema, "unajuaje kwamba huko sahihi?"

Basi nijaribuni kwa Neno. Hima, lijaribuni dhehebu lenu kwa Neno hili. Hebu tuone ni nani aliye sahihi. "Thibitisheni mambo yote," Biblia ilisema.

Mnasema, "Haileti tofauti yoyote, kubatizwa *hivi* ama *vile*." Inaleta tofauti. Hivyo ndivyo Shetani alivyomwambia Hawa.

286 Mtu fulani tayari alikuwa amebatizwa, katika Matendo 19. Mkristo mzuri aliwabatiza, pia, Yohana Mbatizaji. Paulo akasema, "Je, mmempokea Roho Mtakatifu tangu mlipoamini?" Tulisema. . .

Akasema, “Hatujui kama kuna Roho Mtakatifu.”

Kasema, “Basi mlibatizwaje?” Kama mngalilipata, mngalilijua. Mnaona? Kasema, “Mngewezaje . . . Mli—mlibatizwaje?”

Akasema, “Kwa Yohana, yule mtu mashuhuri aliyembatiza Yesu.”

287 Paulo akasema, “Hilo halitafaa kitu sasa. Maana, Yohana kamwe hakubatiza, ila kwa toba, si kwa ondoleo la dhambi; Dhabihu haikuwa imetolewa.” Nao waliposikia haya, wakabatizwa tena, katika Jina la Yesu Kristo.

Vipi kama Musa alisema . . .

Mungu alisema, “Vua viatu vyako, Musa.”

288 Akasema, “Unajua, nilivikaza kwa nguvu kidogo asubuhi ya leo, Bwana. Nitaonyesha heshima zaidi, nitavua kofia yangu”? Hilo lisingefaa kitu. Kamwe hakusema kofia. Alisema viatu.

289 Na huyo ni ibilisi anayejaribu kulipaka Hilo chokaa, kama alivyofanya na mama Hawa. Kila Neno ni Kweli, jinsi tu Mungu ameliandika pale. Hivyo ndivyo ninavyoliamini.

290 Sasa, unaweza kuendelea. Kama ukisema, “Vema, tunayo Kweli,” vema, endelea basi. Hilo ni sawa. Iwapo wewe ni kipofu hivyo, endelea moja kwa moja, ukiyumbayumba gizani. Hili ndilo Neno litakalokuhukumu, ndugu, si kanuni yako ya imani.

291 Loo, inaonekana nzuri. Naam, bwana, inaonekana nzuri. Nawe unasema, “Vema, Ndugu Branham, ngoja kidogo. Mungu abarikiwe, nimewaona wakienda huko nje na kuwaponya wagonjwa.” Loo, hakika, nami pia. “Loo, niliwaona wakinena kwa lugha.” Naam, bwana, nami pia.

292 Sijawahi kuamini, wala hakuna mtu anayeweza kuthibitisha jambo hilo kwa Neno la Mungu, ya kwamba ishara ya kwanza ya Roho Mtakatifu ni kunena kwa lugha. Ninamtaka mtu huyo aje afanye hivyo. Nimelipinga hilo wakati wote. Ninaamini katika kunena kwa lugha. Naam, bwana. Lakini nimeona pepo wakinena kwa lugha. Wachawi na walozi hunena kwa lugha, na kuzifasiri, wakikana kulikuwa na kitu kama Yesu Kristo. Nimewaona watu wakinena kwa lugha, wakiishi na mke wa mtu mwingine; wanasimama, wananiangalia moja kwa moja usoni, ono mbele zake; nikamwita kando, na kumfanya ashuhudie hilo. Ati nanyi mnaita hilo Roho Mtakatifu? Loo, naam.

Mnasema, “Vema, Ndugu Branham, hivi huamini Roho Mtakatifu hunena kwa lugha?” Naam, bwana. Lakini mpe jaribio la Neno. Mnaona?

293 Yane na Yambre walifanya miujiza. Hiyo ni kweli. Sivyo? Naam, bwana. Yane na Yambre, wakati Musa aliposhuka kwenda Misri, kila kitu ambacho Musa alifanya katika njia ya ishara, Yane na Yambre, hao wachawi wawili, wangeweza

kuleta jambo lile lile. Pepo wawili! Musa angesema, "Viroboto!" Wakasema, "Viroboto!" Musa akasema, "Fimbo ardhini!" Wakasema, "Fimbo ardhini!" "Nyoka!" "Nyoka!" Hiyo ni kweli. Wangeweza kutenda miujiza.

294 Biblia ilisema, ya kwamba, "Katika siku za mwisho, ya kwamba, pepo watainuka, wakifanya miujiza, nao wangewadanganya watu." Ni vigumu sana, ndugu, bali hamna budi kuijua Kweli.

295 Yesu alisema, "Wengi watakuja Kwangu siku hiyo na kusema, 'Bwana, Bwana, si nimetenda *hili*, na kutenda *lile*, na kutenda *lile*, na kadhalika, katika Jina Lako?'" Yeye atasema, "Ondokeni Kwangu, ninyi mtendao maovu." Uovu ni nini? Kitu ambacho unajua kwamba ni kibaya, nawe unakifanya, kwa vyovyote vile. Nawe unajua ya kwamba Neno la Mungu ni kweli. Kwa nini unajifanya mnafiki? Kwa sababu ya dhehebu lako, na kuchukua kidogo hapa wala hutachukua hayo mengine. Enyi mtendao maovu! Kasema, "Ondokeni Kwangu. Hata siwakujua kamwe." Sasa, hiyo ni . . . Ama upitie kwa shida kuzimuni humu au baadaye. Kwa hiyo, mnaona? Sasa, kumbukeni, hiyo ni kweli. Hivyo ndivyo Yesu alivyosema.

296 Yane na Yambre walipingana na Musa. Kumbukeni. Nayo Biblia ilisema, "Kama hao walivyopingana na Musa, katika siku za mwisho wangetokea tena, hizo roho, tena." Ati nini? Kabla tu ya ule ukombozi wa watu. Haleluya! Wakati wa ukombozi umewadia.

297 Yesu alisema, katika Mathayo 24 pale, ya—ya kwamba, "Wangewapoteza walio Wateule, kama yamkini." Wateule tu ndio watakaolipata, mmoja tu *hapa* na *pale*. "Walio Wateule, kama yamkini."

298 "Kama vile Yane na Yambre walivyoshindana na Musa, vivyo hivyo na watu hawa walioharibika akili zao kwa mambo ya Neno, kwa Kweli." Nalo Neno ni Kweli. Hiyo ni kweli? Sasa, haya si maziwa machunda, rafiki. Mnaona? Angalieni. Wao . . .

299 Biblia ilisema, Yesu alisema, ya kwamba, "Watafanana sana hata wangewapoteza walio Wateule, kama yamkini." Lakini haiwezekani. Mbegu hiyo itaanguka hapo, kwa sababu ilikusudiwa tangu zamani kuanguka hapo. Mbegu zimetoka; madhehebu yamepanda. Neno limepandwa. Mnaona?

300 Nao Yane na Yambre, wao, hao watu, Biblia ilisema pepo hawa wangetokea katika siku za mwisho nao wangewadanganya watu, kwa miujiza hii na ishara walizoweza kufanya. Utajuaje tofauti yake? Neno. Lile . . . Hata Agano la Kale lilisema, "Wasiponena kulingana na torati na manabii, hamna Uzima ndani yao," kama wakikana jambo moja.

301 Basi nionyeshe mtu mmoja aliyewahi kubatizwa, kwa kutumia cheo cha jina la "Baba, Mwana, Roho Mtakatifu." Kwa nini mnakitumia basi? Kanuni ya imani, enyi watoto chotara,

mliokufa, watoto haramu, mliokufa maradufu, mliong'olewa kwa mizizi! "Na kila shina ambalo ninii Yangu. . . Kila mmea ambao Baba Yangu wa Mbinguni hajaupanda, utang'olewa. Mbingu na nchi zitapita, bali Neno Langu halitapita kamwe," alisema Yesu.

302 Sasa mnaona ni kwa nini nimesimama jinsi nilivyosimama? Nionyesheni mahali pamoja, kama si laana kwa mwanamke kukata nywele zake. Haya basi. Kisha mnanizozea.

303 Halafu watu wanasema, "Ndugu Branham ni nabii. Loo, mwaminini maadamu anazungumza na watu, kuwaambia dhambi zao, na mambo kama hayo. Lakini anapoanza kufundisha, msiamini Hilo." Vema, maskini mnafiki wewe. Hujui chochote. Hivi Biblia haisemi, "Neno la Bwana liliwajia manabii"? Sijiiti nabii. Mimi si nabii; lakini mlisema hivyo. Ninasema yale mliyosema, na kisha mnageuka na kusema jambo kama hilo? Msiseme hamkusema. Hata ninalo limerekodiwa kwenye kanda, mahali mlipolisemea. Hamkujua hilo, sivyo? Nataka tu mseme hamkusema, wakati mmoja. Hayo tu ndiyo ninayotaka mseme. Acha sauti yako inene na wewe tena.

304 "Kama vile Yane na Yambre walivyoshindana na Musa." Watenda miujiza, lakini Neno lilikuwa wapi, Neno la kweli? Hao hapo jamaa wakifanya miujiza. Hao hapo jamaa walioweza kufanya kila kitu katika fani ya miujiza ambao. . .

305 Lakini kulikuwa na manabii wawili waliotiwa mafuta wamesimama pale, ama nabii mmoja na msaidizi wake. Kulikuwa na nabii aliyetiwa mafuta jina lake Musa, aliyesimama pale, alikuwa na BWANA ASEMA HIVI. Hatimaye, yote yalidhihirishwa, kabla ya ule ukombozi. Hiyo ni kweli? Wale waliojiita watenda miujiza walikufa moja kwa moja.

306 Na kile wanachojaribu kufanya, wanajaribu ku—kujibunia mvua ya vuli. Upuuzi. Mbona, mvua ya vuli itaenea ulimwenguni, ndugu. Kumekuwako na mvua ya masika, kupanda maneno. Hiyo ni kweli. Sasa mtaona kile mvua ya vuli itakachotoa. Mtaona kwamba kutakuwako na ushirikiano. Wapentekoste na makundi yote watakusanyika pamoja, nao watawafungia milango hao jamaa ambao hawatausikiliza. Hata hutaruhusiwa kufungua kinywa chako. Kweli. Hapo ndipo atakapokuja. Hapo ndipo atakapoonyesha. Hapo ndipo utakapoona mvua. Loo, jamani! Kaa kimya. Nyamaza. Uh-huh. Liachilie. Loo!

307 Lakini Neno lilikuwa pamoja na nabii huyo aliyetiwa mafuta, kwa sababu Neno la Bwana lilimjia nabii. Sasa, Mungu habadilishi mfumo Wake. La, la. Yeye kamwe hakubadilisha mfumo Wake.

308 Sasa, ilikuwa ni nini? Hapo walisimama watatu tena. Hao hapo wakatoka Yane na Yambre, wakifanya miujiza. Kama vile walivyoshuka, Sodoma, wakafanya maskini mwujiza mmoja,

wakawapofusha watu. Mnaona? Hapo alisimama Ibrahimu mtiwa mafuta, pamoja na Mungu, na msaidizi wake Sara. Hiyo ni kweli? Hapa walisimama Yane na Yambre, wakifanya miujiza, chochote ambacho Musa angeweza kufanya katika ishara ya miujiza, ishara. Hapo lilisimama Neno lililotiwa mafuta, nabii, pamoja na msaidizi wake, msaidizi wake.

309 Loo, laiti ningaliweza kuhubiri juu ya hilo sasa, kwa yapata saa mbili nzuri. Vema. Katika Mwanzo 1, kumbukeni, "Kila mbegu kwa jinsi yake." Haina budi kuwa hivyo daima. Hiyo hapo mifano hiyo yote.

310 Mtu ambaye angesema, angeweza kuamini, ya kwamba Kanisa litapitia kwenye wakati wa Dhiki, sijui ungepata wapi mbegu kwa ajili ya hilo? Wakati hata . . . "Vema," unasema, "Ninaamini inasema *hivi*, kwamba watafanya." Hilo ni sawa. Hivi mliona huko nyuma ambako mvua ilinyesha wakati ule mwingine? Ilinyesha wapi? Nuhu alikuwa ndani ya safina kabla ya hukumu kuanza. Sodoma; Lutu alikuwa ametoka Sodoma kabla halijatukia. Mnaona? Ni hakika. Sisi ni . . .

311 Hatupitii wakati wowote wa Dhiki. Utaondoka katika Unyakuo, moja ya siku hizi. Bila shaka. Tunaninii . . . Kwa nini ikubidi kuhukumiwa? Yeye alistahimili dhiki yangu; Yesu Kristo. Hapo ndipo dhiki yangu ilipotukia, papo hapo. Naam. Nilimkubali, na niko huru. "Nionapo Damu, nitapita juu yenu." Hiyo ni kweli. Musa alilindwa salama pamoja na Israeli, wakati ile dhiki iliposhuka. Hiyo ni kweli. Vema.

312 Kila mbegu haina budi kuja kwa jinsi yake. "Mungu alimfanya mwanadamu kwa mfano Wake, kwa jinsi Yake," apate kuwa Neno Lake duniani. Alilidhihirisha katika Yesu Kristo. Ilikuwa ni nini? Mungu alikuwa ndani ya Kristo. Huyo ni Mtu kwa jinsi Yake. Mnaona? Wakati Mungu, ambaye ni Neno . . . Ni wangapi wanaojua Yeye ni Neno? Wakati Neno lilipokuwa ndani ya Kristo, Mtu, Mtu wa kibinadamu, likijidhihirisha Lenyewe kupitia Kwake, huyo alikuwa ni Mungu, Neno, katika Kristo, likijidhihirisha Lenyewe.

313 "Naye Mungu, hapo mwanzo, alimfanya mtu kwa mfano Wake Mwenyewe." Basi mtu wa namna hiyo ndiye Mungu anayemfanya siku hizi. Seminari na kiatamizi cha kuangulia hutoa lundo la machotara, mnaona, hizo shule. Lakini Mungu anapomwita mtu, yeye yuko katika mfano Wake Mwenyewe, Neno lililofanywa hai ndani yake. Hiyo ni kweli. Huyo hapo. Huyo ndiye mtu wa Mungu, mtu katika mfano Wake Mwenyewe, katika mfano Wake hasa. Naye Yesu alisema, ya kwamba, "Atafanya kazi nizifanyazo Mimi."

314 Kwa hiyo, "Mungu alimfanya mtu kwa mfano Wake Mwenyewe, kwa jinsi Yake." Jinsi Yake! Jinsi Yake ni nini? Neno. Yeye ni Neno. Basi kama mtu akililikana Neno la Mungu, anawezaje kuwa katika mfano wa Mungu? Ulizeni tu hilo

swali. Jiulize. Unawezaje kuwa katika mfano wa Mungu na kulikana Neno la Mungu, wakati Neno ndilo chapa ya nafsi Yake Mwenyewe?

"Loo," anasema, "Halimaanishi Hilo."

315 Ati chapa ya nafsi ya Mungu iseme, "Loo, nililisema, bali kweli sikulimaanisha. Ni—nilikosea hapo. Ni—nitalighairi. Hilo lilikuwa ni kwa ajili ya wakati mwingine. Sikulimaanisha"? Loo, rehema! Takataka, kinyaa cha ibilisi, ambacho alimlisha Hawa. Usimwache ajaribu kushindilia hayo shingoni mwa Mteule, hata hivyo. La, bwana. Hawataamini hilo. "Njoo tu ujiunge na genge letu." Usijiunge na chochote!

316 Huna budi kuzaliwa, sio kujiunga; kiumbe kipya, naam, katika mfano Wake Mwenyewe, wa jinsi Yake, kuwa—kuwa Neno Lake lililodhihirishwa duniani. Sasa, Yesu alikuwa Neno la Mungu lililodhihirishwa. Mnaamini hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Basi tunapaswa kuwa nini? Wana wa Mungu, pia, pamoja na Neno lililodhihirishwa Kanisani, tukiendelea. Huo ndio Mwili wa kisiri wa Kristo, ukiendeleza kazi zile zile ambazo Yesu alifanya alipokuwa hapa duniani. Mnaona? Hao ndio wa jinsi Yake.

317 Sasa, unaweza kuwa na wa Kilutheri kwa jinsi ya Kilutheri, Methodisti kwa jinsi ya Methodisti, Katoliki kwa jinsi ya Katoliki, Pentekoste kwa jinsi yake, Umoja kwa jinsi yake, Utatu kwa jinsi yake.

318 Lakini kama wewe ni wa jinsi ya Mungu, hilo ni tofauti, unaona, wewe ni chapa ya Neno likijidhihirisha Lenyewe. Loo, jamani! Mbona, halina budi. Kama maji yakiimwagikia, haina budi kuzaa. Ndipo, ndipo akampa Uzazi, mfano, naye . . . baada ya . . . Mungu akamfanya mtu kwa mfano Wake Mwenyewe. Kamwe si—sidhani nina wakati wa tamshi hili linalofuata. Ni zuri sana. Lakini si—sitaki kuninii . . . Maneno yote ya Mungu ni mazuri sana, mnaona. Basi angalieni hapa mahali nilipopaswa kuwa, wa—wakati wa chakula cha jioni. Niko tu karibu umbali *huo* kutoka kwake, karibu moja juu ya sita yake. Hum. Vema. Naweza . . . Hebu tuyaachie tu hapo. Mwasemaje? Ndipo sisi . . . Naam. Ni wangapi wanaoweza kurudi alasiri ya leo? Inua mkono wako. Naam. Naam. Vema. Sitaki kuwaweka muda mrefu sana. Nita—nitaninii tu . . . Sitaki kuwachosha. Na sasa nitaninii . . . Sasa, ninyi wavulana wa kanda ziacheni tu kanda ziendelee kwa dakika moja, nami nita—nitaikatiza hii katika dakika moja, mimi mwenyewe. Vema, bwana. Sasa sisi . . .

319 Wazo letu la mwisho hapa lilikuwa, kwamba, Mungu alimfanya mtu kwa mfano Wake Mwenyewe, kwa jinsi Yake. Mungu akamfanya mtu, kwa jinsi Yake. Mnalipata? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Mtu, kwa jinsi Yake. Vema, Yeye alikuwa ni Mtu wa aina gani? Kama utaangalia nyuma uone kile alichokuwa wakati alipofanyika mwili, hiyo ndiyo aina ya mtu

anayemfanya. Hiyo ni kweli? Mtu, kwa jinsi Yake. Amina. Hiyo ni kweli. Sivyo? Huyo ni mtu wa jinsi Yake.

320 Alisema, wakati mwingine, wakati mmoja, kwa mtu fulani, "Unaupendeza moyo Wangu Mwenyewe." Mtu aliyeupendeza moyo Wake, Daudi. Mnakumbuka hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Roho wa Mungu katika Daudi. Daudi, mfalme aliyekataliwa. Sikuzote mtiwa mafuta hukataliwa. Daudi, mfalme aliyekataliwa, alipanda mlimani wakati watu wake mwenyewe . . . Nitahubiri juu ya hili kwa dakika hizi tatu zijazo. Wakati watu wa Daudi mwenyewe wanapaswa kuninii . . . Watu wa jinsi yake walimwondoa mamlakani, mwanawe mwenyewe, na kumfukuza kutoka kwenye kiti cha enzi.

321 Daudi alishuka akaenda kule, na hata mmoja wao akaja huko nje akimtemea mate, mfalme huyo aliyetiwa mafuta. Ndipo maskini jamaa huyu akaja pale, amelemaa katika mafudnisho yake. Biblia ilisema alikuwa mlemavu, mwajua. Naye akaenda, akimtemea mate mfalme huyo. Mtazameni Kristo. Akimtemea mate; yule mjumbe kando yake, (malaika, akiwakilisha), akachomoa upanga, kasema, "Ati kichwa cha mbwa huyo kikae juu yake; anayemtemea mate mfalme huyo?" Malaika akasema, "Nitamwua."

322 Daudi akasema, "Rudisha upanga wako. Sina budi kufanya jambo hili." Akapanda juu ya kilima, cha Yerusalemu, akaangalia chini, mfalme aliyekataliwa, naye akalia.

323 Miaka mia nane kutoka hapo, Mwana wa Daudi, Roho aliyekuwa katika Daudi, kwa sehemu, akasimama juu ya kilima kile kile; Mfalme aliyekataliwa, akitemewa mate na kudhihakiwa. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Ninaweza kuwazia Mungu alisema . . . Malaika wakitembea pale pamoja Naye, wakati alipopanda kwenda Kalvari namna hiyo. "Je, kichwa cha mbwa yule kikae juu yake?"

"Achana naye." Loo, jamani!

324 Wakati unakuja. Lakini vipi kuhusu Daudi wakati aliporudi? Hadithi ilibadilika. Daudi alikuja akiingia kwa mwendo wa ushindi. Jamaa huyu akakimbia, akipiga makelele apate rehema. Hakika.

Waacheni. Yeye atakuja siku moja, katika mamlaka. Ndipo hao, waliokuwa wakicheka, watageuka upande mwingine. Hiyo ni kweli. Waacheni tu.

Lakini, Mungu alisema, "Daudi, wewe ni mtu anayeupendeza moyo Wangu." Mungu anapomwumba mtu, yeye ni wa jinsi Yake.

325 Daudi alisema, "Moyoni mwangu nimelificha Neno Lako, nisije nikakutenda dhambi, Bwana." Kitu pekee alichohitaji kilikuwa ni mvua. Daudi angalikuwa sawa kama tu angalipata mvua hiyo, lakini Roho Mtakatifu hakuwa ametolewa bado.

Alikuwa na Neno, nalo Neno lilikuwa ndani yake, naye angeweza kujua jambo Hilo. Akasema, "Nimelificha moyoni mwangu, Bwana. Halitachanua na kutenda kama linavyopaswa kufanya, bali nimelificha mle, Bwana. Nimelificha mle." Lakini wakati Yesu alipokuja, ambaye alikuwa ni Neno lililodhihirishwa, alitoa Seli Zazi ya Uhai kutoka Kwake, akairudisha kwenye Neno sasa. Na kama kikombe cha Daudi kilifurika, chetu kinapaswa kufanya nini? Hakika. Bila Roho . . . Amina. Yeye si ni wa ajabu? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Mnampenda? ["Amina."]

> Yeye si ni wa ajabu, wa ajabu, wa ajabu?
> Hivi Yesu Bwana wangu si ni wa ajabu?
> Macho yameona, masikio yamesikia, yale yaliyoandikwa katika Neno la Mungu;
> Hivi Yesu Bwana wangu si ni wa ajabu?

Sivyo? Ni wangapi wanaoupenda? Ni wangapi wanaompenda? Loo, jamani! Ajabu!

326 Sasa, ni kali, rafiki. Ni kali sana. Simaanishi kuwa hivyo, mimi mwenyewe. Naam. Natumaini mnaelewa hilo. Mnaona? Lakini leo hii ninatoa tamshi la sababu ya kufanya mambo ambayo nimefanya.

327 Sasa, kwa uchambuzi mdogo tu, kabla hatujafumukana kwa ajili ya . . . kwa ajili ya chakula cha mchana, ni hili. Ninawatakeni mjue ya kwamba mimi . . . Hili limekuwa ndilo lengo langu na kusudi langu, ni Neno la Mungu. Lengo langu ni kumpendeza Yeye. Wala siwezi kusikiliza kila kitu na kuamini Neno la Mungu, wala siwezi kusikiliza kila kitu na kumpendeza Mungu. Lengo langu ni kulijua Neno Lake na kumpendeza Mungu, kwa kumtumikia kwa Neno Lake. Si kwamba nina chochote dhidi ya . . .

328 Sasa, kila mtu humu ndani aliyezaliwa kwa Roho wa Mungu, aliye katika kundi Teule, labda wakati mmoja alikuwa Mmethodisti, Mbaptisti, Mpresbiteri, Mpentekoste, ama kitu kama hicho, mahali fulani. Sasa, mnajua jambo hilo. Mnajua hilo. Kwa hiyo basi, mnaona, mnaposema, "Waendeeni," hivyo ndivyo inavyowapasa kufanya. Kuna mtu mle ndani, kama utapanda Mbegu, kutakuwa na mavuno, siku moja. Itaanguka . . .

329 Baadhi yao watapitia hapo, waseme, "Aa, yeye si kitu ila . . . Yeye ni mdanganyifu." Hivi hawakusema jambo lile lile kumhusu Bwana wetu? "Hakuna kitu Hapo." Vema, basi, kwa nini usilichunguze pamoja nami? "Si kitu ila mdanganyifu!" Mnaona? Basi lichunguze kwa Neno. Unaona? Kama si Neno, basi linadanganya. Unaona? Sasa, kama theolojia yako ni tofauti na Neno, basi si ya kweli. Unaona?

Sasa, wengine watapitia hapo na kusema, “Vema, unajua nini, ninaamini nitalijaribu kwa muda kidogo.” Utasongwa. Hiyo ni kweli. Unaona?

330 Lakini unapojifanya tupu kabisa, useme, “Bwana Yesu, si mimi tena, bali Wewe, tangu sasa na kuendelea.” Unaona? Ndipo litazaa mara mia moja. Mnaamini hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Ninaliamini, pia, kwa—kwa uhuru na haki kwa wote. Hiyo ni kweli. Naam, bwana. Ninatoa ahadi ya utii wangu kwa Bwana wangu, mnaona, kuhubiri Neno Lake na kusimama juu ya Kweli Yake.

331 Kama ikigharimu maisha yangu, ningali ninaendelea vivyo hivyo. Kwa kuwa ningeninii . . . Lingekuwa ni jambo kubwa kwangu, si kutaka kulifanya, lakini kama ilinibidi kulifanya, nitachanganya damu yangu katika dunia hii, kama wale wanaochanganya damu yao kwa ajili ya jambo lile lile. Kama wale waliokufa katika mashimo ya simba; kama wale waliokufa misalabani; wale waliokatwa kwa misumeno; waliofukuzwa kutoka kwenye madhehebu yao; wakazunguka-zunguka huku wamevaa ngozi za kondoo na ngozi za mbuzi; na walikuwa maskini. Ingekuwa ni majaliwa makubwa kwangu. Kama vile wanafunzi wa Kristo waliporudi, nao walikuwa wamehesabu yote kuwa ni furaha kwa sababu waliweza kustahimili shutuma iliyoletwa juu ya Jina Lake. Wangeweza kuteseka hayo kwa ajili Yake, mateso yao madogo. Sitaki kuteseka. Hakuna mtu anayetaka kuteseka.

332 Ningetaka kushikana mikono na madhehebu yote, niseme, “Ndugu, hebu twendeni.” Ningependa kufanya hivyo. Nikifanya hivyo, ninaondoa mkono wangu kutoka kwa Wake. Na iwe mbali nami kamwe kufanya hivyo. Kama nikisimama peke yangu, ninasimama pamoja Naye na Neno Lake. Kwa kuwa, kama Eddie Perronet alivyosema:

> Juu ya Kristo Mwamba imara nasimama;
> Ardhi nyingine yote ni mchanga udidimiao.

Naye Kristo ni Neno. “Hapo mwanzo . . . ”

333 Na ni kitu gani? Kila neno huzaa. “Kila mbegu huzaa kwa jinsi yake.” Mbegu ya kimadhehebu itazaa kwa jinsi yake. Madhehebu ya Kipentekoste yatazaa kwa jinsi yake. Baptisti itazaa kwa jinsi yake. Ni kitu gani? Shirika, daima, daima. Tutaonyesha, alasiri ya leo, Mungu akipenda, jinsi hao walivyoanza, na kilichosababisha jambo hilo, na ambapo Biblia ilisema wangefanya hivyo, na jinsi watakavyoishia, jinsi hasa mwisho utakavokuwa.

334 Mungu awabariki nyote, ndani ya gari. Wengi, ninyi nyote mlio kwenye magari, ambao msingeweza kuingia, sikilizeni kupitia maikrofoni hii. Na Mungu awabariki ninyi mnaosimama karibu na kuta hizi; nanyi mlioketi hapa asubuhi ya leo.

335 Nami ninatumaini ya kwamba, kwa neema ya Mungu, sijasababisha kosa lolote, bali ninajiweka wazi. Sasa, kama mnaamini jambo lile lile ambalo nimesema asubuhi ya leo, si mngesimama vivyo hivyo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Hakika, mngesimama.

Na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo tu.

336 Baba wa Mbinguni mwenye rehema, hatujaribu kufunga mkutano, bali kuusimamisha tu kwa mapumziko mafupi, kwa dakika chache. Na sasa jalia mbegu hizi ambazo zimepandwa asubuhi ya leo, jalia ziwe zimeanguka kwenye udongo mzuri, wenye rutuba. Jalia zizae kwa wingi, Bwana, wingi wa Uzima wa Milele. Sasa tunaomba, Baba, ya kwamba mbegu hizi zilizopandwa zitakuwa zimekaa, zikingojea mvua ya vuli kunyesha. Kungojea! "Wale wamngojeao Bwana, watapata nguvu mpya." Mungu, jalia tusilitangulie Neno; tudumu pamoja na Neno. Tujalie, Bwana. Tubariki sasa.

337 Na wale wanaotoka kwenda kula, ninaomba ya kwamba utawapa chakula chao cha mchana, na—na kubariki chakula chao, na kuwapa nguvu, na kuwarudisha alasiri ya leo, mapema sana, Bwana. Jalia wawe wameketi hapa hekaluni, wakingojea.

338 Pia naomba unisaidie ninapoenda kuomba, kisha nirudi. Ninaomba ya kwamba utanipaka mafuta upya alasiri ya leo. Tujalie, Bwana, ili niweze kuleta kile ninachoamini kuwa ni Neno Lako, kwa watu. Tujalie, Baba.

339 Ninaomba ya kwamba utambariki mchungaji wetu mpendwa, Ndugu Neville, ndugu yetu wa thamani. Dakika chache, kuingia majini hapa, pamoja na kundi la watu, kuingia katika ubatizo.

340 Na, Baba, kukiwapo na yeyote hapa asubuhi ya leo, ambaye amebatizwa vinginevyo mbali na ubatizo wa Kikristo, ambao mtumishi Wako mashuhuri Paulo . . . Naye alisema, ya kwamba alikuwa na Neno la Mungu ndani yake. Naye akasema, "Kama mtu ama malaika, hata Malaika akishuka kutoka Mbinguni," kama vile Shetani alivyokuwa katika umbo la Malaika, "akishuka na kusema lolote tofauti na lile alilosema, na alaaniwe." Baba, tunajua ya kwamba hayo yameandikwa katika Maandiko. Nami naomba, Baba, ya kwamba, ya kwamba lita—litazama mioyoni mwao, ya kwamba Paulo ndiye hasa aliyewafanya watu, ambao hawakuwa wamebatizwa katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zao, yeye ndiye aliyeagiza wabatizwe tena. Jalia liwaendee watu, Baba. Jalia watambue ya kwamba, ibada hii ya ubatizo inakaribia.

341 Jalia watambue ya kwamba hiyo ni Kweli, wakijua ya kwamba hawawezi kutoa Neno moja katika Maandiko, kuunga mkono wazo lao la utatu wa Mungu watatu. Baba, sisi, bila shaka, tunaamini Wewe ni utatu wa ofisi, za Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu. Hakika kabisa tunaamini hilo, Bwana, bali

sio kukufanya Wewe Miungu watatu. Kukufanya Mungu mmoja aliyetumikia ofisi tatu, Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu pia, nalo Jina la Mungu huyo liliitwa Yesu Kristo. Sasa, hilo ni Jina la Baba, Mwana, Roho Mtakatifu.

342 Baba, jalia watu waone jambo hilo na wawe watiifu kwa ubatizo wa maji, kwa ondoleo la dhambi zao. Na jalia maneno haya machache, kwa ajili ya ubatizo, yazame sana moyoni mwa kila mtu, kwa kuwa hatujui tuna muda gani zaidi, Baba. Kunakaribia sana.

343 Adui, kama tunavyotarajia kuzungumzia alasiri ya leo, anaingia kilindi zaidi, anazidi kuwa jasiri, wakati wote. Tangu wamekikalia kiti cha enzi. Wanaingia moja kwa moja. Bwana, tunaona jambo hilo kila mahali. Si ukomunisti, Bwana. Jalia watu waweze kuelewa ya kwamba ni Urumi, "Yule maskini mama kahaba na makahaba wake." Nasi tunawaona, Bwana, wakija, sanamu ya mnyama. Na sisi hapa.

Baba Mungu, uturehemu sasa. Basi jalia sote tuingie kwenye usalama, ndani ya Safina, na tuwe tayari kwa ajili ya mvua ya vuli. Tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

344 Sasa kwenu ninyi mlio humu jengoni, sasa, kama ukitaka kuponyoka ukapate chakula, vema, na, ukitaka, kisha urudi, uingie hapa upesi uwezavyo baada ya ibada.

345 Sasa hebu na tusimame kidogo tu. Hebu—hebu tusimame, pamoja. Ni wangapi wanaoliamini Neno la Bwana? Inua mkono wako. Amina. Loo, Bwana ashukuriwe! *Loo, Jinsi ninavyompenda Yesu.*

Loo, jinsi ninavyompenda Yesu,

Bwana Yesu, bariki leso hizi. Wape, Bwana, upako wa Roho . . .? . . . katika Jina la Yesu.

# *Neno Lililonenwa Ndilo Mbegu Ya Asili 2*

Vema, sasa, hilo ni sawa, Ndugu Kidd. Hilo ni zuri sana. Mahali tulipo hasa. [Ndugu Kidd anamwambia Ndugu Branham jambo fulani—Mh.] Amina. Anataka kusema neno juu ya uponyaji wake.

2 [Ndugu Kidd anasema, "Naam. Mimi ndiye yule jamaa aliyeponywa, miaka miwili iliyopita. Nami nimefanywa tayari nusu nipate kuwaacha. Mama akampigia simu Ndugu Branham, naye akaja, yeye na—yeye na mwanawe. Nao wakaondoka nyumbani hapa saa nane, ndipo akaja na kuniombea. Jinsi... Sikuwa na hisia yoyote kuanzia—kuanzia—kuanzia kiunoni mwangu, kwenda chini, hata kidogo. Ndipo saa moja baada ya yeye kuniombea, alikuwa ameondoka, hisia zote zikarudi. Mungu akaniponya hiyo kansa. Wakasema, 'Yeye hana figo.' Nikapata mengine mapya. Sijui, bali Mungu akayaamsha. Lakini lilitukia kwangu. Umri wa miaka themanini na mmoja, nimekuwa nikitafuta kote katika miaka, nilisaidia kuleta matengenezo kwenye Pentekoste. Hilo hunifurahisha sana. Ndugu Branham anaposema, 'Wote walianza kujenga kuta ndogo za kujitenganisha mmoja na mwingine, wala hawawezi kuwa na uamsho.' Hiyo ni kweli. Amesema kweli kuhusu hilo."—Mh.]

Jambo ndilo hilo tu. Ndugu Ed, hivyo ndivyo ilivyofanya. Loo, hilo si ni zuri sana? Ninaupenda ushuhuda huo mdogo, ndugu.

Sasa redio ya gari imeunganishwa, ndivyo wanavyosema humu ndani, sehemu hii hapa.

3 Kila mtu anajisikia vizuri sasa? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Vema, sasa, tutaanza moja kwa moja sasa hadi usiku wa manane, kisha tutaninii...["Amina."] Tuna furaha sana kwamba Bwana ametusaidia na kutubariki.

Sasa, kabla hatujaanza tena, hebu na tuombe tu kidogo kwa Yule tunayezungumza naye sasa.

4 Baba wa Mbinguni mwenye rehema, unasikia ushuhuda wa mzee huyu mtauwa, mtakatifu. Kote katika nyakati, yeye na maskini mke wake, wakifanya kazi pamoja, na jinsi ambavyo ilimbidi kukushikilia Wewe, na kukuomba Wewe umfanye mumewe mhubiri, naye huyu hapa. Ndipo wakati alipokuwa amelala pale, akifa, madaktari walio bora sana nchini wakisema, ya kwamba, "Amekwisha. Hawezi kuishi ila saa chache. Imekwisha. Mwili wake umeliwa na kansa. Kamwe asingeweza

kutembea hatua nyingine. Maambukizi kwenye vifundo vyake vya miguu, na kadhalika, tayari yamemwondoa." Huyu hapa, miaka kadhaa baadaye, angali anaenda. Tunashukuru sana, Baba. Inathibitisha, ya kwamba, Neno linapopandwa, kisha likamwagiliwa maji, litazaa mazao.

5 Sasa tunaomba, Baba, ya kwamba Wewe utatujalia kuyaelezea Maneno alasiri ya leo, kutoka kwenye Neno Lako. Ni Neno Lako, nasi tunataka kuliweka wazi jinsi tu lilivyo. Na ndipo Wewe ulimwagilie maji, Bwana, kwa Roho. Tunaomba, tunapojikabidhi wenyewe, pamoja na Ujumbe, Kwako, kwamba Wewe ututumie, katika Jina la Yesu. Amina.

6 Sasa kuharakisha moja kwa moja. Mke wangu alikuwa akiniambia, asubuhi ya leo, kuusu jinsi ilivyo vigumu kwa watu, mwajua, huku miguu yao ikikakamaa na kadhalika; akina mama, na—na watu wengine kama mimi, wanaozeeka kidogo, inawabidi kusimama kote namna hiyo. Ninathamini hilo, uaminifu wenu. Na sasa tutarudi moja kwa moja kwenye Ujumbe na kuendelea. Sitaki kuharakisha sana, na hata hivyo ninataka kuharakisha vya kutosha kujaribu kumaliza alasiri ya leo, nikiweza.

7 Ndipo, mara tutakapomaliza, tutaenda moja kwa moja huko—huko Tifton, Georgia, sio ya kawa-. . .mkutano unaoendelea. Tuko kwenye ukumbi wa shule ya sekondari kule, kwa usiku mmoja tu. Hiyo ni kesho usiku, na ibada tu ya kuhubiri. Nami nitakuwa na somo dogo la kawaida, ama kitu fulani nilichohubiri papa hapa, kwa sababu ni kutembeleana tu na watu kule. Hawana mkutano wa kawaida wa kukaa wala chochote kile. Kwa hiyo sisi . . .

8 Na sasa, tu—tuliachia, asubuhi ya leo, tukizungumza juu ya somo letu linalopatikana katika Mwanzo, mlango wa kwanza, ki—kifungu cha 11, hasa. *Neno Lililonenwa Ndilo Mbegu Ya Asili.*

9 Na sasa kusudi langu asubuhi ya leo, na leo hii, ni kujaribu kuwaelezea watu. . .(Hiyo imewashwa? Hmm.) . . . kujaribu kuwaelezea watu, juu ya matendo yangu, na sasa, ni kwa nini nimefanya mambo ambayo nimefanya. Na tukitambua, ya kwamba, kanda hizi zinarekodiwa na zitasambazwa. Watu wengi labda watakuwa wakizisikiliza baada ya mimi kuondoka hapa, kama Yesu akikawia. Lakini nataka kusema ya kwamba ninaamini Neno la Mungu, ya kwamba Hilo, Hilo, ni Kweli.

10 Sasa, tuliachia mahali ambapo ninii. . .ya siku za mwisho, kilichotukia kwa huduma ya wainjilisti ambayo miaka michache iliyopita walikuwa tu wakiitia nchi moto, na inaonekana kana kwamba wote wamekoma hivi punde. Sasa, simaanishi wameondoka hudumani. Wangali wanaendelea, lakini hakuna matokeo, inaonekana. Hawafiki popote. Mnaona? Kuna shida

gani? Shamba limepandwa tayari. Mnaona? Sasa kumbukeni. Msisahau.

11 Mtu fulani aliniomba nilirudie neno hilo la Kiebrania tena, katika Yoeli, mlango wa pili, Yoeli 2:28, ambapo anazungumza juu ya kuja kwa mvua ya masika na ya vuli. Neno *masika* ni neno la Kiebrania m-o-u-r-e-h, *moureh*, ambalo linamaanisha "kufundisha." Kwa maneno mengine, itakuwa ni mvua ya mafundisho na mvua ya mavuno. Sasa tumekuwa na mvua ya mafundisho, nasi tuko tayari sasa kwa ajili ya mvua ya mavuno. Mnajua, mvua ya kwanza ni wakati unapopanda mbegu, hiyo inafanya mazao yako kuanza kukua. Ndipo kabla tu hayajakomaa, inakuja zamu nyingine. Hiyo ndiyo wanayoita mvua ya mavuno. Tunajua ni lini. Mvua za kuchipusha, halafu mvua za yapata Juni, zinaleta mazao yako. Sasa, mvua, tuliona, ilikuwa ni Roho.

12 Na sasa tuliachia mahali nilipotoa mawazo yangu juu ya jinsi jambo hilo lote litakavyokuwa. Hiyo ni kusema, ninaamini ya kwamba ninii—ya kwamba m—mvua imeletwa, mvua. Hiyo ndiyo sababu tunatulia, kwa sababu ardhi tayari imepandwa. Huwezi kupata popote, ni vigumu, ila ambapo pamepandwa. Nayo imepitia kwenye redio, televisheni, kanda, neno, kila kitu. Nchi nzima imepandwa. Mbegu zimepandwa. Sasa, kwamba ni mbegu gani zilizopandwa, huwezi kupata kitu kingine chochote kutoka kwake ila zile mbegu zilizopandwa. Mnaweza kuelewa sasa? Itakuwa ni mbegu zilizopandwa. Sasa, Roho atashuka, bali ataleta mavuno ya mbegu inayoangukia. Sasa, kumbukeni. Vema.

13 Ninabashiri ya kwamba hayo makundi mawili ya kimadhehebu, makundi ya Kipentekoste na ya kiinjilisti, yatafanya kazi pamoja katika dhehebu, yataungana pamoja na yatakuwa wanachama, wote, wa Shirikisho la Makanisa ya Halmashauri, ama Baraza la Makanisa. Tayari wao ni wafuasi wake, wote. Na kutakuja, kupitia kwao, kulazimisha, ama kususia, ambako kutakomesha kila kitu isipokuwa kile ambacho ni cha muungano huo wa makanisa. Hivyo ndivyo ninii. . .Biblia ilisema kwamba kutakuwa na kususiwa, hata kufikia ambapo ingewafanya watu wasinunue wala kuuza isipokuwa wamepokea hii: alama ya mnyama, ambayo ni Urumi; na sanamu ya mnyama, ambayo ni Uprotestanti. Kwamba ile sanamu. . .Yule mnyama alikuwa na nguvu, mamlaka, kuipa hiyo sanamu uhai, kunena, na ikafanya hivyo. Na huo ni Mwungano wa Makanisa, wakati wanapoungana pamoja.

14 Sasa kuna vijana wengi hapa. Sijui, Yesu anaweza akaja alasiri ya leo. Huenda akaja mwaka ujao. Sijui atakuja lini. Lakini kama ninii. . .kumbukeni, endapo sitaishi kuiona Siku hiyo ya Kuja Kwake. . .Ambayo, natumaini kwamba nitaiona, na kwa namna fulani ninaamini nitaiona. Sasa, kama sitaiona, kamwe msiache Neno hili liondoke masikioni mwenu na moyoni

mwenu. Mnaona? Kumbukeni tu, ninanena katika Jina la Bwana.

15 Sasa, ninaamini kwa moyo wangu wote, hivyo ndivyo itakavyoishia. Kutakuwako na kitu kama mwungano, ku—kususiwa. Sehemu zote kama hii hapa zitafungwa. Nawe hutaweza kuzungumza isipokuwa upate ru—ruhusa, ama leseni kutoka kwa Mwungano huu wa Makanisa, kufanya ibada. Ni karibu. . . Inaonyesha inafanya hivyo sasa, hata katika madhehebu. Inaonyesha mahali ilipo. Naam, bwana. Huna budi kuwa nayo. Na hapo ndipo itakapoishia. Huo ndio ubashiri wangu, kama mtumishi wa Kristo, kupitia ufahamu nilio nao wa Neno, na uvuvio. Hapo ndipo itakapofikia. Ninii. . . Ishara zote zinaelekeza kwenye mwisho. Ndio kwanza nimalize kuzungumza juu ya jambo hilo. Na hata ni kwa. . .

16 Yule mwanamwali mpumbavu ameanza kulilia Mafuta. Sasa, kumbukeni, yeye alikuwa ni bikira. Na kama yeye ni bikira, yeye ni kanisa. Mnaona? Tutafikia jambo hilo alasiri ya leo, katika Ufunuo 17. Kama yeye ni bikira, yeye ni kanisa, maana kanisa ni bikira.

Paulo alisema, "Nawaposea Kristo, kama bikira safi."

17 Yule kahaba, wa Ufunuo 17, alikuwa ni kanisa. Yohana alivutiwa naye kwa sababu ya—ya urembo wake, kile alichokuwa. Alikuwa ni kitu cha kupendeza. Lakini, hata hivyo, "Ndani yake ilipatikana damu ya kila mtakatifu wa Yesu Kristo, alikuwa ameuawa ndani yake." Hiyo ni kweli. Ninaamini ni milioni sitini na nane, kwenye kitabu cha wafia imani, ambao kanisa Katoliki la Kirumi limewaua tangu—tangu Mtakatifu Agostino wa Hippo. Waprotestanti milioni sitini na nane wameuawa, na kuandikwa kwenye kumbukumbu ya wafia imani, na kanisa Katoliki, kwa sababu ya kutokubaliana na fundisho lake. Si ajabu Biblia ilisema, "Ndani yake ilionekana damu ya kila mfia imani."

18 Sasa, sasa, hivi Yesu hakusema wakati unakuja, "Wangewaua, wakidhani walikuwa wanamtumikia Mungu"? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Nao ni waaminifu kuhusu hilo. Wao si wanafiki. Wanaamini hilo. Wanafundishwa hivyo.

19 Na wakati Neno hilo. . . Wakati—wakati Neno hilo linapopandwa pale, halina budi kuleta mazao. Hakika, limepandwa. Kumbukeni, tunakaa na, "ile Mbegu." Hilo ndilo somo letu, Mbegu yetu. Neno lililonenwa la Mungu ni Mbegu. Mnaona? Halina budi kurudi kwenye Neno hili, nalo Neno hilo litazaa kile lisemacho.

20 Hiyo ndiyo sababu ninaamini katika uponyaji wa Kiungu. Hiyo ndiyo sababu ninaamini katika maono. Hiyo ndiyo sababu ninaamini katika Malaika. Hiyo ndiyo sababu ninaamini Ujumbe huu, ni kwa sababu unatoka kwenye Neno la Mungu. Na chochote nje ya Neno la Mungu, sikiamini. Inaweza kuwa hivyo,

lakini hata hivyo nitadumu tu na yale Mungu aliyosema, ndipo niwe na hakika kwamba niko sahihi. Sasa, Mungu anaweza kufanya atakalo. Yeye ni Mungu. Lakini maadamu ninadumu na Neno Lake, basi ninajua hilo ni sawa. Ninaamini hilo.

21 Sasa, huyu mwanamwali mpumbavu ni mwanamke. Yeye ni kanisa, lakini hana hekima. Unaona? Yeye amekuwa tu mzembe, na hata hivyo anaitwa—anajiita Bibi-arusi.

22 Basi kumbukeni, kila kitu kinaenda katika tatu, kwa ukamilifu. Tatu ni namba ya ukamilifu.

23 Afisi za Mungu: Baba, Mwana, Roho Mtakatifu. Mungu Baba alikuwa Mungu aliyeishi katika Nguzo ya Moto. Alikuwa akijaribu kuwavuta Israeli Kwake. Wasingekuja. Mungu Baba aliishi ndani ya Mwana, ambalo lilimfanya Mungu Mwana; Mungu yeye yule, chapa ya Mungu, Mbegu ya Mungu iliyodhihirishwa, akijaribu kuwavuta watu Kwake. Wakamsulubisha. Roho Mtakatifu ni Mungu yule yule aliyekuwa hapo mwanzo, katika Mwana wa Mungu, na sasa hapa (ile ofisi nyingine ya Mungu) katika siku za mwisho, ikiishi katika Kanisa; ikijaribu kuleta Neno, Neno lililonenwa, kama ofisi zingine mbili zilivyofanya, kwa watu, nao wanalikataa. Ni jambo lile lile. Ni ofisi tatu ama madhihirisho ya Mungu mmoja akitenda kazi. Naye Mungu katika watu Wake leo hii, katika matendo, ni Mungu katika matendo. Mnaona? Ni Mungu ndani ya watu.

24 Bwana akipenda, ninataka kuzungumza juu ya hilo, kesho usiku, "Mungu katika ulimwengu Wake, Mungu katika Mwanawe, Mungu ndani ya watu Wake," na kadhalika. Sasa, nimezungumza juu ya hilo hapo awali, hapa, ninaamini.

25 Sasa, basi, huyu mwanamwali mpumbavu, wakati alipoenda kununua Mafuta. Alitumwa kununua Mafuta. Alipofanya hivyo, akagundua kwamba alikuwa amechelewa sana. Kwa nini? Kwa nini, rafiki? Mbegu zimepandwa tayari. Mnaona? Kulikuwa na tatu, kufikia wakati wa Sodoma.

Daima kumekuwa na idadi ya tatu, wakati wote.

26 Kuna kuja mara tatu kwa Kristo. Yeye alikuja mara moja kumkomboa Bibi-arusi Wake. Anakuja, tena, katika Unyakuo, kumnyakua Bibi-arusi Wake. Anakuja tena, katika ule Utawala wa Miaka Elfu, pamoja na Bibi-arusi Wake.

27 Kila kitu kiko katika tatu. Tatu ni namba kamili. Tano ni namba ya neema; saba, ukamilifu; kumi na mbili, ibada; ishirini na nne, ama—ama, arobaini, kujaribiwa; na hamsini ni yubile. Neno lenyewe, *pentekoste,* linamaanisha *yubile*, "hamsini." Unaona? Sasa, na sasa, Mungu, katika tarakimu Zake, Yeye ni mkamilifu katika tarakimu Zake. Yeye ni mkamilifu katika Neno Lake. Yeye ni mkamilifu katika matendo Yake. Yeye ni mkamilifu katika kila kitu, kwa sababu Yeye ni Mungu mkamilifu. Naam.

Nasi tunaona ya kwamba katika wanawali hawa . . .

28 Sasa, angalieni, hapo yeye anaitwa "kahaba," katika Biblia. Sasa, nataka dada zangu wa—wanisamehe. Mimi . . . Hivyo ndivyo Biblia ilivyosema. Leo ninazungumza waziwai kabisa. Anamwita, "Yule kahaba, na mama wa makahaba," ambalo ni kitu kile kile. Sasa, kama mkiangalia, kuna "kahaba" aliyenenwa, katika Biblia, ambaye ni kanisa. "Kahaba" aliyenenwa, wa Biblia, huyo ni kanisa. Na "Bibi-arusi" aliyenenwa, katika Biblia, na huyo ni Kanisa. Hao hapo watatu. Tutawafikia, baada ya kitambo kidogo, tukionyesha hao ni bibi-arusi wa nani, na jinsi walivyokataliwa, na yote kulihusu hilo, Bwana akipenda.

29 Sasa, jambo la kwanza, ninataka kusema jambo hili kabla sijalisahau. Msiogope, kamwe msiogope ukomunisti. Ukomunisti unafanya kazi tu katika mikono ya Mungu. Ni kitu kiovu kama tu Mfalme Nebkadreza alivyokuwa, bali alimtuma kule na kuwakatilia mbali Israeli kwa sababu ya kutotii kwao. Wakati, nabii alipowaambia yaliyokuwa yakija, naye akawaambia wakae katika nchi yao na kumkumbuka Mungu. Wasingefanya hivyo. Waliendelea, kwa vyovyote vile, naye mfalme akaja moja kwa moja na kuwachukua, kwa vyovyote vile, maana Yeye alisema angewachukua. Ukomunisti ni kitu ambacho ni . . .

30 Sababu ya ukomunisti kuinuka ni kwa sababu ya uharamu wa kanisa Katoliki, nchi za ng'ambo, huko Urusi. Walichukua pesa zote, na walikuwa—walikuwa wamenyakua kila kitu, na ni hayo tu. Hilo ndilo hasa lililoufanya ukomunisti.

31 Wakati yule mvulana mdogo alipofufuliwa kutoka kwa wafu, huko juu Ufini, hao askari wakubwa wa kikomunisti walisimama pale na kupiga saluti nilipopita, huku machozi yakitiririka mashavuni mwao. Kasema, "Tutampokea Mungu kama huyo, hakika, Mungu anayeweza kufufua wafu na kulitimiza Neno Lake. Hakika." Mnaona? Lakini inapofikia kwenda tu kanisani, na kuishi kama ibilisi na kadhalika, kama walimwengu wengine, wasifanye chochote, basi hawaliamini. Na, kusema kweli, siamini pia. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli.

32 Hakuna Maandiko yanayosema ukomunisti utautawala ulimwengu. Lakini kuna Maandiko, na Maandiko yote, yalisema Urumi utautawala. Kwa hiyo yaelekezeni macho yenu huko.

33 Angalieni, usiku wa leo. Angalieni tu kile kilichotukia hata jana usiku. Huyu seneta wa Kentucky, alisema kuhusu kuwa na Mripablikani ki—kitini kule sasa, anayewakilisha jimbo la Kentucky. Na kusema, "Yeye ni Mprotestanti, naye haliheshimu," yeye ni Mkatoliki. Wanakuwa jasiri wawezavyo kuwa. Na, kumbukeni, kuna mambo mengine yanayoambatana na hayo.

34 Wakati wa wanawali wapumbavu, tunaona jambo hilo. Mambo ambayo hayajawahi kutukia, ambayo hakuna mmoja wa hao watu, hao walimu, kote katika nyakati angeweza kusema mambo haya kama tunavyoweza sasa, maana yametimia. Sasa, mwanamwali mpumbavu na Wapentekoste chotara, hao ni kitu kile kile, wamechanganyika na mambo ya ulimwengu.

35 Sasa kumbukeni, mimi ni mpentekoste, bali si Mpentekoste kwa dhehebu. Ninachukia hilo. Mimi ni mpentekoste kwa tukio. Hatuna budi kuwa na . . . Wamethodisti ni wapentekoste, Wabaptisti ni wapentekoste, Wakatoliki ni wapentekoste, kama wana ujuzi wa kipentekoste. Huwezi kuiundia Pentekoste dhehebu, kwa sababu ni—ni tukio, na ni Mungu. Na Mungu hawezi kuundiwa dhehebu.

36 Sasa, sasa, Yesu ametwambia mambo haya yangekuja, sasa, alitwambia yale yangetukia; mwanamwali mpumbavu angeinuka, na mambo ambayo angefanya; na jinsi ambavyo watu wangeita, katika siku zao, na kutaka Mafuta, lakini wangekuwa wamechelewa mno. Mnaona?

37 Sasa angalieni hizo tatu, hayo makanisa matatu. Huyo hapo yule kahaba; hakuja kwa ajili ya chochote, sasa, yeye anajifikiria mwenyewe. Kulikuwako na yule mwanamwali asiye na hekima, ambaye ni kanisa la Kiprotestanti. Na kulikuwako na Bibi-arusi. Mnaona? Sasa, hizo hapo hatua tatu za kanisa katika siku za mwisho. Sasa angalieni. Tutazileta moja kwa moja kutoka Mwanzo, na kuzileta hapa nje na kuziweka katika Ufunuo, katika Unyakuo, Bwana akipenda.

38 Mambo haya yote yanaonekana halisi. Pentekoste inaonekana halisi. Wazia ninii . . . "Mbona, mimi ni mfuasi wa dhehebu la Kipentekoste." Hilo halimaanishi zaidi ya kama uliishi katika zizi la nguruwe. Haingeleta tofauti hata kidogo. Haingeleta. Ni shaba tu iliayo na upatu uvumao, naam, haidhuru wewe ni wa wapi, kama hujazaliwa na Roho wa Mungu na kumpokea Roho Mtakatifu. Na sababu . . .

39 Kama hujampokea, huamini Neno lote la Mungu, hujampokea Roho Mtakatifu bado. Sawa. Hiyo ni kweli kabisa. Roho Mtakatifu . . . Unapoisikia ile Kweli, na Roho Mtakatifu hakuongozi Kwake, basi kuna roho nyingine humo ndani inayokuzuia usiijue. Kwa hiyo, roho uliyo nayo ndani yako si Roho Mtakatifu. Loo, naam.

40 Sasa tunaona, kama ilivyoendelea, kasema, "Kama vile Yane na Yambre walivyoshindana na Musa." Tulizungumza juu ya jambo hilo, jinsi ambavyo mambo haya yangekuwa katika siku za mwisho sasa.

41 Na nukuu ya mwisho tuliyokuwa nayo, ilikuwa kwamba, "Mungu alifanya kila mbegu kwa jinsi yake." Hiyo ni ninii Yake . . . Mnaona? Ndipo wakati alipomfanya mtu Wake katika mfano Wake, alikuwa ni Mbegu ya Neno Lake. Na wakati

Yesu alipofanyika mwili, Yeye alikuwa mwi—mwili wa Neno la Mungu. Nasi tunapolipokea Neno la Mungu, basi tunakuwa Neno la Mungu katika miili yetu. Mnaona? Kanisa linapaswa kuwa katika hali hiyo.

42 Sasa, basi, akisha kumfanya mtu kwa mfano Wake Mwenyewe. . . "Kwa mfano wa Mungu alimwumba." Sasa, baada ya Yeye kufanya jambo hili . . . Sasa msikose hili. Baada ya Mungu kumfanya mtu Wa—Wake katika mfano Wake Mwenyewe, kwa Neno Lake Mwenyewe lililonenwa, sasa, huyo alikuwa ndiye mtu mkamilifu. Lakini mahali kule kuanguka kulipokujia, ilikuwa ni wakati alipotoa zaotuka kwake, na kumfanyia bibi-arusi. Hapo ndipo palipo na shida sasa. Kama ulikuwa wa kiroho, tayari umelishika. Unaona? Unaona? Yeye . . . Si Adamu aliyepata shida. Adamu siye aliyelitilia shaka Neno. Bibi-arusi wake ndiye aliyelishuku Neno.

Wala si Yesu anayelishuku Neno, kwa kuwa Yeye alikuwa ni Neno. Mnaona? Ni bibi-arusi Wake. Hapo ndipo kuchanganya mbegu kunapokujia.

43 Hakupitia kwa Adamu. Aibu kwenu ninyi msioona hilo. Mnaona? Si kosa la Adamu. Hakuwa na uhusiano wowote nalo. Kama mauti yalipitia kwa Adamu, basi yalipitia kwa Mungu. Mauti huja kwa kuchanganya mbegu.

44 Mauti hayawezi kupitia kwa Neno la Mungu. Mauti huja kwa kulichanganya na dhehebu, na kanuni za imani badala ya Kristo, fundisho la sharti badala ya Neno. Hayaji kwa Neno. Neno ni Uzima. Yesu alisema, "Maneno Yangu ni Uzima." Naye Roho hulihuisha Neno hilo na kulifanya Uzima. Kulichanganya, hapo ndipo mauti yanapotokea.

45 Na ikiwa Adamu ni Neno la Mungu, Neno Lake lililonenwa, Mzao Wake wa asili, kwa kuwa Yeye alikuwa wa kwanza basi kwa uumbaji, basi Adamu Wake wa pili pia alikuwa kwa uumbaji, Neno lililonenwa. Mnafuata? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

46 Sasa, Adamu hakudanga- . . . hakudanganywa. Lakini bibi-arusi wake alidanganywa. Kristo, leo hii, hajadanganywa. Neno halidanganyi. Bibi-arusi ndiye anayedanganya, kwa Neno. Mnaliona? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

47 Sasa, Yeye alimpa bibi-arusi, mfano wa Adamu wa pili. Alimpa Adamu wa kwanza bibi-arusi; akaanguka. Akampa Adamu wa pili, Kristo, bibi-arusi; akaanguka. Hiyo ni kweli kabisa. Kwa nini? Yeye si wa asili. Yeye ni zaotuka.

48 Bibi-arusi siku hizi ni zaotuka. Mnaona? Yeye, anajiita bibi-arusi. Lakini jambo ni kwamba, amefanyizwa kwa nyenzo za kimadhehebu, si kwa Neno; kiasi fulani cha Neno ndani yake, kidogo kumfanya zaotuka, kumfanya wa kinafiki. Hawa aliamini karibu Neno lote, bali akatilia shaka sehemu moja Yake. Leo hii, hata hawezi kufanya Matendo 20 . . . ama Mathayo 28:19

kuafikiana na Matendo 2:38. Mnaona? Inamtatanisha. Hapo ni mahali pamoja padogo tu, kati ya mamia ya pengine.

Sasa, bibi-arusi wa Adamu alikuwa ni mfano wa bibi-arusi wa Adamu wa pili. Sasa, bibi-arusi wa Adamu. . .

[Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Kwani nimekatiza kanda?

49 Bibi-arusi wa Adamu asingeweza kungojea. Mungu alikuwa amewaambia Adamu na Hawa, "Zaeni mkaijaze nchi." Lilikuwa ni jambo linalokuja, ahadi. Yeye hakuwa mke wake, bado, kwa sababu kamwe hakuwa ameishi naye.

50 Bibi-arusi wa Kristo si mke Wake bado. Ile Karamu ya Arusi itafanyika. Mnalipata? Angalieni, loo, hili limekolea.

51 Alikuwa na haraka, ndipo akafanya nini? Akachanganya mbegu yake. Aliichanganya na mbegu ya nyoka. Basi alipofanya hivyo, alileta ni—ninii. . .Alileta nini? Alileta mtoto wa mauti. Mtoto, ambaye, alimpotosha kila mtoto baada yake.

52 Ndipo wakati kanisa la Yesu Kristo lilipopotoshwa katika wakati wa Rumi, baada ya kuzaliwa kwake na bikira, kisha likatolewa kwa Kristo pale Pentekoste, lilininii. . .Lilifanya nini? Lilichanganyana na fundisho la sharti la Kirumi. Nalo kanisa la Kiprotestanti limefanya jambo lile lile. Haliwezi kungojea.

53 Mwanamke aliyeposwa na mwanamume mzuri, kijana, safi, na kabla hawajakutana, amefanya nini? Anapatikana ana mimba ya mtu mwingine. Basi mbegu yake mwenyewe, ambaye ameposwa. . .Mwili wake mwenyewe, ambao umeposwa kwa mpenzi wake, mume aliyemposa, unaonekana umejaa mbegu ya mwanamume mwingine. Ni fedheha iliyoje!

Hilo hasa ndilo Adamu alilopata.

54 Hicho ndicho Kristo amepata. Asingeweza kungojea. Hiyo ndiyo shida ya watu siku hizi. Hawawezi kumngojea Roho Mtakatifu halisi aliweke Kanisa mahali pake. Hawana budi kujitengenezea kitu fulani, kubuni kitu fulani. "Ushahidi wa kwanza, kunena kwa lugha," kupata wafuasi wengi zaidi kanisani. Upuuzi huu wote, badala ya kumngojea Bwana kwa ajili ya dhihirisho halisi la kufufuka kwa Kristo akijitambulisha Mwenyewe miongoni mwa watu. Hawezi kungojea.

55 Alifanya nini? Alitoka akaenda akatiwa mimba na umadhehebu. Kwanza ilikuwa ni Assemblies of God, kisha likaja Umoja, kisha likaja chochote kile baada ya hilo. Sasa yule anayejiita bibi-arusi ametiwa mimba na kila namna ya upuuzi, aibu. Wanawake hawatatilia maanani zaidi yale Neno la Mungu lisemayo, kuliko chochote kile, wala wanaume, au hata wahubiri, kisha ati mnamwita huyo bibi-arusi.

56 Ni kitu gani? Ametiwa mimba. Bibi-arusi wa Kristo amepata mimba ya ulimwengu, akivalia kama ulimwengu, akitenda kama

ulimwengu, makanisa makubwa, mazuri. Nini? Inaonyesha jinsi alivyo. Yeye ni wa ibilisi. Hivyo ndivyo Shetani alivyofanya kwanza, ilikuwa ni kujaribu kujenga ufalme mkubwa mzuri Mbinguni, naye akafukuzwa kwa sababu hiyo, akafukuzwa Mbinguni. Hivyo ndivyo alivyo bibi-arusi wa kisasa wa Kristo, amefukuzwa, kwa sababu ametengwa na Mungu, kwa sababu yeye ni kahaba wala si bikira. Ni la kilindi, bali natumaini mnalipata.

57 Bibi-arusi wa Adamu asingeweza kungojea, bali alichanganya mbegu yake, kinyume na sheria. Kinyume na sheria!

58 Tunapaswa kuamini Neno la Mungu, na Hilo pekee. Sasa, ndugu, hapa na kwenye kanda, mnaona ni kwa nini ninashindania hilo Neno, Neno kwa Neno? Nimewaambia ninaamini hilo ni Kweli ya Mungu. Mungu ameilinda Biblia hiyo. Hana budi kuuhukumu ulimwengu kwa kitu fulani, kupitia Yesu Kristo ambaye ni Neno. Nalo Neno hili lilifanyika mwili, lipate kufanyika Yesu Kristo. Ninaliacha tu lizame ndani. Kumbukeni Neno!

59 Na sasa anamwona amechafuka kabisa. Unafikiri angeoa kitu kama hicho? La hasha. Yeye ni mtakatifu. Mke asingeweza kungojea. Kinyume na sheria!

60 Hilo ndilo Adamu alilokuta. Sasa, ndugu, dada, angalieni nyuma. Ukiangalia kivuli cha kitu chochote, ni chapa yenyewe ya sura halisi ijayo. Kwa hiyo, unaona, ilimbidi Adamu kumpata mke akiwa mja mzito. Naye akasema, "Nyoka alinidanganya." Sasa sisi . . . wewe . . .

61 Nitalichukua pande zote mbili, katika dakika chache tu, Bwana akipenda, mnaona, kuwaonyesha kwamba haiwezekani kwake kuwa kitu kingine chochote.

Sasa, bibi-arusi wa Adamu asingeweza kungojea, bali alisonga mbele kwanza.

62 Hivyo ndivyo alivyo, siku hizi, bibi-arusi leo hii. Anataka kujitengenezea kitu fulani. "Utukufu kwa Mungu," hana budi kujibunia, jukwaani. Hana budi kuwa na kila kitu. Mnaona? Anafanya nini? Kujitengenezea kitu fulani.

63 Angalia linakoelekea. Unaweza kuona hakuna kitu kwake. Ni bandia. Kweli kabisa. Kama sivyo, ulimwengu huu ungewaka moto kwa Nguvu za Mungu; kanisa lingewaka moto. Loo! Ati nini? Wafu wangefufuliwa, na mambo ya kila namna yangekuwa yakitukia.

64 Lakini yeye alipandwa nini, kabla Kristo hajaweza kumfikia. Kabla hajamfikia, kupanda Mbegu Yake Mwenyewe, alikuwa na nini? Mbegu za magugu, ulimwengu, mbegu za kimadhehebu. Hiyo ndiyo sababu anavuna mavuno yake sasa hivi.

Natumaini haliwaudhi, bali natumaini litafikia mahali ambapo nitatumaini ya kwamba Mungu amewapa ninyi. Mnaona?

65 Sasa, yeye alichanganya mbegu yake, kinyume na sheria, kinyume na Neno. Alikuwa akijaribu kupata nini? Sasa sikilizeni kwa makini. Alikuwa anatafuta nini? Hekima.

66 Hekima! Na hivyo ndivyo amefanya siku hizi. Aliwapeleka wahubiri wake shuleni, akawaangua, kwenye mtambo, saikolojia, kila namna ya mambo ambayo yanapaswa... hata hayako katika Biblia. Naye ameyaatamia mayai ya—ya—yake. Na wakati alipomaliza, ametoa bidhaa ya—ya kundi la watu ambao—ambao watapatana juu ya chochote, na kuukataa Ujumbe wenyewe wa Mungu, bila kujua analofanya. Hajui hilo. Haamini, haoni amekosea.

67 Wala Hawa hakufikiri alikuwa amekosea. Hawa alidhani alikuwa sahihi. Na kama huo ulikuwa ni mfano, na huu ni uhalisia wa huo mfano, itabidi utende kazi sawasawa na huo mfano ulivyofanya. Sasa hiyo ni ninii tu, kwangu mimi, hiyo ni mbili mara mbili ni nne tu.

Sasa angalia kilichowapata watoto wa Hawa, wa kwanza aliyezaliwa.

68 Sasa, kama Mungu alisema, "Zaeni," kwa bibi-arusi wake, kwa bibi-arusi wa Adamu, "mkaijaze, zaeni mkaijaze nchi," hilo lilikuwa ndilo agizo la Mungu. Naye mke angaliweza kufanya hivyo, naye mume angefanya hivyo, wakijichanganya pamoja. Lakini ni jambo gani lililotukia? Wakati Adamu alipokuwa tayari kumjia, alikuwa tayari ni mama. Mnaona ninalomaanisha?

69 Sasa jambo lilo hilo limetendeka kwa kanisa la Kristo, bibi-arusi wa Kristo. Sasa tutarudi nyuma zaidi ya hapo, katika dakika moja.

70 Angalieni, katika bibi-arusi huyu, alifanya nini basi? Mtoto wake wa kwanza kuzaliwa, alikuwa ni mtoto haramu. Naye alikuwa amejaa mauti, na kusababisha mauti, na kila mmoja tangu wakati huo ni mauti. Sasa unaona ilibidi iwe ni kujuana kimwili. Mbona unakufa, kama haikuwa ni kujuana kimwili?

71 Wakati, Mungu alitoa agizo ambalo haliwezi kuangamia. Neno la Mungu ni la Milele. Haliwezi kushindwa. Wakati aliposema, "Zaeni mkaijaze nchi," hilo lilikuwa ndilo kusudi la Milele la Mungu. Kutekeleza hilo, huwezi kufa. Kwa sababu ni Neno Lake, huna budi kuishi.

72 Kama mtoto huyo alizaliwa vizuri, kusingekuwako na mauti. Lakini asingeweza kungoja.

73 Hiyo ndiyo shida siku hizi. Unataka namna fulani ya kujifanya bandia, pamoja na kupiga mayowe, kuruka-ruka,

kunena kwa lugha, ama kitu fulani, badala ya kungojea Neno halisi la Mungu lipate kudhihirishwa kupitia kwa Bibi-arusi.

74 Hao watu, wanaolichukua Neno, ndio Bibi-arusi wa kweli wa Mungu anayewazaa Watoto. Hawawezi kufa. Mtoto ambaye Bibi-arusi anamzaa kwa Neno, hawezi kufa, kwa sababu Yeye ni Neno. Amina. Mlilipata? Hawezi kufa, maana yeye ni . . . Mtoto huyo hawezi kufa, kwa sababu yeye ni Mtoto-Neno, yeye ni Mtoto-Mbegu, yeye ni Mtoto wa Milele. Haleluya!

75 Hivyo ndivyo Yesu Kristo alivyokuwa hasa, Mtoto aliyenenwa, wa Milele. Haikumbidi kufa, bali Yeye alikufa kusudi apate kulipa deni. Hivyo ndivyo tu ingeweza kulipiwa. Hakuna mtu mwingine angaliweza kufanya hivyo; wote walizaliwa kwa kujuana kimwili, kwa jinsi ya ibilisi, mpango wake. Mmelipata sasa? Mnaona?

76 Lakini kila mtu, haidhuru kama yeye ni papa, kasisi, askofu, chochote alicho, yeye hufa kwa sababu yeye ni—yeye ni chotara. Hiyo ni kweli kabisa. Alizaliwa kati ya Shetani na Hawa. Nao wanaiita vyovyote mtakavyo. Ilikuwa ni Shetani na Hawa. Neno la asili halikuwa na uhusiano wowote nayo. Neno la asili lilikuwa Uzima. Alikuwa amelichanganya, nalo likaleta mauti.

77 Basi wakati kanisa, siku hizi, ambalo linajiita la Kipentekoste, linajiita Baptisti, chochote watakacho, wanapolichanganya Neno hili na mafundisho ya sharti, huzaa mtoto aliyekufa. Wala hawezi kuwa na Uhai ndani yake. Amekufa, na watoto wake wamekufa. Mungu alisema, "Nitamtupa katika kitanda cha mambo ya ulimwengu, na kuwaua watoto wake." Mungu alisema hivyo, katika Ufunuo. Ni wangapi wanaojua hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] "Kumweka katika kitanda cha mambo ya ulimwengu," hapo ndipo alipo, "na kuwaua watoto wake, hata kwa moto." Tunaangalia ambapo ninii . . . Magugu yaliyo miongoni mwa ngano hupatwa na nini? Kuchomwa moto.

78 Loo, huwezi kulifanya Neno liseme uongo. Ni Kweli. Wakati mwingine mnavurugika, na huenda tukalifanya vibaya. Lakini kama utalifanya liendelee moja kwa moja, litaenda moja-mbili, moja-mbili, moja-mbili, moja-mbili, moja kwa moja.

79 "Akamtupa katika kitanda cha mambo ya ulimwengu." Hawezi kuzaa chochote ila watoto waliokufa. Basi, kama dhehebu linaweza tu kumzaa mtoto chotara, kwa nini unataka kuwa mfuasi wake?

80 Sasa, ndugu, hiyo ndiyo sababu ninalipinga. Yeye ni "kahaba," kwanza kabisa. Biblia ilisema alikuwa "kahaba." Hayo ni maneno waziwazi, bali niliwaambia nitazungumza waziwazi leo. Hivyo ndivyo alivyo. Anafanya uasherati wa kiroho, kwa kuchukua mafundisho ya sharti na kanuni za imani badala ya Neno, akiwafundisha watoto wake kufanya jambo lile lile.

81 Sasa, watoto wake wametoka tumboni, wamekufa. Hana budi kufa, hiyo ni kweli kabisa, sawasawa tu na kila mwanamume. Sikilizeni. Kwa hakika tu kama vile kila mwanadamu anayetoka kwenye tumbo la uzazi la mwanamke atakufa, vivyo hivyo kila mtu aliyezaliwa nao atakufa, maana yeye ni chotara, haramu, na watoto wake ni wanaharamu. Hiyo ni kweli. Natumaini hilo halipiti juu ya kichwa chako.

82 Sasa, Yehova alikuwa na bibi-arusi, wakati mmoja. Adamu alikuwa na bibi-arusi. Yesu alikuwa na bibi-arusi. Yehova alikuwa na bibi-arusi. Mnajua hilo? Ilimbidi kumwacha. Akawa kahaba, kwa hiyo Yeye alimwacha. Hivyo ndivyo alivyosema hasa. Akawa kahaba, kahaba. Ni kitu gani kilichomfanya kufanya hivyo? Laiti tungalikuwa na wakati wa kulisoma. Huenda nikafikia baadhi yake, baada ya kitambo kidogo. Sasa hivi. . .Ilikuwa katika wakati wa Samweli, wakati Israeli ilipokuwa na Mfalme, Mungu. Naye alikuwa bikira. Alikuwa anaenda kuzaa kitu fulani. Basi nini kilitukia? Akaanza kuangalia kote na kuona mataifa mengine yalikuwa na wafalme, kwa hiyo alitaka kuwa kama hao wengine.

Ninyi Wapentekoste mliochukuliwa na mkondo, hivyo ndivyo mlivyofanya hasa.

83 Maskini mhubiri huyu anayeketi hapa, mwenye umri wa karibu miaka mia moja, leo. Wakati Pentekoste ilipopenya, huko nyuma, usingeweza kuwaambia lolote kuhusu madhehebu yoyote. Wasingesikiliza hayo. Waliyaita hayo mambo ya ibilisi, na hao watu walisema kweli.

84 Lakini mlifanya nini? Iliwabidi kutenda kama makanisa mengine. Iliwabidi kuliundia dhehebu. Ndipo, kama alivyosema, mliweka nyua kati yenu, mkaanza kufundisha, "Hatupaswi kufundisha jambo *hili*. Utukufu kwa Mungu! Haleluya! *Hivi*," na kuruka-ruka, kunena kwa lugha. Kasema, "Mweke kama mshiriki; amempokea." Yeye hajabatizwa ipasavyo, si kwa maji wala kwa Roho. Amekosea, na matunda yake yanathibitisha jambo hilo. Ana mbegu mbaya ya kukulia. "Mungu abarikiwe, ndugu, tutakuwekea mikono hapa, na kukufanya mzee. Nitawaambia kile wewe—wewe. . .Tutajenga shirika hili hapa mpaka litakuwa kubwa kuliko la Assemblies." Hivyo ndivyo tu ilivyoendelea. Someni historia ya Kipentekoste mwone kama hiyo si kweli, ama kanisa lolote. Wabaptisti wanataka kuwashinda Wamethodisti. Wamethodisti wanataka kuwashinda Walutheri. Lutheri inataka kuishinda Katoliki. Kila mtu akitaka kumshinda, kumshinda mwingine. Mnaona? Hiyo ni—hiyo ni roho ya madhehebu.

85 Yesu alisema, "Lakini ni wachache watakaookolewa. Mlango ni mwembamba, na njia imesonga, nao watakaoiona ni wachache." Wachache tu! Kama alisema "wachache," hilo ni Neno la Mungu, hiyo Mbegu, kutakuwa na wachache.

Hakutakuwako na makumi ya mabilioni na mabilioni. Watakuwa wachache tu watakaoiona. Hao walichaguliwa tangu zamani Kwake, wanalisikia.

Mvua ya masika imenyesha sasa.

86 Sasa, Yehova alikuwa na bibi-arusi ambaye Yeye alimpenda, lakini alianza kufanya ukahaba (alifanya nini?) akifuata ma—mamlaka mengine ya ulimwengu.

87 Naye alifanya nini na nabii huyu mzee, mtauwa, aliyetiwa mafuta? Ambapo, Neno la Bwana humjia nabii. Alikuja. Nabii huyo mzee, Samweli, akamwendea. Akasema, "Watoto, kusanyikeni mkanizunguke kwa dakika moja. Ninataka kuzungumza nanyi, ninyi nyote. Kwa nini mnataka mfalme? Yehova ndiye Mfalme wenu."

88 Kwa nini mnataka kanuni ya imani? Biblia ndiyo kanuni yenu ya imani. Biblia ndiyo Kweli. Kanuni za imani ni za uongo. Mmekufa, ni za kujibunia.

89 Ati "Kanuni ya imani ya mitume," nionyeshe hiyo katika Biblia. Yeyote aliyepata kusikia kitu kama hicho, "Ninaamini katika ushirika wa watakatifu"? Mtu yeyote anayeamini katika ushirika wa watakatifu, ni mwanamizimu, ushirika wa wafu. Kuna Mwombezi mmoja tu kati ya Mungu na wanadamu, huyo ni Kristo; na Yeye hajafa, bali yu hai milele, amefufuka katika wafu. Waprotestanti wanameza hilo, huku wakiwa na ukosi mduara, nami sijui ni kitu gani kingine; pamoja na katekismo zote za makanisa, wanaimeza vivyo hivyo tu. Wanaipenda, hakika, kama walimwengu wengine.

90 "Loo, mnajua, tulikuwa wapentekoste. Tulisimama chini pembeni, tukiwa na tari mkononi mwetu, na kuomba. Nao wanawake wamesimama pale, na nywele zao ndefu zikining'inia chini, na kumsifu Mungu, na mambo kama hayo."

91 Loo, jamani, masalaale! Mnajua vema kuliko kufanya hivyo. Wangekucheka moja kwa moja usoni pako, Mkristo halisi angekucheka; kusimama huko nje na chungu cha nywele zilizokatwa namna *hiyo,* na sufuria kubwa la rangi namna *hiyo,* na nguo iliyoonekana kama mnyama aliyechunwa ngozi. Na kutoka nje namna hiyo, na kujiita, huko nje, "mtakatifu wa Mungu"? Unajua vizuri zaidi ya hapo. Vivyo hivyo ulimwengu unajua vizuri zaidi ya hapo. Aibu kwenu. Afadhali ukae pembeni, huwezi kutoa zaidi ya hiyo. Mimi si mkosoaji. Sijarukwa na akili. Ninawaambia Kweli, nanyi mtaona katika siku zijazo, hilo. Lakini ni kama tu ilivyokuwa sikuzote. Daima litapita juu, ndipo hawataliona mpaka limeenda mbali sana. Wamefanya hivyo kila wakati. Wamefanya hivyo.

92 Bibi-arusi wa Yehova alitaka kufanya ukahaba na hao watu wengine, kama hao wengine. Hivyo ndivyo bibi-arusi wa Yesu alitaka kufanya.

93 Mzee Samweli, ambaye Neno lilimjia! Neno huwajia akina nani? Manabii. Kitu gani? Maskini nabii huyo akaja, akasema, “Sasa hebu kidogo, enyi watoto. Kwa nini mnataka kutoka mkayafuatilie hayo?” Kasema, “Hivi nimewahi kuwaambia lolote katika Jina la Bwana, isipokuwa lile lililotimia?” Mnakumbuka hilo? Ni wangapi waliowahi kusoma hayo? Hakika, mmeyasoma. “Nimewahi kuwaambia lolote katika Jina la Bwana, pasipo kutimia? Na jambo lingine, je, nilitoka, nikifanya mikutano mikubwa ama kadhalika, na kuwanyang’anya pesa zenu? Je, nilifanya hivyo?” Akasema, “Nimewahi kuwaomba chochote?” Ninazungumza juu ya Samweli sasa, naam, mtu fulani ambaye Neno la Bwana lilimjia. Kasema, “Je, niliwahi kuwaomba mu—mu—muweke *kiasi fulani*, na kufanya *hivi-na-vile*?”

“La.” Wakasema, “La, kamwe hukufanya hivyo. Kamwe hukutwambia lolote ila lililokuwa kweli.”

Akasema, “Basi kwa nini mngetaka kufuata *hayo*?”

Wakasema, “Samweli, wewe, umesema kweli tupu. Lakini tunalitaka, kwa vyovyote vile.”

Hivyo ndivyo hasa kanisa la Kipentekoste lilivyofanya.

94 Hiyo ndiyo sababu sijiungi nao. Hakika. Ninataka kukaa bikira mbele za Mungu, pamoja na Neno Lake. Kama wao. . . Si lazima niwe na maonyesho makubwa na mambo kama haya. Nimeyakataa. Sikutaka kujifunga. Hiyo haikuwa hekima yangu; hiyo ilikuwa ni hekima ya Mungu. Kama ilinilazimu nitoke nje, kusudi nipate. . .ilinibidi kutafuta misaada kwa watu na ibilisi, na kuwaambia, “Naam, sina budi kuwa na *kiasi fulani* kwa ajili ya matangazo ya televisheni, na sina budi kuwa na *kiasi fulani* kwa ajili ya *hili*. Hamna budi kuyalipia,” ingenibidi kuwabembeleza namna hiyo, pia. Lakini sijawahi kuwaambia lolote katika Jina la Bwana ila lile lililotimia. Sikuwaambia lolote ila Neno. Amueni, wenyewe. Nimewahi kuwaomba chochote? La, bwana. La. Mungu ameshughulikia jambo hilo. Sina mipango mikubwa ya kuunga mkono. Nisingekuwa na mmoja. Kila mtu aliye wa Mungu atamsikia Mungu. Kujisikia tu kuongozwa na Roho mahali pa kwenda na jambo la kufanya, na kufanya hivyo, hilo tu ndilo linalohitajika. Niweke hilo. Sio mpango mkubwa mno wa kutengeneza pesa wenye mamilioni ya dola ndani yake, mamilioni na mamilioni na mamilioni, na baadhi yao sasa wanajenga mamilioni na mabilioni ya dola ndani yake.

95 Si—sijisikii vibaya kuhusu kukosoa. Ni ukosoaji unaostahili. Sitaki kuumiza hisia za mtu yeyote. Lakini afadhali niudhi hisia za mwadanadamu, kuliko kuumiza hisia za Mungu. Kama Yeye alikuagiza na kukutuma huku nje, fanya mambo haya, na akalithibitisha miongoni mwa watu, basi unapaswa kulisikia. Ninawaambia Kweli. Mungu anathibitisha kwamba ni Kweli. Ni

kwa ninii tu . . . Sio tu ishara Zake, bali Yeye analithibitisha kwa Neno Lake, ni Kweli. Hiyo ni kweli kabisa.

96 Kwa hiyo bibi-arusi wa Yehova akafanya ukahaba. Naye alifanya nini? Alileta kundi la wana haramu tena. Hiyo ni kweli? Tunajua ni Kweli. Hata ilibidi aondolewe na Mfalme Nebkadreza, na kadhalika.

97 Bibi-arusi wa Kristo amefanya vivyo hivyo. Kuna shida gani? Hawezi kungojea. Loo, la. Huh-uh. Hawezi tu kungojea. Hawana budi kutengeneza kitu fulani. Hawawezi kumngojea Roho Mtakatifu aje aingie Kanisani. Mnaona, inawabidi kupata wengi zaidi katika madhehebu yao.

98 Kama lingalidumu jinsi lilivyokuwa huko nyuma, miaka mia moja iliyopita ama miaka hamsini iliyopita, wakati Pentekoste ilipoanza kwa mara ya kwanza katika siku hizi za mwisho, wakati Neno lilipoanza kuhubiriwa; kama lingalidumu namna hiyo, labda lisingekuwa na zaidi ya washiriki hamsini, leo hii. Hiyo ni kweli. Lakini wangekuwa waliooshwa kwa Damu. Wangekuwa na Nguvu za Mungu ndani yao. Ulimwengu ungekuwa ukitetemeka chini ya ushawishi wake mkuu wa Neno, mwili, likinenwa, Neno kwa Neno.

99 Lakini, siku hizi, mbona, ni shaba iliayo na upatu uvumao. Hiyo ni kweli. Imekuwa tu upuuzi, kichekesho, fedheha kwa ulimwengu, aibu kwa Mungu.

100 Nilienda mahali fulani, Ndugu watatu. Mimi pamoja na ndugu wawili tulienda mahali pale ng'ambo ya pili ya Springfield, Missouri, hivi majuzi asubuhi kwa ajili ya kiamshakinywa, tukija kutoka Arizona. Na maskini mama mmoja pale ambaye Ndugu Wood alinionesha, aliyefanana na Dada yetu Collins; mwenye nywele za shaba, na lundo kubwa la nywele mgongoni. Naye akasema, "Hivi si anaonekana kama mke wa Ndugu Willard Collins?"

101 Nikasema, "Naam." Huyu hapa mama mwenye umri mkubwa zaidi anatokea. Nikasema, "Nadhani huyo ni mama yake. Angalia hilo lundo kubwa la nywele." Nikasema, "Hiyo ni papa hapa karibu na kanisa la Assembly of God, makao makuu ya Assembly of God. Hapo ndipo . . . sababu ya wao kuwa hivyo."

102 Na maskini dada wengi sana wameketi mle ndani wenye nywele kichwa maji, huko nje namna *hiyo*. Hao walikuwa ni wanafunzi. Maskini Riki na hao wote huko nje, mwajua, wakiendelea. Wote wamebeba Biblia mikononi mwao. Kwa hiyo tukawaangalia mpaka wote wakatoka nje, wakicheka kifichifichi, wakicheka, wakipiga makelele, kama tu watu wa kisasa. Hilo—hilo ni zao la Pentekoste linalokuja kwa ajili ya kesho, kama kuna kesho. Kwa nini? Kwa nini? Kwa nini? Kwa sababu hizo ni mbegu zilizopandwa. Kweli kabisa.

Alipotoka nje, wote wakatoka, maskini mama huyu akarudi, akasema, "Naweza kuwafanyia jambo lolote?"

Nikasema, “Nataka kukuuliza swali.”

“Naam, bwana.”

Nikasema, kama mgeni. Nilifikiri huenda anatujua. Nami nikasema, “Ile si ni shule ya Biblia pale ng’ambo?”

Akasema, “Naam, bwana, ndivyo ilivyo.”

Nikasema, “Nadhani mnapata biashara nyingi sana kutoka huko.” Sasa, huyo alikuwa ni Ndugu Fred Sothmann aliyeketi huko nje, na Ndugu Banks Wood pale, wawili wa wadhamini wa kanisa. Nami nikasema . . .

Akasema, “Naam, ndivyo ilivyo.”

Nikasema, “Nadhani wewe ni wa huko?”

Akasema, “La.” Kasema, “Samahani. Sijui.”

Nami nikasema, “Sababu ya kuwazia hilo ilikuwa ni kwa sababu ya nywele hizo nzuri, ndefu ulizo nazo. Nadhani huyo ni mama yako?”

Kasema, “La, bwana.” Kasema, “Yeye hufanya kazi tu hapa.” Akasema, “La, sininii . . . ” Kasema, “Ninapenda nywele ndefu. Nina msichana mdogo. Sina budi kumfanya awe na nywele ndefu, pia.” Kisha kasema, “Mume wangu anapenda nywele ndefu.”

Nikasema, “Mungu ambariki.” Na kwa hiyo akasema, vema, akasema . . . Nikasema, “Vema, ni ajabu. Je, hao walikuwa ni wanafunzi humu ndani, hao wasichana wenye nywele zilizokatwa kwa mikato ya mchongoko namna hiyo, kama mama taifa?”

“Naam.” Tulipotembea . . .

Nikasema, “Asante.”

103 Akatoka nje. Nikasema, “Mungu alimweka mwanamke huyo hapo awe kemeo kwa kundi hilo la watoto waliozaliwa haramu ng’ambo ya barabara.” Hiyo ni kweli.

104 Haramu, wakiyafuata mambo ya ulimwengu! Ni wanawake wangapi waliomfuata Yezebeli, mama taifa wa nchi hiyo, ni wangapi wao mnafikiri wako Mbinguni, usiku wa leo, leo? Mnaona? Mnaona? Mambo ya ulimwengu! “Ukiipenda dunia au mambo yaliyomo katika dunia, kumpenda Mungu hata hakumo ndani yako.” Hao hapo. Ni kitu gani hicho? Mazao yaliyo bora sana ya kesho, katika Pentekoste, shirika kubwa kuliko yote kwenye taifa. Haya basi. Huyo ndiye bibi-arusi. Silipati. Vema.

105 Anajaribu kufanya nini? Loo, yeye hujibunia kuruka-ruka kidogo jukwaani. Si kuifanyia mzaha; ni sawa. Anajibunia kitu kingine. Kwa nini? Kuwaingiza washiriki kanisani. Kuna shida gani? Kamwe hawezi kungojea. Mnaona? Hawezi kumngojea Mungu afanye hivyo. Hawana budi kuwaingiza washiriki mle mahali fulani. Kwa hiyo wanawaambia, “Hamna budi kufanya hivyo,” nao hao wanaondoka. Mnaona? Hiyo hapo ile mbegu,

ikipanda juu moja kwa moja. "Huna budi kufanya hivyo." Nime. . .

106 Mimi ni mmishenari. Nimewaona Waafrika wakichukua damu ya mnyama na kuimwaga juu yao wenyewe, namna *hii*, uchi kabisa, wanaume kwa wanawake. Wakijipaka rangi usoni. Huko ndiko lilikotoka. Rangi ilitokana na tabia ya kipagani; si kwa ajili yetu sisi wanadamu, Wakristo, waaminio, kamwe haikuwa. Hapakuwapo na. . .Mwanamke mmoja, katika Biblia nzima, aliyewahi kujipaka rangi, huyo alikuwa ni Yezebeli, ibilisi. Kwa hiyo basi yeye. . .Walijipaka rangi usoni mwao. Vitu vikubwa virefu masikioni mwao, kama bloku za mbao, Wazulu. Ni bloku ya mbao, kurefusha nyama ya sikio ining'inie chini kabisa *kule*. Wakati mwingine hupasua midomo yao, na kuipanua sana. Wanadhani inapendeza. Wanapaka, juu ya matiti yao na chini kuizunguka miguu yao na kadhalika, damu, kisha wanachukua na kufanya milia kama punda milia. Na kupaza sauti, kucheza katika roho, na kunena kwa lugha, na kuabudu pepo. Ati ushahidi wa Roho Mtakatifu?

107 Nimekuwa moja kwa moja kule India walipokuwa na watembea motoni, na kadhalika, na ninajua ni kweli. Sanamu kubwa mno kule yenye rubi masikioni, kama hereni, na vitu kama hivyo. Nao wanajitesa, na kuchomeka vitu mwilini mwao, na—na kujicharaza wenyewe. Na kushona midomo yao kama wamedanganya, na kufanya vitubio. Na kuchomeka kitara midomoni mwao *hapa*, ama kupitia kwenye kidevu chao, kupitia puani mwao, na kukichomeka namna *hiyo*. Wanachukua ndoana za kuvulia, zilizo na mipira kama ya mti wa Krismasi, waijaze maji, na kuchomeka maelfu yao juu ya miili yao, moja kwa moja kupitia mwilini. Na kupanda kule na kucheza karibu na sanamu hii, namna hiyo, na kumchinja mbuzi na kuabudu namna hii. Na kupitia moja kwa moja kwenye moto mkali sana, bila kuungua. Hebu baadhi yenu Wapentekoste mlijaribu.

108 Lakini ilitendeka, wale wana wa Kiebrania, bali kamwe hawakumjaribu Bwana Mungu wako. Walitupwa tu ndani yake. Hawakujaribu kujitengenezea kitu fulani.

109 Hiyo ndiyo shida ya Wapentekoste siku hizi, wanajitengenezea kitu fulani. Hawawezi kungojea. Ee Mungu! Kamwe hawawezi kungojea, kwa hiyo wanafanya uzinzi. Amina. Magugu, kujitengenezea kitu fulani, nalo linazaa nini? Kama ilivyofanya mara ya kwanza, yule bibi-arusi wa kwanza ambaye asingeweza kungojea.

110 Alileta mauti kupitia kwa mtoto aliyezaliwa haramu, ambaye sisi sote ni watoto wake. Lakini Mungu alikuja katika mwili, kutupa Kuzaliwa kwingine, kuturudisha kuwa wana na mabinti asili wa Mungu. Mnaona? Haya basi. Shahawa za Uhai za Hawa hazikutumika. Kamwe hazikutumika. Kwa nini? Alizichanganya. Akazificha, badala ya Adamu kumjia awe

bibi-arusi, hapo wakati uliokusudiwa utakapotimia. Kama tu vile Kristo atakavyofanya, angekuja kwenye hilo kundi. Kristo angekuja kwa Kanisa Lake. Aliahidi kufanya hivyo.

Mungu aliahidi kuwazidisha, bali iliwabidi kungojea mpaka wakati wa Mungu.

111 Hiyo ndiyo shida siku hizi. Hawataki kungojea wakati wa Mungu. Wanataka kupata kitu kingine. Na kwa hiyo ibilisi ana hekima papo hapo ya kuwapa, kuunda dhehebu, liwe kubwa kuliko hayo mengine.

112 Sasa je, mnaona ni kwa nini ninakipinga kitu hicho? Hakika. Ninakipinga, kwa kila kitu kilicho ndani yangu. Maadamu Neno liko humo ndani, daima litakuwa dhidi yake. Mungu anapinga hilo. Mungu alisema analipinga. Hiyo ni kweli.

113 Asingeweza tu kungojea kamwe, kwa hiyo mbegu ya Hawa haikufanya kazi. Aliichangayana na uongo wa Shetani, bibi-arusi wake wa kupendeza akachafuliwa. Vivyo hivyo na bibi-arusi wa Kristo. Bibi-arusi, ni kitu gani kilichomfanya achafuke, bibi-arusi wa Adamu, sasa? Kwa sababu hakudumu na Neno la Mungu. Hiyo ni kweli?

114 Nauliza. Sasa, kama sivyo, usiseme. Lakini kama ndivyo ilivyo, liseme. Sababu ya nanii wa Mungu. . .Sababu ya bibi-arusi wa Adamu. . .Hao hapo watatu: Adamu, Kristo, Mungu. Sababu ya bibi-arusi Adamu kamwe kutozaa ifaavyo, Mtoto wa Uzima, ni kwa sababu hakuliamini Neno la Mungu. Kama hiyo ni kweli, semeni, "Amina." [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Sababu ya mke wa Yehova kufukuzwa, ama bibi-arusi Wake, ilikuwa ni kwa sababu alilikataa Neno la Mungu, yule nabii. Hiyo ni kweli? ["Amina."] Sababu ya bibi-arusi wa Kristo kupewa talaka, ni kwa sababu amelikataa Neno la Mungu, kama Hawa alivyofanya, kama hao wengine walivyofanya. Kweli kabisa. Wote makahaba, wote wamechafuliwa, mume wao asingeweza kuwafikia. Walikuwa tayari wametiwa mimba kabla mume wao hajawafikia. Ee Mungu, kama hilo si la kusikitisha kuliona! Wazia juu ya kijana mwanamume akimjia mwanamke fulani, na kumpata akiwa na mbegu ya mwanamume mwingine ndani yake. Ni jambo la jinsi gani! Hivyo ndivyo Mungu amefanya. Hivyo ndivyo Adamu alivyofanya. Hivyo ndivyo Kristo amefanya. Loo! Naam.

115 Kamwe hakudumu na Neno, na kusababisha hali ya—ya uchotara. Hivyo ndivyo Israeli walivyofanya. Mnaona mahali alipo? Hivyo ndivyo bibi-arusi wa Kristo alivyofanya. Mnaona mahali alipo? Moja kwa moja ameshikana tena na hao wengine.

116 Bibi-arusi wa Kipentekoste wa Kristo alifanya vivyo hivyo. Hawezi kuzaa Watoto wa kiroho wa Neno, kwa kuwa yeye mwenyewe ni chotara. Anawezaje kufanya hivyo, wakati amejichanganya mwenyewe na madhehebu? Tayari amejiunga nayo, na kadhalika, kama tu walivyo. Ameingia ndani na Baraza

la Makanisa, na kadhalika, chotara tu kama hao wengine walivyo. Anawezaje kufanya hivyo? Hawezi.

Sasa, nina mengi sana ya kusema, nami sina budi tu kuharakisha juu ya haya. Mimi . . . Kila mmoja wao ninataka kuhubiri juu yake. Mnaona? Sasa angalieni.

117 Bibi-arusi wa kweli, haleluya, kutakuwako na Mmoja. Kwa nini? Amechaguliwa tangu zamani. Yeye hataunda dhehebu, kwa sababu amechaguliwa tangu zamani. Mnaona? Haimbidi kuwa na wasiwasi kuhusu madhehebu fulani. Tayari amechaguliwa tangu zamani kupachukua mahali hapo. Angaliemi. Kama vile Mariamu . . .

Ninawatakeni mpate jambo hili sasa, wala msikose. Mko tayari? Semeni, "Amina." [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

118 Kristo atakapokuja kwa Bibi-arusi Wake, atakuwa bikira kama Mariamu alivyokuwa. Kwa maana Mungu hatamleta Kristo kupitia katika tumbo la uzazi la kahaba, wala hatamleta Bibi-arusi. Hawezi kuleta Neno Lake kupitia kahaba wa Neno Lake.

119 Hayo ni maneno ya kutisha, lakini hivyo ndivyo Biblia inavyosema. Ninasema kile Hiyo isemacho. Maana, ni . . . Hili halina budi kufahamika.

120 Bibi-arusi wa kweli, kama vile Mariamu, atakuwa na tumbo bikira la uzazi kwa ajili ya Bibi-arusi wa Neno, ambaye ni Kristo. Wakati Kristo, Neno, atakapomjia Bibi-arusi, Bibi-arusi atakuwa sawasawa na alivyo Yeye, bikira kwa Neno. Ee Mungu!

Natumaini—natumaini yanakolea, Ndugu Neville. Mimi . . .

121 Mnaona? Mnaona? Natumaini mnaelewa. Yeye alikuwa nini? Neno, Neno la Mungu. "Kwenye vazi Lake alikuwa na Jina lililoandikwa, 'Neno la Mungu.'" "Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno, alifanyika mwili akakaa kwetu." Yeye ni Mungu, na Mungu ni Neno.

122 Na wakati Bibi-arusi Wake atakapokuja, atakuwa kitu kile kile alicho Yeye. Bikira! Je, Kristo alikuwa mfuasi wa dhehebu fulani? Je, Yehova alikuwa? Wala na Bibi-arusi Wake. Yeye mke ni sehemu Yake mume. Hahitaji mafundisho ya sharti. Hatakuwa na yoyote. Atakuwa bikira kabisa. Jinsi gani? Kwa Neno. Amina. Ataitikia kila Neno asemalo Mungu, kwa, "Amina! Amina!" Loo! "Na iwe kwangu kulingana na Neno Lako. Amina!" Loo, jamani! Haya basi. Kuliitikia Neno la Mungu.

123 Atakuwa na tumbo bikira la uzazi. Atatoka kwa kitu gani? Tumbo bikira la uzazi, Neno. Yesu alitoka katika nini? Tumbo bikira la uzazi. Mnaona?

124 Wakati Adamu alipomjia mkewe, alikuwa na mimba. Alikuwa amefanya jambo fulani. Alikuwa amechanganywa. Alikuwa chotara, yule mtoto, naye akafa. Lakini wakati

Yusufu alipomjia bibi-arusi wake, alikuwa ametiwa mimba, bali kwa Uzima. Mke wa Adamu, ama bibi-arusi wa Adamu, wakati Adamu. . . Kabla hawajawa pamoja; kama tu Yusufu na Mariamu, kama tu Kristo na Kanisa sasa. Hivi hamlioni? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Mnaona?

125 Na kabla hawajakutana, Adamu na Hawa, alitiwa mimba ya mbegu potovu kutoka kwa nyoka. Ndipo Adamu alipomjia mkewe, alimkuta ametiwa mimba hata kufa. Mnaona? Mauti! Jinsi gani? Amekufa kiroho na kimwili.

126 Lakini wakati Yusufu, yule mwanadamu, alipomjia mkewe. . . Utukufu! Ni vigumu kumshika. Alikuwa ametiwa mimba ya Uzima, Neno la Mungu, mwili tumboni mwake.

127 Kurudisha Neno hilo lililonenwa, kurudisha Neno hilo la Mungu ambalo lilikuwa ni Neno hapa, likapitia katika tumbo la uzazi la mwanadamu. Amina. Mungu atafanya hivyo, kwa vyovyote vile. Yeye alilinena, na halina budi kuwa hivyo. Amina. Huyo ni Mungu wetu. Loo, hilo limekolea, ndugu, kama unaweza kuliyeyusha, unaweza kulipiga.

128 Hapo ndipo alipoona, wakati—wakati Adamu alipomjia mke wake, alitiwa mimba ya mbegu mbaya. Wakati Yo-. . . Mbegu hiyo ilikufa. Yusufu akamjia wake, alikuwa ametiwa mimba. Sasa, ni kitu gani kilichosababisha kutiwa mimba tofauti? Kwa sababu kwamba mke wa Adamu alitilia shaka Neno. Hiyo ni kweli? Bibi-arusi wa Yusufu aliliamini Neno. Hiyo ndiyo tofauti.

129 Kwa hiyo, ni nini, basi? Ni Neno, loo, hilo Neno la thamani. Ndivyo ilivyo. Ulimwengu uliumbwa kwa Neno la Mungu. Haleluya! Hapo ndipo mahali pangu, papo hapo. Acha madhehebu yote na kila kitu kingine kianguke, wafanye watakachofanya. Juu ya Neno hilo ninasimama.

130 Hiyo ndiyo sababu nimefanya yale niliyofanya. Hiyo ndiyo sababu nimeyaangusha madhehebu. Mnasema, "Vema, yeye ni ninii tu. . . huyavunja makanisa." Walisema jambo lilo hilo kumhusu Bwana wetu. Mnaona? Wanalisema kila wakati. Mnaona?

131 Sasa, sasa, Yeye alimpata. Kristo anamjia bibi-arusi Wake; anampata vipi? Jambo lile lile. Kwa nini? Mara ya kwanza alipoanza. . . Sasa sikilizeni. Sitaki mlikose hili. Alipoanza safari, alikuwa bikira. Angekuwa sawa. Akaendelea moja kwa moja, kanisa hilo la mwanzoni, lilikuwa zuri sana. Mungu alimpa bibi-arusi, naye alifanya nini? Kama unajua historia, katika mwaka wa 606, anashuka moja kwa moja kule chini na kujitia mimba kwa mafundisho ya sharti ya Kirumi, madhehebu. Na tangu hapo, na kuendelea, yule "mama kahaba" wa kale, katika Biblia, akazaa makanisa, nayo yalikuwa "malaya," ambao ni kahaba. Hao ni Waprotestanti, kwa sababu walizaliwa, kila mmoja wao, naye, na kila mmoja alichukua kitu chake

mwenyewe, dhehebu. Sasa mnaona ni kwa nini ninalipinga? Vema.

132 Sasa, kwa kuwa kuzaliwa kwa Neno ni Kristo, si kwa kuchafuliwa na madhehebu. Kanisa la mwanzoni, hakuna madhehebu, Neno tu, na kumwagiliwa maji na Roho. Ndugu, ninii. . . Mungu aliweka Neno chini namna hiyo, naye Roho Mtakatifu akalimwagilia maji, na Yeye huyo akaondoka. Aliwazaa watoto. Bila shaka.

133 Lakini kanisa hili haliwezi kufanya hivyo. Limejiundia dhehebu sana. Mnaona? Haliwezi kufanya hivyo. Limejichanganya na ulimwengu. Angalieni kile walichofanya, sasa. Sasa nini?

Mungu alithibitisha Neno Lake kupitia Mwili Wake. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

134 Ndipo akaanza kufanya ukahaba, kama mke wa Adamu alivyofanya huko Edeni, na mke wa Yehova alivyofanya katika siku za Samweli, ambaye alijitwalia mfalme. Akamtaliki Mungu, Mume wake aliyemposa na Neno Lake; na nabii Wake, njia Yake ya kulitoa Neno Lake; kisha akaanza kufanya ukahaba, kama mataifa mengine. Ndipo Mungu akamtaliki. Ndivyo amefanya siku hizi. Tendo lile lile.

135 Wana wa huyo bibi-arusi hufanya uzinzi, mnaona, na. . . Bibi-arusi, Mwana wa Mungu. . . Bibi-arusi Wake kutoka Pentekoste, bikira kwa Neno, alifanya ukahaba na kufanya uzinzi kama tu mke wa Adamu alivyofanya, kama tu vile mke wa Yehova alivyofanya. Na huyu hapa mke wa Mwana, anaanza kufanya ukahaba, akifanya uzinzi na miungu ya Kirumi; wingi, miungu! Na kwa ajili ya wapenzi wake, miungu wa Kirumi, alijaribu kumchukua Mume wake mwenyewe na kumgawanya vipande vitatu, ili kuwafurahisha wapenzi wake. Mungu awarehemu. . . Hakika, wana mamia ya miungu; loo, hakika, Astarte, mungu-jua, na—na Baalimu, mungu-jua, na malkia wa mbinguni, na upuuzi huo wote hapo. Kwa hiyo, bibi-arusi, kuwafurahisha wapenzi wake wenye sifa mbaya.

136 Hivi Mungu hakunena kule katika Nyimbo za Sulemani, na kusimulia jinsi mke Wake alivyokuwa si kitu ila kahaba, na kuketi akiwa wazi wakati wote, na kumchukua kila mpenzi aliyepitia? Ninazungumza waziwazi, lakini hivyo ndivyo Biblia ilivyosema. Kila mwanamume aliyetaka kukimbia naye, angeweza kukimbia naye.

137 Hilo ndilo jambo lile lile bibi-arusi wa Kristo amefanya. Akajifungua kwa kila tabia chafu na potovu ya kila shirika walilopata kuwa nalo, akifanya jambo lile lile.

138 Nitakosolewa kwa ajili ya Hili. Hilo ni sawa. Nitabarikiwa kwa ajili Yake, pia, kwa kuwa itakuwa ni Kweli. Ni Kweli ya Mungu. Maana, Yeye anataka isemwe, na Hili hapa. . . Ninajaribu niwezavyo kuisema. Mnaona?

139 Alijaribu kuwafurahisha wapenzi wake wengi. Kwa kufanya hivyo, akachanganyisha mbegu, akajaribu kuchanganya pamoja na wapenzi wake, Neno la Mungu. Kwa hiyo haingefaa kitu, kwa hiyo akasema, “Likane Hilo,” na kutoa neno lake mwenyewe. Sasa yeye anadai kuwa ni Neno, mwenyewe. Lakini msiwaache Wakatoliki . . . ama Waprotestanti wawakosoe Wakatoliki, maana wanafanya vivyo hivyo katika baraza la makanisa yao wenyewe, kufanya ukahaba. Si ajabu wanaitwa malaya. Hilo ni kali, sivyo? Hilo lilichuna ngozi mgongoni mwako, bali hilo ndilo linalohitajika kufanywa, kukuamsha wakati mwingine. Sawa. Hivyo ndivyo alivyofanya hasa. Alimwacha Yesu, Mume-Neno.

140 Na kama vile Samweli, walimwacha Samweli wakamchukua Sauli. Wakamwacha nabii, aliyetiwa mafuta kwa Neno, wakamchukua mfalme mwenye fimbo ya kifalme. Wakati, hatimaye angekuja kwa yule Mfalme, ile fimbo ya kifalme katika ule Utawala wa Miaka Elfu. Lakini sasa amekataliwa. Alienda kwa Mataifa kwa ajili ya Bibi-arusi. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Ni Neno.

141 Sasa, alimwacha Yesu, Neno; Yesu, Neno; na kuolewa na mtu mwingine, anayeitwa papa, kwa mafundisho ya sharti. Sasa yeye hana Yesu. Yeye ana papa. Sasa hatuna . . . Waprotestanti hawana Yesu. Wana dhehebu, kitu kile kile, sanamu ya mnyama. Kwa hiyo, hawezi kuwapa watoto wake Uzazi wa-Neno, hata mmoja wao. Yeye mwenyewe ni kahaba. Biblia ilisema alikuwa. “Alikuwa na kikombe mkononi mwake, naye alikuwa akiwapa watu mafundisho yake, ambayo yalikuwa ni chukizo, uchafu wa uasherati wake.” Uasherati ni nini? Ni kuishi kichafu. Na mafundisho yake anayowapa watu, ni uchafu wa uasherati wake. “Na wafalme wa dunia, na wote, walilewa kwa mvinyo wa uasherati wake.” Kweli kabisa. Waangalieni. Jamani, wangeikata koo yako, katika dakika moja, kwa ajili ya jambo hilo. Si Wakatoliki tu, bali Waprotestanti.

142 Sikilizeni, ninyi Wamethodisti. Ni nani aliyemwua Joseph Smith? Sasa payukeni. Ingawa, siamini mafundisho yake, wala siamini yenu. Hilo haliko huko nje; liko hapa. Hiyo ndiyo sababu. Joseph Smith alikuwa na haki ya kuhubiri dini yake hapa katika taifa hili, kadiri mlivyo nayo, lakini mlimwua hapa juu Illinois. Mkampiga risasi, bila sababu, kwa sababu alikuwa na kitu tofauti kidogo. Halafu mnapayuka-payuka kuhusu kanisa Katoliki. Tokeni kwenye lundo hilo la upuuzi, ninyi Wamethodisti mliokusudiwa Uzima wa Milele. John Wesley angepinduka kaburini mwake; mkitenda namna hiyo. Hakika, atafanya hivyo. John Wesley kamwe hakuanzisha kanisa kama hilo. Kundi la akina Riki na Elvis walifanya hivyo baada ya kifo cha John, hiyo ni kweli, sio John Wesley.

143 Si maskini hao wapentekoste wa mwanzoni waliopata kufanikisha matokeo kama haya. Ni kundi lile lile, baada

ya kifo hiki. Hiyo ni kweli. Yesu Kristo asingeanzisha kitu kama tulicho nacho sasa, kinachoitwa Pentekoste, wala Roho Mtakatifu. Lakini ni kitu mlicho nacho hapa, badala yake.

144 Lakini Roho Mtakatifu ni kitu wasichoweza kuua sasa. Atamchukua Bibi-arusi, kwa vyovyote vile. Amina. Atamchukua Mmoja, kwa vyovyote vile. Alisema atafanya hivyo; alimchagua tangu awali.

145 Alimwacha Yesu, Neno-Mume wake, apate kuolewa na papa, kwa hiyo hawezi Kuzaa, Kuzaa kiroho. Anaweza kuzaa kimadhehebu, sasa. Ana mbegu nyingi za hayo. Hawezi kuzaa Uzao wa kiroho. Yeye, kwa sababu alikuwa kahaba, kitu pekee anachoweza kutoa ni maisha ya kimadhehebu na upuuzi chungu nzima.

146 Kanisa Katoliki, lenyewe, limeundwa juu ya ushirikina kiasi wa Ukristo na—na lundo la Urumi.

147 Na kanisa la Kipentekoste ni baya vivyo hivyo, kundi la kurukaruka, na kupaza sauti, na kunena kwa lugha, na mambo kama hayo. Kwa jumla, hasira ya kutosha kupigana na msumeno uvumao, na kukufukuza kwenye kusanyiko lao. Kama Mungu akiingia mle ndani na kuwafufua wafu, kama hukukubaliana nao, wangekufukuza kama wewe hukuwa wa dhehebu lao.

148 Sasa, maskini huyu "mama kahaba," nitamrejea kwa dakika moja. Anadai mamlaka ya kusamehe dhambi. Lakini, huhukumiwi kwa madai yako, hujulikani kwa madai yako. Unajulikana kwa matendo yako. Angewezaje kusamehe dhambi? Mwangalieni.

149 Wakati Yesu alipofanya jambo lile lile, wao walisema... "Nihukumuni, nionyesheni mahali sikuliamini Neno." Anadai mamlaka ya kusamehe dhambi, lakini hizo huja tu kwa Neno. Hiyo ni kweli. Mungu, pekee, ndiye anayeweza kusamehe dhambi. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Hivi hao Mafarisayo hawakusema hivyo? Nia, shida ya kundi la wanafiki vipofu ilikuwa ni nini? Mbona? Kwa sababu hawakuona huyo aliyesimama pamoja nao alikuwa ni Neno. Yeye ni Neno. Utukufu kwa Mungu. Hiyo ndiyo sababu Yeye angeweza kusamehe dhambi. Alikuwa Mungu. Alikuwa ni Neno lililodhihirishwa.

Sasa kanisa Katoliki linasema Yesu aliwapa mamlaka. Aliwapa; alilipa Kanisa mamlaka. Hiyo ni kweli. Tunaamini hilo.

150 Binti zake wote ni makahaba. Binti zake wote, binti zake wa kimadhehebu, ni makahaba. "Ndugu Branham, hilo ni Neno kubwa." Si Neno langu. Hilo ni Neno Lake. Hiyo ni kweli kabisa. Si langu. Ni Lake. Vema.

"Vipi," unasema, "wakoje, walifanyikaje makahaba? Vema, wao ni watu wazuri, *hivi-na hivi*."

151 Sisemi neno juu ya jambo hilo. Sisemi kile walicho. Sisemi Wakatoliki si watu wazuri, wazuri kama mtu yeyote. Wao ni wanadamu, kama tulivyo sisi. Lakini, inapofikia kwenye maskini kanisa hilo la kale, liko makosani. Waprotestanti ni vivyo hivyo. Methodisti ni zuri kama Baptisti ama Wapentekoste, ama mtu mwingine yeyote. Wote ni sawa.

152 Lakini jambo lenyewe ni kwamba, anawezaje basi kuwa kahaba? Kwa nini? Mpe jaribio la Neno. Hivyo ndivyo unavyojua. Uh-huh. Mjaribu kwenye Neno, wakati mmoja, uone asemayo. "Loo, bila shaka, tunafundishwa katika seminari ya kwamba—ya kwamba siku hizo hazininii. . . Ni. . . Ilikuwa hivyo, lakini, hah, hiyo ilikuwa huko nyuma kabisa katika siku za mitume. Hiyo ilikuwa tu kwa ajili ya mitume, pekee." Ninyi mnaojiita Kanisa la Kristo, "Ati mnanena ambapo Biblia inanena, na kunyamaza. . . " Vema, ningetaka kuwasikia mkizungumza sasa. Uh-huh. Uh-huh. Uh-huh. La. Nyamazeni. Neno la Mungu hunyamazisha kila kitu, ndugu. Hakuna mtu anayeweza kujivuna. Hiyo ni kweli.

153 Binti zake wote ni makahaba. Vipi? Sawasawa na mama yao, wakifanya uasherati wa kiroho dhidi ya Neno. Hivyo ndivyo kanisa Katoliki lilivyokuwa kahaba, hivyo ndivyo binti zake walivyofanyika makahaba, jambo lile lile, uasherati wa kiroho dhidi ya Neno.

154 Yeye na binti zake wana tumbo la ukahaba. Ni mauti tu yanayoweza kutoka kwao. Mungu hawezi kuleta uhai kupitia mauti. Na chochote kinachozaliwa kimekufa hakiko hai. Na je, ninii. . . Kama vile Ayubu alivyosema, "Je, unaweza kutoa kitu kilicho safi kutoka katika kitu kichafu? La, hata kimoja." Sawa. Anawezaje kuzaa, mwenyewe, wakati amekufa, yeye mwenyewe? Anawezaje kuwa bikira wakati yeye ni kahaba? Mnaona? Haya basi. Hilo ndilo jambo lote. Loo, jamani!

Sasa tutafikia kitu kilichokolea sana, kilichojaa vitamini, kuanzia Mwanzo hadi Ufunuo. Angalieni.

155 Basi yeye na binti zake wana tumbo la uzazi la ukahaba. Ni mauti tu yanayoweza kutoka kwao. Ukitaka kujiunga na madhehebu, ukifikiri uko sawa, angalia mahali unapofikishwa. Unafikishwa moja kwa moja katikati ya mauti. Kweli kabisa. Kama huwezi kuona hilo sasa, wewe ni kipofu kiroho. Unaona?

156 Sasa, hebu turudi nyuma sasa na tuchukue tena, kisha tushuke tupate jambo fulani. Mnakumbuka ibada ya Jumapili iliyopita ilikuwa nini? "Lango la nafsi." Mnakumbuka? Sasa, kuna tumbo la uzazi la kimwili. Kuna tumbo la uzazi kwa ajili ya roho. Mliamini hilo? Kuna tumbo la uzazi la kiroho na tumbo la uzazi la kimwili. Nayo nia ndiyo tumbo la uzazi kwa roho. Kwa nini?

157 Sasa kumbukeni. Niliwaambia Jumapili iliyopita, na kuwachorea hapa. Hisi hizi tano zinazoingia kwenye mbegu

hii kutoka nje; kuona, kuonja, kugusa, kunusa, kusikia. Tano upande wa ndani; dhamiri, na—na kadhalika, tano kutoka ndani. Sasa, upande wa Uzima, kuna moja tu. Hiyo ni kusema, uko kwenye msingi wa hiari ya kujichagulia, kukubali, kuchukua ama kuachilia. Mnaona?

Hivyo ndivyo uzinzi. . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Hebu kidogo. [Sehemu tupu kwenye kanda.]

158 Hivyo ndivyo uzinzi unavyofanywa, kiroho; wakati wewe, ukijua vizuri zaidi, kwa Neno la Mungu, kwa kujamiiana kwa nia, unakuchukua uongo wa ibilisi, dhidi ya Neno la Mungu.

159 Hivyo ndivyo hasa Hawa alivyofanya, kwa kujamiiana kiroho, kwanza, kulikotokana na kuamini uongo wa Shetani, kuingia katika tumbo la uzazi la nia yake. Hilo liliichafua nafsi yake, likaweka mauti nafsini, ndipo tendo la kawaida likatukia.

160 Na hiyo ndiyo njia pekee ambayo mwanamke anaweza kufanya uzinzi dhidi ya mumewe, ni kwanza kumwacha mwanamume fulani amshawishie hilo, ndipo basi ampokee mwanamume mwingine ambaye si mumewe. Ndipo amefanya uzinzi.

161 Basi wakati bibi-arusi wa Yesu Kristo anaporuhusu kanuni za imani za kujibunia na mafundisho ya sharti yachukue mahali pa Neno la Mungu, anafanya uzinzi. Hivi Yesu hakusema, "Kila amtazamaye mwanamke. . . amekwisha kuzini naye moyoni mwake; amtazamaye mwanamke kwa kumtamani, amekwisha kuzini naye"? Kwa nini? Aliliacha liingie niani mwake. Hilo ndilo tumbo la uzazi linaloanzisha vitu hivyo. Shetani akaingia.

162 Tulipandwa kwa Neno. "Siku moja, nitaleta Uhai duniani na kuzidi-. . . kuijaza dunia." Kile Hawa alichoshindwa kufanya, Mariamu alikifanya. Alilichukua Neno. Hawa alichukua uongo wa Shetani. Mariamu akachukua Neno la Mungu. Na kupitia kwa Uzao wa Mariamu, anaijaza dunia tena, kupitia kwa Bibi-arusi Wake, kupitia Neno, ndipo ataleta ule Utawala wa Miaka Elfu. Kupitia hayo Neno linatangazwa, na Neno linapandwa katika kila moyo uliokusudiwa tangu zamani. Naye Roho anashuka na kulitia maji, nao hawawezi kufa. "Nitamfufua tena katika siku za mwisho." Loo, ndugu, dada, hilo—hilo ni halisi.

163 Ni kitu gani? Nia ndiyo tumbo la uzazi la roho, (Nini?) kuingiza ama kutoa. Hivyo ndivyo wanavyofanya uzinzi, ni kuchukua, kumwacha Shetani fulani, roho wa ibilisi aweke ndani yao kitu fulani dhidi ya Neno la Mungu. Ndipo amefanya uzinzi.

164 Hawa alipokea. . . Sikilizeni jambo hili. Neno-mbegu mbaya, uongo wa Shetani dhidi ya Neno la Yehova, matokeo yake yalikuwa mauti.

165 Sasa, tutatoka kwenye somo hili, katika dakika chache. Lakini ninataka kulifanya lipondwe vizuri sana kabla

halijashuka chini, mahali ambapo inanibidi kusimamia. Nitaruka ukurasa mmoja hapa, yapata sasa, kwa dakika moja.

166 Sasa angalieni. Hawa, a—alifanya nini? Alipokea mbegu mbaya. Alifanyaje jambo hilo? Kuamini uongo wa Shetani. Ni wangapi wanaosema hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Mbona, hakika, ni kweli. Hakika. Alipokea uongo wa Shetani. Angezaa nini, kwa kufanya hivyo? Shetani alisema, "Unajua, hili ni tukufu. Hili ni jambo zuri sana. Unajua uliumbiwa hilo? Mbona, kwa kweli uliumbiwa kusudi hili."

"Loo, kweli?"

"Loo, linapendeza macho. Ni zuri. Unapaswa. Unapaswa kulijaribu."

"Lakini Bwana Mungu alisema, 'Si—si—sio hivyo, bado.' Ngoja, ngoja kidogo. La. La."

"Lakini, unajua . . . "

"Loo, tukifanya hivyo, tutaninii . . . "

"Loo, hakika hamtakufa."

167 Ibilisi huyo mwenye ulimi mjanja. Hana kwato na mkia uliogawanyika, la, kama vile wangejaribu kuwafanya mwamini. Yeye ni mjanja nyuma ya mimbara. Kweli. Uh-huh. Ama, maskini Riki fulani aliyechana nywele zake kama bata, ameketi kwa mgongo wake huko nje, kumdhuru binti fulani wa mama, huyo ndiye jamaa aliyekuja huku na maskini kitu kidogo cha kupendeza . . . Loo, nitaachilia hilo.

168 Sasa, lile tumbo la uzazi, Hawa alipokea neno-mbegu mbaya. Sasa sikilizeni kwa makini sana sasa. Tutafuatilia jambo hili moja kwa moja, Bwana akipenda. Alipokea neno la uongo. Lilifanya nini? Lilikuwa ni uongo wa Shetani, kasema, "Angekuwa mwenye hekima."

169 "Vema, angeweza kuwa mfuasi wa lile kanisa kubwa. Angewaziwa vizuri mjini. Mbona, angekuwa kama watu wengine." Huh! Hakika. Hivyo ndivyo bibi-arusi wa Yehova alivyoamini hasa. Hiyo ni kweli kabisa.

Hivyo ndivyo hasa Shetani angejaribu kusema wakati Neno lilipomjia Mariamu. Lakini yeye alimtupilia mbali.

Kasema, "Jambo hili linawezekanaje?"

Kasema, "Roho Mtakatifu atakutia uvuli. Ni Neno la Mungu."

Kasema, "Na iwe kwangu kulingana na Neno Lako." Hiyo ilileta Uzima. Haya basi.

"Vema, mnajua," Shetani alisema, "wote watakucheka." Maskini msichana huyo mwenye mashavu ya waridi hakujali hilo.

170 Moja kwa moja akapanda kwenda huko Uyahudi. "Unajua, nitapata Mtoto," kabla hajahisi chochote, kwa sababu Neno lilikuwa tayari limewekwa pale. Hivyo tu. Haikumbidi kupitia mstari wa maombi, mara ya pili, mwajua. La, la. La, bwana. La, bwana. Aliamini. Hakuwa na ishara yoyote ya uhai. Kamwe hakuwa na dalili ya mimba, hata kidogo. Kamwe hakuhisi chochote. Kama . . . Kila kitu kilikuwa tu jinsi kilivyokuwa. Lakini akaenda, akimwambia kila mtu, "Nitapata Mtoto." Kwa nini? "Mungu alisema hivyo." Ni kitu gani hicho? Uzao wa kifalme wa Ibrahimu.

"Ati utapata mtoto, Ibrahimu, kwa mwanamke huyo?"

"Mungu alisema hivyo."

"Vema, uliniambia hivyo, miaka ishirini na mitano iliyopita."

"Ninajua, lakini Mungu alisema hivyo."

Jambo ndilo hilo. Haya basi. Hilo ni jambo lile lile. Unasemaje leo?

"Vema, unajua dhehebu litakufukuza."

"Lakini Mungu alisema hivyo. Mungu alisema hivyo."

"Vema, unajua, kama ukibatizwa namna hiyo . . . "

"Vema, Mungu alisema hivyo." Jambo ndilo hilo. Jambo ndilo hilo. Huyo hapo bikira wako. Huyo hapo. Sio tu kwa ubatizo, bali chochote kile, Neno lingine lote. Unaona?

Kwa hiyo, nini? Hili lilikuwa la kimwili na la kiroho pia, kwa Hawa. Kwanza, na wakati wowote.

171 Niliwaambia, na kuwaomba, asubuhi ya leo, akina dada, mnisamehe, ili niweze kutaja hilo. Wakati wowote mwanamke anapochukua hatua mbaya . . . Ninazungumza juu ya Kristo na Bibi-arusi sasa.

172 Lakini wakati wowote mwanamke anapochukua hatua mbaya, inambidi kwanza kuipokea niani mwake. Sawa. Jamaa fulani mjanja hana budi kumshawishi, naye anasikiliza hilo dhidi ya uamuzi wake bora, ndipo hilo tendo linatendwa.

173 Kwa hiyo, kwanza, alimshambulia, Shetani alishambulia nia ya Hawa. Na katika tumbo la uzazi la nia yake, akatilia shaka Neno la Mungu, ndipo tendo lenyewe likaja.

174 Na njia pekee tunayoweza kuzaliwa mara ya pili ni, kwanza, katika tumbo la uzazi la niani, kulipokea Neno, ndipo Roho anakuja juu ya Hilo na kulihuisha. Haya basi. Hilo ndilo linalofanya hilo. Hayo ndiyo mafundisho halisi ya Injili, ndugu. Ninaamini, kama Mtakatifu Paulo angalikuwa amesimama, leo hii, angefundisha jambo lile lile ninalofundisha, katika saa hii. Vema.

Matokeo yalikuwa nini kwa—kwake? Mauti ya kimwili na ya kiroho.

175 Matokeo ya wale wanaokubali njia nyingine ni nini? Inaingia katika mizaha hii waliyo nayo siku hizi, mauti ya kimwili na ya kiroho pia. Mwili na roho pia vitaangamizwa, havitakuwako tena. Hiyo ni kweli kabisa.

176 Angalieni, tumbo la uzazi la Mariamu. Tumbo la uzazi la Mariamu, ile nia ya kimwili, mnaona, lilikuwa ndilo tumbo bikira la uzazi. Kwa nini? Aliamini Neno la Mungu. Haidhuru mtu yeyote alikosoa kiasi gani, ni mambo mangapi mtu mwingine aliyosema, hayo hayakuwa na uhusiano wowote nalo. Aliamini Neno la Mungu, haidhuru. Loo, laiti ningalimalizana na hilo. Mnalipata? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Mnaona? Mnaona? Kwanza ilikuwa nia yake. Kabla lile tendo halijatendeka katika tumbo lake halisi la uzazi, tendo hilo ilibidi litendeke *humu* ndani, kwanza, kumruhusu Roho aingie kufanya kazi iliyosalia. Loo, jamani!

177 Utukufu! Kabla Kuzaliwa halisi kiroho kuweza kutokea, Neno halina budi kujitafuta Lenyewe kote niani mwako, kuliamini. "Yeye ayasikiaye Maneno Yangu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa Milele, wala hataingia Hukumuni, bali ni . . . ama kupitia wakati wa ile Dhiki, bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani." Jambo ndilo hilo. Loo, jamani!

Sasa angalia. Tumbo bikira la uzazi, nia yake; nia bikira, kuliamini Neno la Mungu.

178 Mbona, unasema, "Sasa angalia hapa. Loo, wasema, Ndugu Branham, isingeweza kuwa hivyo. Haiwezekani. John Wesley angeliona hilo. *Nanii* angeliona." Huh!

179 Hakika, ibilisi angeweza kumwambia Mariamu jambo lile lile. "Wewe ni nani? Mbona, wewe ndiwe maskini kuliko wote mjini. Wewe si kitu ila kijana mdogo, mwenye umri wa miaka kumi na sita, kumi na minane, hapa chini ukibeba maji kutoka kwenye pampu hii. Baba, amefariki; mama yako, maskini mwanamke kipofu huko chini. Ungewezaje kamwe . . . Vipi?" Ana alikuwa mama yake, tunaambiwa. "Utafanyaje hilo kamwe?"

180 "Sikiliza, mama yangu mkongwe ni mwanamke kipofu, lakini ni mwanamke mtauwa. Kupitia midomo yake, amepanda mbegu moyoni mwangu. Nimelisoma kutoka katika Neno la Mungu, ya kwamba Mungu alisema, katika Isaya 9:6, 'Bikira atachukua mimba.'"

181 Haleluya! Unaweza kuona? Neno linachukua mwili. Haya basi. Mungu atakuwa na Kanisa. Litazaliwa kwa Neno la Mungu, kwa sababu ni Neno lililo hai la Mungu. Mnaliona?

"Unajuaje? Mbona, linaenda . . . Unajua utakavyoitwa, tangu sasa na kuendelea? Utaitwa . . . "

182 "Sijali kile ninachoitwa. Hilo halina uhusiano wowote nalo. Na iwe kwangu kulingana na Neno la Bwana." Loo,

kila mtu angeweza kusema hivyo leo? Loo, la—laiti watu kweli wangeweza, kutoka moyoni mwako, sisi sote tungeweza kusema hivyo, mnaona, "Na iwe kwangu kulingana na Neno Lako, Bwana." Jamani! Ulimaanishe kweli. Mmoja ama wawili, ama mahali fulani huko nje, litachukua waliochaguliwa tangu zamani ambao kweli wanamaanisha hilo. Na, ndugu, utaona cheche zikiruka papo hapo. Hiyo ni kweli. Wakati kweli unayo hayo hapo, kukabiliana na hayo yanayokuja, huko kumwagiliwa maji kunaanza kushuka juu ya Neno hilo. Naam, bwana.

183 Sasa, ilikuwa ni nini? Nia bikira, tumbo la uzazi, tumbo bikira la uzazi kwa ajili ya huyo mtoto mchanga. Matokeo? Uzima wa Milele.

184 Hawa, mwanamke mzuri kadiri . . . kadiri alivyokuwa, bikira kadiri alivyokuwa, lakini kwanza aliacha shaka liingie, kwa neno, uongo wa ibilisi. Alifanya nini? Akawasiliana naye kwa njia mbaya. Mtoto wake alikuwa nini? Mauti.

185 Mariamu, nia bikira, tumbo bikira la uzazi. Ibilisi alipojaribu kumjaribu, naye akaja . . . Ndipo Malaika akamjia basi na kusema, "Utapata Mtoto."

Shetani akasema, "Sasa, ah, afadhali uulizie Hilo."

Malaika akasema, "Ni tendo la Mungu."

186 Na bila shaka alifikiria juu ya Isaya 9:6. Akasema, "Tazama, mimi ni mjakazi wa Bwana." Matokeo yake ni nini? Kuzaliwa na bikira, Neno la Milele ndani yake, naye akazaa Uzima wa Milele. Vema.

187 Bibi-arusi wa Yehova alichanganya, bibi-arusi wa Yehova alichanganya mbegu. "Ulisemaje sasa, Ndugu Branham? Asubuhi ya leo, ulisema, 'Bibi-arusi wa Yehova alifanya uzinzi.'" Sitaliacha.

188 Sasa hebu na tuangalie kwa makini sana sasa. Sasa tuna yapata tu saa nyingine moja, nadhani. Nina baadhi hapa, itanibidi tu kuruka baadhi yake, kisha nianze kusoma katika dakika chache tu, mnaona, na kusoma tu upesi niwezavyo, nipate kulitoa. Sasa, saa nyingine, naamini tutatoka, kama tu mtanivumilia na kuomba pamoja nami. Mnaona?

189 Sasa, bibi-arusi wa Yehova alikosea wapi? Vema. Yehova alituma nini kwa bibi-arusi Wake huko Misri? Alimwahidi Ibrahimu ya kwamba bibi-arusi Wake, ule uzao, ungekaa huko Misri kwa muda wa miaka mia nne. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Wakati ulifika kwa Neno kutimizwa.

Je, sisi tumefikia wakati wa kutimizwa kwa Neno? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Hakika. Kwa ajili ya ukombozi, kutolewa nje. Vema.

190 Walilipataje Neno? Hivi waliunda madhehebu, kundi la watu wakakusanyika, na makuhani, na kusema, "Sasa, ndugu, tu—tutakuwa na kura hapa. Na imepitishwa, kwa kauli moja,

kwamba tutakuwa na dhehebu linaloitwa 'Mafarisayo', na, kupitia hilo, Mungu atatenda kazi"? Mungu kamwe hakutenda jambo kama hilo, kamwe hakutenda.

191 Yeye aliwatumia nini? Nabii. "Nalo Neno la Bwana lilimjia nabii." Akamwinua moja kwa moja miongoni mwao, nabii. Na kumpaka mafuta na kumthibitisha, moja kwa moja katikati ya hao pepo wengine wakifanya kazi, pamoja na miujiza na kadhalika, kwa sababu Musa alidumu na Neno.

192 Akalichukua kundi hilo la watu; umati uliochanganyikana ukaondoka pamoja nao. Walipofika ng'ambo ya pili, wakielekea nchi ya ahadi, kabla hawajafika kule, bibi-arusi Wake wa thamani akafanya uzinzi na Moabu. Niambieni hakufanya hivyo, sasa. Alifanyaje jambo hilo? Nabii mwongo, dhidi ya Neno la Mungu. Hata hivyo, alikuwa na ishara zote, na taratibu zote, alikuwa wa kiroho tu kama Musa, ama vile vile tu.

193 Angalieni. Sikilizeni. Sikilizeni kwa makini sasa. Hawa hapa Israeli wameketi kambini, wasio wa kimadhehebu. Sawa. Ilikuwa ni kitu gani? Walikuwa na nabii aliyepakwa mafuta pamoja nao. Walikuwa na Nguzo ya Moto. Mwamba uliotokwa na maji, kuwanywesha. Walikuwa wanaendelea vizuri. Na nini? Walikuwa na madhabahu saba. Hilo ni kamilifu. Juu ya madhabahu hizo waliwekwa wanyama saba safi, kondoo dume. Naye kondoo dume aliwakilisha Kuja kwa Kristo.

194 Moabu. Ilikuwaje wakati Balaamu aliposhuka kwenda kule? Alijenga madhabahu saba kama tu waliyokuwa nayo. Usinene juu yao, kimsingi, maana afadhali ujue unachozungumzia.

195 Yesu alisema, "Karibu iwadanganye walio Wateule." Limefunuliwa kiroho. Unalishika, ndipo basi ni Neno, unaona Neno likidhihirishwa.

196 Angalieni. Hawa *hapa* juu hapa; huyu *hapa* Moabu. Kukaa kwake. . .Hapana shaka ila alikuwa ni askofu, hakika, jamaa mashuhuri. Naye akajenga madhabahu saba. Akaweka kondoo dume saba juu yake, akinena ya kwamba aliamini ya kwamba kulikuwa kunakuja Masihi. Ndugu, kama wangefikia kwenye kanuni za kimsingi, ilibidi Mungu awatambue wote wawili.

197 Wakati Kaini alipomjengea Bwana madhabahu, mwana wa Shetani alipomjengea Bwana madhabahu, alijenga madhabahu ya namna ile ile ambayo Habili alijenga. Wote wawili waliabudu. Wote wawili walienda kanisani. Wote wawili walilipa zilizowapasa. Wote wawili waliwajibika. Waliinama na kumwabudu Mungu yeye yule. Ndipo mmoja akapokelewa, na huyo mwingine akapotea.

Ilikuwaje? Yesu alisema, "Juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu."

198 Kanisa Katoliki linasema, "Kuna mwamba pale, Kanisa limejengwa juu yake, ama, ninii. . .Na Petro alikuwa ndiye

mwamba huo." Nalo kanisa Katoliki linasema ya kwamba Petro amezikwa ndani yake. Huo ni uongo, lakini, kadiri niwezavyo kuona. Kuanzia wakati waliposema Petro amezikwa mle ndani, Biblia ilisema alikuwa huku Yerusalemu. Mnaona? Kamwe hakuwa kule Pal-. . . kule. Lakini, hata hivyo, wanasema alikuwa kule. Kwa kweli hakuna taarifa ya Paulo kuwako kule, bali katika historia. Lakini wanasema "Petro," angezikwa kule, kama alizikwa. Hiyo inaleta tofauti gani? Hilo silo Yesu alilokuwa akizungumzia. Mnaona jinsi walivyochanganyisha vitu?

Vema, Protestanti ilisema, "La. Yesu alisema Yeye alikuwa ndiye Mwamba huo." Sasa, Yeye kamwe hakulisema.

199 Alisema, "Heri wewe, Simoni, mwana wa Yona. Mwili na damu havikukufunulia Hilo, 'Wewe ni Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai.' Mwili na damu. . . Hukujifunza Hilo katika seminari. Dhehebu fulani halikukufundisha Hili. Lakini Baba Yangu aliye Mbinguni amelifunua. Na juu ya mwamba huu, Kweli ya kiroho, iliyofunuliwa ya Neno la Mungu, nitalijenga Kanisa Langu. Na malango ya kuzimu hayawezi kulishinda."

200 Moabu walifanya jambo lile lile. Akashuka kule na kuwafundisha wana wa Israeli, kasema, "Sasa tazameni hapa, enyi marafiki." Sasa, hilo ndilo jambo lile lile alilofanya Pentekoste. Sasa angalieni. "Sasa angalieni hapa, si sote tuko sawa? Hivi hatumwamini Mungu yeye yule? Sisi sote ni sawa." Watoto wa Moabu walikuwa binti wa Lutu. Mnaona maskini kundi hilo, waliotoroka kule chini? Bado wangali ni kero. Mnaona? Hao hapo, wasumbufu. Mnaona? Walikuwa huko juu. Nao walikuwa na. . . "Mbona," akasema, "sasa angalia hapa, mnajua sisi sote ni sawa." Ni wangapi wanaojua ya kwamba hao walikuwa watoto wa Lutu? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Hakika. Kutoka kwa baba yao wenyewe, uzinzi, na kusema, "Sasa, sisi sote ni kitu kimoja."

201 "Mnajua, ninyi Methodisti, na ninyi Baptisti, na sisi Presbiteri, na wote. . . Mbona, hakika, tunataka Mafuta yenu kidogo. Sisi sote ni sawa." Nao walifanya nini? Walioana miongoni mwao. Na hivyo ndivyo Pentekoste ilivyowafanyia Waprotestanti. Aliolewa katika muungano wa makanisa. Alijiundia dhehebu. Naye yuko wapi? Kama vile tu Israeli walivyokuwa, waliachwa kwa sababu ya uasherati wa kiroho na uasherati wa kimwili pia. Mungu alimkataa, tangu wakati huo na kuendelea. Hata wale watoto waliofanyika Wasamaria walilaaniwa. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Hakika, alikuwa hivyo. Yehova alimwacha.

202 Bibi-arusi wa Kristo alifanya vivyo hivyo, akachanganya mbegu yake ya kimadhehebu, na kumwacha Kristo, mume wake aliyemposa. Enyi kundi la Wapentekoste wakavu mliooshwa! Mna shida gani? Ufunuo, mlango wa 3 na kifungu cha 20,

tunaona, katika unabii, Yesu Kristo nje ya kanisa Lake Mwenyewe, katika Wakati huu wa Laodikia, akibisha mlango, akijaribu kurudi. [Ndugu Branham aligongagonga mimbarani—Mh.] Picha ya kusikitisha kuliko zote katika Biblia. Alifanya nini? Akaanza kufanya ukahaba.

203 Yesu ajapo, Yeye anabisha kwa sababu gani? Yesu anarudi kumpokea Bibi-arusi Wake, basi wakati alipokuja kubisha mlangoni, alifungiwa nje. [Ndugu Branham aligongagonga mimbarani—Mh.] "Mbona, huwezi kuingia humu ndani. Huwezi kufanya uamsho. Chukua. . .Hebu nione makaratasi yako ya kuwekwa wakfu." Mtu aliyejazwa na Roho wa Mungu, Maneno halisi, ya kweli ya Mungu, Neno la Mungu lililodhihirishwa miongoni mwa huduma yake, hakuna hata jambo moja unaloweza kusema dhidi yake, utovu wa uadilifu wala chochote kile. Ni nani anayeweza kumshtaki juu ya jambo hilo? Akaja kwenye dhehebu, "Mbona, yeye si wa Umoja. Yeye si Assembly. Yeye ni Utatu. Yeye si Utatu. Yeye ni Assembly." Enyi maskini kundi la watu haramu. Aibu kwenu. Mungu, akiwa nje!

204 Lakini Yohana alisema nini, yule mjumbe wa mwisho kule chini, kabla ya Kuja Kwake? "Yeye anaweza kutoka katika mawe haya kumwinulia Ibrahimu watoto. Msije, mkisema, 'Sisi ni wafuasi wa *hili*. Sisi ni wafuasi wa *lile*.' Mungu anaweza, mawe haya, kumwinulia Ibrahimu watoto." Vema.

Tunapoendelea sasa, loo, jinsi ninavyopenda hili!

205 Bibi-arusi wa Kristo, kama vile bibi-arusi wa Adamu na wengine wote, wanachanganya mbegu na kumtoa Kristo nje, kwa ajili ya dhehebu lake. Hakika alifanya hivyo. Hakika alifanya hivyo. Alimkataa Mungu, atakayekuwa mume wake, kama Hawa alivyofanya. Alikubali magugu ya mauti uongo wa Shetani. Matokeo yake, kanisa lililokufa, la kawaida limezaliwa naye. Sasa, "Unasema uongo." Kasema, "Huo ni uongo." Wapentekoste wako wako wapi? Wao ni baridi kuliko Wabaptisti walivyo. Hakika. Mnajua nini? Inaonekana kama picha mbaya sasa hivi, sivyo?

206 Lakini Yoeli alisema nini, katika Yoeli 2:28? "Lakini nitarudisha, asema Bwana."

Uh! Kama vile Adamu alivyomkuta mkewe ametiwa mimba na mbegu ya mauti, ya uongo wa Shetani aliokuwa ameukubali.

Yusufu alimkuta mkewe ametiwa mimba na Mbegu ya Mungu, ambayo, lile Neno alilokuwa amelikubali.

207 Yote yanahusu nini? Ninajaribu kusema nini? Sasa, kwenu ninyi watu mlio—mlio hewani, ninyi watu huko nje kwenye gari, ninyi watu maskanini, mnaona ni kwa nini nimekaa jinsi nilivyojaribu kukaa papa hapa, na kulishutumu jambo hilo? Si kwamba nina neno dhidi ya hao wanaume, hao wanawake. Sina neno hata moja dhidi yao, lakini si—siwezi kupitia kwenye

uwanja hu—huo. Kamwe siwezi kufanya hivyo, kwa sababu ni kosa.

208 Jinsi nilivyo na Andiko hapa ningetaka kuchukua, juu ya Yesu, juu ya majaribu Yake, wakati alipojaribu kumpata! Kasema, "Nitakupa falme hizi zote za ulimwengu. Ni zangu." Mnaona? Jambo lile lile alipomjia Hawa. Mnaona? Kwanza, kwa kugeuza mkate, kuhusu kula, na kadhalika. Mnaona? "Nitafanya haya yote kama utaniabudu. Wewe njoo tu ujiunge na kundi letu."

Yesu akasema, "Imeandikwa, 'Mtu hataishi kwa mkate tu, bali kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu.'"

209 Ni kitu gani? Baadhi yenu wahubiri sasa, ambao mnaogopa sana kuchukua msimamo wenu, mnahofia kwamba hata hawatawaruhusu kuingia kwenye hilo shirika. Utafanya nini kingine, basi? Wangekufukuza. Ninakuhurumia, jambo la kwanza, kwa ajili ya udhaifu wako. Hiyo ni kweli. Imani yako katika Mungu iko wapi?

210 Waliniambia jambo lile lile. Hakika. Nilifanya kazi miaka kumi na saba, mpaka Mungu aliponitoa na kunijenga karibu na hili, ndipo nikawazia, "Sasa, Shetani, njoo sasa, uone mahali lilipo."

211 Unapotambua kweli kwamba Mungu amekufunulia Ukweli wa jambo hilo, hakuna kitu ulimwenguni kitakachokushinda ndani yake. Hivyo tu. Huwezi kushindwa kabisa; si wewe, bali Mungu aliye ndani yako. Sio Kristo, bali, sio ule mwili, bali Hili, Neno lililokuwa ndani Yake. Si Mariamu, bali Neno lililozaliwa kutoka kwake.

212 Sasa, kwa hiyo, mwanadamu ataishi kwa kitu gani? Si kwa tiketi yake ya posho, bali kwa Neno la Mungu. Si kwa madhehebu yenu yanayowaandalia mahali. "Vema, hebu nionyeshe hati zako za utambulisho. Je, uko katika hali nzuri? Huna budi kuzichunguza. Vema, naam, wewe, unasimama katika cheo, yapata asilimia mia moja. Vema, tunaweza kukupokea kwa siku chache, kwa ajili ya uamsho, tukujaribu tuone utakalofanya." Loo, jamani! Mungu anawezaje kufanya kazi katika kundi kama hilo, "Limekufa mara mbili, likang'olewa toka mizizini," lenye mizizi, lililooza, na kadhalika? Loo, jamani! Hilo hapo lingine.

213 Loo, enyi watu, Mungu awabariki! Nisikieni! Siwezi kuamini chochote ila Neno la Mungu. Nataka liwe maisha yangu, kila kitu nilicho mimi. Ninawatakeni mfanye vivyo hivyo. Hebu matembezi yenu, mazungumzo yenu, hatua zenu, kila kitu mfanyacho, kiwe katika Neno la Mungu. Hebu nia ya Kristo iingie ndani yenu, na—na hiyo itakutia mimba kwa Neno. Usipofanya hivyo, ukiruhusu nia ya dhehebu iingie ndani, utatiwa mimba ya kimadhehebu. Ukiruhusu nia ya Kristo iingie ndani yako, Yeye hawezi kulikana Neno Lake Mwenyewe, maana

Yeye ni Mungu. Tiwa mimba na Neno, na uliamini. Sijali kama wakikuweka nje, wakusukume nje, wakufukuze, na kila mlango umefungwa, utaenda vivyo hivyo tu. Amina. Whiu! Sina budi kuharakisha sasa. Ah!

214 Kristo sasa anajitwalia Mwenyewe Bibi-arusi, atiwe mimba kwa Mbegu-Neno Lake Mwenyewe tumboni Mwake, tumbo la uzazi ni—niani Mwake, wala halitachanganyikana na takataka zozote za kimadhehebu. Yeye ni bikira Kwake.

215 Loo, ninakumbuka nimeketi pale chumbani, siku tatu mle ndani, nikiomba na kumngojea Bwana, na kufunga. Wakati hilo liliponigusa, niliwazia, "Ee Mungu, ni kitu gani? Mimi hapa, katika picha. Mimi hapa. Kama nikileta kiasi hiki kanisani, nitakuwa wapi? Nitawasukumia nchani. Nifanye nini? Tayari nimeliona kanisa kama kila mfano na kivuli, na kadhalika, nikaonyesha limekwisha. Utafanya nini?"

216 Ndipo nikawazia juu ya Neno hilo, "Nitarudisha, asema Bwana. Nitarudisha." Kumbukeni ule msonobari wa kale, wakati moto unapoupiga na kuuteketeza kabisa; hutikisa mbegu, hata hivyo. Mbegu hiyo inazaa mpya. Hiyo ni kweli. Ile miti ya kale inateketezwa na madhehebu na kadhalika, bali bado kunabakia Mbegu ya Neno. Nalo. . .Ne-. . .Neno la Mungu, litarudi tu moja kwa moja, litajizaa tena, hakika tu kabisa. Naam. Sasa, sasa, hatalikosa. Angalieni. Lakini Kristo. . .

217 Tunaamini tuko katika wakati wa mwisho. Sivyo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Je, mnaamini ya kwamba kabla hamjapata mazao, sasa, hamna budi kupanda mbegu? ["Amina."] Mnaona ni kwa nini nimeyaacha makanisa yanifukuze, yaniambie kila kitu, kuniita majina ya kila namna, kadhalika, na kudumu tu moja kwa moja pamoja na Neno hilo? ["Amina."] Mnaona? Kuna mmea, Mbegu imepandwa. Tayari imepandwa, ewe rafiki. Tayari imepandwa. Ninaweza kulisema sasa. Imekwisha. Vema. Tayari imepandwa. Loo, naam. Vivyo hivyo na mbegu ya kimadhehebu, hizo zingine zote.

218 Kama vile Ndugu yetu mashuhuri, wa thamani Billy Graham alivyosema papa hapa Louisville, kasema, "Paulo angeweza kuchukua Biblia. . ." Alichukua Biblia, kasema, "Sasa, Paulo angeweza kuingia mjini na kufanya uamsho. Angepata mwongofu mmoja. Arudi mwaka uliofuata, ana sitini kutoka kwa huyo mmoja." Kasema, "Ninaweza kwenda na kufanya uamsho wa majuma sita, na kuwa na—kuwa na waongofu elfu ishirini. Kisha nirudi baada ya miezi sita wala siwezi kupata ishirini."

219 Ni kitu gani? Wao si waongofu. Wao ni waongofu kwa umadhehebu, hivyo tu. Bila shaka. Una mmea. . .Unaona, ukipanda mbegu ya kimadhehebu, hiyo ndiyo unayopata. "Njoo sasa, ndugu, jiunge na kanisa, andika jina lako kwenye kitabu." Hayo tu ndiyo wanayojua. Sawa.

220 Pentekoste imefanya vivyo hivyo. Wananena kwa lugha, na kadhalika, "Hilo tu ndilo likupasalo kufanya. Hayo umeyapata. Njoo, jiunge na kanisa." Vema. Chukua ubatizo wako wa uongo, na kadhalika, na uendelee, "Na hilo tu ndilo likupasalo kufanya." Unaona?

221 Lakini Kristo ajapo, Yeye anakuja kwa ajili ya bikira pamoja na . . . Kanisa lisilo na hata doa moja wala kunyanzi moja la madhehebu au kitu kingine chochote, mafundisho ya sharti yaliyochanganyikana nalo. Litakuwa ni Neno, na Hilo pekee.

222 Sasa, loo, jamani, sisi hapa! Bwana abarikiwe! Sasa tunakuja kwenye Mwili tupate kuwa Bibi-arusi wa Kristo, sasa tuwe "nyama ya nyama Yake, na mfupa wa mfupa Wake." Sasa, tutaharakisha sasa. "Nyama ya nyama Yake, na mfupa wa mfupa Wake." Kwa nini . . .

223 Niwaulizeni swali. Kwa nini mvua zenu zote, huko nyuma kabisa, hazikumleta bibi-arusi kwa Kristo? Nawatakeni mnijibu hilo. Kama . . . Kuja Kwake kumechelewa. Tunaamini jambo hilo. (Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, uvumilivu, Yeye anamweka tayari Bibi-arusi Wake.) Mbona hizi mvua . . . Kwa nini ninyi Wapentekoste huko nyuma, miaka michache iliyopita, wakati mlipoanza, miaka arobaini, hamsini iliyopita, kwa nini hamkumleta Kristo, Bwana-arusi, kwa bibi-arusi? Nitaacha hilo lizame, kwa dakika moja. Kwa nini? Kwa sababu mlimtia mimba, ninyi wenyewe, kwa dhehebu lenu. Hivyo ndivyo mlivyofanya hasa. Yeye hatamwoa kahaba. Ataoa bikira. Ni wazi, lakini hiyo ni Kweli. Mnajua Hilo, kwa njia wazi. Haiwabidi kushangaa. Siyumbi-yumbi kulihusu. Niwaambieni Kweli. Kwa nini halikumleta? Kwa nini halikumleta Kristo, kumleta Kristo kwake? Kwa sababu hafai. Alimpata katika uzinzi.

224 Ndio sababu hasa watoto hawaishi milele wanapozaliwa; Adamu alikuta mkewe ametiwa mimba.

225 Hiyo ndiyo sababu ikambidi Yehova kumchukua Bibi-arusi Mmataifa; alimkuta ametiwa mimba.

226 Hivyo ndivyo hasa Kristo hana budi kujipatia Bibi-arusi sasa; amekuta linalojiita kundi limetiwa mimba. Yeye atapanda Mbegu Yake. Mtu fulani ataipata, kwa sababu wamechaguliwa tangu zamani kuwa Kanisa mwishoni mwa safari.

227 Kama vile wa Adamu na wa Yehova, aliwakuta wametiwa mimba na mafundisho ya kujibunia ya madhehebu. Kama ile Kweli ya Mungu, katika Mwanzo 1, "Kila mbegu imezaa kwa jinsi yake." Kwa hiyo, wakati Roho aliposhuka juu yake, kumbe mtu alikuwa huko kwenye tumbo lake la uzazi, na kulijaza mbegu za kimadhehebu za mawazo yake mwenyewe, kwa hiyo hiyo ndiyo sababu anapaswa kuwa jinsi alivyo, wala Kristo asingeweza kumjia. Hum! Hilo ni gumu, sivyo?

228 Siku moja, nilikuwa huko juu kwenye Green's Mill. Nilikuwa nikiomba kwa siku kadhaa; imekuwa miaka mingi iliyopita. Nilipanda nikaenda hapa juu Mishawaka. Kamwe sikusema jambo hili kwenye kanda hapo kabla. Nilienda Mishawaka. Mnakumbuka kuhusu yule mvulana mweusi? Nilikuwa tu nimewapata Wapentekoste; kamwe sikujua kulikuwa na kitu kama hicho. Nami nikaenda kule juu na kukutana nao; nilifikiri nilikuwa pamoja na kundi la Malaika. Niliwaona wakinena kwa lugha na kadhalika. Sikuwahi kusikia habari zake, hapo awali. Lakini hao hapo, wakikimbia huku na huku sakafuni, wakinena kwa lugha. Nikawaza, "Jamani, hilo ni zuri sana." Ile UPC ya kale, na P.A. ya W., na aina hizo zote, waliungana. Walikuwa na . . . Kulikuwa na ubaguzi kati ya watu weupe na weusi wakati huo. Iliwabidi kufanya mkutano wao kaskazini. Ulikuwa huko Mishawaka, Indiana. Jamani!

229 Nilikuwa na dola moja na senti sabini na tano, za kutosha tu kunifikisha nyumbani. Nikaweka nikeli yake kwenye maskini u- . . . maskini maandazi ya kale ama—ama roli, zimekaa siku mbili ama tatu. Nikashuka nikachota jagi la maji, kwenye bomba la maji. Kisha nikaenda nje kwenye shamba la mahindi. Kisha nikachukua viti vyangu kutoka kwenye Ford yangu kuukuu, na kuvilaza chini; nikabinya suruali yangu kwa ajili ya usiku huo, suruali yenye milia niliyokuwa nimeivaa, na maskini fulana ya mikono. Basi kesho yake asubuhi nikashuka tena. Sikutaka kula pamoja nao. Nilikaribishwa, bali sikutaka kula pamoja nao, maana sikuwa na kitu cha kuweka katika matoleo yao.

230 Na kwa hiyo nikaenda kutafuta kujua. Siku hiyo, wangecheza, na wangeruka-ruka, na wangeimba katika Roho. Nikawazia, "Loo, jamani, hilo linasikika zuri. Lo!" Mtu mmoja angesimama na kunena kwa lugha, na *huyu* atoe tafsiri. Na, ndugu, ilikuwa hivyo. Aliwaita watu, huko nyuma kwenye kusanyiko. Nikawaza, "Loo, ndugu, hilo ni zuri sana."

"Mwambie Bi Jones," ama *Fulani-wa-fulani*, "aje sasa hivi. Bwana anamwita." Huyu hapa anakuja. Hiyo ni kweli.

231 Ndipo *huyu* ananena kwa lugha, huyo mwingine anafasiri. Nikawaza, "Loo, jamani, jamani! Ule Utawala wa Miaka Elfu unakaribia kuanza. Huu ndio. Na, kwa hiyo, laiti ningaliweza tu kuamkuana na hao watu watauwa kwa mkono," nikawaza.

232 Ndipo nikamwendea mmoja wao, nilipokuwa nje, nikitembea huku na huku. Hawakunijua. Nilikuwa maskini jamaa mdogo huko nje. Na kwa hiyo nikatembea kuzunguka kanisa, na baada ya kitambo kidogo, walipokuwa na mapumziko kidogo. Ndipo nikakutana na mtu fulani huko nje, nami . . . mmoja wao. Nami nikamsalimia kwa mkono. Nikasema, "U hali gani, ndugu?"

233 Sasa, mwajua, Mungu amenipa karama ndogo hapa, nipate kujua mambo wakati anapotaka niyajue. Mnaona? Nikawazia,

"Laiti ningaliweza kumfanya azungumze, na kumwacha aseme jambo fulani, ningetafuta kujua kama kweli ilikuwa kweli ama si kweli."

Kwa hiyo nikamwona huyo, ilionekana kana kwamba ndio viongozi wake. Nikamsalimia kwa mkono. "U hali gani, ndugu?"

Kasema, "Njema!"

Nami nikazungumza naye kidogo, naye alikuwa Mkristo halisi. Alikuwa hivyo. Nikawaza, "Mungu asifiwe!"

234 Baada ya kitambo kidogo nikafika pembeni, nikamfikia mtu huyu mwingine. Nikasema, "U hali gani, ndugu?" Ndipo nikaanza kuzungumza naye. Kama niliwahi kuzungumza na mnafiki, huyo hapo alikuwa mmoja wao. Alikuwa mtu mwenye nywele nyeusi, naye amepata mtoto kwa mwanamke mwenye nywele nyeupe. Watoto wawili waliozaliwa na mwanamke mwenye nywele nyeupe. Nililiona katika ono moja kwa moja mbele yangu.

235 Nikawaza, "Sasa nimechanganyikiwa kweli. Sasa, Roho yuyo huyo angewezaje, mmoja awe juu ya mtu, na mtu mtauwa, huyo mwingine juu ya ibilisi, mnafiki?" Nikawazia, "Mungu, a—afadhali niachane na kitu hicho chote. Sijui." Nilikuwa tu na yapata umri wa miaka kumi na tisa, ishirini. Nikawaza, "Afadhali niachane na kitu hicho. Vema, sijui. Hilo lingewezekanaje kamwe? Siwezi kusema neno juu yake, siwezi kusema neno dhidi yake, bali ninajua mtu huyo amekosea." Ndipo Roho yuyo huyo, ninamwangalia, angeingia ndani, apate matokeo yale yale. Nikawazia, "Kuna kasoro hapa, mahali fulani. Ni hayo tu." Nikamwambia mtu huyu . . .

Akasema, "Umewahi kumpokea Roho Mtakatifu?"

Nikasema, "Siamini nina kile ninyi jamaa mlicho nacho."

Kasema, "Utukufu kwa Mungu! Umewahi kunena kwa lugha?"

Nikasema, "La, bwana."

Akasema, "Hujampata."

Nikasema, "Vema, si—sidhani nimempata." Unaona? Nikasema, "Hili ni jambo jipya. Sijawahi kumwona, kusikia habari Zake." Nikasema, "Vema . . . "

Akasema, "Vema, nenda mle ndani ukampokee. Hakika. Yeye yuko kwa ajili yako."

Nikasema, "Asante, bwana."

Nikawaza, "Ndugu, sitaki ulicho nacho." Kwa hiyo basi ni—nikaliangalia kidogo. Nikaendelea kuzunguka, kitambo kidogo, na kuendelea kuzunguka.

Nikatoka nikaenda mwituni usiku huo, ndipo ni—nikawazia, "Mungu, unirehemu. Ninaenda nyumbani." Nikaenda

nyumbani. Nisingeweza kusema chochote juu yake ama dhidi yake.

236 Wakati mmoja, nilikuwa hapa juu kwenye Green's Mill, kwenye maskini pango langu la kale ambako ninaenda sikuzote, mlijualo. Nilikuwa mle ndani, juu ya jambo lingine. Siku tatu ama nne, nilikuwa huko juu nikifunga na kuomba. Kukaingia kuvu pangoni, nami nikatoka, alasiri moja. Kulikuwa kuzuri, na jua lilikuwa linawaka, majani. Kulikuwa na gogo kuukuu lililoanguka namna *hii*, chini yake tu, chini kuelekea kwenye kijito. Nami nikaketi pale, nikiyasugua macho yangu, nimerudi kwenye lile pango lenye giza kwa kitambo kidogo. Nikaiweka Biblia chini namna *hiyo*. Nikawaza, "Vema, ninaamini nitasoma baadhi kutoka katika Biblia. Nami nitaegemea nyuma kwenye tawi hili hapa na kupumzika tu, na kuegemea nyuma." Nilijaa mavumbi, kila mahali. Nami nikaanza kusoma.

237 Ndipo nilipoichukua Biblia, ilikuwa ni Waebrania, mlango wa 6. Mnaona? "Kwa maana hao waliokwisha kupewa nuru, na kufanywa washirika wa Roho Mtakatifu, endapo wataanguka, kuwafanya upya tena hata wakatubu. Kwa kuwa mvua huja juu ya nchi, mara kwa mara, kuilima, kuiandaa kwa ajili ya yale tuliyo nayo, miiba na michongoma, iliyo karibu na kukataliwa, itateketezwa."

238 Nikawaza, "Vema, ni kitu gani hicho? Simama." Nikawaza, "Hiyo ilikuwa ni nini? Loo," nikasema, "nadhani ni jambo fulani tu." Ikaondoka. Sikuwa . . . Nilikuwa huko juu nikiomba kuhusu jambo lingine. Nami nikaweka Biblia yangu chini tena.

Nikasema, "Vema, nadhani nitafungua nijipatie kitu cha kusoma," namna hiyo.

239 Ndipo upepo ukaja ukairudisha moja kwa moja. Nilikuwa katika Agano la Kale. Ukaipeperusha moja kwa moja kurudi kwenye Waebrania, mlango wa 6. Nikaangalia chini tena. Hiyo hapo. Nikaangalia. Nikaichukua. Nikaisoma tena, jambo lile lile. "Vema," nikawaza, "jamani, kwani unakuwa mshirikina, Bill?"

240 Kwa hiyo nikawaza, "Vema, nitasoma hapa." Nami ni—nikaanza kusoma, wala nisingeweza kuvutiwa na chochote. Nikawaza, "Vema, ninaamini nitainua tu mikono yangu na kumsifu Bwana." Nikaiweka Biblia chini, namna *hiyo*. Nikainua mikono yangu, na kumsifu Bwana.

Nilipoinua mikono yangu, upepo ukaenda, "Whiu!" Ukapulizia tena. Na ulipofanya hivyo, niliangalia kule chini, Waebrania 6. Nikaisoma tena.

241 Nikawaza, "Hilo linamaanisha nini? Siwezi kuelewa." Nilikuwa tayari nimesahau kuhusu lile wazo la Kipentekoste. Ndipo nikawaza, "Hilo linamaanisha nini?" Nilikuwa nimeketi pale. Nikawaza, "Kuna kitu humo ndani, Bwana?"

242 Nikawazia, “Sasa, ninaamini katika kuteuliwa. Naam. ‘Hao waliokwisha kupewa nuru, washirika wa Roho Mtakatifu,’ mnaona, ‘na kulionja Neno la Mungu.’” Nikasema, “Hao ni wale waaminio wakwamia mpakani ambao watakuja moja kwa moja, karibu kufikia kile kitu halisi, kisha warudi, kama tu walivyokuwa katika siku za Yoshua.”

243 Yoshua na Kalebu walivuka. Lakini hawa walikwamia tu mpakani, mnaona, “walionja.” Waliona matendo mema ya Mungu, kisha wakayakataa. Watu huketi kanisani, wakati wote, wanasema, “Ninaamini Hilo, Ndugu Branham,” bali kamwe hawalisogelei. Mnaona, haiwezekani kwao kuvuka kamwe. Kwa hiyo, basi, wanafikia mahali hapo. Nawe unawahubiria wanawake wenye nywele fupi, mwaka ujao wana nywele fupi vivyo hivyo tu. Unawahubiria wanaume la kufanya, wanafanya vile—vile vile tu, mnaona; kamwe usione. Waaminio wakwamia mpakani wanaosema, “Loo, naam, ninaamini ni kweli.”

244 Nikasema, “Bila shaka, ninaamini hilo.” Lakini, hili, ilipofikia mahali hapo, ‘Bali michongoma na miiba iliyo karibu na kukataliwa, ambayo mwisho wake ni kuteketezwa.’” Nikawaza, “Hilo linamaanisha nini? Siwezi kulipata.”

245 Nikaketi hapo kidogo. Nikawaza, “Mungu, kwani hili ni jambo unalotaka nijue? Niko hapa juu nikitafuta ono kutoka Kwako, Bwana, kujua tu la kufanya kuhusu huduma kule chini, nami ni—ninataka uniambie, Baba.”

246 Ndipo nikaangalia upande wa pili wa lile bonde, kuelekea juu. . .Ilikuwa huko juu kabisa ya Charlestown, nikielekea kwenye Soko Jipya, upande *ule*. Nikavuka kilima. Ndipo nikaangalia, nami nikaona pale kama upinde wa mvua ukining’inia juu ya bonde. Na kupitia kwenye upinde huu wa mvua, nikaona kitu fulani kikizunguka. Nikaangalia, kumbe ilikuwa ni ulimwengu. Na hapa akatokea Mtu aliyevaa mavazi meupe.

247 Sasa, wengi wenu ninyi watu hapa ni wachanga sana kujua jambo hili. Mnakumbuka wakati tulipokuwa tukitapanya mbegu kwa ninii yetu . . . unaweka mfuko mkubwa mno ubavuni mwako, unazichota kwa mkono wako na kuzitupa? Bw. Wood, unakumbuka jambo hilo, kutapanya mbegu namna hiyo. Unazichota mikononi mwako na kuzitapanya namna *hiyo*, unaacha upepo uzipeperushe kwe—kwenye udongo.

248 Nami nikamwona Mtu aliyevaa mavazi meupe, akivuka namna *hiyo*, akipanda mbegu. Nikamwona akienda moja kwa moja kwenye mpindiko wa dunia. Nikawaza, “Sijui hilo linamaanisha nini?” Kisha nikaangalia. Mara tu alipougeuza mgongo Wake, huyu hapa akaja mjanja kwelikweli, akakaribia, akionekana namna *hiyo*. Alikuwa na gunia lililojaa, naye alikuwa akipanda magugu nyuma Yake. Akaizunguka dunia,

angali akiangalia, akinyemelea, mwajua, akizitupa namna *hii*. Naye akaizunguka dunia.

249 Ndipo nikaona zikichipuka, ndipo ngano ikatokea. Kisha yakatokea magugu, vichomi, miiba, michongoma. Na yote ilikuwa ikikua, pamoja.

250 Ndipo ukame mkuu ukatokea. Nami nikaona maskini hiyo ngano imeshikilia maskini kichwa chake, ikifanya, "Hema, hema, hema, hema, hema, hema, hema!" Ikifa tu kwa ukosefu wa maji. Ndipo nikamwona maskini kwekwe huku kichwa chake kimeinama, "Hema, hema, hema, hema!" Ikifa tu kwa ukosefu wa maji. Na kila mtu akaanza kuomba apate maji.

251 Mara, mvua kubwa ikanyesha, katika kujibu maombi. Ndipo mvua ikanyesha, kote duniani. Mara hayo maji yalipoipiga dunia, maskini hiyo ngano ikaruka juu, ikasema, "Utukufu! Utukufu! Utukufu! Utukufu!" Ndipo maskini lile gugu likaruka juu, likapiga makelele, "Utukufu! Utukufu! Utukufu! Utukufu!"

252 Vema, nikawaza, "Sasa hiyo ni nini?" Ndipo wakati huo tu . . . "Vema, ngano hiyo ilikuwa ikipiga kelele. Ninaweza kuona jambo hilo. Lakini hilo kwekwe lilimaanisha nini?"

Ndipo akasema, "Soma Waebrania 6."

253 "Mvua huwanyea wenye haki na wasio haki." Jambo ndilo hilo. Hiyo ndiyo sisi . . . sababu hatukuwa na Bibi-arusi aliye tayari kwa ajili ya Kristo sasa. Tulipanda mbegu za kimadhehebu badala ya Neno. Imefanya nini? Ilileta watoto wengine zaidi wa kimadhehebu. Hiyo ni kweli. Lakini mle miongoni mwake kuna ngano iliyoanguka. Vema. Lakini, angalia, Roho yule yule anayemfanya mwaminio halisi wa kweli—wa kweli kunena kwa lugha, yule Roho halisi anayemfanya mwaminio halisi Mkristo, unaona, kwa sababu inalimwagilia maji Neno fulani, Mbegu. Roho yuyo huyo hufanya kitu fulani, kibadala Chake, kama yule chotara wa Hawa, humfanya chotara kufurahi vivyo hivyo, kupaza sauti kwa wingi, wanajisikia wenye furaha tu juu Yake kama hao wengine. Lakini ukweli wake ni upi? Hiyo mbegu ni mbaya, kwanza kabisa. Kwa hiyo madhihirisho yenu yote ya kimwili hayamaanishi chochote.

254 "Nijaponena kwa lugha za wanadamu na Malaika, wala sina upendo, hainifaidi chochote. Nijapoweza kuhamisha milima, wala sina upendo, hainifaidi chochote. Nijapotoa mali yangu yote kuwalisha maskini, kama sina upendo, hainifaidi chochote; kama nikinena kwa lugha kama wanadamu na Malaika, inakuwa kama shaba iliayo na upatu uvumao." Mnaona? Si kitu.

255 Sikilizeni, enyi kanisa! Ati Pentekoste? Ni bure! Kwa nini? Ni mbegu chotara. Haiwezi kuja kwenye Neno. Sasa, haya basi.

256 Mwili unaozaa Mwili wa Kristo, tena, hauna budi kutoka kwenye tumbo bikira la uzazi, Neno. Sawa.

257 Hiyo ndiyo sababu. Sikilizeni hili. Hiyo ndiyo sababu alipata, "Milioni moja zaidi katika mwaka wa '44." Huo ulikuwa ni msemo wa Kibaptisti. Hiyo ndiyo sababu madhehebu ya Kipentekoste, ambayo hayangeweza kutoa Uzazi wa kiroho, kuleta madhihirisho pamoja na Kristo, kwa sababu ilikuwa tu ni mvua ya kupanda. Naye amezaa kanisa la kimadhehebu. Naye ameungana na—na wa Kiinjilisti mashuhuri, naye amekwenda katika njia ya Kora. Amekwenda pamoja na madhehebu. Hiyo ndiyo sababu.

258 Sasa hebu turudi kwenye Agano la Kale, kwa mifano fulani. Ndipo, nitaanzia hapa, katika dakika chache, juu ya jambo fulani, na kuwaachilia mwende. Hebu na turudi kwenye Agano la Kale, kwa mifano fulani, kuthibitisha mambo haya. Sasa, nimechukua saa kadhaa hapa, nikiliweka hili. Sasa tutabadilisha somo, tubadilishe mpango.

259 Sasa, kwanza, nina kitu fulani, ninapofikia tu . . . Nina kurasa cha—chache hapa, halafu sina budi kuninii . . . Loo, jamani, jamani, jamani, hakika sivyo, hilo. Itanibidi tu kuharakisha, upesi sana. Nitalisoma, mnaona, nitalisoma tu upesi niwezavyo, maana ninajua hatuna ila tu mu—muda mfupi sana sasa. Mnaona? Sasa, mmechoka? [Kusanyiko linasema, "La."—Mh.] Loo, vema, basi, ni mimi. Vema. Twendeleeni, hilo ni sawa.

260 Sasa, hiyo ndiyo sababu tuna mambo hayo yote tuliyo nayo. Sasa, mambo haya yote nimesema, kama hayaambatani na Biblia, ama—ama kuafikiana na Neno la Mungu, yamekosea, yamekosea, picha hii yote. Sasa nitayapitia tu baadhi ya haya haraka, pasipo kuyaelezea. Lakini kuyapitia tu haraka, ili tuweze kuyafikia, na, ninawaahidi, upesi tu niwezavyo.

261 Nina mahali hapa, ambapo niliingia sana katika Roho. Nilikuwa . . . Nililipandisha kanisa juu, kulionyesha na kulithibitisha katika Neno hapa, kile hasa ambacho kimetukia, njiani mwote. Ndipo nilipofanya hivyo, nikawazia, "Bwana, nina watu wanaosimama hapa sasa. Nitawafanya wasimame pale. Niwaambie nini? Siwezi kutabiri ya usoni. Siwezi kuwaambia la kufanya. Nifanye nini? Nitawaacha wamesimama nchani." Nikainua mkono wangu, nikasema, "Mungu, nafikiri ninafanya hili kwa mapenzi Yako. Sijawahi kufanya hivi, sikuwahi kulifanya hapo kabla, maana Mbegu haikuwa imepandwa bado." Nikasema, "Sasa nina . . . na—naamini wakati wangu wa kulisema umewadia. Lakini, sasa, nitasema nini sasa?"

262 Na dhahiri tu kama unavyoisikia sauti yangu, Kitu fulani kikasema, "Itwae kalamu yako."

263 Nitawasomeeni, katika dakika moja. Basi nilipomaliza, hilo hapo, jibu hasa. Hata sikujua nilichokuwa nikiandika;

nilianza tu kuandika. Basi nilipomaliza, niliweka kalamu chini. Nikaangalia. Nikawaza, “Mungu, uturehemu! Hilo hapo, papo hapo. Hilo ndilo ninalotafuta.” Sasa, kuna mambo fulani ambayo ilinibidi kuruka. Tutayafikia, katika muda mfupi, Bwana akipenda.

264 Agano lote la Kale lilikuwa ni mifano inayoelekeza kwa Kristo na Kanisa Lake. Mnaamini Adamu na Hawa walielekeza kwa Kristo na Kanisa Lake? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Mnaamini Yehova na mke Wake walielekeza kwa Kristo na Kanisa Lake? [“Amina.”] Vema, kama hao ni—ni—ni mifano, na hii ni kitu halisi, hakina budi kuwa kama huo mfano. Maana, mfano huchukua kutoka kwa—kutoka kwa. . .Kitu halisi kinachukua kutoka kwa mfano.

265 Kristo ndiye Kichwa, Jiwe la kweli la Mungu. Mnaamini hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Neno la kweli! Bibi-arusi ndiye Mwili. Mnataka Maandiko juu ya haya, kusudi mpate kuyachunguza? Ni—nilikuwa ninataka kusoma Maandiko, bali sitayasoma. Petro wa Kwanza 2:1 hadi 6, Waefeso 5:22. . . Mnaona? Petro wa Kwanza 2:1 hadi 6, Waefeso 5:23. Someni mlango huo, yote miwili, humo ndani. Mnaona? Agano la Kale: Kristo.

266 Angalieni hapa. Hebu tuchukue tu hili, kwa mfano. Labda kama mke wangu hakuchukua dola yangu. . .Hii hapa. Kulipia sambusa kadha, muda mfupi uliopita. Samahani, marafiki, sikupaswa kusema hivyo. Lakini nina mke mzuri. Sasa, nyuma ya dola hii. . .Isingalikuwa kwa ajili yake, nisingekuwa na hiyo dola, nadhani. Rehema ya Mungu ikitupa sisi, naye akinisaidia.

267 Sasa, nyuma ya hii, inaonekana kana kwamba, kama hiyo ni pesa yetu, muhuri wa Marekani upande wa kushoto wa dola unapaswa kuwa ndio muhuri mkuu katika nchi hii. Hiyo ni kweli? Lakini ni kwa nini, ile piramidi, inaitwa “Muhuri Mkuu”? Hata pesa yenu haina budi kulishuhudia. Naam.

268 Kila unapotuma postikadi, ama barua, inakubidi kushuhudi-. . .Inashuhudia, “Mwaka wa Bwana wetu, 1962.” Kila kitu kinamshuhudia Kristo. Mnaona?

269 Je, mliona ya kwamba, ule muhuri mkuu, ni piramidi? Mtu yeyote anajua ya kwamba ile piramidi haikuwekwa jiwe la kufunika juu yake? Ni wangapi wanaojua hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Hakika. Nimekuwa huko Misri, Cairo. Naam. Kamwe haikuwa na jiwe la kufunika. Kwa nini? Lilikataliwa, lile jiwe la pembeni. Hilo lilikuwa ndilo jiwe la pembeni lililoshikilia jengo hili, ndilo jiwe la msingi. Ni wangapi wanaojua jiwe la msingi ni nini? Tao linapojengwa, basi jiwe la msingi linalishikilia pamoja. Jiwe la pembeni ndilo linaloshikilia jengo. Hiyo ni kweli? Nalo jiwe la pembeni katika piramidi lilikuwa ndilo jiwe la kufunika, lilikuwa ndilo jiwe la msingi, lililishikilia lote pamoja. Sasa, jiwe hili la msingi

lilikataliwa. Mliona hapo juu? Limesimama juu yake, juu ya piramidi.

Sasa hiyo iliwakilisha nini wakati Henoko alipoijenga? Haya hapa yaliyotukia. Ni kama tu kuja kwa Kanisa la Injili. Mnaona?

270 Sasa, huko chini katika sehemu pana ya piramidi, kunawakilisha siku za mwanzoni za yale matengenezo. Kujiita tu Mkristo, kulikana kanisa Katoliki, kulimaanisha utauawa kwa ajili yake. Ndipo wakaja . . . Wakahubiri kuhesabiwa haki kwa imani. Halafu kukaja . . .

Sasa angalia zile *tatu* zikirudi tena.

Moja kwa moja akaja John Wesley, akihubiri utakaso. Kanisa likaingia zaidi katika uchache, mnaona, likashuka *hivi*.

271 Ndipo baada ya siku za John Wesley za kutakaswa, likaja kanisa la Kipentekoste, kisha Mungu akachukua masalio kutoka kwa hao. Kila mmoja akilikubali Neno. Mnaona? Sasa, ilipofikia kwa Wapentekoste, iliikatia karibu zaidi, kwa sababu ilikuwa ni kule kurudishwa kwa karama, kulileta juu moja kwa moja.

272 Ni kitu gani? *Huku* chini kabisa, ni mbali sana na sura ya kichwa. *Hapa* chini, ni karibu kidogo na kichwa. *Hapa* juu, ni karibu zaidi kidogo. Lakini hilo halina budi kuwa, kabisa, kuingiana na hayo mengine. Halina budi kuchongwa.

273 Katika piramidi hiyo, unaweza kuchukua wembe wala huwezi kuupitisha katikati ya miamba hiyo ambamo mota ilikuwa; imeunganishwa vizuri sana. Walisema hekalu la Sulemani lilikuwa vile vile. Mnaona?

274 Mungu anawaondoa Wateule kutoka kwenye kanisa hilo la Kipentekoste, hilo chotara, akiwatoa, na kulimalizia Neno. Nalo halina budi kufanana sana mpaka Neno Lenyewe litaungana na Neno hili. Hilo hapo jiwe la Kichwa linakuja, na vigelegele, "Neema, neema, neema ya ajabu." Jiwe la Kichwa!

275 Haya basi, namna hii, mnaona, *pale*. Mnaona jinsi ilivyo pana sana *hapa* chini? Nayo inaendelea kukaribia zaidi, zaidi, zaidi, ile huduma. Baada ya kitambo kidogo, hapa akaja . . . Huyu *hapa* Luther; kuhesabiwa haki, amehesabiwa haki. Huyu *hapa* Wesley anakuja; kundi lililotakaswa. Hawa *hapa* Wapentekoste wanakuja; kurudishwa kwa karama. Sasa Mungu anachukua kutoka hapo, akilichonga kundi, kufanya huduma inayofanana kabisa na Neno hilo hapo, kwa sababu halina budi kupatana na Neno. Huyo hapo Bibi-arusi; ampeleke juu.

276 Sasa, Kristo alidhihirishwa apate kuziharibu kazi za ibilisi. Mnaamini hilo? Sasa, siwezi kueleza haya yote. Nitalipitia tu, upesi tu sasa, nigusie sehemu muhimu kusudi msikae sana. Kristo alidhihirishwa apate kuziharibu kazi za ibilisi. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Nyote mnaamini hilo. Hiyo ndiyo sababu Yeye . . . Yeye alikuwa ni nini? Neno la Mungu, ambalo huharibu kazi za yule chotara, ibilisi. Hiyo ni

kweli? Alifanywa, kufanya hivyo. Alizaliwa apate kuwa hivyo, kuharibu kazi za ibilisi.

277 Sasa, Mwili Wake unapaswa kufanya vivyo hivyo. Kwa sababu, Mwili ni, kichwa na mwili viko pamoja. Hiyo ni kweli? Kama Kristo ndiye Kichwa, alikuwa Neno, Mwili Wake hauna budi kuwa kitu kile kile kama Kichwa Chake kilivyokuwa. Hiyo ni kweli? Kanisa la Neno, lililozaliwa kwa Neno, lililozaliwa na bikira kutokana na Neno! Si wa kimadhehebu sasa; aliyezaliwa na bikira kutoka kwa Neno!

Jinsi Mwili unavyofanya kazi ni kwa Kichwa. Hiyo ni kweli?

278 Mwili wangu hauwezi kusogea mpaka kichwa changu kiuambie usogee. Vema, vipi kama kichwa changu ni nyama na mwili wangu ni zege? Huh! Hauwezi kusogea. Kichwa kinaweza kusema, "Sogea, sogea, sogea, sogea, sogea," bali hakuna kitu cha kuupelekea huo ujumbe. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

Vema, kama Kichwa changu ni Kristo, na mwili wangu ni dhehebu, utafanyaje kazi? Usafi na ukahaba vinawezaje kufanya kazi pamoja? Uh-huh.

279 Ninalipenda, ndugu, nitawaambia. Ninapenda kuhubiri juu ya baadhi ya haya, kidogo. Jinsi Mwili unavyotenda kazi ni kwa Kichwa, nacho Kichwa ni Neno. Hiyo ni kweli? Kichwa ni Neno.

280 Linganisha kanisa la kisasa sasa. Kwa nini hatuna miujiza ndani yake? Kwa nini hatuna Neno ndani yake? Hawezi kulifikishia Neno. Madhehebu yanalikomesha. Hakika. Tuseme, huyu hapa anakuja mtu mzuri, mtakatifu wa Mungu, akihubiri Neno la Mungu, moja kwa moja liwezavyo kutoka kwenye Biblia; dhehebu, "Uhm! La. La, bwana. Mwondoeni hapa." Mnaona, mwili hauwezi kusogea. Unaona? Kusukumiwa mbali, inabidi.

281 Sasa, Mwili hubeba kazi, huendeleza kazi, na kufanya kazi ambazo Kichwa kinauamuru kufanya. Ha-ha-ha!

282 Niambieni mahali alipopata kusema, "Undeni dhehebu." Niambieni ambapo Kichwa chote—chote kinasema, "Ni sawa kwa wanawake kukata nywele zao." Huh? Taja. Hakuna. Niambieni ambapo Kichwa kiliwahi kusema, "Kazi hizi ninazifanya, bali nyinyi hamtazifanya." Niambieni hapo.

283 Lakini, Kichwa kilisema hivi. Mkitaka kuandika Maandiko hayo, nitawapa. Yohana 14:12, "Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya," huo ni Mwili Wake. Mnaona?

284 Mnaona sasa ni kwa nini nimekuwa na bidii sana na—na aina ya Mbegu niliyopanda kwa ajili ya Mwili? Mvua itanyesha hivi karibuni sasa; ninamaanisha, mvua halisi. Na haina budi kuwa na Mbegu ya kuangukia. Natumaini nitaishi nipate kuliona. Mnaelewa sasa? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Litakuwa ni Neno lililo hai kama lilivyokuwa hapo mwanzo, Neno lililonenwa la Mungu; litakuwa na Nguvu Zake, kwa kuwa

ziko ndani Yake, katika Mwili Wake Mwenyewe, akifanya kazi kwa njia Yake Mwenyewe.

285 Angalieni ahadi ambazo Mungu aliupa Mwili huu. Sasa tunafikia jambo fulani. Tunakuja kwenye Mlima Sayuni sasa. Hebu na tuangalie kile Yeye alichouambia Mwili huu; ninamaanisha, uliozaliwa na bikira. Sasa tunaona ninii—tunaona uigaji wake. Tunauona kila siku. Lakini hebu tuje kwenye Mwili halisi, tuone kile Yeye alichosema kuhusu Huu. Hebu tuangalie. Vema. Haya hapa aliyoahidi.

286 Mnaamini ya kwamba Yohana 3:16 ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Sina budi tu kusoma hili. Hakuna lingine. Vema. Wewe, huenda nikaninii. . . Kila mtu anayeamini Yohana 3:16, "Mungu aliupenda sana ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe wa pekee," na kadhalika, semeni amina. ["Amina."]

287 Ninawapa changamoto kuamini yaliyosalia. Ninazungumza juu ya Mwili, sasa.

288 Hebu tuchukue Yohana 20, kwanza kabisa. Vema. Tuchukue Yohana, mlango wa 20, na hebu tuone. Yohana, mlango wa 20, nasi tutaanzia kwenye, loo, ningesema yapata kifungu cha 19. Yohana Mtakatifu 20, ninaamini hicho ndicho nilichoandika hapa chini, na kuanzia kifungu cha 19. Sasa sikilizeni kwa makini.

289 Ninawapa changamoto kuliamini. Loo, na—najisikia vizuri tu. Loo, laiti ningaliweza tu. . . La—laiti ningaliweza tu kumwona Roho Mtakatifu akijongea hapa, namna *hiyo*, aseme, "Sasa, ni Mimi." Sikilizeni.

> *. . . jioni siku ile ile, siku ya kwanza ya juma, milango imefungwa mahali walipokutanika wanafunzi . . . milango imefungwa mahali walipokutanika wanafunzi kwa hofu ya Wayahudi, akaja Yesu, akasimama katikati,* akawaambia, *Amani iwe kwenu.*
>
> *Naye akiisha* kusema. . . *Naye akiisha kusema hayo, akawaonyesha mikono yake na ubavu wake.* Basi wale *wanafunzi* wake. . . (Hebu tuone.) . . . *ubavu wake.* Na wakati. . . *Basi wale wanafunzi wakafurahi walipomwona Bwana.*
>
> *Basi Yesu akawaambia . . . Amani iwe kwenu: . . .* (Loo, mko tayari?) . . . *kama Baba yangu alivyonituma mimi,* (Yeye ni Neno, Mbegu, Neno-Mbegu) . . . *mimi nami nawapeleka ninyi.*

Mnaamini? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Msisimame. Kuna zaidi yake.

> *Naye akiisha kusema hayo, akawavuvia,* akawaambia, *Pokeeni Roho Mtakatifu:*
>
> *Wo wote mtakaowaondolea dhambi, wameondolewa; na wo wote mtakaowafungia dhambi, wamefungiwa.*

290 Je, hiyo ni Kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Yeye alimwambia nani hayo? Yule Mzao, Neno. Kwa nini? Wangeweza tu kuzaliwa kwa—kwa Neno. Hiyo ndiyo sababu. Mnaamini hilo? ["Amina."]

Hebu tuchukue Mathayo 16 sasa, kwa dakika moja tu. Mathayo 16:19, hebu na tusome jambo hili, kwa dakika moja tu. Vema.

> *Nami nitakupa wewe funguo za ufalme wa mbinguni: na lolote utakalolifunga duniani, litakuwa limefungwa mbinguni: na lolote utakalolifungua duniani, litakuwa limefunguliwa mbinguni.*

291 Ninawapa changamoto kuliamini. Kama hilo si Neno, Yohana 3:16 si Neno. Kwa nini uchukue baadhi yake na usichukue hayo mengine? Neno lote la Mungu ni kweli, bali halina budi kuingia katika tumbo bikira la uzazi, ambamo hakuna kitu ila Mbegu iliyo humo. Mnaamini? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Vema.

292 Sasa angalieni jambo hili kwa makini sana. Ninajua yule kahaba analidai, nao wanaziondoa dhambi kwa nguvu zao za kimadhehebu, lakini waangalieni watoto wao. Kila ukumbi wa dansi, wanakata nywele zao, wamejipaka rangi kama wachekeshaji, wanaume huko nje wakiishi na wake za watu wengine, wakifanya ubembe, wakizurura huku na huku mitaani, wakioga mchanganyiko, kadhalika. Hakika. Wanasamehe, wanaondoa dhambi, kwa njia yao wenyewe, bali matunda yao yanaonyesha ni kitu gani. Si sawa kwao. La, bwana. Wanafanya nini? Wanavaa kaptura, wanakata nywele zao, wanajipodoa. Yesu alisema, "Kwa matunda yao wanajulikana," kwamba wao ni mbegu ya aina gani. Hivyo ndivyo ilivyo. Mbegu ya kimadhehebu inatoa msamaha wa kimadhehebu. Kweli kabisa.

293 Mungu alisema, "Neno na liwe kwa jinsi Yake." Na ndivyo ilivyo. Hiyo ni kweli. Loo, ndugu, Maandiko ni ya kweli. Mnaamini? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

294 Naye Roho Mtakatifu anashuhudia karama iliyokusudiwa tangu zamani ambayo Kanisa linadai linayo. Ati nini? Kwa kulitia Neno maji, kuitikia Neno, kwa "amina." Wakati liliposema, "Tubuni mkabatizwe, Jina la Yesu Kristo." "Amina." Wakati linaposema mambo haya mengine. "Amina." Jambo ndilo hilo. "Amina," kwa kila kitu, mnaona, huliitikia Neno. Naye Mungu kwa. . .alikusudia karama kuja, kuondoa dhambi, bali ilitolewa kwa Neno-Mwili uliojazwa na Roho. Maana, Neno linaweza, tu, kusamehe dhambi, kwa sababu Neno ni Mungu.

295 Jinsi Mafarisayo walivyokuwa wa kweli! Nilitaja, asubuhi ya leo, tungefikia jambo hili. Sasa, nimemaliza muda wangu. Lakini Ma—Mafarisayo walisema, "Mtu huyu husamehe dhambi. Tunajua yeye ni mkufuru. Mungu pekee ndiye anayeweza

kusamehe dhambi. Naye mtu huyu anasamehe dhambi." Bila kujua ya kwamba Huyo alikuwa ni Neno. Neno husamehe dhambi, maana ni Mungu.

296 Na wakati unapokuwa si mali yako . . . Mungu anajua, alijua, na alijua tangu zamani kwa kujua tangu zamani, ni nani angeichukua karama hii na ni nani angeitumia kwa njia ifaayo. Wale walio nayo wanathibitishwa na Neno la Mungu, pamoja na Neno lingine lote na Roho. Hilo ni dhahiri?

297 Wengine wangetaka uamini huja kwa elimu, masomo, digrii; kama ukienda shuleni kwa muda mrefu sana, kama ukiwa askofu, ukasomea kuwa papa, ama ukiwa kadinali, ama kitu kama hicho. Kwamba, wengine wangetufanya tuamini ya kwamba huko ndiko inakotoka, wakati mtu, kwa kuwekea mikono, anakufanyia kitu cha kufanya jambo hilo. Lakini wako nje ya Neno.

298 Warumi 11:29 ilisema, "Karama na miito havina majuto." Mungu huvitoa. Na pia Yohana 15:16, mkitaka kuiandika.

299 Sikilizeni kwa makini sasa. Jinsi Yesu alivyokuwa tofauti, katika siku Zake, na madhehebu ya siku Zake. Wangeelekeza nyuma kwake . . . Jinsi ningetaka kushikilia hili kwa muda kidogo! Whiu! Wangeelekeza nyuma begani mwao, huko nyuma kote katika wakati, na kusema, "Sisi ni wanafunzi wa Musa. Tunajua ya kwamba Mungu alimtokea Musa, katika kichaka kilichowaka moto. Tunajua."

300 Walijua, walijua historia ya Musa, bali hawakumjua Mungu wa Musa. Maana, Yeye alisimama mbele yao, katika Yohana 6, na kusema, "Musa asijakuwako, Ibrahimu asijakuwako, MIMI NIKO," kile kichaka kilichowaka moto. Walijua historia ya Musa.

301 Ndivyo ilivyo leo. Wanamjua Mungu . . . Wanadai wanajua Neno la Kristo, bali hawamjui Mungu aliyekuwa ndani ya Kristo. Moto wa kuchorwa! Ni nani anayeweza kupata joto kwa moto wa kuchorwa, ujuzi wa seminari? Walimjua Musa, bali si Mungu wake. Yesu angeweza na kweli alisema . . .

302 Amina. Sikilizeni jambo hili, ndugu. Whiu! Sasa najisikia kama Daudi akilizungusha lile kombeo sasa. Natumaini sionekani mwenye kukufuru kwenu, enyi marafiki. Niko sawa, lakini ninajisikia tu vizuri. Ninaanza tu, ninajisikia vizuri sasa.

303 Yesu angeweza na kweli alisema, "Baba aliyenituma yuko ndani Yangu. Na kama vile alivyonituma Mimi, nami nawatuma ninyi," kwa wanafunzi Wake. "Baba aliyenituma yu pamoja Nami. Nisipozitenda kazi za Neno lililoahidiwa la Baba Yangu, basi msiniamini Mimi, kwa sababu hizo ndizo zinazonishuhudia Mimi."

Haleluya! Loo, enyi kanisa, mko wapi? Yesu alisema . . .

Wanasema, "Loo, tunajua ya kwamba Mungu kweli alifanya jambo *hili*, bali sio siku hizi."

Yesu alisema, "Zile zile . . ."

"Tunajua Mungu alikuwa pamoja na Musa."

304 "Lakini Mungu aliyekuwa pamoja Nami yuko ndani Yangu. Kwa sababu, kama hamliamini jambo hilo, angalieni yaliyoandikwa kunihusu Mimi. Angalieni kile Maandiko yalisema ningefanya, na, kama silingani na Maandiko, basi msiniamini Mimi."

305 Hebu niseme jambo hili, si kwa kukufuru, bali hebu niseme hivyo kuhusu Ujumbe ninaohubiri. Mungu asipouthibitisha Huu kuwa ni Kweli, basi si Kweli. Lakini kama Neno linathibitisha ninawaambia Kweli, basi liaminini Neno. Hayo ndiyo yanayoshuhudia kama ninasema Kweli au la. Hayo ndiyo ushuhuda. Hayo—hayo yanashuhudia kwa ajili ya ninii yangu . . . kwa ajili ya huduma aliyonipa. Aliahidi jambo hili katika siku za mwisho. Hili hapa. Alisema kile lingefanya. Hili hapa. Tunaingia moja kwa moja ndani yake sasa. Angalieni kama ni Kweli au la. Acheni Mungu ashuhudie. Kama kazi, mambo ninayohubiri hayatoi ushuhuda, kwamba ni Kweli, basi si Kweli. Lakini kama Neno linanena juu ya jambo hili, nalo hili hapa, basi mtafanya nini kulihusu?

306 Yesu alisema, "Ninawajua. Mnafikiri mnamjua Musa. Mnajua, huenda mlijua historia ya Musa, bali hamumjui Mungu wake. Kwa kuwa, nilikuwako kabla ya Musa. Mimi Ndiye niliyezungumza na Musa. Mimi ni yule 'MIMI NIKO.' Mimi ni Neno."

307 Wasingeweza kuona hilo, maana wao ni wa baba yao, ibilisi. Madhehebu yao yasingewaruhusu kuliona. Hilo halikulizuia Neno kuendelea, vivyo hivyo tu. Liliwaangukia wengine, kweli, na kutoka hapo akaja Bibi-arusi, kizazi hicho. Vema. Ni tofauti jinsi gani, moto wa kuchorwa!

308 Yesu angeweza—angeweza kusema, "Baba aliyenipeleka," yuko pamoja Naye. "Na kazi nizifanyazo Mimi, zinashuhudia, kwa sababu ninafanya mambo yale yale Maandiko yalisema ningefanya."

309 Wayahudi walimjua Mungu wao wa kihistoria. Vivyo hivyo sasa. Naam. Kwa nini walimjua Mungu wa kihistoria? Ni kwa sababu walikuwa na uzao wa kihistoria. Kwa nini hawakumpokea? Kwa sababu lilichanganyikana na madhehebu.

Yesu alijua ni Nani aliyemtuma, kwa kuwa Yeye aliyemtuma alikuwa ndani Yake.

310 Wala hapakuwa na dhehebu lililofunganishwa Naye. Amina. Niambieni ni lipi. "Alitoka shule gani?" Wanasema, "Alipata wapi hekima hii? Elimu hii ilitoka wapi?" Wasingeweza kupata shule ambayo Yeye aliwahi kwenda.

311 Na, hata hivyo, akiwa na umri wa miaka kumi na miwili, aliwafadhaisha waandishi na Mafarisayo. Loo, jamani! Hilo lilinena habari zake. Kwa nini hawakumwambia jambo fulani, kama mtoto? Alikuwa ni Neno la Mungu. Wasingeweza kustahimili Hilo.

312 Si ajabu watu walishangaa mno kwa Mafundisho Yake! Uliwahi kusoma hilo? Marko 1:22, kama ukitaka kuliandika. "Watu wakashangazwa mno na Mafundisho Yake, kwa sababu alifundisha kama mtu mwenye mamlaka." Alijua alichokuwa akizungumzia. Mnaona?

313 Kanisa sasa linapaswa kuwa na sehemu maradufu ya Roho. Kwa kuwa ni kweli, kama vazi la Eliya lililomwangukia Elisha, sehemu maradufu, kitu kile kile kilitoka kwa Yesu Kristo. Sasa, mnasema, "Loo, Ndugu Branham, unanena kuhusu Kanisa Lake." Hiyo ni kweli. Huo ni Mwili Wake.

314 Je, mke wangu si ni sehemu ya mwili wangu, na mke wako si sehemu ya mwili wako? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] "Nyama ya nyama yako, na mfupa wa mfupa wako," kwa ndoa takatifu. Hiyo ni kweli? ["Amina."] Hiyo ndiyo sababu Mkristo hapaswi kumwoa kahaba. Mnaona? Hilo si sawa, la, bwana, maana linavunja mambo yote ya Mungu.

Unasema, "Loo, sasa, Ndugu Branham, ngoja kidogo. Unanena kuhusu Roho wa Kristo kuwa juu ya . . . "

315 Biblia ilisema itakuwa hivyo. Hiyo ni kweli? Isaya 9:6, ilisema—ilisema, "Kwa ajili yetu Mtoto amezaliwa, tumepewa Mwana; ataitwa Jina lake Mshauri, Mfalme wa Amani, Mungu mwenye nguvu, Baba wa milele. Na Ufalme Wake hautakuwa na mwisho. Na uweza wa kifalme utakuwa juu ya ninii Yake . . . " Nini? [Kusanyiko linasema, "'Bega.'"—Mh.] Hiyo ni sehemu ya Mwili Wake. Jamani! Huo ni Mwili Wake. Sivyo? ["Amina."] "Mabega Yake" ni Mwili Wake. Serikali ya duniani iko wapi? Katika Mwili Wake.

316 "Watakatifu wataihukumu dunia." Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Paulo alisema, "Thubutuni kupelekana mahakamani, wala si mbele ya kanisa." Vema. Mnaona? "Watakatifu watauhukumu ulimwengu."

317 Serikali itakuwa juu ya nini? Juu ya mabega, Mwili Wake. "Serikali itakuwa juu ya mabega Yake," hiyo ni sehemu ya ule Mwili. Ni kitu gani? Nguvu zake za duniani. Nguvu za Mungu za duniani ni Neno Lake lililofanyika mwili katika Mwili Wake hapa duniani, zikitimia.

318 Musa . . . Sikilizeni. Hebu tuyakwepe baadhi yake. Wajumbe wa Mungu sikuzote wamekataliwa. Mnaamini hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Musa alikataliwa. Hiyo ni kweli? ["Amina."] Yesu alikataliwa. Naye Luka alisema, katika 10:16, kama unataka kuliandika hilo. Vema. Kukataliwa!

319 Samweli wa Kwanza 8:7, ujumbe wa Mungu ulikataliwa. Mungu alikuwa na mjumbe, nabii, aitwaye Samweli. Mnaamini hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Walimkataa pamoja na ujumbe wake. Wakauchukua ulimwengu.

320 Hii ni sheria ya—ya Mungu. Hii itaninii . . . Sijui kama niseme hili ama nisiseme. Hii ni sheria ya Mungu. Sheria ya Mungu ni kumpokea mtumishi aliyethibitishwa.

321 Hebu—hebu tuthibitishe tu hilo, kwa dakika moja. Ninataka kuchukua moja ya Maandiko hapa, Yohana 13:20. Hebu tuone tu. Nina jambo fulani lililoandikwa hapa, kidogo limeingia niani mwangu tu wakati huo. Loo, naam, hili hapa.

> *Amin, amin, nawaambia, Yeye* ampokeaye mtu yeyote *nimpelekaye,* anipokea *mimi; naye* anipokeaye *mimi,* ampokea *yeye aliyenipeleka.*

322 Mtumishi aliyethibitishwa! Loo, ndugu, kuna mahubiri elfu moja yaliyowekwa papa hapa sasa. Mnaona? Hiyo ni kweli. Loo, jamani! Ni sheria ya Mungu. Lipokeeni.

Samweli alishuka na kusema, "Nataka kuwaulizeni jambo fulani. Je, nimewahi kuwaambia lolote katika Jina la Bwana ambalo halikutimia?"

Kasema, "La."

"Je, nimewahi kuchukua sadaka yoyote kujenga majengo makubwa, na kufanya mambo mengi sana na kujitukuza?"

"La."

"Je, Mungu amethibitisha, kujibu Neno ambalo nimesema?"

"Naam."

"Vema, mbona hamnisikii?"

Yesu aliwaambia Mafarisayo . . .

"Tunajua umezaliwa katika uasherati."

323 Akasema, "Ni nani kati yenu anayeweza kunihukumu kwamba nina dhambi? Hebu niwaonyeshe Neno la Mungu, mwone kama mnaliamini, mwone kama Mungu analithibitisha ndani yenu. Na hebu ninene kwa nafsi Yangu, kama nikinena Mwenyewe, mimi ni mwongo. Lakini kama nikinena habari za Mungu, na Mungu ananena kupitia Kwangu, kwa Neno Lake, basi ni Kweli. Basi, ni nani anayeamini Neno la Mungu, Mimi au ninyi?" Ha-ha! Hilo liliwaweza.

324 Yesu alisema, "Yeye awapokeaye wale ninaowatuma, anipokea Mimi." Na, sasa, hao anaowatuma. "Nao wanipokeao Mimi humpokea Yeye aliyenipeleka." Laiti tungalikuwa na wakati wa kukawia juu ya hilo. Unaweza tu kumtumikia Mungu wakati . . . Unaweza tu kumtumikia Mungu kama ufanyavyo na—na kuwaamini watumishi ambao Mungu anawatuma. Unaweza tu kumtumikia Mungu duniani, unaona, wakati watumishi wa Mungu waliotumwa duniani kwa uvuvio wa

Kiungu wanapokufasiria Neno. Mnaamini hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

325 Mnataka kuandika Maandiko juu yake? Wakorintho wa Kwanza 14:16. Paulo alisema, "Nifuateni kama ninavyomfuata Kristo," pia, 11:1. Luka 10:16, angalia yale aliyosema, yale Yesu aliyosema pale. Luka 10:16, naamini tuko karibu sana nalo hapa. Hebu tuone linavyosema wakati mmoja hapa, Luka 10:16, wakati wakiandika hayo mengine. Sasa, hiyo ni Wakorintho wa Kwanza 14:16, pia 11:1, na Luka 10:16.

326 Sasa hebu tusome. Naendea Luka 10:16, hapa, kusoma tu huku nyote mkiangalia hayo mengine sasa, kwa muda kidogo tu. Vema. Sisi hapa.

> *Awasikilizaye ninyi anisikiliza mimi;. . .awakataaye* ninyi, anikataa *mimi;*. . .anikataaye *mimi,* anamkataa *yeye aliyenipeleka.*

327 Hiyo inathibitisha ya kwamba Mungu hunena Ujumbe Wake kupitia kwa watumishi Wake. Daima imekuwa hivyo. Hiyo ni kweli.

328 Sasa, nguvu za Kanisa liaminilo. "Kristo ana mamlaka yote mbinguni na duniani." Mnaamini hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Sasa, vipi kama Yeye yuko ndani yenu? Je, Kristo ana nguvu zote? ["Amina."] Mathayo 28:18. Vema. Yeye ni Neno-Mbegu katika Mwili Wake. Na Yeye, ndani yetu, anakuwa Neno-Mbegu ndani yetu. Ati nini? Yote aliyokuwa Mungu, aliyamimina ndani ya Kristo; na yote aliyokuwa Kristo, yalimiminwa ndani ya Kanisa. Hayo ndiyo mamlaka.

329 Sasa angalieni. Kumbukeni sheria ya Mungu ya kuzaa tena, sasa, kumbukeni, "Kwa jinsi yake." Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Uzao wa Kristo, Neno, hauna budi kupitia katika Mwili Wake. Ha, ha, ha, ha, ha!

330 Mnachoka? [Kusanyiko linasema, "La."—Mh.] Vema. Hebu kidogo tu sasa. Hebu tutulieni tu na kuomba. Ninataka kuingiza jambo hili, vizuri sana. Ninataka hili liingie ndani kabisa.

331 Mbegu ya Kristo lazima, l-a-z-i-m-a, lazima ije kupitia Mwili Wake; si kupitia dhehebu, bali kupitia kwa Mbegu ya Neno iliyozaliwa mara ya pili, lazima ipitie. Sasa, kumbukeni. Ni kitu gani? Mbegu ya Kristo.

Mbegu yangu huja namna gani? Kupitia mwilini.

Mbegu ya mtofaa inakujaje? Kupitia mwilini.

332 Mbegu ni kupitia kwa Mwili, na Kanisa ni Mwili wa Kristo. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Kanisa la Biblia! Kuzaliwa huku kunamzaa (huko ni Kuzaliwa upya) Yeye Mwenyewe katika Mwili, Kanisa Lake, ni Neno Lake, kusudi watu waweze kuona thibitisho la Waebrania 13:8, "Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele." Mnaamini? ["Amina."] Hawa si ma-. . .machotara wa kimadhehebu, sasa. Hawa ni wale walio

kwenye mzingo, wakingojea kuhesabu kinyumenyume, mnajua ninalomaanisha, wakijiandaa kuchukua roketi. Utukufu! Hawa si chotara wa kimadhehebu; hawasimami Hapa ndani, la. La, bwana. Ni ule Uzao.

333 Paulo alihofu kwamba watu wangeangalia namna fulani ya maneno makubwa ambayo angeweza kutamka, baadhi ya elimu yake. Wakorintho wa Kwanza 2:1 hadi 8. Mkitaka kuliandika. Wakorintho wa Kwanza 2:1 hadi 8, Paulo alisema, "Sikuja kwenu kamwe, nikinena maneno ya kiakili, mwajua, kusudi imani yenu iwe katika kitu fulani cha seminari. Lakini nilikuja kwenu kwa urahisi, katika nguvu na dhihirisho la Roho Mtakatifu, ili kwamba Neno lenu . . . ili imani yenu ikae katika Neno la Mungu." Naam, bwana.

334 Ingawa, makanisa ya kimadhehebu yatazidi idadi ya Bibiarusi, elfu moja kwa mmoja. Mnaamini hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Mnaamini Biblia inafundisha hilo? ["Amina."] Isaya 54:1. Yeye aliahidi jambo hilo. Kwa kuwa . . .

335 M—mnataka mimi—mnataka nilisome? Vema, hebu tulifungue. Mnataka kuona ni wapi, ambapo Yeye aliahidi kwamba wangewazidi kwa wingi. Hebu tufungue Isaya 54, 53, 54:1.

> *Imba, wewe uliye tasa, wewe usiyezaa; paza sauti yako kwa kuimba, piga kelele, wewe usiyekuwa na utungu: maana watoto wake aliyeachwa ni wengi kuliko watoto wa mke aliyeolewa, asema* BWANA.

336 Ha-ha-ha-ha! Hiyo ni kweli? Watoto wa yule kahaba ni wengi kuliko Mke aliyeolewa. Hakika. Ni wengi kuliko sisi, mara nyingi. Ingawa wao—ingawa wana idadi kubwa zaidi, hawana baba wa kweli.

337 Sasa, aina za kimadhehebu wamewakilishwa katika Yuda 8-13. Hilo ni kanisa la kidunia, "Mawingu yasiyo na mvua, yanayotoa povu la aibu yao wenyewe."

338 Kanisa la Kipentekoste linawakilishwa, la kundi hilo la kimadhehebu, katika Timotheo wa Pili 3:1 hadi 8, "Wenye mfano wa utauwa." Uzao wao huzaa wa jinsi yao. Angalieni, yule towashi . . .

339 Loo, hapa, tutaingia katika jambo fulani lenye kilindi sasa. Sasa angalia hili Kanisa-Mbegu, Kanisa hili halisi lenye Mbegu halisi ya kiume, ya kweli.

Angalieni, huyo towashi alikuwa pamoja na D.D. wote.

340 Sasa kumbukeni, Mungu kamwe hakukabidhi—Mungu kamwe hakukabidhi mahubiri Ya—Yake na Injili Yake kwa Malaika. Ni wangapi wanaojua hilo? Ni wangapi wanaojua ya kwamba Wagalatia 1:8 ilisema, "Kama Malaika akija kutoka Mbinguni na kuhubiri jambo lingine mbali na walilokuwa wamehubiri, na lilaaniwe"? Kwa hiyo, Malaika amekosea kama

yeye ni tofauti na Neno. Mungu alishuka akaja chini ya Malaika, na kuwakabidhi wanadamu, ambao walikuwa wana. Mnaamini hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Sasa angalieni. Sasa, Yeye kamwe hakuikabidhi Malaika. Angalieni, Yeye hakufanya hivyo.

Sasa, Filipo alikuwa amekwea kwenda Pentekoste, Yerusalemu, kuabudu. Ni wangapi wanaosema "amina" kwa hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

341 Huyo towashi, alikuwa pamoja na ma-D.D. na ma-L.D. wote, na kila kitu. Lakini kwa nini hakupata kitu? Alishuka akaja, akisoma unabii wa Isaya.

342 Ingawa Malaika alimwelekeza Filipo kwake, lakini Mbegu ya Uhai ilibidi ije kupitia kwa Mwili, Filipo. Ah! Loo, ndugu, sasa tuko mstarini. Hiyo Mbegu ilitoka wapi? Kupitia kwa Malaika? Malaika alimwonyesha mahali pa kwenda. Malaika ni mjumbe. Huyu *hapa* ni mwana. Filipo alikuwa na Chembe ya uhai, Ujumbe, Neno. Hivyo ndivyo Mtoto anavyoweza kuzaliwa. Filipo akaweka mikono yake juu yake. Filipo akambatiza katika Jina la Yesu Kristo. Hapo akatokea Roho wa Mungu. Hakika. Sasa, ilibidi ile Chembe ya uhai itoke kwenye ule Mwili. Mwili gani? Mwili wa Kristo. Sahihi. Naye Filipo alikuwa mshiriki wa ule Mwili.

343 Sasa sikilizeni. Jambo lile lile lilitukia katika Matendo 10:48. Petro alikuwa juu ya nyumba. Malaika alimwelekeza nyumbani kwa Kornelio. Lakini Neno lilitoka wapi? Mwili. Loo, loo, loo, loo, loo! Ninajisikia vizuri sana, najisikia kuendelea na safari. Malaika alikuja na kusema, "Usijali. Usiite kitu chochote kichafu. Endelea tu, usiwazie chochote."

344 "Basi Petro alipokuwa akisema Maneno haya," si Malaika, si kadinali. "Petro alipokuwa akisema Maneno haya." Kitu gani? Yeye alikuwa ule Mwili. Alikuwa na Neno. Neno likashika. Loo, ndugu! Whiu! Huh! Loo, jamani! Malaika aliliongoza, bali Uhai ulipitia katika Mwili wa Kristo.

345 Paulo, alipokuwa njiani kwenda Dameski, ono lilimwelekeza. Lakini Anania ndiye aliyekuwa na ile Chembe ya uhai, alikuwa na Neno. Amina. Nabii huyo, Anania, aliona ono lililosema, "Panda kule, ukamwekee mikono."

346 Kasema, "Ndugu Sauli, Bwana alikutokea barabarani, ukishuka kuja huku." Alijuaje? Alikuwa na Neno. Neno la Bwana lilimjia nabii. Akatabiri, akapanda kule juu na kusema, "Yeye amekuja, amenituma hapa juu, nipate kuweka mikono yangu juu yako, nawe ungeponywa na kumpokea Roho Mtakatifu. Upate kuona." Magamba yakaanguka kutoka machoni mwake. Akaamka, akabatizwa, Jina la Yesu, akaenda kusoma.

Malaika alimwelekeza, hiyo ni kweli, bali Paulo ndiye aliyekuwa na Mbegu-Seli zazi.

347 Inahitaji Roho wa Mungu, ile Mbegu, kutoa Uzima wa Milele. Whiu! Jamani!

348 Je, ni saa nane bado? [Kusanyiko linacheka. Mtu fulani anasema, "Imepita."—Mh.] Najua hilo. Lo! Nitasoma baadhi, basi. Hebu nisome tu kwa yapata dakika kumi. Sivyo? ["Amina."] Nina wazo zuri, ningeweza kukaa hapa, lakini afadhali niendelee kidogo hapa. Nasi tuna wakati wetu. Ni Saa tano kasoro dakika ishirini na tano. Sijui tutafika Georgia saa ngapi. Laiti ningaliweza kusimama na kutoa maoni juu ya jambo hili kidogo tu. Lakini nitalisoma tu polepole sana. Sikilizeni kwa makini. Hili hapa nililochukulia kalamu, sehemu yake.

349 Mnaona, marafiki, kile nilicho nacho, jinsi nimesimama jinsi nilivyofanya? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Mnaona ni kwa nini ninashindania, "Ondokeni kwenye hayo madhehebu mkapate Kanisa halisi la Mungu"? ["Amina."] Mnaona ni kwa nini haina budi kutoka kwenye Neno? ["Amina."] Haliwezi kuja kwa hekima ya mwanadamu. Halina budi kuja kwa Neno la Mungu. Hiyo ndiyo sababu ninaamini Neno jinsi tu lilivyoandikwa. Sitaongeza chochote wala kuondoa chochote. Nilihubiri tu namna hiyo, niendelee tu kusonga mbele.

350 Sasa, ndugu, ninyi nyote mlio kwenye kanda, msipokubaliana nami, nitawaombea. Kama nimekosea, niombeeni.

351 Nitasoma baadhi yake sasa. Ninii tu. . . Nawatakeni msikilize hili kwa makini sana. Hapa ndipo Roho aliposema, "Itwae kalamu." Ingenibidi kuachilia baadhi Yake, bali sina budi kuwaletea baadhi Yake. Vema.

[Ndugu Branham anasoma aya ya 352 hadi 379—Mh.]

352 Sasa, haya ndiyo ninayojaribu kuwaambia. Sheria ya kuzaa, kuzaa kwa jinsi yake, Mwanzo 1:11. Siku hizi za mwisho, Kanisa-Bibi-arusi wa kweli anakuja kwenye Jiwe la Kichwa, litakuwa Kanisa kuu, Jamii kuu, wakati ninii. . . inapokaribia lile Jiwe kuu la Kichwa. Watafanana sana, sana Naye, hata watakuwa katika sura Yake hasa, wapate kuungana Naye. Watakuwa Mmoja. Watakuwa ndio dhihirisho lenyewe la Neno la Mungu aliye hai. Madhehebu hayawezi kamwe kutoa Hili. Hii itakuwa . . . Wataleta kanuni zao za imani na mafundisho ya sharti, yaliyochanganywa na Neno, na—na kuleta mazao chotara.

353 Mwana wa kwanza alikuwa Mbegu-Neno la Mungu lililonenwa. Alipewa bibi-arusi. (Ninapitia tu upya. Roho sasa anachukua yale niliyosema. Mnaona?) Bibi-arusi, kuji-. . . kujizaa mwenyewe. Akaanguka. Mnaona, hivyo ndivyo . . . Bibi-arusi alipewa, kujizaa mwenyewe tena, mwana mwingine wa Mungu. Lakini akaanguka, kwa kuchanganya mbegu, mnaona. Kujizaa mwenyewe; bali akaanguka, ikamfanya afe.

354 Mwana wa pili, Mbegu-Neno la Mungu lililonenwa, alipewa bibi-arusi, kama Adamu. Lakini kabla hajaweza kumwoa,

alikuwa ameanguka, pia. Kwa kuwa alipewa uhuru wa kujichagulia, kama mke wa Adamu alivyopewa, kuliamini Neno la Mungu na kuishi, ama kulitilia shaka kisha kufa. Naye akalitilia shaka.

355 Ndipo kutoka kwenye kundi dogo la Mbegu ya kweli ya Neno, Mungu atamkabidhi Kristo Bibi-arusi mpendwa, Bikira, Bikira wa Neno Lake. Na kupitia kwao, na kwa wao, yatatimizwa yote yaliyoahidiwa kwa ajili ya Neno Lake katika yule Bikira asiyejua kanuni za imani za kujibunia wala mafundisho ya sharti.

356 Neno la ahadi liko ndani Yake Mwenyewe, kama lilivyokuwa ndani ya Mariamu, Mungu Mwenyewe akidhihirishwa. Yeye atatenda Mwenyewe, kwa Neno Lake Mwenyewe la ahadi, apate kutimiza yote yaliyoandikwa juu Yake, kama alivyofanya alipotoka kwenye tumbo bikira la uzazi. Mfano wa tumbo la uzazi la Roho sasa, vivyo hivyo na Bikira sasa, akilikubali Neno Lake, "Na iwe kwangu kama ulivyosema." Ingawa lilisemwa na Malaika, wakati likiwa bado ni Neno lililoandikwa, Isaya 9:6.

357 Watampenda, watawapenda walio Wake, na watakuwa na uwezo Wake, kwa sababu Yeye ndiye Kichwa chao. Nao ni raia Wake, chini ya Kichwa Chake. Uongozi wa Kristo ulikuwa ni Wake.

358 Angalieni ni mpatano ulioje! Yesu kamwe hakufanya lolote mpaka alipomwona Baba, ama, Baba alipomwonyesha Yeye kwanza. Mpatano kati ya Mungu na Kristo, mnaona, Yohana 5:19. Vivyo hivyo Bibi-arusi naye, Naye humwonyesha Neno Lake la Uzima. Yeye humwonyesha, Naye hulipokea. Kamwe halitilii shaka. Hakuna kitu kinachoweza kumdhuru, si hata mauti. Kwa kuwa Mbegu ikipandwa, maji yataifufua tena. (Amina. Ndipo nikapata "Haleluya!" kubwa mno.) Hii hapa siri. Neno liko ndani ya Bibi-arusi, na nia ya Kristo, kujua kile anachotaka kifanywe na Neno. Naye anakifanya katika Jina Lake. Yeye ana BWANA ASEMA HIVI. Ndipo linarutubishwa, kwa hiyo Roho Mtakatifu analitia maji mpaka limekomaa na kutumikia kusudi Lake.

359 Wanafanya tu mapenzi Yake. (Amina. Nitaamini hilo.) Hakuna mtu anayeweza kuwashawishi vinginevyo. Wana BWANA ASEMA HIVI la sivyo wanatulia. Ndipo watafanya kazi za Mungu, kwa kuwa ni Yeye Mwenyewe ndani yao akiendeleza Neno Lake kutimiza, kama alivyofanya katika siku Zake. Mambo yote, alipokuwa hapa, hakuyakamilisha yote alipokuwa hapa, kwa kuwa wakati haukuwa umetimia bado.

360 Sasa hebu na tusimame kama Yoshua na Kalebu. (Sasa angalieni kwa makini. Hili litakuwa na msingi wa kiroho.) Sasa hebu na tusimame kama Yoshua na Kalebu, tunapoiona ile Nchi ya ahadi ikianza kuonekana. Wakati wa kutolewa unakaribia. Yoshua, katika Kiebrania, maana yake ni *Mwokozi*,

naye anawakilisha kiongozi aliyeahidiwa wa wakati wa mwisho kulivusha Kanisa. Kalebu anawakilisha yule mwaminio wa kweli aliyekaa na Yoshua. Mungu alianzisha Israeli kama bikira kwa Neno Lake. Lakini walitaka kitu tofauti. Vivyo hivyo na kanisa la siku za mwisho.

361 Angalia jinsi Mungu hakuihamisha Israeli mpaka wakati Wake Mwenyewe uliokusudiwa. (Sasa sikilizeni. Hili litamaanisha jambo fulani.) Yoshua aliungojea wakati huo. Haidhuru, ni kiasi gani huenda watu walisema, "Mungu alitupa nchi, ile ahadi. Hebu twende sasa tukaiteke." Huenda walisema, "Yoshua, ulipoteza agizo lako. Umekwisha kabisa. Kwa nini hufanyi kitu? Ulikuwa ukifanya, ukijua BWANA ASEMA HIVI katika dakika moja, na yaliyokuwa mapenzi ya Mungu." Lakini nabii huyu mwenye hekima, aliyetumwa na Mungu alijua ahadi ya Mungu, lakini pia alijua kuingojea ahadi hiyo, uamuzi dhahiri kutoka kwa Mungu kwa ajili ya wakati wake. (Angalieni mifano hii. Sasa angalieni.) Basi wakati ulipowadia, Mungu akampa Yoshua, ambaye alikuwa amekaa pamoja na Yeye, kwa Neno, kwa sababu asingeweza kuwatumaini wengine. Angeweza kuwa na imani naye. Vivyo hivyo itajirudia.

362 Kama vile yule nabii mwenye nguvu aliyetiwa mafuta, Musa, alivyojua Mungu angemtumia. Kwa kuwa alikuwa amemthibitisha Musa kuwa mtumishi Wake, kwa kuzaliwa kwake kwa njia ya kipekee, katika wakati ufaao ambao, ukombozi wa uzao wa Ibrahimu ulikuwa umewadia. (Mnalipata?) Musa kamwe hakukaa Misri na kubishania mambo yake ya Kimaandiko nao. Kamwe hakubishana na makuhani. Lakini alienda nyikani na kumngojea Bwana, mpaka—mpaka watu walipokuwa tayari kumpokea. Ilibidi aje kuwashuhudia, lakini wasingempokea. Mungu akamwita nabii Wake nyikani. Mungu alikuwa ameshuhudia alikuwa amemchagua. Lakini kule kungojea hakukuwa kwa Musa, bali ili watu wapate kujiandaa kumpokea Musa. Musa alifikiri watoto wangeelewa kwamba alikuwa ametumwa. (Sikuliandika kamwe; Yeye aliliandika.) Ndivyo ilivyo sasa.

363 Kama vile Eliya, baada ya yule nabii mwenye nguvu aliyethibitishwa ambaye Neno la Mungu lilimjia, alikuwa amemaliza kuhubiri ujumbe Wake kwa hayo makundi ya kisasa ya Marekani ya Mama Taifa, pamoja na makundi yao yaliyojikata nywele na kujipaka rangi ya Yezebeli. Mungu akimthibitisha nabii Wake; kila wakati alipotabiri, ilikuwa ni kweli. Ilimbidi Mungu kumwita atoke hudumani, mpaka alipokipiga kizazi hicho kwa mapigo makuu, kwa kukataa ujumbe wa nabii Wake na Neno la Mungu ambalo alikuwa amewatumia. Mungu alimtuma nyikani, mafichoni, hata mfalme asingeweza kumwita atoke. Na wale waliojaribu kumshawishi dhidi ya mapenzi ya Mungu, walikufa kwa kufanya hivyo. (Ee Mungu! Whiu. Uh!) Lakini wakati Mungu aliponena na

nabii Wake mwaminifu kwa ono, kutoka nyikani akaja na BWANA ASEMA HIVI. Alifanya nini? Moja kwa moja kwenye Neno, akarudi kwenye Neno, akaleta mawe kumi na mawili na kuyafingirisha pamoja.

364 Kama vile Yohana Mbatizaji, mtangulizi mwaminifu wa Kristo, nabii aliyetiwa mafuta. Si shule ya baba yake, si shule ya Kifarisayo, hakuna dhehebu lingeweza kumwita kutoka nyikani ambako Mungu alikuwa amemtuma, mpaka akasikia Sauti ya Mungu. "Masihi amekaribia." (Mnasikiliza, nia ya kiroho? Ningesema nini zaidi hapa. Ninaruka jambo fulani hapa sasa.)

365 Ni tofauti jinsi gani siku hizi, wengi wanaojiita wainjilisti wanadai wanalo jibu kwa...kutoka kwa Mungu, kwa ajili ya watu. Kama tu vile Kora alivyofanya, akikana, akipinga mamlaka ya nabii wa Mungu aliyethibitishwa, aliyetiwa mafuta, Musa, akidai alikuwa na jibu. Huu ulikuwa ni mpango wa kutengeneza pesa, pia, ndama wa dhahabu; kama vile wengi wafanyavyo siku hizi, majengo makubwa, shule kubwa, viangulio vya kuangua vifaranga vya uzao ule ule wao. Ndipo watu, wakati huo kama vile sasa, wakaliangukia. Baada ya kulisikia Neno la kweli la Mungu, kupitia kwa nabii aliyetiwa mafuta ambaye alithibitishwa, waliuangukia uongo wa Kora. Nabii aliyethibitishwa na Mungu, naye Mungu alijua...na alijua Mungu alikuwa amewaambia. Israeli walijua Mungu alikuwa amewaambia, dhahiri, ya kwamba angewathibitisha manabii Wake kwa Neno Lake. Kora hakuwa nabii wa Kimaandiko, bali lilionekana ni zuri sana kwa watu, kama vile linavyoonekana sasa. Leo, leo hii ni damu mikononi mwako, mipira ya moto jukwaani, mafuta katika vidole vyako. Na jambo lilo hilo hutoa wahubiri wanawake, nywele fupi, zilizokatwa, vipodozi. Mna nini? Usingefikiri ya kwamba watu wangeangukia jambo hilo, lakini walianguka kwa Kora. Nao wanafanya jambo lile lile sasa, na kuliacha Neno la kweli, kwa ajili ya madhehebu. Kaptura, inaonyesha ni mbegu ya namna gani iliyo ndani yao.

366 Lakini, Mungu ashukuriwe, Israeli wote hawakumfuata Kora. Wengine walikaa karibu na Musa, yule nabii aliyetiwa mafuta akiwa na Neno la Mungu. Ndivyo ilivyo, leo, kwa wengi wa Wateule wa Mungu, kwa Neno Lake na Roho Wake.

367 Kumbukeni, magugu, kwekwe, zinapaswa kukusanywa na kufungwa matita-matita. (Hiyo ni kweli?) Hili limetimia. Makanisa haya ya kimadhehebu yaliyoasi yamefungwa kwa nguvu zaidi kuliko yalivyowahi kufungwa. Wamefunganishwa pamoja katika muungano wa makanisa, tayari kwa mioto ya hukumu ya Mungu. (Sikuandika hili kamwe. Ninajisikia ya kwamba Yeye aliliandika.) Wapentekoste wamejaa, wanavyojiita, sawa na wao. Lile Neno-ngano litakusanywa siku moja, baada ya Wao kuondoka, kwa ajili ya ninii ya Bwana.

368 Mungu ameahidi. . .Iweni waangalifu. Mungu ameahidi Malaki 4 kwa ajili ya siku hii ya mwisho. Na Malaki 4 bado haijatimia, lakini haina budi kutimia, kwa kuwa ni Neno la Mungu lililorutubishwa lililonenwa kupitia nabii Malaki. Yesu alirejea kwenye jambo hilo. Itakuwa tu kabla ya kule Kuja kwa Kristo, mara ya pili. (Sikilizeni kwa makini sasa.) Maandiko yote ambayo hayajatimia, hayana budi kutimia, kabla ya wakati huo. Biblia inapaswa kumalizika, ku—kumalizwa. Kipindi cha Mataifa kitamalizika, pamoja na wakati wa kanisa, wakati mjumbe huyu aliyetiwa mafuta atakapowasili. Bila shaka, atapanda Mbegu ya Biblia nzima, moja kwa moja kutoka kwa yule nyoka hadi kwa yule mjumbe katika mvua ya masika. Ndipo atakataliwa na watu wa kimadhehebu, kama babu yake, Yohana na Eliya, kama ilivyonenwa na Bwana wetu.

369 Watu, kama vile Eliya alivyokuwa mara ya kwanza, kwa wakati wa Ahabu, itatendeka hapa katika nchi hii, kwa kuwa nchi hii ni mfano wa Israeli. Someni au msikilize *Dini ya Yezebeli*. Kama vile nchi hii, babu zetu, kwa kuabudu jinsi walivyotaka, walikuja katika nchi hii na kuwafukuza wenyeji na kuiteka, vivyo hivyo na Israeli walichukua mamlaka walipotoka Misri. Tulikuwa na watu watauwa, kama vile Washington, Lincoln. Wao walikuwa na watu mashuhuri, watauwa, kama Daudi na kadhalika. Ndipo wakamleta Ahabu kwenye kiti cha enzi na Yezebeli nyuma yake, kumwongoza. Vivyo hivyo na sisi.

370 Kwa hiyo ni kwenye wakati huu, katika nchi hii, ambapo mtu huyo atatokea, kwa kuwa liko katika Maandiko na ni BWANA ASEMA HIVI. Ndipo katika mvua ya vuli utakuja Mlima Karmeli, shindano la kuamua. Biblia ikitimia, kikamilifu! Yohana Mbatizaji, "Mjumbe Wake mbele ya uso Wake," katika Malaki 3. Alipanda mvua ya masika na akakataliwa na makanisa, madhehebu, Mafarisayo na Masadukayo katika siku zake. Yesu akaja na akawa na mashindano ya kuamua ya Mlima wa Kugeuka Sura. Mtangulizi huyu, wa siku za mwisho, atapanda kwa ajili ya mvua ya masika. Yesu atakuwa shindano la kuamua kati ya madhehebu na kanuni za imani, ambalo ni Neno Lake, atakapokuja, shindano la kuamua, kule Kunyakuliwa kwa Bibi-arusi Wake. La kwanza lilikuwa Mlima Karmeli, la pili lilikuwa Mlima wa Kugeuka Sura, la tatu litakuwa Mlima Sayuni. (Utukufu!)

371 Tabia ya Eliya, tabia ya Musa, tabia ya Yohana, wakiacha huduma yao, wengi wa watu hawakuwaelewa. Ilikuwa ni kwa sababu walikataliwa, na Ujumbe wao. Mbegu ilikuwa imepandwa. Hukumu ilikuwa inafuata. Nao walikuwa ni ishara kwa watu, kutoka kwa Mungu, ya kwamba hukumu ilikuwa imekaribia. Kupanda kulikuwa kumekwisha.

372 Ninaamini, siku moja, Bibi-arusi halisi wa Kristo atalazimika kuacha kuhubiri Neno la Mungu. Biblia inatabiri juu yake, katika Ufunuo 13:16. (Kama unataka kuliandika.)

Madhehebu yatamlazimisha kukoma, la sivyo achukue alama yake. Ndipo, wakati, Mwana-Kondoo atamchukua Bibi-arusi Wake na kumhukumu kahaba kwa ajili ya jambo hili.

373 Kumbukeni, Musa, aliyezaliwa kwa ajili ya hiyo kazi, ilimbidi kumngojea Mungu apate karama ya ziada kwa ajili ya kazi hiyo. Ilimbidi kurudi nyuma na kungojea, na kwa ajili ya wakati uliowekwa na Mungu. Ilibidi farao fulani awe kwenye kiti cha enzi, na ilibidi watu wawe wana shauku ya Mkate wa Uzima, kabla Mungu hajamrudisha.

374 Sasa, kukiweko na maelfu ya watenda ishara katika siku hii ya mwisho, imesababisha kizazi cha watafuta ishara ambao hawajui lolote tena kuhusu mwenendo wa kweli wa Mungu na Neno Lake katika siku hizi za mwisho. Kama nilivyosema: wape damu na mafuta, na maonyesho ya kimwili jukwaani, nao wataliunga mkono, liwe ni Neno la Mungu au la, liwe ni la Kimaandiko au la. Yesu ametuonya juu ya mambo kama hayo wakati wa mwisho. Kama nilivyosema: katika Mathayo 24, roho mbili, zinazofanana sana, "Itawadanganya walio Wateule kama yamkini."

375 Unawezaje kuwatofautisha? Wape jaribio la Neno. Unawezaje kujua jambo hilo? Nena Neno, uone wanayosema kulihusu. Kama hawaliamini Neno, hawana Seli Zazi-Mbegu ndani yao. Wao ni wa yule mwovu, na wanawadanganya. Kama vile bibi-arusi wa kwanza alivyodanganywa, na bibi-arusi wa pili alivyodanganywa, wao ni wadanganyaji wa bibi-arusi wa tatu, kwa kulichanganya Neno, ama kujaribu kufanya hivyo. Mungu kamwe hakuweka ishara mbele ya Neno Lake. (Amina. Hilo ni kali sana.) Mungu kamwe hakuweka ishara mbele ya Neno Lake. Ziliongezwa kwa ajili ya thibitisho la Neno, bali Neno ndilo la kwanza. Kuthibitisha jambo hilo, Eliya alimwambia yule mwanamke, "Niokee keki kwanza," ndipo uangalie mwujiza ukitendeka. Njoo kwenye Neno, kwanza, kisha uone huo mwujiza. Neno-Mbegu, Lenyewe, ndilo Roho Mtakatifu hutia nguvu.

376 Mjumbe aliyetumwa kutoka kwa Mungu anawezaje kuamini tu baadhi ya Maandiko na si Neno lote, akane sehemu Yake? Nabii wa kweli wa Mungu atalitangaza Neno katika siku za mwisho. Madhehebu yatamchukia. Hatacheza nao hata kidogo. Atakuwa kama alivyokuwa wakati alipokuja katika kule Kuja kwa kwanza kwa Kristo, "Enyi uzao wa nyoka." Lakini waliochaguliwa tangu zamani watasikia na watajiweka tayari kwa ajili ya kuhesabu kinyumenyume. Uzao wa kifalme wa imani ya Ibrahimu, kama yeye, ukilishikilia Neno la Mungu, haidhuru, kwa kuwa alikuwa amekusudiwa tangu zamani.

377 Yule mjumbe wa Malaki 4 atatokea kwenye wakati uliokusudiwa na Mungu. Sote tunamtafuta. Tunaamini atakuja. Hiyo ni kulingana na Neno Lake. Itakuwa katika

wakati wa mwisho. Ambapo, ni wakati sasa wa kuliona. Yeye atakuwa—atajiweka wakfu ipasavyo kwa Neno, kama vile daima wameonyeshwa na Neno la Mungu na kuthibitishwa. Mungu atathibitisha yale anayohubiri kuwa ni Kweli, kama alivyomfanyia Eliya, kwa kuwa Eliya yuaja, akijitayarisha kwa ajili ya Unyakuo wa Mlima Sayuni. Yesu alisema, "Katika siku za mwisho itakuwa kama wakati wa Lutu."

378 Mahubiri yake yatakuwa kwa Roho na mkondo wa nguvu za Neno la Mungu. Kwa sababu mengi sana yameitwa Kweli ya Mungu, wengi watamwelewa vibaya mjumbe huyu wa kweli. (Nimeandika hapa, u-n-a-b-i-i, "Unabii.") Kwa sababu, kwa sababu mengi sana yameitwa Kweli ya Mungu na waigizaji, wahudumu wengi wa kweli watakosa kumfahamu mjumbe huyo.

379 Kwa kuwa, unabii wa wakati wa mwisho utajirudia, naamini. Kama vile yule mtangulizi wa kwanza alivyokuja kutoka nyikani na kupaza sauti, "Tazama Mwana-Kondoo wa Mungu," mtangulizi wa pili labda atafanya vivyo hivyo kwa kuwaelekeza watu kwa Bibi-arusi aliyezaliwa na Neno. Bibi-arusi wa Kristo ataelekezwa angani, katika kule kuonekana kwa Yesu. Akipaza sauti, "Tazama Mwana-Kondoo wa Mungu," yatatoka midomoni mwake. (Mungu atusaidie kuwa tayari kwa ajili ya tukio hili lililo karibu.)

Afadhali niliache, kutoka papa hapa.

380 Mnaamini? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Kwa nini imekuwa hivi? Je, mna ufahamu bora zaidi sasa? ["Amina."] Ni Neno, marafiki. Hii imekuwa kama saa sita, karibu sana nayo, saa tano na nusu, ama saa sita. Kuna mengi zaidi yangeweza kusemwa. Lakini hakika Roho Mtakatifu, kufikia wakati huu, ame—amelizamisha sana ndani yenu, hata mnajua kile ninachozungumzia. Tuko kwenye wakati wa mwisho. Mbegu zimepandwa sasa. Mvua ya vuli iko karibu kuja.

381 Kumbukeni, kutakuwako na kusanyiko kubwa sana la kimadhehebu hivi karibuni sana, litakuwa la kuogofya sana, nao watajileta pamoja katika Muungano huu wa Makanisa. Na ndipo kanisa la namna hii litafungwa, kadiri wajuavyo. Ni kwenye wakati huo, ambapo Yesu ataonekana, Naye ataonyesha ni yupi Bibi-arusi na yupi siye. Basi kumbukeni, marafiki Wakristo, mimi ni mwanadamu, ninaweza kukosea. Lakini Mungu, akiwa ni Mungu, hawezi kukosea. Maneno yote yaliyoandikwa hayana budi kutimizwa. Yesu alisema hivyo. Kwa hiyo tuna vitu hapa katika Maandiko ambavyo havina budi kutimia, na hilo ni mojawapo ya mambo, huku kususiwa kunakokuja.

382 Lakini kabla ya kuja kwa kususiwa huku, kwa kutiwa alama ya mnyama, hapana budi kuwe na Mbegu iliyopandwa, ili Mungu atoe Kanisa kutoka kwake. Mnaelewa sasa? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Mbegu haina budi kupandwa. Mbegu ya kimadhehebu, nao watafanya mfano ama sanamu ya mnyama,

kanisa la Rumi. Na hapana budi kuwe na Bibi-arusi wa kweli. Nasi tunafahamu ya kwamba yule anayejiita bibi-arusi amekataliwa.

383 Bibi-arusi wa Adamu alikataa kuleta Uzima. Alileta mauti. Sisi ni mazao yake, miili yetu. Sote tunakufa. Tuangalie, unaweza kuona.

384 Bibi-arusi wa Yehova alikufa, Yeye alimtaliki, na kuchukua watu kutoka kwa Mataifa, kwa ajili ya Jina Lake. Hiyo ni kweli? Jina Lake; kama vile mwanamke anavyochukua jina la mwanamume, bibi-arusi. Sasa yeye amefanya nini? Jambo lile lile walilofanya wakati ule mwingine, akajiundia dhehebu, akajichafua.

385 Lakini katika kila kizazi, kila uamsho huleta nabii fulani wa Mungu. *Nabii* ni "mhubiri, mhubiri wa kweli juu ya Neno, anayedumu na Neno," nao wanaleta uamsho unaomkusanya huyo Mteule kutoka kwenye kizazi hicho.

386 Ndipo linaingia kwenye mbegu, ndipo Mungu kamwe hatalitumia tena. Ninamwomba mwanatheolojia yeyote, mwanahistoria yeyote, kuniambia wakati mmoja ambapo dhehebu liliwahi kuinuka. Kamwe halikuinuka. Lillikufa lilipounda dhehebu, na hapo ndipo lilipolala. Ninawazia juu ya Dwight Moody, Moody Bible, imekufa kama usiku wa manane.

387 Ninawazia juu ya Wamethodisti, Wapentekoste, Wapresbiteri, Walutheri, Wanazarayo, Wapilgrim Holiness, watu watauwa walioinuka, Buddy Robinson, na—na George Whitefield, na hao watu wote mashuhuri, watauwa waliohubiri Injili. Nacho kizazi hicho kilipokea Mbegu iliyopandwa kwa ajili yao. Kama vile mahindi, kama ilikuwa ni ubua, kama ilikuwa ni jani, kama ilikuwa ni kishada, kama ilikuwa punje; chochote kile, mhudumu huyo alileta Neno la siku hiyo. Iliita kutoka kwenye pepo nne za dunia na kuwachukua Wateule wa kizazi hicho. Kupitia hao Wateule, imejengwa Nyumba ya Mungu aliye hai.

388 Sasa, huduma hii hapa haina budi kuchongwa kufikia mahali ambapo kazi zile zile alizofanya Yesu, kwa sababu, atakapokuja, lile Jiwe la Kichwa litaingia moja kwa moja ndani Yake. Kwa sababu hawataninii. . .Kutakuwako na Unyakuo utakaokuja, nao watachukuliwa, na huo Mwili uliosalia utakuja pamoja Nao, Naye ataenda Mbinguni. Si dhehebu, enyi marafiki; Kanisa la Neno la Mungu! Mnaamini hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

Hizi hapa baadhi ya leso hapa.

389 Sasa naenda. Ninaenda, sijui ni wapi. Ninatafuta, kama mnavyotafuta nyinyi, mapenzi ya Mungu. Laiti ningaliweza kukaa kwenye maskani hii; siwezi kufanya hivyo. Kuna maelfu; ninasikia kilio, roho mchafu akiwararua. Siwezi kulala, ni vigumu. Ninawasikia watoto wadogo wakilia, na kuwaona

akina mama wakiwasukuma watoto wao kwenye mstari wa maombi; kumwona mama fulani akimpepea mtoto mchanga; akishikilia shuka juu yake, kumkinga na mvua, uani. Moyo wangu unawahurumia sana.

390 Nilipoijenga maskani hii, ile siku niliyoweka jiwe la pembeni huko nje, ninakumbuka ono lile, asubuhi hiyo. Limeandikwa papo hapo kwenye jiwe la pembeni, kasema, "Hii siyo maskani yako." Kasema, "Fanya kazi ya mwinjilisti. Timiliza huduma yako." [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Ninalipenda. Ninawapenda watoto wa Mungu kila mahali. Sijui ataniongoza wapi. Sijui. Ninangojea. Nimekuwa nikingojea kwa mwaka mmoja. Huenda nikangojea kwa miaka miwili, naweza kungojea kwa mitatu. Sijui. Sijui hatua inayofuata. Ninaingojea. Lakini nafikiri, kulingana na Maandiko, Neno limepandwa. Jambo linalofuata ni kule kuja kwa Roho.

391 Billy Graham huenda akahubiri kila mahali. Oral Roberts, hao watu wacha Mungu, huenda wakahubiri kila mahali. Bwana anaweza akanituma kupanda Mbegu mahali pengine, shamba fulani. Lakini ninaamini taifa letu limepandwa mbegu. Ninaamini liko tayari kwa mavuno sasa.

392 Wakati Roho atakaposhuka, na kunakuwa na uamsho miongoni mwa watu, hayo madhehebu yataungana pamoja hakika tu kama ninavyosimama mimbarani, ndipo Kanisa la Mungu litaondoshwa. Nao watafanya njama sana, mpaka watayaunganisha, na kumsusia mtu yeyote asiye wao.

393 Rumi itatautawala ulimwengu kwa saa moja tu. Itatawala kwa kipindi kidogo. Sio ukomunisti. Urumi utautawala ulimwengu, ukishirikiana na Uprotestanti, katika mfano wa kanisa la kimadhehebu ambalo Mungu amelikataa. Hiyo ni karibu tu kadiri ninavyolijua Neno la Mungu.

394 Nawapenda. Ninawathamini. Labda nitarudi yapata Jumapili, juma moja. Ninashuka kwenda huko Florida sasa, Bwana akipenda; huko chini Georgia, kwa ajili ya kesho usiku. Nina maskini mikutano michache iliyotapakaa kote, kama Bwana akiongoza. Nina kitabu kilichojaa hiyo, ambacho Ndugu Roberson, ama, Borders alinitumia, hivi majuzi. Nadhani kuna, vema, kuna mahali ambapo kuna makanisa thelathini na arobaini yaliyo tayari kushirikiana, lakini Roho anaonekana kunishikilia. Sijui ni kwa nini. Sijui ni kwa nini. Kwa hiyo niombeeni, nitawaombea, kwamba pamoja tuweze kusimama. Mungu na atusaidie. Jalia kusiwe na mmoja wenu hapa ambaye atashindwa na ataukosa huo wakati mkuu unaokuja.

395 Sasa, nimeshtakiwa kwa mambo mengi, marafiki. Na nina hatia ya mambo mengi. Mimi ni mzembe; hiyo ni kweli. Sijui ni kwa nini, inabidi mtu fulani anisukumie kwenye kona, kunifanya nipigane vita. Sijui. Hayo ni maumbile. Nimefanya mambo ambayo sikupaswa kufanya, si kwa makusudi, bali

ni—niliyavamia. Na hilo ndilo linalonifanya niogope sana, katika kuona katika siku hii, siku tunayoishi, nanyi mnaona sasa kile ninachoamini. Ninataka kusikia kutoka kwa Mungu, ikiwezekana, kabla sijachukua hatua, mnaona, maana sitaki kumkosea. Ninataka kuwa pamoja Naye, kila mahali. Nami nawatakeni mniombee.

396 Basi, kumbukeni, nimewaambia Kweli. Nami nawashukuru kwa kuketi hapa siku hii yote, tangu mapema asubuhi ya leo. Wengi wenu mmesimama kuzunguka kuta, kwenye kumbi, bado, miguu na viganja vikikakamaa. Mkiwa mmeketi nje kwenye magari, karibu betri zenu zinazima, kutokana na kusikiliza. Nayo haya hapa, yote yako kwenye kanda. Hao wavulana wamezirekodi huko nyuma. Mtaweza kuzipata. Na kama mkizipata, zipelekeni nyumbani na kuzichunguza kwa makini sana, kwa hekima, mwone yale Bwana atakayowafunulia.

397 Mnampenda? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Teddy yuko wapi? [Mtu fulani anasema, "Papa hapa."] Kabla tu hatujaombea leso hizi pamoja na watu, ninataka kumwombea kila mmoja wenu. Ninataka kuimba wimbo huu sasa. Ndipo Ndugu Neville atatoa matangazo yake kwa ajili ya ibada hiyo nyingine.

Nampenda, napenda . . .

Mnalipenda Neno Lake? Basi mnampenda.

Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

Yeye si ni wa ajabu? Na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo tu.

398 Baba wa Mbinguni, nikijisikia kuongozwa kufanya jambo hili sasa kwa saa nyingi za kuhubiri, kueleza, nikifanya vizuri nijuavyo, kwa ajili ya wanadamu wenzangu, nikijaribu kuwafanya waelewe mambo ambayo nimesema, na kwa nini nimefanya mambo haya. Ninakuletea sasa, Bwana, watu hawa, watu hawa wanaoonekana na wale watu watakaosikia kanda hizi baadaye. Mungu Mwenyewe na atupe Tafsiri ya Kiungu. Nami nina hakika, Bwana, kama nilililleta Neno, litawashukia wale ambao limekusudiwa tangu zamani kuwashukia. Neno Lako ni Kweli.

399 Baba, ninasikitika kwamba nilikukosea, mara nyingi. Ninaomba unisamehe. Ninaomba uwasamehe wasikilizaji wangu, wanaoonekana na wasioonekana, dhambi zao zote. Kwamba, Bwana Mungu, tunatambua ya kwamba tuko kwenye mwisho wa safari. Kila ishara iko papa hapa mbele zetu. Nina hakika mtu wa kiroho, Bwana, anashika yale niliyosema hivi punde dakika chache zilizopita. Ninaomba ya kwamba wataelewa, Bwana. Na kile tulicho . . . mahali tulipo. Tuko

karibu na kitu fulani. Tunaweza kuyasikia mawimbi makubwa. Tuko karibu.

400 Tusaidie, Bwana, tusaidie. Ninamwombea kila mtu binafsi aliyeketi hapa. Ninaomba kwa ajili ya leso hizi zinazowawakilisha wagonjwa. Nisaidie, Bwana, kwamba niombe maombi ya imani, kwa ajili ya wote.

401 Sasa, kwa wale walio na moyo wazi kwa ajili ya Neno la Mungu, kwa imani, ninapanda Mbegu hii. Ninaipanda katika Jina la Yesu Kristo, nikimwamini Mungu. Lakini, Bwana Mungu, ninaikabidhi Kwako sasa. Imwagilie maji. Tuma Roho juu Yake, Bwana, hilo Neno lililorutubishwa pale; kwamba Wewe ni Mungu yeye yule mkuu, kuponya; Mungu yeye yule mkuu, kuokoa; Mungu yeye yule mkuu, katika ufufuo. Wewe ni Mungu. Jalia lizae Zao, Bibi-arusi kwa ajili ya Bwana Yesu, tumbo la uzazi lililotakaswa la moyo, kupokea Neno. Tujalie, Bwana. Ninawakabidhi Kwako, uchague kutoka hapa, Bwana, ikiwezekana kila mmoja, Bibi-arusi Wako, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Napenda . . .

Sasa peana mikono na mtu fulani.

Na- . . .

Peaneni tu mikono, bakini vitini mwenu na kupeana mikono.

Kwani . . .

Nyote pamoja sasa, huku mmeinua mikono yenu.

Na- . . .
Na kununua ninii wangu . . .

402 Sasa, baada ya Neno kuwa na saa sita za maonyo, ninawaamuru kwenye hatua ya kwanza. “Tubuni,” na kuangalia juu, “mkabatizwe,” katika dakika chache, “katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi yako, na Mungu aliahidi kukupa Roho Mtakatifu. Kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu na kwa watoto wenu, na kwa watu wote walio mbali.” Ni kwa Wamethodisti, Wabaptisti, Wakatoliki, Wapresbiteri. “Na yeyote atakayelipokea Neno, na aje.” Mnaamini hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

Ninawapa sasa mchungaji, kwa ajili ya ibada iliyosalia. Ataandaa mambo sasa, tunapojitayarisha kwa ajili ya ubatizo. Ndugu Neville.

Sasa ketini kidogo tu.

403 Vema, Ndugu Neville, sasa, mchungaji wetu, atawaambia kuhusu utaratibu wa ibada sasa hivi, katika dakika moja tu. Mungu awabariki, mpaka nitakapowaona.

62-0318 Neno Lililonenwa Ndilo Mbegu Ya Asili
Branham Tabernacle
Jeffersonville, Indiana Marekani

SWAHILI

©2024 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org